# Language: Swahili

## Book: Luke

---

## Luke

### Chapter 1

1 Wengi wamejitahidi kuweka katika mpangilio simulizi kuhusu masuala ambayo yametimizwa kati yetu, 2
kama walivyotupatia sisi, ambao tangu mwanzo ni mashahidi wa macho na watumishi wa ujumbe. 3 Hivyo
nami pia, baada ya kuchuguza kwa uangalifu chanzo cha mambo haya yote tokea mwanzo - nimeona ni
vema kwangu pia kukuandikia katika mpangilio wake - mheshimiwa sana Theofilo. 4 Ili kwamba uweze
kujua ukweli wa mambo uliyofundishwa. 5 Katika siku za Herode, mfalme wa Yudea, palikuwa na kuhani
fulani aliyeitwa Zekaria, wa ukoo wa Abiya. Mke wake alitoka kwa binti za Haruni, na jina lake aliitwa
Elizabeti. 6 Wote walikuwa wenye haki mbele za Mungu; walitembea bila lawama katika amri zote na
maagizo ya Bwana. 7 Lakini hawakuwa na mtoto, kwasababu Elizabethi alikuwa tasa, na kwa wakati huu
wote wawili walikuwa wazee sana. 8 Sasa ilitokea kwamba Zakaria alikuwa katika uwepo wa Mungu,
akiendelea na wajibu wa kikuhani katika utaratibu wa zamu yake. 9 Kulingana na desturi ya kuchagua ni
kuhani yupi atakayehudumu, alikuwa amechaguliwa kwa kura kuingia katika hekalu la Bwana na hivyo
angefukiza uvumba. 10 Kundi lote la watu lilikuwa likiomba nje wakati wa kufukizwa kwa ufumba. 11 Sasa
malaika wa Bwana alimtokea na kasimama upande wa kulia wa madhabahu ya kufukizia. 12 Zakaria
alitishika alipomuona; hofu ikamwangukia. 13 Lakini malaika akamwambia, "Usiogope Zakaria,
kwasababu maombi yako yamesikika. Mke wako Elizabeth atakuzalia mwana. Jina lake utamwita Yohana.
14 Utakuwa na furaha na uchangamfu, na wengi watakufurahia kuzaliwa kwake. 15 Kwa kuwa atakuwa
mkuu mbele ya macho ya Bwana. Hatakunywa divai au kinywaji kikali, na atakuwa amejazwa na Roho
Mtakatifu tangu tumboni mwa mama yake. 16 Na watu wengi wa Israel watageuzwa kwa Bwana Mungu
wao. 17 Atakwenda mbele za uso wa Bwana katika roho na nguvu ya Eliya. Atafanya hivi ili kurejesha
mioyo ya baba kwa watoto, ili kwamba wasiotii wataenenda katika hekima ya wenye haki. Atafanya hivi
kuweka tayari kwa Bwana watu ambao wameandaliwa kwa ajili yake." 18 Zakaria akamwambia malaika,
"Nitawezaje kujua hili? Kwasababu mimi ni mzee na mke wangu miaka yake imekuwa mingi sana." 19
Malaika akajibu na kumwambia, "Mimi ni Gabrieli, ambaye husimama mbele za Mungu. Nilitumwa
kukwambia, kukuletea habari hii njema. 20 Na tazama, hutaongea, utakuwa kimya, hutaweza kuongea
mpaka siku ile mambo haya yatakapotokea. Hii ni kwasababu ulishindwa kuamini maneno yangu ambayo
yatatimizwa kwa wakati mwafaka." 21 Sasa watu walikuwa wakimsubiri Zakaria. Walishangazwa kwamba
alikuwa anatumia muda mwingi hekaluni. 22 Lakini alipotoka nje, hakuweza kuongea nao. Wakatambua
kwamba alikuwa amepata maono alipokuwa hekaluni. Aliendelea kuonesha ishara na alibaki kimya. 23
Ikatokea kwamba siku za huduma yake zilipokwisha aliondoka kurudi nyumbani kwake. 24 Baada ya
Zakaria kurudi nyumbani kutoka kwenye huduma yake hekaluni, mke wake akawa mjamzito. Naye
hakutoka nyumbani mwake kwa muda wa miezi mitano. Akasema, 25 "Hili ndilo amabalo Bwana amefanya
kwangu aliponitazama kwa upendeleo ili kuiondoa aibu yangu mbele za watu." 26 Sasa, katika mwezi wa
sita wa mimba ya Elizabeti, Mungu alimwambia malaika Gabrieli kwenda kwenye mji wa Galilaya uitwao
Nazareti, 27 kwa bikra aliyekuwa ameposwa na mwanaume ambaye jina lake lilikuwa Yusufu. Yeye
alikuwa wa ukoo wa Daudi, na jina la bikra huyo lilikuwa Mariamu. 28 Akaja kwake na akasema, "Salaam,
wewe uliyepokea neema kuu! Bwana amependezwa nawe." 29 Lakini maneno ya malaika yalimchanganya
na hakuelewa kwa nini malaika alisema salaam hii ya ajabu kwake. 30 Malaika akamwambia, "Usiogope,
Mariamu, maana umepata neema kutoka kwa Mungu. 31 Na tazama, utabeba mimba katika tumbo lako na
utazaa mwana. Nawe utamwita jina lake 'Yesu.' 32 Atakuwa mkuu na ataitwa Mwana wa Aliye Juu Sana.
Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi baba yake. 33 Atatawala juu ya ukoo wa Yakobo milele na
ufalme wake hautakuwa na mwisho. 34 Mariamu akamwambia malaika, hili litatokea kwa namna gani,
maana sijawahi kulala na mwanaume yeyote? 35 Malaika akajibu na akamwambia, "Roho Mtakatifu
atakujia juu yako, na nguvu ya Aliye Juu Sana itakuja juu yako. Kwa hiyo, mtakatifu atakayezaliwa ataitwa
Mwana wa Mungu. 36 Na tazama, ndugu yako Elizabeti anaujauzito wa mwana kwenye umri wake wa
uzee. Huu ni mwezi wa sita kwake, ambaye alikuwa anaitwa mgumba. 37 Maana hakuna lisilowezekana

kwa Mungu." **38** Mariamu akasema, "Tazama, mimi ni mtumishi wa kike wa Bwana. Acha iwe hivyo
kwangu sawa sawa na ujumbe wako." Kisha malaika akamwacha. **39** Ndipo katika siku hizo Mariamu
aliondoka na kwa haraka alikwenda katika nchi ya vilima, kwenye mji katika nchi ya Yudea. **40** Alikwenda
nyumbani mwa Zekaria na akamsalimia Elizabeti. **41** Sasa, ilitokea kwamba Elizabeti aliposikia salamu ya
Mariamu, mtoto tumboni mwake akaruka, na Elizabeti akajazwa na Roho Mtakatifu. **42** Akapaza sauti
yake na kusema kwa sauti kuu, "umebarikiwa wewe zaidi miongoni mwa wanawake, na mtoto aliyemo
tumboni mwako amebarikiwa. **43** Na imekuwaje kwangu kwamba, mama wa Bwana wangu ilipasa aje
kwangu? **44** Kwa kuwa tazama, iliposikika masikoni mwangu sauti ya kusalimia kwako, mtoto tumboni
mwangu akaruka kwa furaha. **45** Na amebarikiwe mwanamke yule ambaye aliamini ya kwamba ungetokea
ukamilifu wa mambo yale aliyoambiwa kutoka kwa Bwana." **46** Mariamu akasema, nafsi yangu inamsifu
Bwana, **47** na roho yangu imefurahi katika Mungu Mwokozi wangu. **48** Kwa maana ameiangalia hali ya
chini ya mtumishi wake wa kike. Tazama, tangu sasa katika vizazi vyote wataniita mbarikiwa. **49** Kwa
maana yeye aliyemweza amefanya mambo makubwa kwangu, na jina lake ni takatifu. **50** Rehema yake
inadumu toka kizazi hata kizazi kwa wale wanao mheshimu yeye. **51** Ameonesha nguvu kwa mkono wake;
amewatawanya wale ambao walijivuna juu ya mawazo ya mioyo yao. **52** Amewashusha chini wana wa
wafalme toka katika viti vyao vya enzi na kuwainua juu walio na hali ya chini. **53** Aliwashibisha wenye njaa
kwa vitu vizuri, bali matajiri amewafukuza mikono mitupu. **54** Ametoa msaada kwa Israeli mtumishi wake,
ili kukumbuka kuonesha rehema **55** (kama alivyosema kwa baba zetu) kwa Abrahamu na uzao wake
milele." **56** Mariamu alikaa na Elizabeti yapata miezi mitatu hivi ndipo akarudi nyumbani kwake. **57** Sasa
wakati ulikuwa umewadia kwa Elizabeti kujifungua mtoto wake na akajifungua mtoto wa kiume. **58** Jirani
zake na ndugu zake walisikia jinsi Bwana alivyoikuza rehema kwake, na wakafurahi pamoja naye. **59** Sasa
ilitokea siku ya nane kwamnba walikuja kumtahiri mtoto. Ingewapasa kumwita jina lake, "Zekaria," kwa
kuzingatia jina la baba yake, **60** Lakini mama yake akajibu na kusema, "Hapana; ataitwa Yohana." **61**
Wakamwambia, hakuna hata mmoja katika ndugu zako anayeitwa kwa jina hili." **62** Wakamfanyia ishara
baba yake kuashiria yeye alitaka jina aitwe nani. **63** Baba yake akahitaji kibao cha kuandikia, na
akaandika, "Jina lake ni Yohana." Wote wakashangazwa na hili. **64** Ghafla mdomo wake ukafunguliwa na
ulimi wake ukawa huru. Akaongea na kumsifu Mungu. **65** Hofu ikawajia wote walioishi karibu nao.
Mambo haya yakaenea katika nchi yote ya vilima vya Yudea. **66** Na wote walioyasikia wakayatunza
mioyoni mwao, wakisema, " Mtoto huyu kuwa wa namna gani?" Kwasababu mkono wa Bwana ulikuwa
pamoja naye. **67** Baba yake Zekaria alijazwa na Roho Mtakatifu na akatoa unabii, akisema, **68** "Asifiwe
Bwana, Mungu wa Israeli, kwa sababu amesaidia na alishughulikia wokovu kwa watu wake. **69**
Ametuinulia pembe ya wokovu katika nyumba ya mtumishi wake Daudi, kutoka miongoi mwa mwa ukoo
wa mtumishi wake Daudi, **70** kama alivyosema kwa kinywa cha manabii wake waliokuweko katika nyakati
za kale. **71** Atatuoka kutoka kwa adui zetu na kutoka mikononi mwa wote wanaotuchukia. **72** Atafanya hivi
kuonesha rehema kwa baba zetu, na kukumbuka agano lake takatifu, **73** kiapo alichokisema kwa
Abrahamu baba yetu. **74** Aliapa kuthibitha kwamba ingewezekana kumtumikia Yeye bila hofu, baada ya
kuokolewa kutoka katika mikononi ya adui zetu. **75** katika utakatifu na haki mbele zake siku zetu zote. **76**
Ndiyo, na wewe mtoto, utaitwa nabii wa Aliye Juu Sana, kwa kuwa utaenenda mbele za uso wa Bwana ili
kumwandalia njia, kuwaandaa watu kwa ajili ya ujio wake, **77** kuwafahamisha watu wake kwamba,
wataokolewa kwa njia ya kusamehewa dhambi zao. **78** Hili litatokea kwa sababu ya huruma ya Mungu
wetu, sababu ambayo jua tokea juu litatujia, **79** kuangaza kwao wakaao gizani na katika uvuli wa mauti.
Atafanya hivi kuiongoza miguu yetu kwenye njia ya amani." **80** Sasa, yule mtoto akakua na kuwa mwenye
nguvu rohoni na alikaa nyikani mpaka siku ya kujitokeza kwake kwa Israeli.

---

## Luka 01 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

Baadhi ya tafsiri hupendelea kuweka sala ndefu au unabii mbele kidogo ya maandiko nyingine. Kwa sababu hii, ULB na tafsiri nyingine nyingi za Kiingereza huingiza mistari ya 1:46-55, 68-79.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

### Dhana maalum katika sura hii

#### "Ataitwa Yohana"

Haikuwa jambo la kawaida katika ichi ya Mashariki ya Karibu kumwia mtoto jina ambalo sio jina la jamaa. Kwa kuwa Elizabeti na Zakaria hawakuwa na mtu aliyeitwa "Yohana" katika familia yao, jina hili liliwashangaza sana kwa watu wengine.

### Takwimu muhimu za matamshi katika sura hii

Luka hatumii maneno mengi magumu. Lugha yake ni rahisi na ya moja kwa moja.

---

## Luke 1:1

**Taarifa kwa Ujumla**
Luka anaeleza kwanini anamwandikia Theofilo.

**mada**
"taarifa" au "simulizi za kweli"

**kati yetu**
Neno "yetu" katika kauli hii linaweza au haliwezi kutomhusisha Theofilo.

**Alikabidhi kwetu sisi**
"Sisi" katika kauli hii Theofilo hahusiki.

**Kabidhiwa kwao**
"kupewa wao" au "iliyotolewa kwao"

**Watumishi wa ujumbe**
Unaweza kuhitaji kupambanua kwamba ujumbe ni nini. NI: "kumtumikia Mungu kwa kuwaambia watu habari zake" au "kufundisha watu habari njema kuhusu Yesu"

**Ilichunguzwa kwa uangalifu**
"kutafiti kwa makini." Luka alikuwa makini kutafuta uhakika wa kile kilichotokea. Huenda alizungumza na watu mbalimbali ambao waliona kilichotokea kuhakikisha anachokindika kuhusu tukio hili ni sahihi.

**Mheshimiwa sana Theofilo**
Luka alisema hivi kuonesha heshima na taadhima kwa Theofilo. Hii inaweza kumaanisha kwamba Theofilo alikuwa afisa mhimu serikalini. Sehemu hii tumia mfumo unaotumika kwenye utamaduni wako kumwongelea mtu mwenye mamlaka ya juu. Baadhi ya watu wanaweza kupendelea pia kuweka salamu mwanzoni na kusema "kwa ... Theofilo" au "Mpendwa ... Theofilo."

**Mheshimiwa sana**
"mheshimiwa" au "muungwana"

**Theofilo**
Jina hili linamaana "rafiki wa Mungu." Linaweza likaweka wazi tabia ya mtu huyu au inaweza kuwa ndilo jina lake halisi. Tafsiri nyingi limetumika kama jina lake.

## Luke 1:5

**Kauli unganishi:**
Malaika anatoa unabii kuzaliwa kwa Yohana

**Taarifa ya Jumla**
Zakaria na Elizabethi watabulishwa. Mistari hii inatoa taarifa ya historia kuwahusu wao.

**Katika siku za Herode, mfalme wa Uyahudi**
"Wakati ambao Mfalme Herode alitawala katika Uyahudi"

**palikuwa na uhakika**
"Palikuwa pa uhakika" au "palikuwa na." Hii ilikuwa njia ya kutambulisha mhusika mpya katika katika historia. Fikiria namna lugha yako inavyofanya.

**mgawo**
Inafahamika kwamba hii inarejea kwa makuhani. NI: "mgawo wa makuhani au "kundi la makuhani."

**wa Abiya**
"ambaye alitokea ukoo wa Abiya." Abiya alikuwa mhenga wa kundi la makuhani na wote waliokuwa wanatokea kwa Haruni, ambaye alikuwa kuhani wa kwanza katika Israeli.

**"Mke wake alikuwa akitokea katika mabinti wa Haruni."**
"Mke wake alitokea ukoo wa Haruni" Hii inamaanisha anatokea katika mfumo ule ule wa kikuhani kama Zakaria. "mke wake pia alitokea pia ukoo wa Haruni" au "Zakaria na mke wake wote wawili walitokea kwa Haruni."

**"Kutokea kwa mabinti wa Haruni"**
"tokea ukoo wa Haruni"

**mbele za Mungu**
"mbele za macho ya Mungu" au "kwenye mtazamo wa Mungu"

**amri zote na maagizo ya Bwana**
"yote ambayo Bwana alishaamuru na aliyotaka"

**Lakini**
Hili neno la kutofautisha kwamba yafuatayo hapa ni kinyume cha yaliyotarajiwa. watu walitarajia kwamba kama walifanya yaliyosahihi, Mungu


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

angeliwaruhusu kuwa na watoto. Ingawa wanandoa hawa walifanya yaliyo sahihi, hawakuwa na mtoto yeyote.

## Luke 1:8

**Sasa ikaja kuwa**
Hii kauli ilitumika kubadili simulizi kutoka taarifa za mwanzo kwenda kwa wahusika.

**katika utaratibu wa mgawo wake**
"ilipokuwa zamu ya kundi lake" au "wakati ulipowadia wa kundi lake kuhudumu"

**kutokana na desturi ya kuchagua kuhani yupi ambaye ... achome ubani**
Sentensi hii inatupa sisi taarifa kuhusu wajibu wa kikuhani.

**taratibu za kidesturi**
"mfumo wa kiutamaduni" au "njia yao ya kawaida"

**kuchagua kwa kura**
kura ilikuwa ni jiwe lenye alama ambalo lilitupwa au viringishwa chini ili kwamba liwasaidie kuamua jambo fulani. Makuhani waliamini kwamba Mungu aliielekeza kura kuwaonesha kile walichokitaka makuhani kuchagua.

**hivyo anaweza kuchoma ubani**
Makuhani walikuwa wanachoma harufu nzuri kama sadaka kwa Mungu kila asubuhi na jioni katika madhabahu maalumu ndani ya hekalu.

**mkutano wote wa watu**
"Idadi kubwa ya watu" au "Watu wengi"

**nje**
Kiwanja ilikuwa ni eneo linalolizunguka hekalu. NI: "nje ya jengo la hekalu" au "kwenye kiwanja nje ya hekalu."

**katika wakati**
"kwenye muda uliopangwa." Haikowazi kama ilikuwa muda wa asubuhi au jioni kwaajili ya sadaka ya ubani.

## Luke 1:11

**Sentensi Unganishi:**
Wakati Zakaria anafanya wajibu wake hekaluni, malaika anakuja kutoka kwa Mungu kumpa ujumbe.

**Sasa**
Neno hili linazingatia mwanzo wa kitendo katika historia,

**alimtokea**
"ghafla alikuja kwake" au "ghafla alikuwa pale pamoja na Zakaria." Hii inaweka wazi kwamba malaika alikuwa pamoja na Zakaria, na siyo tu maono.

**Zakaria ... alikuwa katekewa ... woga ukamwangukia**
Hizi kauli mbili zinamaana ileile, na zinasisitiza jinsi Zakaria alivyokuwa na hofu.

**Zakaria alipomuona**
"Zakaria alipomwona malaika" Chanzo cha hofu kilikuwa kushituliwa na ile asili ya malaika. Zakaria hakufanya kitu chochote kibaya.

**Hofu ikaja juu yake**
Hofu ni kitu kinachofafanuliwa kama kwamba shambulio au Zakaria alizididiwa nguvu.

**Usiogope**
"usiendelee kuniogopa mimi" au "Wewe hutakiwi kuniogopa mimi"

**maombi yako yamesikiwa**
"Mungu amesikia ambacho uliomba." Kinachofuata kinadokeza na kingeliongezwa: "ataruhusu hiyo." Mungu hakukomea kusikia tu alichoomba Zakaria; pia alikuwa anaelekea kutenda.

**utazaa mwana**
"mwana wa kiume kwaajili yako" au "kuzaa mtoto wako wa kiume"

## Luke 1:14

**Kwaajili**
"Kwasababu" au "Katika nyongeza kwa hili"

**shangwe na kufurahia**
Haya maneno mawili yanamaanisha jambo lilelile na yangeliweza kuunganishwa kama lugha haina maneno yanayofanana. NI: "furaha sana."

**kwa kuzaliwa kwake**
"kwasababu ya kuzaliwa kwake"

**atakuwa mkuu mbele ya macho ya Bwana**
"atakuwa mtu mhimu sana kwaajili ya Bwana" au "Mungu atamstahilisha kuwa mtu mhimu sana" (UDB)

**atajazwa na Roho Mtakatifu**
Hii itatajwa kama kauli tendwa: NI: "Roho Mtakatifu atamwezesha" au "Roho Mtakatifu atamwongoza." Hakikisha haieleweki sawa na ambavyo roho mchafu anaweza kumfanya mtu.

**toka tumboni mwa mamaye**
watu tayari walishawahi kujazwa na Roho Mtakatifu, lakini hakuna hata mmoja aliyesikia mtoto ambaye hajazaliwa kajazwa na Roho Mtakatifu.

## Luke 1:16

**Watu wengi wa Israeli**
Inaeleweka kama japo Zakaria haikuwekwa, kauli hii ingelitafsiriwa kama "wengi wa koo za Israeli" au "wengi wenu ambao ni watu wa Mungu, Israeli."


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

Kama mabadiliko haya yakifanyika, hakikisha kwamba "Mungu wao" imebadilishwa kuwa "Mungu - wao (wingi)."

**kurudi**
"kirudi nyuma" au "rejea"

**atakwenda mbele ya uso wa Bwana**
Yeye angelitangulia kutangaza kwa watu kwamba Bwana angelikuja kwao.

**mbele ya uso wa**
"uso wa" iko hapa ni nahau ambayo inarejea kwenye ule uwepo wa Bwana. Wakati mwingine iliondolewa kwenye tafsiri. NI: "kabla."

**katika roho na nguvu ya Eliya**
"pamoja na ile roho na nguvu alizokuwa nazo Eliya." Neno "roho" liwe linarejea kwa Roho Mtakatifu wa Mungu au mwenendo wa Eliya au namna ya kufikiri. Hakikisha kwamba neno "roho" halimaanishi mzimu au roho mchafu.

**badilisha mioyo baba kuwaelekea watoto**
"Kushawishi baba kutunza watoto wao tena" au "kuwasababisha baba kurejesha uhusiano na watoto"

**rejesha mioyo**
"kurejesha moyo" ni sitiari kwaajili ya kubadili nia ya mtu fulani kuelekea hali fulani.

**asiyetii atatembea**
"tembea" ni sitiari kwa namna mtu anaishi na kutenda. NI: "asiyetii atatenda" au "asiyetii ataishi"

**asiyemtii**
"watu ambao hawatii"

**fanya tayari kwaajili ya Bwana**
haijasemwa jinsi watakavyo kuwa tayari. Hii ilidokeza taarifa zingeliongezwa. NI: "jitayarishe kuamini ujumbe wa Bwana" au "uwe tayari kumtii Bwana."

## Luke 1:18

**Namna gani naweza kujua hili?**
"Jinsi gani naweza kujua kwa hakika kwamba ulichosema kitatokea"? "kujua" kunamaanisha kujifunza kupitia uzoefu, akipendekeza Zakaria alikuwa akiuliza kutokana ishara kama uthibitisho. Hii inaweza kusemwa wazi kama: NI: "unaweza kufanya nini kuthibitisha kwangu kwamba hiki kitatokea?"

**Mimi ni Gabrieli, ambaye nasimama katika uwepo wa Mungu**
Hii inasemwa kama kukemewa kwa Zakaria. Uwepo wa Gabrieli, unakuja moja kwa moja kutoka kwa Mungu, itakuwa inatosha kumthibitishia Zakaria.

**ambaye husimama**
"ambaye hutumika"

**nilitumwa kuzungumza na wewe**
Hii inaweza. kusemwa kwenye mtindo wa kutenda. NI: "Mungu alinituma kusema kwako."

**tazama**
Neno "tazama" hapa linatutaarifu kuwa makini kwa taarifa zinazofuata za ku.shangaza

**ukimya, kutoweza kuzungumza**
Hii inamaanisha kitu kilekile, na vilirudiwa kusisitiza ukamilifu wa ukimya wake. NI: "kutoweza kuzungumza kabisa" au "hawezi kuzungumza kwa vyovyote."

**kutoamini maneno yangu**
"usiamini yale niliyosema"

**kwa wakati sahihi**
"kwa wakati ulioandaliwa"

## Luke 1:21

**Sasa**
Hii inadokeza kuhama katika simulizi kutokana nakilichotokea ndani ya hekalu kwenda kilichotokea nje. NI: "Wakati huo" au "Wakati malaika na Zakaria wanazungumza."

**Walitambua kwamba alishapata maono wakati akiwa hekaluni. Aliendelea kuwafanyia ishara na alibaki kimya.**
Mambo haya huenda yalitokea muda uleule, na ishara za Zakaria ziliwasaidia watu kuelewa kwamba amepata maono. Inaweza ikawa msaada kwa wasikilizaji wako wabadili utaratibu kuonesha hivyo. NI: "Yeye aliendelea kuwafanyia ishara na alibaki kimya. Hivyo walitambua kwamba alipata maono wakati akiwa ndani ya hekalu."

**maono**
maelezo yaliyotangulia yanaashiria kwamba Gabrieli alikuja kweli kwa zakaria hekaluni. Watu, hawajui hilo, walidhani Zakaria aliona maono.

**ilitokea**
Kauli hii inahamisha simulizi kwenda mbele ambapo huduma ya Zakaria ilikuwa inaishia.

**alikwenda nyumbani kwake**
Zakaria alikuwa haishi Yerusalemu, ambapo palikuwa na hekalu. Alisafiri kwenda kwenye mji alioishi.

## Luke 1:24

**Baada ya siku hizi**
Kauli "siku hizi" inarejea wakati Zakaria alikuwa anatumika hekaluni. Hii inawezekana kulisema hili kwa uwazi. NI: "Baada ya Zakaria kurudi nyumbani tokea kwenye huduma hekaluni."

**mke wake**
"mke wa Zakaria"

**alijitenga mwenyewe**
"hakuondoka nyumbani kwake" au "alibaki peke yake ndani"

**Hiki ndicho alichokifanya Bwana kwaajili yangu**
Kauli hii inarejea ukweli kwamba Bwana alimruhusu apate ujauzito.

**hiki ndicho**
Hili ni tamko zuri la mshangao. Yeye alikuwa na furaha sana kwa kile alichokitenda Bwana kwaajili yake.

**aliniangalia mimi kwa upendeleo**
"Kuangalia" ni nahau ambayo inamaanisha "kutendea" au "kushughulikia." NI: "tazama kwa wema" au "alinihurumia"

**aibu yangu**
Hii inarejea kwenye aibu aliyoihisi kwa sababu alikuwa hawezi kuwa na watoto.

### Luke 1:26

**Taarifa kwa Jumla**
Malaika Gabrieli anamtangazia Mariamu kwamba anakwenda kuwa mama wa mtu ambaye ni Mwana wa Mungu.

**kwenye mwezi wake wa sita**
"katika mwezi wa sita wa mimba ya Elizabeth." Hii ilikuwa lazima kulisema wazi kama ingelichanganya na mwezi wa sita katika mwaka.

**malaika Gabrieli alikuwa katumwa kutokea kwa Mungu**
Hii inaweza kusemwa kwenye mtindo wa kutenda: NI: "Mungu alimwambia malaika Gabrieli nenda"

**Yeye ni wa nyumba ya Daudi**
"Yeye niwa kabila lilelile kama Daudi" au "Yeye alikuwa ukoo Mfalme Daudi" (UDB)

**kaposwa**
"rehani" au "kuahidiwa kuolewa." wazazi wa Mariamu waliweka msimamo kwaajili yake atamwoa Yusufu.

**jina la bikra alikuwa Mariamu**
Hii inamtambulisha Mariamu kama mhusika mpya katika simulizi.

**Alikuja kwake**
"Malaika alikuja kwa Mariamu"

**Salaamu**
Hii ilikuwa ni salamu ya kawaida. Inamaana: NI: "furahia" au "uwe na furaha."

**ninyi ambao mnaupedeleo mkubwa**
"ninyi ambao mmepokea neema kubwa!" au "ninyi mmepokea wema maalumu!"

**Bwana yuko pamoja na wewe**
"pamoja nawe" ni nahau ambayo inadokeza kutiwa moyo na kukubalika. NI: "Bwana kafurahishwa na wewe."

**alikuwa na wasiwasi sana ... salamu hii ingekuwa ya aina gani.**
Mariamu alifahamu maana ya maneno hayo, lakini hakuelewa kwanini malaika alimwambia salaamu hii ya kushangaza.

### Luke 1:30

**Usiwe na hofu, Mariamu**
Malaika hakutaka Mariamu kuwa na woga kwa ujio wake, kwasababu Mungu alimtuma ujumbe mzuri.

**umepata wema wa Mungu**
Nahau "kupata fadhila" inamaana kupokelewa vizuri na mtu fulani. Sentensi inaweza kugeuzwa kuonesha Mungu kama mtenda. NI: "Mungu ameamua kutoa neema yake" au "Mungu anaonesha wema wake."

**utakuwa na ujauzito tumboni mwako na kuzaa mwana ... Yesu ... Mwana wa aliye Juu Sana**
Mariamu atazaa "mwana" atakayeitwa "Mtoto wa aliye Juu Sana" (UDB). Yesu ni mtoto aliyezaliwa na mama mwanadamu, na Yeye vilevile ni Mwana wa Mungu. Maneno haya yatafsiriwe kwa uanglifu sana.

**ataitwa**
Maana zinazowezekana ni 1) "watu watamwita" au 2) "Mungu atamwita."

**Mwana wa aliye Juu Sana**
Hii ni sifa mhimu kwa Yesu, Mwana wa Mungu.

**Kupewa kiti cha mhenga wake Daudi**
Kiti kinawakilisha mamlaka ya mfalme kutawala. NI: "kumpa mamlaka kutawala kama mfalme kama baba yake Daudi alivyofanya"

**hapatakuwa na mwisho kwa ufalme wake**
Kauli hasi ""hakuna mwisho" sisitiza kwamba utaendelea milele. Pia inaweza kusemwa kwa kauli chanya. NI: "ufalme wake hautaisha."

### Luke 1:34

**Namna gani hili litatokea**
NI: "Hili linawezekana kwa namna gani?" Ingawa Mariamu hakuelewa jinsi itakavyotokea, yeye hakuwa na shaka kwamba ingelitokea.

**Mimi sijalala pamoja na mwanaume yeyote**
Mariamu alitumia hali halisi kusema kwamba hajawahi kuhusika kwenye tendo la ngono. NI: "Mimi ni bikra" (UDB)

**Roho Mtakatifu atakuja juu yako**
utungaji mimba wa Mariamu ungelianza na ujio wa Roho Mtakatifu kwake.

**atakuja juu**
"kuja ghafla" au "atakutokea"

**nguvu ya aliye Juu Sana**
Ilikuwa ni nguvu ya Mungu ingelikuja zaidi ya kawaida kumsababisha Mariamu kuwa mjamzito hata wakati akiwa bado akabaki bikra. Hakikisha hii haidokezi hali au muungano wa ngono - huu ulikuwa muujiza.

**itakuja juu yako**
"utafunikwa kma kivuli"

**mtakatifu**
"mtoto mtakafu" au "mtoto mchanga mtakatifu"

**atakuwa akiitwa**
Maana zinazowezekana 1)"watu watamwita" au 2) Mungu atamwita

**Hivyo mtakatifu atakayezaliwa ataitwa Mwana wa Mungu**
Ingawaje mama yake Yesu alikuwa mwanadamu, Mungu zaidi ya kawaida alimweka Yesu tumboni mwake. Hivyo basi, Mungu alikuwa Baba yake, na Yesu alikuwa anaitwa "Mwana wa Mungu."

**Mwana wa Mungu**
Hii ni sifa mhimu kwaajili ya Yesu.

## Luke 1:36

**Na anglia**
Huu udhihirisho hapa unasisitiza umhimu wa kauli inayomhusu Elizabeth ambayo inafuata.

**ndugu yako Elizabeth**
Kama unataka kusema uhusiano maalumu, Elizabeth huenda alikuwa shangazi wa Mariamu au shangazi - mkubwa.

**pia anaujauzito wa uzeeni mwake**
"pia anaujauzito, ingawa tayari kazeeka, pia mjamzito na atazaa mtoto." Hakikisha haieleweki kama ingawa wawili Mariamu na Elizabethi walikuwa wazee walipopata ujauzito.

**mwezi wa sita kwake**
"mwezi wa sita wa ujauzito wake"

**Kwaajili**
Kwa sababu" au "Hii inaonesha hivyo"

**hakuna lisilowezekana kwa Mungu**
Kauli yake inamashaka maradufu inaweza kutamkwa kwa kauli chanya. NI: "Hii inaonesha Mungu anaweza kufanya kitu chochote." Ujauzito wa Elizabethi ulithibitisha kwamba Mungu anaweza kufanya lolote - hata kumwezesha Mariamu kuwa mjamzito bila kushiriki na mwanaume.

**Tazama**
Mariamu anatumia udhihirisho huo huo kama malaika kusisitiza jinsi alivyokuwa anajali kuhusu uamzi wake kujikabidhi kwa Bwana.

**Mimi ni mtumishi wa kike wa Bwana**
Chagua udhihirisho ambao unaonesha unyenyekevu na utii kwa Bwana. Yeye alikuwa hajiinui juu ya kuwa mtumishi wa Bwana.

**Acha hii itokee kwangu**
"Acha hii itokee kwangu." Mariamu alikuwa anadhihirisha utayari wake kwa mambo yatakayo tokea kwamba malaika alishamwambia yalikuwa karibu yatokee.

## Luke 1:39

**Sentensi Unganishi**
Mariamu anakwenda kumtembelea ndugu yake Elizabethi ambaye alikuwa anakaribia kumzaa Yohana.

**aliinuka**
Nahau hii inamaanisha hakusimama tu, lakini pia "alikuwa tayari." NI: "alianza kutoka" au "alikuwa tayari"

**nchi ya vilima**
"eneo la vilima" au "sehemu ya milima ya Israeli"

**Alikwenda**
Hii inadokeza kwamba Mariamu alimaliza safari yake kabla ya kwenda nyumbani kwa Zakaria. Hii ingelisesemwa wazi. NI: "Yeye alipofika, alikwenda."

**Sasa ilitokea**
Kauli ilitumika kuonesha tukio jipya katika sehemu ya simulizi hii.

**Katika tumbo lake**
"katika tumbo la Elizabethi"

**karuka**
"sogea ghafla"

## Luke 1:42

**alipaza sauti ... lisema kwa nguvu**
Kauli hizi mbili zinamaanisha kitu kilekile, na zinatumika kusisitiza namna Elizabethi alivyokuwa kasisimka. Zingeliweza kuwekwa katika kauli moja. NI: "liotamka ghafla kwa sauti." (UDB)

**alipaza sauti yake**
Nahau hii inamaanisha "aliongeza kiwango cha sauti yake"

**umebarikiwa kati ya wanawake**
Nahau "kati ta wanawake" inamaana "zaidi kuliko wanawake wengine."

**matunda ya tumbo lako**
Mtoto wa Mariamu analinganishwa na matunda ya mti unaozaa. NI: "mtoto katika tumbo lako" au "mtoto utakayemzaa" (UDB)

**Na kwa nini hii imetokea kwangu kwamba mama wa Bwana wangu aje kwangu?**
Elizabethi alikuwa haulizi apate taarifa. Alikuwa anaonesha jinsi alivyoshangaa na alivyokuwa na furaha kwamba mama wa Bwana amekuja kwake. NI: "Jinsi ilivyokuwa ajabu kwamba mama wa Bwana amekuja kwangu!"

**mama wa Bwana**
Hii inarejea kwa Mariamu. "wewe, mama wa Bwana wangu." (UDB)

**Tazama**
Kauli hii inatuamsha tusikilize kushangaa kwa kauli ya Elizabethi inayofuata.

**aliruka kwa furaha**
"lisogea ghafla kwa furaha" au "ligeuka kwa haraka kwa sababu alikuwa na furaha!"

**ilikuja masikioni mwangu**
Hii nahau inamaana "nilisikia."

**"amebarikiwa yeye ambaye kaamini**
"ninyi mlio amini mmebarikiwa" au "kwa sababu mliamini, mtakuwa na furaha"

**pale pangekuwa na utimilifu wa mambo**
"mambo haya yangelitokea kweli" au "mambo haya yangelikuwa kweli"

**mambo ambayo yalisemwa kutoka kwa Bwana kwake**
Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji. " ujumbe ambao Bwana amempa" au "mambo yale uliyo ambiwa na Bwana"

## Luke 1:46

**Maelezo kwa ujumla:**
Mariamu anaanza wimbo wa kumsifu Bwana Mwokozi wake.

**Nafsi yangu inasifu ... roho yangu inashangilia**
Mariamu anatumia mtindo wa ushairi pale anaposema mambo yale yale katika njia mbili mhimu. ikiwezekana tafsri haya katika tofauti ndogo ya maneno au kauli ambayo inamaana inayofanana.

**Nafsi yangu ... roho yangu**
Yote "nafsi" na "roho" ... hurejea kwenye viungo vya kiroho vya mtu. Mariamu anasema kwamba ibada yake inatokea kwenye mtima wake wa ndani. NI: "utu wangu wa ndani ... moyo wangu" au "Mimi ... Mimi."

**imefurahi ndani**
"amehisi kufurahi sana" au "alikuwa na furaha sana"

**Mungu Mwokozi wangu**
"Mungu, ambaye ndiye aniokoaye mimi" au "Mungu ananiokoaye mimi"

## Luke 1:48

**Kwa yeye**
"Kwa sababu yeye"

**alitazama pale**
"alitazama pale kwa makini" au "alijali"

**hali ya chini**
"umaskini." Familia ya Mariamu ilikuwa siyo tajiri.

**Angalia**
Kauli hii inatoa wito kwa kauli inayofuata.

**tokea sasa na kuendelea**
"sasa na badaye"

**vizazi vyote**
"watu wote katika vizazi vyote"

**yeye ambaye anauweza**
"Mungu, mwenye nguvu" (UDB)

**jina lake**
Hapa "jina" hurejea kwenye hali yote ya Mungu. NI: "Yeye."

## Luke 1:50

**Rehema Yake**
"rehema ya Mungu"

**tokea kizazi kwenda kizazi**
"kutoka kizazi kimoja kwenda kizazi kinachofuata" au "kupitia kila kizazi" au "kwa watu wa kila majira"

**alionesha nguvu kwa mkono wake**
"mkono wake" ni lugha picha inayorejea mkono wa nguvu wa Mungu. NI: inaonesha kwamba Yeye ananguvu sana."

**tawanyika**
"fukuza katika uelekeo mbalimbali"

**mawazo ya mioyo yao**
"moyo" ni nahau ambayo inarejea kwenye mawazo ya mtu ya ndani. NI: "mawazo katika utu wao wa ndani."

### Luke 1:52

**amewashusha chini wafalme kutoka kwenye enzi zao**
Enzi ni kiti ambacho mtawala anakalia, na ni mfano wa mamlaka. Kama mfalme akiondolewa kwenye enzi yake, inamaanisha hana mamlaka tena ya kutawala. NI: "Yeye amechukua mamlaka ya wafalme au "watawala kuacha kutawala."

**amewashusha chini wafalme ... amewainua juu wenye hali ya chini**
Kupingana kati ya hali hizi mbili iwekwe wazi katika tafsiri kama inawezekana.

**hali ya chini**
"umaskini." Familia ya Mariamu walikuwa siyo tajiri. Angalia livyotafsriwa 1:48.

**amewainua ambao wana hali ya chini**
Katika neno picha hili, watu ambao ni wa mhimu wako juu zaidi ya wale ambao si mhimu. NI: "amefanya watu wanyenyekevu kuwa wa mhimu" au "amewapa heshima ambao watu wengine hawakuwaheshimu."

**amewalisha wenye njaa ... matajiri wameondoka bila kitu**
Kutofautisha kati ya matendo wawili yaliyo kinyume itengenezwe tafsiri iliyowazi kama inawezekana.

**kashibisha wenye njaa na chakula kizuri**
Maana zinazowezekana ni 1) "amewapa wenye njaa chukula kizuri wale" au 2) "kawapa wahitaji vitu vizuri,"

### Luke 1:54

**Maelezo kwa ujumla**
UDB inarekebisha mistari hii kuwa daraja ili kutunza kwa pamoja taarifa zinazohusu Israeli.

**ametoa msaada kwa**
"Bwana amesaidia"

**Israeli mtumishi wangu**
Kama wasomaji watachanganya hiki na mtu anayeitwa Israeli, itatafsiriwa kama "mtumishi wake, taifa la Israeli" au "Israeli, mtumishi wake."

**Hivyo kama vile**
"ili kwamba"

**kukumbuka**
Mungu hawezi kusahau. Ambapo Mungu "hukumbuka," hii nahau inayomaanisha Mungu anatenda kutokana na ahadi yake aliyotoa mapema.

**kama alivyosema kwa baba zetu**
"hakika kama alivyoahidi kwa wahenga wetu angelifanya." "Kauli hii inaleta taarifa ya nyuma ahadi ya Mungu kwa Abrahamu." NI: "kwa sababu aliahidi kwa wahenga wetu angelikuwa na rehema."

**uzao wake**
"wazawa wa Abrahamu"

### Luke 1:56

**Kauli Unganisha**
Elizabethi anajifungua mtoto wake na Zakaria anamwita jina mtoto wao.

**alirudi nyumbani kwake**
"Mariamu alirudi nyumbani kwake" au "Mariamu alirudi kwenye nyumba yake"

**Sasa**
Neno hili linaonesha mwanzo wa tukio linalofuata katika historia.

**Jirani zake na ndugu zake**
"majirani na ndugu wa Elizabethi"

**alizidisha rehema yake kwaajili yake**
""amekuwa mwema sana kwake" UDB

### Luke 1:59

**Sasa ilitokea katika hiyo siku ya nane**
"Sasa wakati mtoto akiwa na siku nane" au NI: "Ndipo, siku ya nane baada ya mtoto kuzaliwa"

**wao**
Hii huenda wanarejea kwa Zakaria na rafiki na ndugu wa Elizabethi.

**kumtahiri mtoto**
Hii ilikuwa sherehe ya kawaida wakati mtu alipokuwa anamtahiri mtoto rafiki zake wapaswa kuwa hapo kusherehekea pamoja na hiyo Familiya. NI: "sherehe kwaajili ya kutahiriwa kwa mtoto."

**Wangeliweza kumwita yeye**
"Walikuwa wanaenda kumwita yeye" au "Walitaka kumwita yeye jina." Hii ilikuwa desturi ya kawaida.

**kama jina la baba yake**
"jina la baba yake"

**kwa jina hili**
"kwa jina hilo" au "kwa jina lilelile"

### Luke 1:62

**Wao**
Hii inarejea kwa watu ambao walikuwa pale kwaajili ya sherehe ya kutahiriwa.

**alifanya ishara**
"alitaja." Pengine Zakaria alikuwa hawezi kusikia, vilevile kuzungumza, au watu walikisia kwamba hangeliweza kusikia.

**kwa baba yake**
"kwa baba wa mtoto"

**jinsi alivyotaka awe anaitwa**
"jina ambalo Zakaria alitaka kumpa mtoto"

**Baba yake aliomba ubao wa kuandikia**
Inaweza ikasaidia kusema jinsi Zakaria "alivyoomba," Sababu hakuweza kuzungumza. NI: "Baba yake alitumia mikono kuwaonesha watu kwamba alihitaji wampe ubao wa kuandikia"

**ubao wa kuandikia**
"kitu fulani unachoweza kuandika"

**alistaajabishwa**
"shangaa sana" au "stajaabishwa"

## Luke 1:64

**kinywa chake kilifunguliwa ... ulimi wake uliwekwa huru**
Hizi kauli mbili ni maneno picha ambayo pamoja yanasisitiza kwamba Zakaria aliweza kuzungumza ghafla.

**kinywa chake kilifunguliwa na ulimi wake uliwekwa huru**
Kauli hizi zinaweza pia kusemwa katika mtindo wa kutenda. NI: Mungu akafungua kinywa chake na kuuweka huru ulimi."

**Hofu ikawajia wote ambao waliishi karibu nao**
"Wote walioishi karibu na Zakaria na Elizabethi walikuwa na hofu." Walikuwa wamepigwa butwaa kwa njia ya Mungu ya miujiza kumrejeshea Zakaria uwezo wa kuzungumza. NI: "Kila mmoja aliyeishi karibu nao walikuwa katika hofu ya Mungu."

**wote ambao waliishi**
Hii hairejei tu kwa wale majirani wa karibu lakini kwa kila mmoja ambaye aliishi eneo hilo.

**wote waliowasikia wao**
Neno "wao" hapa linarejea kwenye mambo yaliokwisha tokea.

**wote waliosikia**
Hii inarejea kwenye kundi kubwa la watu walioishi Uyahudi yote.

**kusema**
"kuuliza"

**Mtoto huyu atakuja kuwa kuwa nani?**
"Aina gani ya ukuu ambao atakuwa nao mtoto huyu akikua?" Hii pia inawezeakana kwamba swali hili lilikuwa linamaanisha kuwa ni kauli ya kuwashangaza kwa kile walichisikia kuhusu mtoto. NI: "Mtoto huyu atakuwa mkuu wa namna gani!"

**mkono wa Bwana ulikuwa pamoja naye**
Kauli hii "mkono wa Bwana" inarejea nguvu za Mungu. "Nguvu za Mungu zilikuwa pamoja naye" au "Mungu alikuwa anafanya kazi ndani yake kwa nguvu."

## Luke 1:67

**Kauli Unganisha:**
Zakaria anasema kilichotokea kwa Yohana mtoto wake.

**Zakaria Baba yake alikuwa kajazwa na Roho Mtakatifu**
Hii inaweza kusemwa kwenye mtindo wa kutendea. NI: "Roho Mtakatifu alimjaza Zakaria baba yake."

**Baba yake**
baba wa Yohana

**alitoa unabii, akisema**
fikiria njia za asili za kuanza kunukuu moja kwa moja katika lugha yako. NI: "alitoa unabii na alisema" au "alitoa unabii na hiki ndicho alichokisema"

**Mungu wa Israeli**
"Israeli" hapa anarejea kwa taifa la Israeli. Uhusiano kati ya Mingu na Israeliungelisemwa moja kwa moja. NI: "Mungu ambaye anatawala juu ya Israeli" au "Mungu ambaye Israeli anamwabudu."

**watu wake**
"watu wa Mungu"

## Luke 1:69

**pembe ya wokovu kwaajili yetu**
pembe ya mnyama ni mfano kwaajili ya nguvu zake kujitetea yenyewe. Maana hii isemwe wazi. NI: "mtu fulani mwenye nguvu kutuokoa sisi."

**ndani ya nyumba ya mtumishi wake Daudi**
"Nyumba" ya Daudi inawasilisha familia yake, hasa, ukoo wake, NI: "katika familia ya mtumishi wake Daudi" au "ambaye ni ukoo wa mtumishi wake Daudi"

**kama alivyosema**
"kama tu Mungu alivyosema"

**alisema kwa kinywa cha manabii wake watakatifu**
Mungu aliwawezesha manabii kuzungumza neno alilotaka wao wazungumze. udhibiti wa Mungu unaweza kusemwa NI: "alisababisha manabii wake watakatifu kusema."

**kwa mdomo wa**
Hii inazungumzia ujumbe wa manabii kama ilikuwa midomo inasema maneno NI: "kwenye maneno ya"

**walikuwapo katika ulimwengu wa kale**
"waliishi zamani"

**kuleta wokovu**
Hii inarejea kwenye wokovu wa mwili, zaidi kuliko wokovu wa kiroho.

**adui zetu ... wote wanaotuchukia**
Hizi kauli mbili kimsingi zinamaanisha jambo lilelile na zimerudiwa kusisitiza jinsi adui zao walivyokuwa na nguvu kinyume chao.

**kutoka katika mkononi mwa**
Itakuwa ni msaada kusema tena "wokovu" hapa. NI: "wokovu kutokana na mkono wa."

**mkono**
"nguvu" au "udhibiti." Neno "mkono" linakwenda pamoja na nguvu ambazo zinatumika kuwaumiza watu wa Mungu

### Luke 1:72

**kuonesha rehema**
"kuwa na huruma kwa" au "kutenda kutokana na rehema yake kwao"

**kumbuka**
Hapa neno "kumbuka" linamaana kuendelea kujitoa au kukamilisha kitu fulani.

**agano lake takatifu ... kiapo ambacho alikisema**
Kauli hizi mbili zinarejea kwenye kitu kile kile. Zimerudiwa kuonesha kujali kwa Mungu juu ya ahadi kwa Abrahamu.

**kutoa idhini kwetu**
"kufanya iwezekane kwaajili yetu"

**kwamba sisi, tumekombolewa ... tumtumikie yeye bila hofu**
Inaweza ikasaidia kubadili mtindo wa kauli hizi. NI: "kwmba tungelimtumikia yeye bila bila hofu baada sisi kuokolewa kutoka katika nguvu za adui wetu."

**kutoka katika mkono wa adui zetu**
"mkono" inarejea kudhibiti au nguvu ya mtu. Hii inaweza kusemwa wazi. NI: "kutoka katika udhibiti wa adui zetu."

**bila hofu**
Hii inarejerea nyuma kwenye hofu ya adui zao. NI: "bila kuwaogopa adui zetu"

**katika utakatifu na haki**
Hizi zinaweza kudhihirishwa kama matendo. NI: "kuishi katika njia safi na kutenda haki"

**mbele yake**
Nahau hii ambayo inamaanisha "katika uwepo wake"

### Luke 1:76

**ndiyo, na wewe**
Zakaria anatumia kauli hii kuanza hotuba yake moja kwa moja kwa mtoto wake. Unaweza kuwa na njia ile ile ya kuhutubia moja kwa moja katika lugha yako.

**huyu, mtoto, ataitwa nabii**
Watu watatambua kwamba huyu ni nabii. Hii inaweza ikasemwa katika mtindo wa kutendea. NI: "watu watajua kwamba wewe ni nabii."

**wa aliye Juu Sana**
"ambaye anamtumikia aliye Juu Sana." Hii inarejea kwa Mungu. NI: "ambaye anazungumza kwaajili ya Mungu aliye Juu Sana."

**kwenda mbele za uso wa Bwana**
Nahau hii inamaana "kwenda mbele za Bwana" au "kuja mbele za Bwana."

**kuwapa maarifa ya wokovu watu wake**
"kuelezea wokovu kwa watu wake" au "hivyo watu wake waweze kufahamu wokovu"

**kwa msamaha wa dhambi zao**
"kupitia msamaha wa dhambi zao." Pia inaweza kusemwa katika mtindo wa kutendea. NI: "kwa sababu Mungu amewasamehe"

### Luke 1:78

**Maelezo kwa ujumla**
Kupitia katika mistari hii : "sisi" inahusisha watu wote.

**kwa sababu kawaida ya huruma iliyotolewa na Mungu wetu**
Hii inaweza kusaidia kusema kwamba rehema ya Mungu inatusaidia sisi. NI: "kwa sababu Mungu anahuruma na na rehema kwetu."

**jua linachomoza kutoka juu ... kuchomoza juu**
Mwanga kwa kawaida ni sitiari kwa ukweli. Hapa, jinsi jua linavyochomoza mwanga wake juu ya nchi ilitumika kama mfano wa jinsi mwokozi anavyotoa ukweli wa kiroho kwa watu.

**angaza juu**
"toa maarifa kwa" au "toa mwanga wa kiroho kwa"

**wao wanaokaa gizani**
Giza hapa ni sitiari kwa watu wasio na kweli. Hapa, watu ambao wanapungukiwa ukweli wa kiroho wanasemwa kama kwamba wanakaa gizani. NI: "watu wasiojua kufanya kweli"

**giza... kivuli cha kifo**
kauli hizi mbili zinafanya kazi pamoja kusisitiza giza nene la kiroho kwa watu Mungu huwaonesha rehema kwao.

**katika kivuli cha mauti**
kivuli ni sitiari kwa kitu fulani ambacho kinakabili. Hapa, inarejea kwenye giza la kiroho ambalo litawasababisha kufa. NI: "ambao wanakaribia kufa."

**ongoza miguu yetu**
Kuongoza mtu kutembe ni sitiari ya kuongoza ufahamu wa kiroho. NI: "tuongoze" au "Tufundushe."

**miguu yetu**
"miguu" inatumika kuwakilisha mtu kwa ujumla. NI: "sisi"

**katika njia ya amani**
"njia ya amani" ni sitiari kwaajili ya njia inayomsababisha mtu kuwa na amani na Mungu. NI: "kuishi maisha ya amani" au "kutembea katika njia ambayo inatuongoza kwenye amani."

### Luke 1:80

**Maelezo kwa ujumla:**
Hii inatuambia kwa kifupi kuhusu miaka ya Yohana kuongezeka.

**Sasa**
Neno hili linatumika hapa kuonesha kituo kwenye mfululizo wa habari kuu. Luka anahama kwa haraka kutoka kuzaliwa kwa Yohana kwenda kwenye huduma yake.

**kuwa na nguvu katika roho**
"kukomaa kiroho" au "kuimarisha uhusiano na Mungu"

**alikuwa katika mwitu**
"aliishi katika mwitu." Luka hasemi katika umri gani Yohana alianza kuishi mwituni.

**mpaka**
Hii siyo lazima kuonesha hoja ya kumalizia. Yohana anaendelea kuishi katika pori hata baada ya kuanza kuhubiri hadharani.

**siku ya kujitokeza kwake**
"alipoanza kuhubiri hadharani"

**siku**
Hii ilitumika hapa katika dhana ya jumla ya "wakati" au "fursa"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 2

1 Sasa katika siku hizo, ikatokea kwamba Kaisari Agusto alitoa agizo akielekeza kwamba ichukuliwe sensa
ya watu wote wanaoishi duniani. 2 Hii ilikuwa ni sensa ya kwanza iliyofanyika wakati Krenio akiwa gavana
wa Siria. 3 Hivyo kila mmoja akaenda mjini kwake kuandikishwa sensa. 4 Naye Yusufu aliondoka pia
katika mji wa Nazareti huko Galilaya na akasafiri Yudea katika mji wa Bethlehemu, ujulikanao kama mji
wa Daudi, kwa sababu alitokea katika ukoo ya Daudi. 5 Alikwenda huko kujiandikisha pamoja na
Mariamu, ambaye alikuwa amemposa na alikuwa akitazamia mtoto. 6 Sasa ilitokea kwamba, wakiwa kule
wakati wake wa kujifungua mtoto ukawadia. 7 Akajifungua mtoto wa kiume, mzaliwa wake wa kwanza,
akamzungushia nguo mwilini kumkinga na baridi mtoto. Ndipo akamweka kwenye kihori cha kulishia
wanyama, kwa sababu haikuwepo nafasi kwenye nyumba za wageni. 8 Katika eneo hilo, walikuwapo
wachungaji walioishi mashambani wakilinda makundi ya Kondoo wao usiku. 9 Ghafla, malaika wa Bwana
akawatokea, na utukufu wa Bwana ukang'aa kuwazunguka, na wakawa na hofu sana. 10 Ndipo malaika
akwaambia, "Msiogope, kwasababu nawaletea habari njema ambayo italeta furaha kuu kwa watu wote. 11
Leo Mwokozi kazaliwa kwaajili yenu mjini mwa Daudi! Yeye ndiye Kristo Bwana! 12 Hii ndiyo ishara
ambayo mtapewa, mtamkuta mtoto amefungwa nguo na amelala kwenye hori la kulishia wanyama." 13
Ghafla kukawa na jeshi kubwa la mbinguni likaungana na malaika huyo wakamsifu Mungu, wakisema, 14
"Utukufu kwa Mungu aliye juu sana, na amani iwe duniani kwa wote ambao anapendezwa nao." 15 Ikawa
kwamba malaika walipokwisha kuondoka kwenda mbinguni, wachungaji wakasemezena wao kwa wao, "
Twendeni sasa kule Bethlehemu, na tukaone hiki kitu ambacho kimetokea, ambacho Bwana
ametufahamisha." 16 Wakaharakisha kule, na wakamkuta Mariamu na Yusufu, na wakamuona mtoto
amelala kwenye hori la kulishia wanyama. 17 Na walipoona hivi, wakawajulisha watu kile walichokuwa
wameambiwa kumhusu mtoto. 18 Wote waliosikia habari hii wakashangazwa na kile kilichosemwa na
wachungaji. 19 Lakini Mariamu akaendelea kufikiri kuhusu yote aliyokwisha kuyasikia, akiyatunza moyoni
mwake. 20 Wachungaji wakarudi wakimtukuza na kumsifu Mungu kwa ajili ya kila kitu walichokwisha
sikia na kuona, kama tu ilivyokuwa imenenwa kwao. 21 Ilipofika siku ya nane na ilikuwa ni wakati wa
kumtahiri mtoto, wakamwita jina Yesu, jina alilokwishapewa na yule malaika kabla mimba haijatungwa
tumboni. 22 zao zilizotakiwa za utakaso zilipopita, kulingana na sheria ya Musa, Yusufu na Mariamu
wakampeleka hekaluni kule Yerusalemu kumweka mbele za Bwana. 23 Kama ilivyoandikwa katika sheria
ya Bwana, "Kila mwanaume anayefungua tumbo ataitwa aliyetolewa wakfu kwa Bwana." 24 Wao vilevile
walikuja kutoa sadaka kulingana na kile kinachosemwa katika sheria ya Bwana, "Jozi ya njiwa au makinda
mawili ya njiwa." 25 Tazama, palikuwa na mtu katika Yerusalemu ambaye jina lake alikuwa akiitwa
Simeoni. mtu huyu alikuwa mwenye haki na mcha Mungu. Yeye alikuwa akisubiri kwa ajili ya mfariji wa
Israeli, na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake. 26 Ilikuwa imekwisha funuliwa kwake kupitia Roho Mtakatifu
kwamba yeye hangelikufa kabla ya kuwomwona Kristo wa Bwana. 27 Siku moja alikuja ndani ya hekalu,
akiongozwa na Roho Mtakatifu. Ambapo wazazi walimleta mtoto, Yesu, kumfanyia yale yaliyopasa
kawaida ya sheria, 28 ndipo Simeoni alimpokea mikononi mwake, na akamsifu Mungu na kusema, 29
"Sasa ruhusu mtumishi wako aende kwa amani Bwana, kulingana na Neno lako. 30 Kwa kuwa macho
yangu yameuona wakovu wako, 31 ambao umeonekana kwa macho ya watu wote. 32 Yeye ni nuru kwa ajili
ya ufunuo kwa Wamataifa na utukufu wa watu Israeli." 33 Baba na Mama wa mtoto walishangazwa kwa
mambo ambayo yalizungumzwa juu yake. 34 Ndipo Simeoni akawabariki na akasema kwa Mariamu mama
yake, "Sikiliza kwa makini! Mtoto huyu atakuwa sababu ya kupotea na kuokoka kwa watu wengi katika
Israeli na ni ishara ambayo watu wengi wataipinga. 35 Pia ni upanga utakaochoma nafsi yako mwenyewe,
ili kwamba mawazo ya mioyo ya wengi yadhihirike". 36 Nabii mwanamke aliyeitwa Ana pia alikuwako
hekaluni. Yeye alikuwa binti wa Fanueli kutoka kabila la Asheri. Alikuwa na miaka mingi sana. Naye aliishi
na mume wake kwa miaka saba baada ya kuoana, 37 na ndipo akawa mjane kwa miaka themanini na
minne. Naye hakuwahi kuondoka hekaluni na alikuwa akiendelea kumwabudu Mungu pamoja na kufunga
na kuomba, usiku na mchana. 38 Na kwa wakati huo, alikuja pale walipo akaanza kumshukuru Mungu.
Aliongea kumhusu mtoto kwa kila mtu ambaye alikuwa akisubiri ukombozi wa Yerusalemu. 39
Walipomaliza kila kitu walichotakiwa kufanya kuligana na na sheria ya Bwana, walirudi Galilaya, mjini
kwao, Nazareti. 40 Mtoto alikua, na akawa na nguvu, akiongezeka katika hekima, na neema ya Mungu
ilikuwa juu yake. 41 Wazazi wake kila mwaka walikwenda Yerusalemu kwaajili ya sikukuu ya Pasaka. 42
Alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili, walikwenda tena wakati mwafaka kidesturi kwa ajili ya
sikukuu. 43 Baada ya kubaki siku zote kwa ajili ya sikukuu, walianza kurudi nyumbani. Lakini mvulana
Yesu alibaki nyuma mle Yerusalemu na wazazi wake hawakujua hili. 44 Walidhani kwamba yumo kwenye
kundi walilokuwa wakisafiri nalo, hivyo walisafiri safari ya siku. Ndipo wakaanza kumtafuta miongoni wa

ndugu na marafiki zao. 45 Waliposhindwa kumpata, walirudi Yerusalemu na wakaanza kumtafuta humo. 46
Ikatokea kwamba baada ya siku tatu, wakampata hekaluni, akiwa ameketi katikati ya waalimu,
akiwasikiliza na kuwauliza maswali. 47 Wote waliomsikia walishangazwa na ufahamu wake na majibu
yake. 48 Walipomwona, walistaajabu. Mama yake akamwambia, "Mwanangu, kwa nini umetutendea hivi?
Sikiliza, baba yako na mimi tumekuwa tukikutafuta kwa wasiwasi mkubwa." 49 Akawaambia, "Kwa nini
mmekuwa mkinitafuta? Hamkujua kwamba lazima niwe kwenye nyumba ya Baba yangu? 50 Lakini
hawakuelewa nini alichomaanisha kwa maneno hayo. 51 Ndipo akaenda pamoja nao mpaka nyumbani
Nazareti na alikuwa mtii kwao. Mama yake alihifadhi mambo yote moyoni mwake. 52 Lakini Yesu
aliendelea kukua katika hekima na kimo, na akazidi kupendwa na Mungu na watu.

---

## Luka 02 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

Baadhi ya tafsiri hupendelea kuweka sala ndefu au unabii mbele kidogo ya maandiko nyingine. Kwa sababu hii, ULB na tafsiri nyingine nyingi za Kiingereza huingiza mistari ya 2:14, 29-32.

### "Dhana maalum katika sura hii"

### Hakukuwa na nafasi kwao

Maelezo ya Luka kuhusu kuzaliwa kwa Kristo hauna maelezo mengi kama vile injili nyingine. Huenda Luka hakufikiri kama maelezo haya yalikuwa muhimu, labda kwa sababu ya habari za kuzaliwa katika injili nyingine.

---

### Luke 2:1

**Maelezo kwa ujumla**
Hii inatoa maelezo ya nyuma kuonesha kwanini Mariamu na Yusufu wanatakiwa kuondoka kwaajili ya kuzaliwa kwa Yesu.

**Sasa**
Neno hili ni alama ya kuanza kwa sehemu mpya ya simulizi.

**ikaja ikawa kwamba**
Kauli hii ilitumika kuonesha kwamba huu ni mwanzo wa wajibu. Kama lugha yako inayo njia ya kuonesha kuanza kwa kuwajibika, unaweza ukatumia hiyo. Baadhi ya tafsiri haziweki kauli hii.

**Kaisari Agusto**
"Mfalme Agusto" au "Mtawala Agusto." Agusto alikuwa mtawala wa kwanza wa dola ya Rumi.

**alitoa agizo likielekeza**
Amri hii huenda ilinabebwa na wajumbe kupitia katika dola. NI: "wajumbe waliotumwa maelekezo ya amri"

**kwamba ichukuliwe sensa ya watu wote wanaoishi katika ulimwengu**
Hii inaweza kusemwa katika mtindo wa kutendea. NI: "kwamba waorodheshe watu wote wanaoishi katika ulimwengu wa kirumi" au "wahesabu watu wote katika ulimwengu wa kirumi na waandike majina yao."

**ulimwengu**
eneo la dunia lililotawaliwa na serikali ya Rumi au "nchi zilizoongozwa na dola ya Kirumi"

**Krenio**
Krenio aliteuliwa kuwa mtawala wa Siria/Shamu

**kila mmoja alikwenda**
"kila mmoja aliondoka" au "kila mmoja alikuwa anakwenda"

**mji wa kwao**
Inaweza ikasaidia kusema kwamba "ya kwake" hairejei kwenye mji ambao alikuwa akiishi. NI: "ni mji ambao wahenga wake waliishi."

**kuandikishwa kwaajili ya sensa**
"kuwa na majina yameandikwa kwenye orodha" au "kuwekwa kwenye idadi kiofisi"

### Luke 2:4

**Maelezo kwa ujumla**
UDB inaweka sawa hii mistari miwili kuwa daraja ambalo litatengeneza urahisi wa kufupisha sentensi.

**pia Yusufu**
Hii inamtambulisha Yusufu kama mhusika mpya katika simulizi.

**kwenye mji wa Daudi**
Taarifa hizi zilizotangulia kuhusu umhimu wa wa Bethlehemu. Ingawa ulikuwa mji mdogo, Mfalme

Daudi alizaliwa pale, na ulikuwapo unabii kwamba masihi atazaliwa pale. NI: ambao ulikuwa unaitwa mji wa Daudi"

**kwa sababu alikuwa wa nyumba na familia ya Daudi**
"kwa sababu Yusufu alikuwa wa uzao wa Daudi"

**Kuandikisha**
Hii inamaanisha kutaarifu kwa afisa kule hivyo wamhusishe naye kwenye wajibu. Tumia kauli kwaajili ya afisa mwandikishaji wa serikali ikiwezekana.

**pamoja na Mariamu**
Mariamu alisafiri pamoja na Yusufu kutoka Nazarethi. Ni wazi kwamba wanawake pia walihitajika, hivyo Mariamu angelihitaji kusafiri na kuandikishwa vile vile.

**ambaye alikuwa kaposwa naye**
"mchumba wake" au "aliyekuwa ameahidi kwake." Wachumba walihesabiwa kisheria wameoana, lakini pale isingelikuwa kukaribiana kimwili kati yao.

### Luke 2:6

**Kauli Unganishi:**
Hii inatuambia kuzaliwa kwa Yesu kwa tangazo la malaika kwa wachungaji.

**Maelekezo kwa ujumla:**
UDB inapanga upya mistari hii katika mstari daraja ili kutunza pamoja undani kuhusu mahali walipokaa.

**Sasa ikaja kwamba**
Kauli hii inaweka alama ya kuanza kwa tukio linalofuata katika simulizi.

**wakati wakiwa pale**
"wakati Mariamu na Yusufu walikuwa Bethlehemu"

**wakati ukawadia wa kuzaa mtoto**
"ilikuwa ni muda wa kujifungua mtoto wake"

**alimsetiri kwa nguo nadhifu**
Hii ilikuwa ni njia ya kawaida kwa akinamama kukinga na kutunza watoto wao kiutamaduni. ungesema hii wazi: NI: "akasetiri joto kwa kumfunga blanketi vizuri" au "akamfunga kumsetiri kwa blanketi."

**alimlaza katika kihori**
Hiki kilikuwa aina ya kiboksi au chombo ambacho watu waliweka nyasi kavu au chakula kingine ndani yake kwaajili ya chakula cha wanyama. kilikuwa safi sana na kilikuwa laini na kavu kama nyasi kavu ndani kama sponji kwa mtoto. Wanyama kawaida walitunzwa karibu na nymbani kuwalinda kiusalama na kuwalisha kwa urahisi. Ni dhahiri Mariamu na Yusufu walibaki kwenye eneo ambalo lilitumika kwaajili ya wanyama.

**hapakuwa na nafasi kwaajili yao katika nyumba za wageni**
"hapakuwa na mahali kwaajili yao kwenye vyumba vya wageni." Hii huenda ilikuwa kwa sababu ya watu wengi walikwenda Bethlehemu kujiandikisha. Luka anaongeza kama taarifa ya iliyokwishakutolewa.

### Luke 2:8

**Malaika wa Bwana**
""malaika kutoka kwa Bwana" au "malaika anayemtumikia Bwana"

**aliwatokea**
"akaja kwa wachungaji"

**utukufu wa Bwana**
chanzo cha mwanga mweupe ulikuwa ni utukufu wa Bwana, ambao uliwatokea kwa wakati ule ule kama malaika.

### Luke 2:10

**usiwe na hofu**
"koma kuwa na hofu"

**kwamba zitaleta furaha kwa watu wote**
"kwama zitawafanya wote kufurahi sana"

**watu wote**
Baadhi wanafahamu hii kurejea kwa Wayahudi. Wengine wanaelewa inarejea kwa watu wote.

**mji wa Daudi**
Hii inamaanisha Bethlehemu

**Hii ni ishara itakayotolewa kwenu**
Hii inaweza kusemwa kwenye mtindo tendea. NI: "Mungu atawapa ishara hii" au "mtaona ishara hii inayotoka kwa Mungu."

**ishara**
""uthibitisho." Hii pengine inaweza kuwa ishara kuthibitisha kwamba kile ambacho malaika alikuwa anasema ni kweli, au inaweza kuwa ishara ambayo ingelisaidia wachungaji kumtambua mtoto.

**atasetiriwa katika nguo nadhifu**
Hii ilikuwa njia ya kawaida kwamba mama alimlinda na kutunza watoto wao katika utamaduni huo. NI: "alisetiriwa vema katika blanketi itunzayo joto" au "alifungwa kwaufanisi kwenye blanketi." Angalia jinsi ilivyotafsiriwa 2:2.

**Kalala katika kihori cha kulishia**
Hiki kilikuwa kiboksi au kitu ambabacho watu waliweka humo majani au chakula kwaajili ya kula ng'ombe. Angalia jinsi ilivyotafsiriwa katika 2:6.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

### Luke 2:13

**idadi kubwa, ya jeshi la mbinguni**
Neno "jeshi la mbinguni" hapa itarerejea kwenye jeshi halisi la malaika, au inawezakuwa sitiari kwaajili kikundi cha malaika kilicho andaliwa. NI: "kundi kubwa la malaika kutoka mbinguni." (UDB)

**kumsifu Mungu**
"kumpa sifa Mungu"

**Utukufu kwa Mungu juu sana**
Maana zinazowezekana ni 1) "Toa heshima kwa Mungu aliye mahali pa juu sana" au 2) "Toa heshima ya juu sana kwa Mungu."

**hapa duniani iweze kuwa amani kati ya watu ambao ameridhishwa nao**
"wale watu ambao wako duniani ambao Mungu ameridhishwa nao basi wawe na amani"

### Luke 2:15

**Ikawa**
kauli hii ilitumika kuonesha kubadili kwa masimulizi kwenda kwenye ambacho wachungaji walifanya baada ya malaika kuondoka.

**kutoka kwao**
"kutoka kwa wachungaji"

**Baina ya mtu na mtu**
"kwa mmoja na mwingine"

**ngoja nasi ... kwetu**
Tangu wachungaji walikuwa wanazungumza mmoja na mwingine, lugha ambayo inamtindo wa kuhusisha kwa "sisi" na "nasi" tumia mtindo wa kuhusisha hapa.

**ngoja nasi**
"nasi tuta"

**jambo hili ambalo limetokea**
Hii inarejea kuzaliwa kwa mtoto, na siyo kuonekana kwa malaika.

**kalala katika kihori cha kulishia**
Hii ilikuwa aina fulani ya boksi au kitu ambacho watu waliweka nyasi kavu au chakula kwaajili ya wanyama kula. Angalia jinsi ilivyotafsiriwa katika 2:6.

### Luke 2:17

**ambacho kilikuwa kimesemwa kwao na wachungaji**
Hii inaweza ikasemwa kwenye mtindo wa kutendea. NI: ""kile ambacho malaika waliwaambia wao wachungaji."

**mtoto huyu**
"mtoto"

**kile ambacho kilizungumza kwao na wachungaji**
Hii inaweza kusemwa katika mtindo wa kutendea. NI: "ambacho wachungaji waliwaambia."

**kuyatunza moyoni mwake**
hazina ni kitu fulani ambacho ni cha thamani sana na kizuri. Mariamu alifikiri mambo aliyoambiwa kuhusu mtoto wake kuwa ni mazuri sana. NI: "kuyakumbuka kwa makini" au "kuyakumbuka kwa furaha."

**walirudi**
"wakarudi mashambani kwenye kondoo"

**kumtukuza na kumsifu Mungu**
haya yanafanana na yanasisitiza jinsi walivyochangamka kuhusu kile ambacho Mungu kafanya. NI: "sema juu ya kusifu ukuu wa Mungu."

### Luke 2:21

**Maelezo kwa ujumla:**
Sheria Mungu aliyowapa Wayahudi waamini aliwaambia lini mtoto mvulana atahiriwe na sadaka ipi wazazi walete.

**ilipokuwa mwishoni mwa siku ya nane**
kauli hii inaonesha muda ukapita kabla ya tukio jipya.

**mwishoni mwa siku ya nane**
"ilikuwa siku nane baadaya kuzaliwa kwake" au "alikuwa na umri wa siku nane"

**aliitwa**
Yusufu na Mariamu walimwita jina lake.

**jina alilokwishakuwa amepewa na malaika**
Hii inaweza kusemwa katika mtindo wa kutendea. NI: "jina ambalo malaika alimwita."

### Luke 2:22

**wakati hesabu iliyotakiwa ... ilishapita**
Hii inaonesha kupita kwa muda kabla ya tukio jipya.

**hesabu iliyotakiwa ya siku**
Hii inaweza kusemwa kwenye mtindo wa tendea. NI: "hesabu ya siku ambazo Mungu alitaka."

**kwaajili ya kujitakasa kwao**
"kwaajili ya wao kuwa safi kiutaratibu." Pia unaweza kuisema nafasi ya Mungu. "Mungu kutaka wao wawe safi tena."

**kumkabidhi kwa Bwana**
"kumleta kwa Bwana" au "kumleta yeye kwenye uwepo wa Bwana." Hii ilikuwa ni sherehe kutambua nia ya Mungu kwa mtoto mzaliwa wa kwanza ambaye ni wa kiume.

**kama ilivyo andikwa**
Hii inaweza kusemwa katika mtindo wa tendea. NI: "kama alivyo andika Musa" au "walifanya hivyo kwa sababu Musa aliandika."

**kila mwanaume ambaye anafungua tumbo**
"fungua tumbo" ni nahau ambayo inarejea kwa mtoto wa kwanza kutoka tumboni. Hii ilirejea kwa wote wanyama na wanadamu. NI: "kila mzaliwa wa kwanza mtoto ambaye ni mwanaume."

**hicho ambacho kilisemwa katika sheria ya Bwana**
"ambacho sheria ya Bwana inasema." Hii ni sehemu tofauti katika sheria. Inarejea kwa wanaume, iwe mzaliwa wa kwanza au sivyo.

### Luke 2:25

**Kauli Unganishi:**
Wakati Mariamu na Yusufu wako hekaluni, waliwaona watu wawili: Simeoni, ambaye alimsifu Mungu na kutoa unabii kuhusu mtoto, na nabii mke Ana.

**Tazama**
Neno "tazama" linatuashiria mtu mpya katika simulizi. Lugha yako inaweza ikawa na njia ya kutenda hivi.

**alikuwa mwenye haki na mcha Mungu**
Kauli za nadharia hizi zinaweza kudhihirishwa kama matendo. NI: "alifanya kilichokuwa kinamridhisha Mungu na alitii sheria za Mungu."

**mfariji wa Israeli**
Hili ni jina jingine la "Masihi" au "Kristo." NI: "ndiye ambaye atafariji Israeli."

**Roho Mtakatifu alikuwa juu yake**
"Roho Mtakatifu alikuwa pamoja naye." Mungu alikuwa pamoja naye katika njia maalumu na alimpa hekima na maelekezo katika maisha yake.

**ikafunuliwa kwake na Roho Mtakatifu**
Hii inaweza kusemwa katika mtindo tendea. NI: "Roho Mtakatifu akamwonesha" au "Roho Mtakatifu akamwambia."

**asingalikufa kabla hajamwona Kristo Bwana**
"angelimwona Masihi Bwana kabla hajafa"

### Luke 2:27

**ikatokea**
Baadhi ya lugha zinaweza kusema "kwenda"

**aliongozwa na Roho Mtakatifu**
Hii inaweza kusemwa katika mtindo tendea. NI: "kama Roho Mtakatifu alivyo mwelekeza."

**kwenye hekalu**
"katika kiwanja cha hekalu." Makuhani tu wangeliigia kwenye jengo la hekalu.

**wazazi**
"wazazi' wa Yesu"

**desturi ya sheria**
"desturi ya sheria ya Mungu"

**Sasa mpe ruhusa mtumishi wako aende kwa amani**
"Mimi mtumishi wako; niruhusu niende katika amani." Simeoni alikuwa anarejea kwake mwenyewe.

**ondoka**
Hii ni tasifida imaanishayo "kufa"

**kutokana na neno lako**
"kama ulivyosema" au "kwasababu ulisema ningeli"

### Luke 2:30

**macho yangu yameona**
Udhihirisho huu unamaanisha, "Nimeona mwenyewe" au "Mimi, Mwenyewe, nimeona"

**wokovu wako**
Udhihirisho huu unarejea kwa mtu ambaye angeleta wokovu - mchanga Yesu--ambaye Simeoni alikuwa amembeba. NI: "mwokozi ambaye umemtuma" au "yeye ambaye ulimtuma kuokoa" (UDB)

**ambacho wewe**
inategema na jinsi unavyo tafsiri kauli iliyopita, hii inahitaji kubadilishwa kuwa "ambaye wewe."

**umeandaa**
"umepanga" au "ulisababisha itokee"

**Nuru**
Sitiari hii inamaanisha kwamba mtoto atasaidia watu kuona na kufahamu njia inasema mwanga husaidia watu kuona barabara. NI: "huyu mtoto anawezesha watu kuelewa nuru inavyoruhusu kuona barabara."

**kwaajili ya ufunuo**
iwe lazima kusema ambacho kimefunuliwa. NI: "ambacho kitaufunua ukweli wa Mungu."

**Udhihirisho**
itakuwa lazima kusema udhihirisho ni nini, NI: "kwamba itadhihirisha ukweli wa Mungu"

**utukufu kwa watu wako Israeli**
"atakuwa sababu kwamba utukufu utakuja kwa watu wako Israeli"

### Luke 2:33

**mambo ambayo yalisemwa kumhusu yeye**
Hii inaweza ikasemwa katika mtindo wa kutendea. NI: "mambo ambayo Simeoni aliyasema kumhusu yeye."

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**alimwambia Mariamu mama yake**
"alisema kwa mama wa mtoto, Mariamu." Hakikisha haieleweki kama Mariamu ni mama wa Simeoni.

**Tazama**
Simeoni alitumia udhihirisho huu kumwambia Mariamu kwamba ambacho anachokwenda kukisema ni cha mhimu sana kwake.

**mtoto huyu ni mstaakabali wa kuanguka na kuinuka kwa wengi katika Israeli.**
Neno "kuinuka" na "kuanguka" yanadhihirisha kugeuka kutoka kwa Mungu na kumkaribia Mungu karibu. "mtoto huyu atasababisha watu wengi katika Israeli kuanguka kutoka kwa Mungu au kuinuka karibu na Mungu."

**kwaajili ya ishara ambayo ilikataliwa**
"kwaajili ya ujumbe kutoka kwa Mungu kwamba watu wengi watapinga"

**upanga utapenya nafsini mwako**
Sitiari hii inafafanua huzuni ya ndani ambayo Mariamu angeliisikia. NI: "Huzuni yako itakuwa maumivu ingawa kama upanga utapenya moyoni mwako."

**mawazo kutoka kwenye "mioyo" mingi yatadhihirishwa"**
NI: "mawazo ya watu wengi yatawekwa wazi."

## Luke 2:36

**Nabii mke jina lake Ana pia alikuwa pale**
Hii inatambulisha mhusika mpya katika simulizi.

**Fanueli**
"Fanueli" ni jina la mwanaume.

**miaka saba**
"miaka 7 "

**baada ubikra wake**
"baada ya kuolewa naye"

**mjane kwa miaka themanini na minne**
miaka minne - Maana zinazowezekana 1) kawa mjane kwa miaka 84 au 2) alikuwa mjane na alikuwa na umri wa miaka 84.

**hakuondoka hekaluni**
Hii huenda ni maana iliyokuzwa kwamba alitumia muda mwingi katika hekalu hii ilionekana kama kwamba hakuondoka pale. NI: "kila mara alikuwa hekaluni" au "daima alikuwa hekaluni."

**akifunga na kuomba**
"kujinyima chakula na maombi"

**akawajia karibu yao**
"kuwafuata" au "alikwenda kwa Mariamu na Yusufu"

**wokovu wa Yerusalemu**
Hapa neno "wokovu" lilitumika kurejea kwa mtu ambaye angetenda. NI: yule ambaye angeokoa Yerusalemu" au "mtu ambaye angeleta baraka za Mungu na fadhila tena kwa Yerusalemu."

## Luke 2:39

**Kauli Unganishi:**
Mariamu, Yusufu na Yesu waliondoka Bethlehemu na kurudi kwenye mji wa Nazarethi kwaajili ya utoto wake.

**wao walitakiwa kufanya kutokana na sheria ya Bwana**
Hii inaweza kusemwa katika mtindo wa kutendea. NI: "kwamba sheria ya Bwana iliwataka kufanya."

**mji wa kwao, Nazarethi**
Kauli hii inamaana waliishi Nazarethi. Hakikisha haieleweki kama mji ulio milikiwa.

**kuongezeka katika hekima**
"kuwa na hekima zaidi" au "alijifunza ambayo yalikuwa ya hekima"

**neema ya Mungu ilikuwa juu yake**
"Mungu alimbariki" au "Mungu alikuwa pamoja naye kwa namna pekee"

## Luke 2:41

**Kauli Unganisha**
Wakati Yesu akiwa na umri wa mika 12, huenda Yerusalemu pamoja na familia yake. Wakati akiwa pale, anauliza na kujibu maswali kwa waalimu hekaluni.

**Wazazi wake walikwenda ... sherehe ya Pasaka**
Haya ni maelezo ya nyuma. (angalia:

**Wazazi wake**
"Wazazi wa Yesu"

**wakapanda tena**
Yerusalemu ulikuwa juu ya mlima zaidi kuliko ya maeneo mengine, hivyo wilikuwa kawaida kwa Waisreli kusema wanapanda kwenda huko Yerusalemu.

**kwa muda wa kidesturi**
"muda wa kawaida" au "kama walivyofanya kila mwaka"

**baada ya kubaki kwa siku nyingi kwaajili ya sherehe**
"Wakati wote wa kusherehekea sikuu ulipokwisha" au "Baada ya kusherehekea sikukuu kwa siku zote zilizotakiwa"

**sikukuu**
Hili ni jina lingine la kwaajili ya sherehe ya Pasaka, sababu ilihusisha kula chakula cha sherehe.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**Walidania**
"walifikiri"

**walisafiri safari ya siku nzima**
"walisafiri siku moja" au "walikwenda umbali wa kama watu wanatembea siku moja"

### Luke 2:45

**ikatokea kwamba**
Kauli hii ilitumika hapa kuashiria umhimu wa tukio katika simulizi. Kama lugha yako ina namna ya kufanya hivi, ufikiri kuitumia hapa.

**katika hekalu**
Hii inarejea kwenye kiwanja cha hekalu. Makuhani tu walioruhusiwa ndani ya hekalu. NI: "katika kiwanja cha hekalu" au "kwenye hekalu."

**katikati ya**
Hii haina maana ya katikati kabisa. Zaidi, inamaanisha, "kati" au "pamoja na" au "kuzunguka."

**waalimu**
"waalimu wa dini" au "wale ambao waliwafundisha watu kuhusu Mungu"

**wote waliosikia walishangaa**
Walikuwa hawawezi kuelewa namna gani mvulana wa miaka kumi na miwili asiye na elimu ya dini ajibu vizuri hivyo.

**kwenye ufahamu wake**
"kwa kiwango kipi alielewa" au "kwamba yeye anaelewa mengi sana kuhusu Mungu"

**majibu yake**
"kwa namna alivyo wajibu vizuri" au "kwamba yeye aliwajibu maswali yao vizuri sana"

### Luke 2:48

**Walipomwona yeye**
"Wakati Mariamu na Yusufu wanamwona Yesu"

**kwanini umetutendea namna?**
Hii ilikuwa kumkemea kwa kupindisha kwa sababu hakwenda pamoja nao wakati wa kurudi nyumbani. NI: usingefanya hivi!"

**Sikiliza**
Hili neno daima linatumika kuonesha mwanzo wa tukio jipya au mhimu. Hii pia inaweza kuonesha kutumika mahali tukio linapoanzia. Kama lugha yako inakauli ambayo inatumika kwa njia hii, fikiri ikiwa itaonesha uasili ikitumika hapa.

**Kwa nini mlikuwa mnanitafuta mimi?**
Yesu alitumia maswali mawili kuwakemea wazazi wake kwa upole, na kuanza kuwaambia kwamba analo kusudi kutoka kwa Baba yake wa mbinguni ambalo wao hawakulielewa. NI: "mlikuwa hamhitajiki kunijali mimi."

**ninyi hamkujua ... nyumbani?**
Yesu anatumia swali hili la pili kujitahidi kusema kwamba wazazi wake wangejua kuhusu kusudi ambalo Baba alimtuma. NI: "Ninyi mngejua ... nyumbani."

**Baba yangu**
Kwenye miaka 12, Yesu, Mwana wa Mungu, alielewa kwamba Mungu alikuwa Baba yake halisi (siyo Yusufu, mume wa Mariamu).

**ndani ya nyumba ya Baba yangu**
Maana zinazowezekana ni 1) "katika nyumba ya Baba yangu" au 2) "kuhusu biashara ya Baba yangu." Ikiwa kwa lolote, ambalo Yesu alisema "Baba yangu" alikuwa anarejea kwa Mungu. Kama alimaanisha "nyumba," basi alikuwa anarejea hekalu. Kama alimaanisha "biashara," alikuwa anarejea kwenye kazi ya Mungu aliyopewa kuifanya. Lakini sababu ya mstari unaofuata anasema kwamba wazazi wake hawakuelewa ambacho alichokuwa anawaambia hao, ingelikuwa vema usifafanue zaidi.

### Luke 2:51

**alirudi nao nyumbani**
"Yesu alirudi nyumbani pamoja na Mariamu na Yusufu"

**ulikuwa utii kwao**
"aliwatii" au "kwa njia zote aliwatii"

**alihifadhi mambo yote moyoni mwake**
"alikumbuka mambo yote kwa makini" au "kwa furaha alifikiri kuhusu mambo haya." Maneno "kuhifadhi" au "moyo" yanaashiria kwamba Mariamu alijali mambo haya kuwa ni yanamhusu kwa kina na ni mhimu.

**kukua katika hekima na kimo**
"kuwa na hekima sana na nguvu." Hivi vinarejea kwenye akili na kukua kimwili.

**kuongezaka kupata fadhila kwa Mungu na watu**
Hii inarejea kukua kiroho na kijamii. Hii ingetofautishwa. NI: "Mungu alimbariki zaidi na zaidi, na watu walimpenda zaidi na zaidi."


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 3

1 Sasa, katika mwaka wa kumi na tano wa utawala wa Kaisari Tiberia, wakati Pontio Pilato alikuwa
gavana wa Uyahudi, Herode alikuwa mkuu wa mkoa wa Galilaya, na Filipo ndugu yake alikuwa mkuu wa
mkoa wa Iturea na Trakoniti, na Lisania alikuwa mkuu wa mkoa wa Abilene, 2 na wakati wa ukuhani
mkuu wa Anasi na Kayafa, Neno la Mungu lilimjia Yohana mwana wa Zakaria, jangwani. 3 Alisafiri katika
mkoa wote kuzunguka Mto Yordani, akihubiri ubatizo wa toba kwa ajili ya msamaha wa dhambi 4 Kama
ilivyoandikwa katika kitabu cha maneno ya Isaya nabii, "sauti ya mtu aliaye nyikani, "Itengenezeni tayari
njia ya Bwana, yatengenezeni mapito yake yaliyoonyoka. 5 Kila bonde litajazwa, kila mlima na kilima
vitasawazishwa, barabara zilizopinda zitanyoshwa, na njia zilizoparaza zitalainishwa. 6 Watu wote
watauona wokovu wa Mungu." 7 Hivyo, Yohana akawaambia makutano makubwa ya watu waliomjia
wapate kubatizwa na yeye, "Ninyi uzao wa nyoka wenye sumu, nani aliwaonya kuikimbia gadhabu
inayokuja? 8 Zaeni matunda yanayoedana na toba, na msianze kusema ndani yenu, "Tunaye Ibarahimu
ambaye ni baba yetu; kwa sababu nawaambia ya kwamba, Mungu anaweza kumwinulia Ibrahimu watoto
hata kutokana na mawe haya. 9 Tayari shoka limeshawekwa kwenye mzizi wa miti. Hivyo, kila mti usiozaa
matunda mema, hukatwa na kutupwa motoni. 10 Kisha watu katika makutano walimuuliza wakisema,
"Sasa tunatakiwa tufanyeje?" 11 Alijibu na kuwaambia, "kama mtu ana kanzu mbili anatakiwa atoe kanzu
moja kwa mwingine ambaye hana kabisa, na ambaye ana chakula na afanye vivyo hivyo." 12 Kisha baadhi
ya watoza ushuru walikuja pia kubatizwa, na wakamwambia, "Mwalimu, tunatakiwa kufanya nini? 13
Akawaambia, "Msikusanye fedha zaidi kuliko mnachotakiwa kukusanya." 14 Baadhi ya maaskari pia
wakamuuliza wakisema, "Na sisi je? Tunatakiwa tufanye nini?" Akawambia, "Msichukue fedha kwa mtu
yeyote kwa nguvu, na msimtuhumu mtu yeyote kwa uongo. Ridhikeni na mishahara yenu." 15 Sasa, kwa
kuwa watu walikuwa na shauku ya kumngojea Kristo atakaye kuja, kila mmoja alikuwa anawaza moyoni
mwake kuhusu Yohana kama yeye ndiye Kristo. 16 Yohana akajibu kwa kuwaambia wote, "Mimi
nawabatiza ninyi kwa maji, lakini kuna mmoja ajaye ambaye ana nguvu kuliko mimi, na sisitahili hata
kufungua kamba za viatu vyake. Atawabatiza ninyi kwa Roho Mtakatifu na kwa moto. 17 Pepeto lake liko
mkononi mwake ili kusafisha vizuri uwanda wake wa kupepetea ngano na kuikusanya ngano ghalani
mwake. Lakini, atayateketeza makapi kwa moto ambao hauwezi kuzimika. 18 Kwa maonyo mengine mengi
pia, alihubiri habari njema kwa watu. 19 Yohana alimkemea pia Herode mkuu wa mkoa kwa kumuoa
Herodia, mke wa ndugu yake na kwa maovu mengine mengi ambayo Herode alikuwa ameyatenda. 20
Lakini baadaye Herode alifanya uovu mwingine mbaya sana. Alimfunga Yohana gerezani. 21 Kisha ilitokea
kwamba, wakati watu wote walipokuwa wakibatizwa na Yohana, naye Yesu alibatizwa pia. Wakati
alipokuwa akiomba, mbingu zikafunguka. 22 Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili
kama njiwa, wakati huo huo sauti ikaja kutoka mbinguni ikisema, "Wewe ni Mwanangu mpendwa.
Ninapendezwa sana na wewe." 23 Sasa Yesu mwenyewe, alipoanza kufundisha, alikuwa na umri upatao
miaka thelathini. Alikuwa ni mwana (kama ilivyotadhaniwa) wa Yusufu, mwana wa Eli, 24 mwana wa
Mathati, mwana wa Lawi, mwana wa Melki, mwana wa Yana, mwana wa Yusufu, 25 mwana wa Matathia,
mwana wa Amosi, mwana wa Nahumu, mwana wa Esli, mwana wa Nagai, 26 mwana wa Maati, mwana wa
Matathia, mwana wa Semeini, mwana wa Yusufu, mwana wa Yuda, 27 mwana wa Yoanani, mwana wa
Resa, mwana wa Zerubabeli, mwana wa Shealtieli, mwana wa Neri, 28 mwana wa Melki, mwana wa Adi,
mwana wa Kosamu, mwana wa Elmadamu, mwana wa Eri, 29 mwana wa Yoshua, mwana wa Eliezeri,,
mwana wa Yorimu, mwana wa Matathi, mwana wa Lawi, 30 mwana wa Simeoni, mwana wa Yuda, mwana
wa Yusufu, mwana wa Yonamu, mwana wa Eliyakimu, 31 mwana wa Melea, mwana wa Mena, mwana wa
Matatha, mwana wa Nathani, mwana wa Daudi, 32 mwana wa Yese, mwana wa Obedi, mwana wa Boazi,
mwana wa Salmoni, mwana wa Nashoni, 33 mwana wa Abinadabu, mwana wa Aramu, mwana wa
Hesroni,, mwana wa Peresi, mwana wa Yuda, 34 mwana wa Yakobo, mwana wa Isaka, mwana wa
Ibrahimu, mwana wa Tera, mwana wa Nahori, 35 mwana wa Seruig, mwana wa Ragau, mwana wa Pelegi,
mwana wa Eberi, mwana wa Sala, 36 mwana wa Kenani, mwana wa Arfaksadi, mwana wa Shemu, mwana
wa Nuhu, mwana wa Lameki, 37 mwana wa Methusela, mwana wa Henoko, mwana wa Yaredi, mwana
Mahalalei, mwana wa Kenani, 38 mwana wa Enoshi, mwana wa Sethi, mwana wa Adamu, mwana wa
Mungu.

---


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

# Luka 03 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

Baadhi ya tafsiri hupendelea kuweka nukuu mbele kidogo ya maanidko nyingine za Agano la Kale. ULB na tafsiri nyingine nyingi za Kiingereza huingiza mistari ya 3:4-6, ambayo ni nukuu kutoka Agano la Kale.

### Dhana maalum katika sura hii

### Haki

Maelekezo ya Yohana kwa askari na watoza ushuru katika sura hii si ngumu. Ni mambo ambayo yaliyopaswa kuwa wazi kwao. Aliwaagiza kuishi kwa haki.

### Nasaba

Nasaba ni orodha ambayo hurekodi mababu au wazao wa mtu. Orodha hizo zilikuwa muhimu sana katika kuamua nani aliyekuwa na haki ya kuwa mfalme, kwa sababu mamlaka ya mfalme mara nyingi ilipokelewa au kurithiwa kutoka kwa baba yake. Ilikuwa pia ya kawaida kwa mtu yeyote mashuhuri kuwa na kumbukumbu ya kizazi.

### Takwimu muhimu za matamshi katika sura hii

### Sitiari

Unabii mara nyingi huhusisha matumizi ya sitiari ili kueleza maana yake. Utambuzi wa kiroho unahitajika kwa tafsiri sahihi ya unabii. Unabii wa Isaya ni sitiari ndefu unaoeleza huduma ya Yohana Mbatizaji and

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

### "(Herode) alimfunga Yohana gerezani"

Tukio hili linaweza kuchanganya kwa sababu mwandishi anasemaYohana alifungwa na kisha anasema alikuwa akibatiza Yesu. Mwandishi huenda anatumia maneno haya kwa kutarajia wakati Herode anamfunga Yohana. Hii inamaanisha kwamba taarifa hii iliandikwa kabla ya tukio lenyewe katika maandishi.

---

### Luke 3:1

**Sentensi unganisha**
Maelezo kwa Ujumla

**Katika mwaka wa kumi na tano wa wa utawala wa Kaisari Tiberio**
"Wakati akitawala Kaisari Tiberio ikiwa miaka kumi na tano"

**Filipo ... Lisania**
Haya ni majina ya watu.

**Iturea na Trakoniti...Abilene**
Haya ni majina ya maeneo ya utawala

**Kipindi cha ukuhani mkuu wa Annasi na Kayafa**
"Wakati ambapo Anasi na Kayafa walikuwa wakihudumu pamoja kama kuhani mkuu." Anasi alikuwa kuhani mkuu, na wayahudi waliendelea kumtambua hivyo hata baada ya Warumi walipomteuwa mtoto wake mkwe, Kayafa, kuchukua nafasi yake kama kuhani mkuu.

**neno la Mungu likaja**
"Mungu alisema neno lake"

### Luke 3:3

**Akihubiri ubatizo wa toba**
Neno "Ubatizo" na "Toba" yanaweza kuelezewa kama vitendo. AT: "na alihubiri kwamba watu wale inapaswa kubatizwa kuonyesha kwamba walikuwa wakitubu."

**Kwa ajili ya msamaha wa dhambi**
"Ili kwamba dhambi zao zingeweza kusamehewa" au "ili kwamba Mungu angeweza kusamehe dhambi zao." Toba ilikuwa kwamba Mungu aweze kusamehe dhambi zao.

### Luke 3:4

**Maelezo kwa Ujumla**
Mwandishi, Luka, kanukuu mstari kutoka nabii Isaya tokana na Yohana Mbatizaji.

**Kama ilivyoandikwa...nabii**
Misitari 4-6 ni nukuu kutoka Isaya. Ingeweza kuelezewa katika hali ya kutenda. AT: "Hii ilitokea kama Isaya alivyokuwa ameandika katika kitabu chake" au "Yohana aliyatimiza maneno ambayo Isaya alikuwa ameyaandika katika kitabu chake."

**Sauti ya mtu inapazwa nyikani**
Hii inaweza kudhihirishwa kama sentensi. NI: "Sauti ya mmoja inapazwa ikisikika katika nyika" au "Wanasikia sauti ya mtu fulani inapazwa katika nyika"

**Itengenezeni njia ya Bwana ... tengeneza mapito kwa unyoofu**
Kauli hizi mbili kimsingi ni kitu kile kile.

**Tayarisha njia ya Bwana**
"Andaa njia kwaajili ya Bwana." Kufanya hivi kunawakilisha kujiandaa kusikia ujumbe wa Bwana anapokuja. Watu hufanya hivi kwa kutubu dhambi zao. NI: "Andaa kusikia ujumbe wa Bwana anapokuja" au "Tubu na uwe tayari kwaajili ya ujio wa Bwana"

**njia**
"pa kupita" au "barabara"

## Luke 3:5

**Kila bonde litajazwa...kila mlima na kilima vitasawazishwa**
Watu wanapoandaa barabara kwa ajili ya mtu mhimu anayekuja, wanasawazisha maeneo yaliyoinuka na kujaza maeneo ya mabonde ili kusawazisha barabara. Hii ni sehemu ya msemo wa neno lililozungumzwa katika msitari ulioelezwa juu.

**Kila bonde litajazwa**
Hii inaweza kuelezewa katika hali ya kutenda. AT: "Watalijaza kila eneo la bonde katika barabara.

**Kila mlima na kijilima vitasawazishwa**
Hii inaweza kuelezwa katika hali ya kutenda. AT: "watasawazisha kila mlima na kilima"" au "Wataondoa kila eneo la mwinuko katika barabara"

**Angalia wokovu wa Mungu**
Hii inaweza kuelezewa kama tendo. AT: "Jifunze jinsi Mungu anavyookoa watu kutoka katika dhambi."

## Luke 3:7

**Kubatizwa na Yeye**
Hii inaweza kuelezewa katika hali ya kutenda. AT: "Kwa Yohana kuwabatiza"

**Enyi kizazi cha Nyoka wenye sumu**
Katika sitiari hii, nyoka wenye sumu ni hatari na wanawakilisha uovu. AT: "Ninyi nyoka waovu wenye sumu!" au "Ninyi ni waovu kama nyoka wenye sumu."

**Nani aliyewaonya ... kuja?**
Hakuwatarajia haswa kujibu. Yohana alikuwa anawakemea watu kwasababu walikuwa wanamwomba awabatize, lakini hawakutaka kuacha kutenda dhambi. AT: "Hamwezi kuikimbia gadhabu ya Mungu namna hii" au "Hamwezi kuepuka gadhabu ya Mungu kwa kubatizwa."

**Kutoka kwenye ghadhabu inayokuja**
Neno "gadhabu" linatumika hapa kumaanisha adhabu ya Mungu kwa sababu gadhabu yake inaizidi hiyo. AT: "kutoka kwenye adhabu ambayo Mungu anaituma" au "kutoka kwenye gadhabu ya Mungu ambayo yuko karibu kuiachilia"

## Luke 3:8

**Zaeni matunda yanayoendana na toba**
Katika mfano huu, tabia ya mtu inalinganishwa na mti. Kama tu kwa mmea linavyotarajiwa kuzaa tunda linaloendana na aina ya mmea, mtu ambaye anasema kwamba ametubu, anatarajiwa kuishi kwa haki. AT: "Zaeni aina ya tunda linaloonyesha kwamba umetubu" au "fanya mambo mema yanayoonyesha kwamba umegeuka kutoka katika dhambi zako."

**Mkisema wenyewe ndani yenu**
"Kusema mwenyewe" au "kufikiri mwenyewe"

**Tuna Ibrahimu aliye baba yetu**
"Abrahamu ni Baba yetu" au Sisi ni uzao wa Ibrahimu. "kama inaeleweka kwanini wangesema hili, unaweza pia kuongeza habari imaanishayo: "Hivyo Mungu hatatuadhibu sisi."

**Kumwinulia Ibrahimu watoto**
Nahau hii inamaanisha "Umba watoto kwa ajili ya Ibrahimu" au "sababisha watu kuwa wafuasi wa Ibrahimu."

**Kutokana na mawe haya**
Labda Yohana alikuwa anamaanisha mawe halisi kando ya Mto Yordani.

## Luke 3:9

**Shoka limeshawekwa dhidi ya mzizi wa miti**
Shoka ambalo liko tayari kukata mizizi ya mti ni mfano wa adhabu iliyo karibu kuanza. Inaweza pia kuelezwa katika hali ya kutenda. AT: "Mungu ni kama mtu aliyeweka shoka lake dhidi ya mzizi wa miti."

**Kila mti usiozaa tunda jema hukatwa chini**
Hii inaweza kuelezwa katika hali ya kutenda. AT: "Hukata chini kila mti usiozaa tunda jema."

**Kutupwa motoni**
"Moto" pia ni mfano wa adhabu. Hii inaweza kuelezwa katika hali ya kutenda. AT: "Hulitupa ndani ya moto"

## Luke 3:10

**Maelezo unganishi:**
Yohana anaanza kujibu maswali ambayo watu kwenye mkutano wanamuuliza.

**Walimuuliza, wakisema**
"Walimuuliza na kusema" au Walimuuliza Yohana"

**Alijibu na kusema kwao**
"Aliwajibu, akisema" au "aliwajibu" au "alisema"

**Fanya hivyohivyo**
"Fanya jambo hilohilo." Inaweza kwa msaada kuelezea hasa inavyomaanisha. AT: "Mpe chakula mtu ambaye hana kabisa."

## Luke 3:12

**Kubatiza**
Hii ingeweza kuelezwa katika hali ya kutenda. AT: "Kwa Yohana kuwabatiza."

**Msikusanye fedha zaidi**
"Msiombe fedha zaidi" au "Msitake fedha zaidi." Watoza ushuru walikuwa wakikusanya fedha zaidi kuliko walivyokuwa wanatakiwa. Wanapaswa kuacha kufanya hivyo.

**Zaidi kuliko mnavyotakiwa**
Kifungu hiki kinaonyesha kwamba mamlaka ya watoza ushuru hutoka Rumi. AT: "zaidi kuliko kile Warumi wamewaamuru kuchukua."

## Luke 3:14

**Maaskari**
"Watu wanaotumika jeshini"

**Na sisi je? Tunapaswa kufanya nini?**
Vipi na sisi maaskari, tunapaswa kufanya nini?" Yohana haunganishwi katika maneno "sisi" na "sisi." Maskari walimaanisha kwamba alikuwa amewaambia makutano na watoza ushuru wanachotakiwa kufanya na walitaka kujua kama maaskari wanachotakiwa kufanya.

**Msimshutumu yeyote kwa uongo**
Inaonekana kwamba maaskari walikuwa wanatengeneza tuhuma za uongo dhidi ya watu ili kujipatia fedha. AT: "kwa namna ileile, msimshutumu yeyote kwa uongo ili mjipatie fedha kutoka kwao" au "Msiseme kwamba mtu asiye na hatia amefanya kitu kinyume cha sheria."

**Rizikeni na mishahara yenu**
"Toshekeni na malipo yenu"

## Luke 3:15

**Kama watu**
"Kwa sababu watu." Hii inamaanisha watu walewale waliokuja kwa Yohana.

**wasiwasi katika mioyo yao**
Udhihirisho huu hapa unamaanisha "fikiria juu yao kwa utulivu"

**Yohana alijibu kwa kusema**
Jibu la Yohana kuhusiana na mtu mkuu ajaye ni wazi inamaanisha Yohana siyo Kristo. Inaweza kusaidia kusema hili wazi kwaajili watu wako, kama UDB, inavyofanya. "Hapana, Mimi siye"

**Nawabatiza kwa maji**
"Nawabatiza kwa kutumia maji" au "Nawabatiza kwa nyenzo ya maji"

**Haistahili hata kufungua kamba za viatu vyake**
Kufungua kamba za viatu ilikuwa ni wajibu wa mtumwa. Yohana alikuwa anasema kwamba yule atakayekuja ni mkubwa kiasi kwamba Yohana hakustahili hata kuwa mtumwa wake. AT: "Hafikii umuhimu hata kulegeza kamba za viatu vyake."

**Viatu**
"Viatu vilivyotengenezwa kwa ngozi" au "Aina ya viatu vya wazi vyenye kamba za ngozi"

**Atawabatizeni kwa Roho Mtakatifu na kwa moto**
Huu mfano unalinganisha ubatizo wa kawaida unamleta mtu katika muunganiko na maji kwenye ubatizo wa kiroho unaowaleta katika muunganiko na Roho Mtakatifu na moto.

**Moto**
Hapa neno "moto" linamaanisha 1) hukumu au 2) utakaso. Inafaa kuionda kama moto

## Luke 3:17

**Pepeteo lake liko mkononi mwake**
Kama mkulima alivyo tayari kutenganisha mbegu za ngano kutoka kwenye pumba hivyo, ndivyo ilivyo kwa Kristo alivyo tayari kumhukumu mwanadamu. AT: "Anashikilia pepeteo kwasababu yuko tayari."

**Pepeteo**
Hiki ni chombo cha kurushia ngano juu hewani kutenganisha mbegu kutoka kwenye pumba. Mbegu nzito huanguka kurudi chini na pumba azisizotakiwa hupulizwa mbali na upepo. Inafanana na kirushio.

**Uwanda wake wa kupepetea**
Mahali pa kupepetea ni eneo ambapo ngano iliwekwa katika kuiandaa kuipepeta. "Kusafisha" AT: "Eneo lake" au "Eneo ambako hutenganisha mbegu kutoka kwenye pumba"

**Kukusanya ngano**
Ngano ni nafaka inayokubalika kuitunza na kuhifadhi.

**Kuzichoma pumba**
Pumba hazitumiwi kwa chochote, hivyo, watu huyachoma zote.

### Luke 3:18

**Maelezo kwa ujumla**
Simulizi inaelezea nini kinaenda kutokea kwa Yohana lakini halijatokea kwa wakati huu.

**Kwa maonyo mengine mengi**
"Pamoja na hoja zingine za nguvu nyingi"

**Herode Tetraki**
Herode alikuwa Tetraki, siyo mfalme. Alikuwa na utawala unaokomea eneo maalumu katika mkoa wa Galilaya.

**Kwaajili ya kumuoa mke wa ndugu yake Herodia**
"kwa sababu Herode alimuoa Herodia, mke wa ndugu yake." Huu ulikuwa uovu kwa sababu kaka wa Herode alikuwa hai. Hii inaweza kusemwa wazi. AT: "kwasababu alimuoa mke wa kaka yake, Herodia, wakati kaka yake akiwa hai"

**Alimfunga Yohana gerezani**
"Aliwaambia askari wake kumuweka Yohana jela

### Luke 3:21

**Sentensi unganishi**
Yesu anaanza huduma yake kwa ubatizo wake.

**Sasa ikawa kwamba**
Msemo huu ni mwanzo wa tukio jipya katika hadithi. Kama lugha yako ina njia kwa ajili ya kufanya hii, unaweza kufikiria kutumia hapa.

**wakati watu wote walikuwa wakibatizwa na Yohana**
"Wakati Yohana alikuwa akibatiza watu wote." Neno "watu wote" inahusu watu akiwemo na Yohana.

**batizwa**
"Yesu alibatizwa na Yohana." Baadhi ya makundi wanaweza kuchanganywa kwamba Yohana alikuwa anabatiza wakati Herode alimweka gerezani kwenye mstari uliotangulia. Ikiwa hivyo, inaweza ikasaidia kuwaambia kwamba tukio hili lilitokea kabla Yohana hajakamatwa. UDB inaliweka hivi "Lakini kabla ya Yohana hafungwa gerezani" mwanzoni mwa mstari huu.

**Yesu pia alibatizwa**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo wa kutendea. NI: "Yohana alimbatiza Yesu, vilevile"

**mbingu zimefunguka**
"Anga likafunguliwa" au "anga likawa wazi." Hii ni zaidi ya kusafisha mawingu, lakini siyo wazi nini maana yake. Ni uwezekano ina maana kwamba shimo alionekana katika anga.

**Roho Mtakatifu kwenye umbo la mwili alishuka juu yake**
"Roho Mtakatifu akashuka juu Yesu"

**kama la njiwa**
"Katika hali ya kimwili Roho Mtakatifu alionekana kama njiwa"

**Wewe ni Mwanangu, ambaye nakupenda**
Mungu Baba anaongea na Mwanaye ("ambaye nampenda"), Yesu ni Mungu Mwana, wakati Mungu Roho shuka juu ya Yesu. watu wa Mungu kupendana na kufanya kazi pamoja kama Baba, Mwana, na Roho.

**Mwanangu, ambaye nampenda**
Hili ni jina muhimu kwa Yesu, Mwana wa Mungu

### Luke 3:23

**Maelezo kwa ujumla**
Luka anaorodhesha mababu wa Yesu kwa njia ya uzao wa baba yake mlezi, Yusufu.

**Wakati**
Neno hili limetumika hapa kuthibitisha mabadiliko kutokana na hadithi ya taarifa za msingi kuhusu kuhusu umri Yesu na mababu.

**umri wa miaka thelathini**
"umri wa miaka 30"

**Alikuwa mwana (kama ilivyodhaniwa) wa Yusufu**
"Ilidhaniwa kwamba alikuwa ni mwana wa Yusufu" au "Watu walidhani kuwa yeye ni mwana wa Yusufu"

**mwana wa Eli, mwana wa Mathati, mwana wa Lawi**
fikiria jinsi watu wanavyoorodhesha wahenga katika lugha yako. Utumie mfumo huohuo kwa orodha yote. Mifumo inyoowezekana ni 1) "ambaye alikuwa mwana wa Heli, ambaye alikuwa mwana wa Mathat, ambaye alikuwa mwana wa Lawi" 2) Yusufu alikuwa mwana wa Heli, Heli alikuwa mwana wa Mathat, baba wa Mathat alikuwa Lawi"

**mwana wa Eli.**
"Yusufu alikuwa mwana wa Eli" au "baba Yusufu alikuwa Eli"

### Luke 3:25

**mwana wa Matathia, mwana wa Amosi ... Joda**
Huu ni mwendelezo wa orodha ya mababu wa Yesu. Tumia namna ile ile kama ulivyotumia kwenye mistari ile iliyotangulia.

### Luke 3:27

**mwana wa Yohanani, mwana wa Resa ... Levi**
Matumizi maneno sawa kama wewe kutumika katika mistari uliopita. AT "ambaye alikuwa mwana

wa Yohanani, ambaye alikuwa mwana wa Resa ... Levi" au "Joda alikuwa mwana wa Yohanani, Yohanani mwana wa Resa ... Levi" au "baba Joda ilikuwa Yohanani, baba Yohanani aliitwa Rhesa ... Levi. " Hii ni muendelezo wa orodha ya mababu Yesu.

### Luke 3:30

#### mwana wa Simoni, mwana wa Yuda

Matumizi maneno sawa kama wewe kutumika katika mistari uliopita. "Ambaye alikuwa mwana wa Simeoni ambaye alikuwa mwana wa Yuda" au "Levi mwana wa Simeoni, Simeoni alikuwa mwana wa Yuda" au" baba Levi aliitwa Simeoni, baba Simeon alikuwa Yuda"

### Luke 3:33

#### mwana wa Aminadabu, mwana wa Admini

Matumizi maneno sawa kama wewe ulivyotumika katika mistari iliyopita. "Ambaye alikuwa mwana wa Aminadabu, ambaye alikuwa mwana wa Admini" au "Levi alikuwa mwana wa Aminadabu, Simeoni ni mwana wa Admini" au "baba Nashon ilikuwa Aminadabu, Aminadabu baba aliitwa Admin"

### Luke 3:36

#### mwana wa Kainani, mwana wa Arfaksadi

Tumia maneno sawa kama uliyotumia katika mistari iliopita. "Ambaye alikuwa mwana wa Kenani, ambaye alikuwa mwana wa Arfaksadi" au "Levi alikuwa mwana wa Kenani, Kenani alikuwa mwana wa Arfaksadi" au "baba Shela alikuwa Kenani, Kenani baba aliitwa Arfaksadi"

---

## Chapter 4

[1] Kisha, Yesu akiwa amejaa Roho Mtakatifu, alirudi kutoka Mto Jordani, na aliongozwa na Roho jangwani
[2] kwa siku arobaini, na huko alijaribiwa na Ibilisi. Wakati huo hakula chochote, na mwisho wa wakati huo
alihisi njaa. [3] Ibilisi akamwambia, "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, liamru jiwe hili kuwa mkate." [4] Yesu
akamjibu, "Imeandikwa; 'mtu hataishi kwa mkate pekee." [5] Kisha Ibilisi alimwongoza juu kwenye kilele
cha mlima, na akamwonyesha falme zote za dunia kwa muda mfupi. [6] Ibilisi akamwambia, "Nitakupa
mamlaka ya kutawala falme hizi zote pamoja na fahari zake. Naweza kufanya hivyo kwa sababu vyote
vimekabidhiwa kwangu nivitawale, na ninaweza kumpa yeyote nitakaye kumpa. [7] Kwahiyo, kama
utaniinamia na kuniabudu, vitu hivi vyote vitakuwa vyako." [8] Lakini Yesu alijibu na kumwambia,
"Imeandikwa, "lazima umwabudu Bwana Mungu wako, na lazima umtumikie Yeye peke yake." [9] Baadaye
Ibilisi alimwongoza Yesu hadi Yerusalemu na kumweka sehemu ya juu kabisa ya jengo la hekalu na
kumwambia, "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, jitupe chini kutoka hapa. [10] Kwa sababu imeandikwa,
"Atawaagiza malaika zake wakutunze na kukulinda, [11] na watakuinua juu mikononi mwao ili kwamba
usiumize miguu yako juu ya jiwe." [12] Yesu akijibu alimwambia, "Imenenwa, "usimjaribu Bwana Mungu
wako." [13] Ibilisi alipomaliza kumjaribu Yesu, aliendа zake na kumwacha hadi wakati mwingine. [14] Kisha
Yesu alirudi Galilaya kwa nguvu za Roho, na habari kumhusu yeye zikaenea na kusambaa katika mikoa
jirani yote. [15] Alifundisha katika masinagogi yao, na kila mmoja alimsifu. [16] Siku moja alikwenda
Nazareti, mji ambao alilelewa na kukulia. Kama ilivyokuwa desturi yake aliingia kwenye sinagogi siku ya
sabato, na alisimama kusoma maandiko. [17] Alikabidhiwa gombo la nabii Isaya, hivyo, alilifungua gombo
na akatafuta sehemu iliyoandikwa, [18] "Roho wa Bwana yuu juu yangu, kwa sababu alinitia mafuta
kuhubiri habari njema kwa maskini. Amenituma kutangaza uhuru kwa wafungwa, na kuwafanya wasioona
waweze kuona tena. Kuwaweka huru wale wanaogandamizwa, [19] kuutangaza mwaka ambao Bwana
ataonesha wema wake." [20] Kisha akalifunga gombo, akamrudishia kiongozi wa sinagogi, na akaketi chini.
Macho ya watu wote waliokuwa katika sinagogi yalimwangalia yeye. [21] Alianza kuzungumza nao akisema,
"Leo andiko hili limetimizwa masikioni mwenu." [22] Kila mmoja pale alishuhudia kile alichokisema Yesu, na
wengi miongoni mwao walishangazwa na maneno ya hekima yaliyokuwa yakitoka katika kinywa chake.
Walikuwa wakisema, "huyu ni kijana tu wa Yusufu, siyo hivyo?" [23] Yesu akawaambia, "hakika mtasema
methali hii kwangu, "Tabibu, jiponye mwenyewe. Chochote tulichosikia ukifanya Kapernaumu, kifanye
hapa pia kijijini kwako." [24] Pia alisema, "hakika nawaambia ninyi, hakuna nabii anayekubalika katika nchi
yake." [25] Lakini nawaambia ninyi kweli kwamba kulikuwa na wajane wengi Israel katika kipindi cha Eliya,
wakati mbingu ilipofungwa kusiwe na nvua kwa miaka mitatu na nusu, wakati kulipokuwa na njaa kubwa
katika nchi yote. [26] Lakini Eliya hakutumwa kwa yeyote mmoja wao, lakini kwa mjane mmoja tu aliyeishi
Sarepta karibu na mji wa Sidoni. [27] Pia, kulikuwa na wakoma wengi Israel katika kipindi cha Elisha nabii,
lakini hakuna hatammoja wao aliyeponywa isipokuwa Naamani mtu wa Siria. [28] Watu wote ndani ya
sinagogi walijawa na gadhabu walipoyasikia haya yote. [29] Walisimama na kumsukumizia nje ya mji, na
kumwongoza mpaka kwenye ukingo wa mlima wa mji ambapo mji wao ulijengwa juu yake, ili waweze
kumtupa chini. [30] Lakini alipita salama katikati yao na akaenda zake. [31] Kisha alitelemkia Kapernaumu,
katika mji wa Galilaya. Sabato moja alikuwa akifundisha watu ndani ya sinagogi. [32] Walishangazwa na
mafundisho yake, kwasababu alifundisha kwa mamlaka. [33] Sasa siku hiyo ndani ya sinagogi, kulikuwa na
mtu aliyekuwa na roho ya pepo mchafu, na alilia kwa sauti ya juu, [34] "Tuna nini nawe, Yesu wa Nazareti?
Umekuja kutuangamiza? Ninajua wewe ni nani! Wewe ni mtakatifu wa Mungu!" [35] Yesu alimkemea pepo
akisema, "Nyamaza kimya, na umtoke mtu huyu!" Pepo yule alipomtupa mtu yule chini katikati yao,
alimtoka yule mtu bila ya kumsababishia maumivu yoyote. [36] Watu wote walishangaa, na waliendelea
kuzungumzia jambo hilo kila mmoja na mwenzake. Wakasema, "Ni maneno ya aina gani haya?"
Anawaamuru roho wachafu kwa mamlaka na nguvu na watondoka." [37] Hivyo, habari juu ya Yesu zilienea
kila sehemu katika maeneo yanayozunguka mkoa huo. [38] Kisha Yesu aliondoka katika mji huo na akaingia
katika nyumba ya Simoni. Sasa, mama mkwe wake na Simoni alikuwa anaumwa homa kali, na wakamsihi
kwa niaba yake. [39] Hivyo, Yesu alimsogelea, akaikemea ile homa na ikamwachia. Ghafla alisimama na
akaanza kuwatumikia. [40] Jua lilipokuwa likizama, watu walimletea Yesu kila mmoja aliyekuwa mgonjwa
wa maradhi ya aina mbalimbali. Aliweka mikono yake juu ya kila mgonjwa na akawaponya wote. [41]
Mapepo pia yaliwatoka wengi wao yakilia kwa sauti na kusema, "Wewe ni mwana wa Mungu!" Yesu
aliwakemea mapepo na hakuwaruhusu waongee, kwa sababu walijua kwamba yeye alikuwa ni Kristo. [42]
Wakati kulipopambazuka, aliendа eneo lisilokuwa na watu. Makutano ya watu walikuwa wakimtafuta na
wakaja katika eneo alilokuwapo. Walijaribu kumzuia asiende mbali na wao. [43] Lakini akawaambia,

"Lazima pia nihubiri habari njema za ufalme wa Mungu katika miji mingine mingi, kwa kuwa hii ndiyo sababu nilitumwa hapa." **44** Kisha aliendelea kuhubiri ndani ya masinagogi katika uyahudi wote.

---

## Luka 04 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

Baadhi ya tafsiri hupendelea kuweka mbele kidogo nukuu za Agano la Kale. ULB na tafsiri nyingine nyingi za Kiingereza huingiza mistari ya 4:10-11, 18-19, ambayo ni nukuu kutoka Agano la Kale.

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

### Yesu alijaribiwa na shetani

Ingawa ni kweli kwamba shetani aliamini kwa hakika kwamba angeweza kumshawishi Yesu kumtii, ni muhimu kuonyesha kama Yesu hakutaka kumtii hata kidogo.

---

### Luke 4:1

**Sentensi Unganishi**
Ibilisi amkuta Yesu aweze kumjaribu akose baada ya Yesu kufunga kwa siku arobaini 40.

**Ndipo Yesu**
Hii inarejea baada ya Yohana kumbatiza Yesu. NI: "Baada ya Yesu kuwa kabatizwa"

**akaongozwa na Roho**
Hii inaweza katika mfumo wa kutenda. NI: "Roho alimwongoza"

**Kwa siku arobaini yeye alijaribiwa**
Tafsiri nyingi zinasema kwamba majaribu yalikuwa kwa siku zote arobaini. UDB inasema "Wakati akiwa pale, Ibilisi aliendelea kumjaribu" kuweka hili wazi.

**siku arobaini**
"siku 40"

**alikuwa akijaribiwa na shetani**
Hii inaweza kusemwa katika mfumo wa kutenda. NI: "ibilisi alimjaribu asimtii Mungu"

**Hakuna alichokula**
Neno "yeye" linarejea kwa Yesu.

### Luke 4:3

**Kama ni mwana wa Mungu**
Ibilisi anamtega Yesu afanye muujiza huu ili kwamba athibitishe yeye ni "mwana wa Mungu"

**hili jiwe**
Ibilisi ama anashikilia jiwe au ananyooshea kidole kwenye jiwe lililokaribu.

**Yesu alimjibu**
Kukataa kwa Yesu kukosolewa na Ibilisi iko wazi kwenye jibu lake. Itaweza kusaidia kusemwa hili kwa wazi kwa kundi lako, kama inavyofanya UDB "Yesu alijibu, Hapana, sitafanya hivyo"

**Hii imeandikwa**
Nukuu inatoka kwa Maandiko ya Musa katika Agano la Kale. Hii inaweza kusemwa kwa kauli tendaji. NI: "Musa ameandika katika maandiko"

**Mtu haishi kwa mkate pekee**
Neno "mkate" linarejea kwenye chakula kwa ujumla. Chakula kama ukilinganisha kwa Mungu, chenyewe tu, hakitoshi, kumtosheleza mtu. Yesu ananukuu maandiko kwanini asibadili jiwe mkate. NI: "watu hawahawezi kuishi kwa mkate tu" au "siyo chakula tu ambacho kinamfanya mtu aishi" au "Mungu anasema vitu mhimu zaidi ya chakula"

### Luke 4:5

**mahali pa juu**
mlima mrefu

**katika muda mfupi**
hapo hapo au "kwa ghafla"

**nimepewa mimi haya**
Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji. Huenda kwamba maana "wao" inarejea 1) mamlaka na fahari ya falme au 2) falme NI: "Mungu ameyatoa kwangu"

**kama utainama chini ... kuniabudu**
Kauli hizi mbili zinafanana sana. Zinaweza kuwekwa pamoja. NI: "kama utainama chini katika kuniabudu"

**Itakuwa ya kwako**
"Nitakupa wewe ufalme hizi zote, pamoja na fahari zake"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

### Luke 4:8

**Lakini Yesu alijibu ... imeandikwa**
Utofauti huu unamaanisha kwamba Yesu alikataa kufanya kile alichoambiwa na Ibilisi. Itakuwa msaada kusema hiki wazi kwa hadhara yako. NI: "Lakini alijibu, 'Hapana, sitakuabudu wewe, kwa sababu imeandikwa" (UDB)

**alijibu na akamwabia**
"akamjibu" au "alimjibu"

**Imeandikwa**
Hii inaweza ikasemwa katika kauli tendaji. NI: "Musa ameandika katika maandiko"

**Utamwabudu Bwana Mungu wako**
Yesu alikuwa ananukuu amri kutoka kwenye maandiko kusema kwanini hataweza kumwabudu Ibilisi.

**Wewe**
Hii inarejea kwa watu katika Agano la Kale waliopokea amri ya Mungu. Unawea kutumia kauli ya umoja 'wewe' sababu kila mtu ilikuwa atiii, au ungetumia kauli ya wingi "ninyi" sababu watu walipaswa kuitii.

**yeye**
Neno "yeye" anarejea kwa Mungu.

### Luke 4:9

**ncha ya juu sana**
Hii ilikuwa ni ncha kwenye paa la hekalu. Kama mtu akianguka kutokea kule, angejeruhiwa sana au kufa.

**Kama wewe ni mwana wa Mungu**
shetani alikuwa anamkosoa Yesu athibitishe kwamba alikuwa Mwana wa Mungu

**Mwna wa Mungu**
Hiki ni cheo mhimu kwaajili ya Yesu.

**jitupe mwenyewe chini**
"ruka chini ardhini"

**Kwa kuwa imeandikwa**
Ibilisi anamaanisha kwamba nukuu yake kutoka Zaburi inamaanisha Yesu hataumia kama ni Mwana wa Mungu. Hii inwaeza kusemwa wazi, kama inavyofanya UDB. NI: "Hutaumia" sababu imeandikwa"

**imeandikwa**
Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji. NI: "mwandishi ameandika"

**Yeye atatoa maagizo**
"Yeye" inarejea kwa Mungu. Ibilisi kwa sehemu alinukuu kutoka Zaburi kwa juhudi kumshawishi Yesu kuruka kutoka juu ya jengo.

### Luke 4:12

**Hii ilisemwa**
Yesu anamwambia Ibilisi kwanini hatafanya kile ambacho Ibilisi amemwabia kufanya. Kukataa kwake kufanya inaweza kusemwa wazi. NI: "Hapana, sitafanya hivyo, kwasababu ilisemwa"

**Hii ilisemwa**
Yesu ananukuu kutoka maandiko ya Musa katika Kumbukumbu la Torati. Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji. NI: "Musa amesema" au "katika maandiko Musa alisema"

**Usimweke Mungu wako katika majaribu**
Maana zinazowezekana ni 1) Yesu hataweza kumjaribu Mungu kwa kuruka kutoka katika hekalu, au 2) Ibilisi hawezi kumjaribu Yesu kuona kama yeye ni Mwana wa Mungu. inafaa zaidi kutafsiri mstari kama ilivyoelezwa zaidi kuliko kujaribu fafanua maana.

**Mpaka wakati mwingine**
"mpaka tukio lingine"

**lishamaliza kumjaribu Yesu**
Hii haimaanishi kwamba Ibilisi alikuwa kafanikiwa katika majaribu yake - Yesu alipinga kila jaribio. Hii inaweza ikasemwa wazi. Ni: "lishamaliza kujaribu kumjaribu Yesu" (UDB) au "pumzika kujaribu kumjaribu Yesu"

### Luke 4:14

**Sentensi Unganishi:**
Yesu alirudi Galilaya, akifundisha katika Sinagogi, na anawaambia watu pale kwamba yeye anatimiza maandiko ya Isaya nabii.

**Ndipo Yesu alirudi**
Hii inaanza simulizi jipya katika habari.

**katika nguvu ya Roho**
"na Roho alikuwa anampa yeye nguvu." Mungu alikuwa pamoja na Yesu kwa namna maalumu, anamwezesha yeye kufanya vitu ambayo kawaida watu wasingeviweza.

**habari kumhusu yeye zikaenea**
Wale waliomsikia Yesu waliwaambia watu wengine kuhusu yeye, na ndipo wale watu wengine waliwaambia hata zaidi kuhusu yeye. Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji. NI: "watu wakaeneza habari kuhusu Yesu" au "watu waliwaambia watu wengine kuhusu Yesu" au "maarifa kumhusu yeye yalikuwa yakipita kutoka kwa mtu kwenda mtu mwingine"

**kupitia katika eneo lote linalozunguka ukanda**
Hii inarejea kwenye maeneo au mahali karibu na Galilaya.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**likuwa anasifiwa na wote**
"kila mmoja alisema mambo makuu kuhusu yeye" au "watu wote walimsema vizuri "

## Luke 4:16

**mahali yeye alipokuziwa**
mahali wazazi wake walipomlelea " au "pale alipoishi alipokuwa mdogo" "mahali alipokulia"

**kama ilivyokuwa desturi yake**
"kama alivyofanya kila sabato." ilikuwa siyo mazoea ya kawaida kwenda kwenye sinagogikwenye siku ya sabato.

**Yeye alipewa Gombo la nabii Isaya**
Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji. NI: "mtu fulani alimpa gombo la nabii Isaya"

**Gombo la nabii Isaya**
Hii inarejea kwenye kitabu cha Isaya imeandikwa kwenye gombo. Isaya aliandika maneno miaka mingi kabla, na mtu fulani mwingine aliyanukuru kwenye gombo.

**mahali ambapo palikuwa pameandikwa**
"mahali katika gombo palipo na maneno haya." Sentensi hii inaendelea katika mstari unaofuata.

## Luke 4:18

**Roho wa Bwana iko juu yangu**
"Roho Mtakatifu yuko pamoja nami kwa namna maalumu." Wakati mtu fulani anasema hivi, anathibitisha kunena maneno ya Mungu.

**aliniweka wakfu mimi**
Katika Agano la Kale, mafuta ya upako yalimiminwa juu ya mtu aliyepewa nguvu na mamlaka kufanya kazi maalumu. Yesu anatumia sitiari hii kurejea kwa Roho Mtakatifu kuwa juu yake kumwandaa kwaajili ya kazi. NI: "Roho Mtakatifu yuko juu yangu kuniwezesha" au "Roho Mtakatifu alinipa mimi nguvu na mamlaka"

**maskini**
"watu maskini"

**kutangaza uhuru kwa mateka**
"kuwaambia ambao walikuwa wametekwa kwamba wako huru" au "kuwaweka huru wafungwa wa vita"

**kupona macho kwa wale vipofu**
"kumpa kipofu kuona" au "kumfanya kipofu aweze kuona tena"

**wekwa huru wale ambao wanagangamizwa**
"weka huru wale ambao tumikishwa vibaya"

**kutangaza mwaka wafadhila ya Bwana**
"mwambia kila mmoja kwamba Bwana tayari amebariki watu wake" au "tangaza kwamba huu ni mwaka ambao Bwana ataonesha wema wake"

## Luke 4:20

**bingilisha gombo**
gombo lilikuwa limefungwa kwa kubingilishwa kama bomba kutunza kile kilichoandikwa ndani yake.

**mhudumu**
Hii inarejea kwa mtumishi wa sinagogi ambaye alileta na kutunza kwa uangalifu and unyenyekevu gombo linalobeba maandiko.

**yalikuwa yamekazwa kwake**
Lahaja hii inamaanisha "yalikuwa yameelekezwa kwake" au "walitazama kwa makini kwake"

**maandiko haya yametimizwa mkiwa mnasikiliza**
Yesu alikuwa anasema hivyo kutimiza unabii kwa vitendo na hotuba kwa wakati wake kabisa. Hii inaweza ikaelezwa katika kauli tendaji. NI: "Sasa hivi ninatimiza inatimiza ambacho maandiko yalisema mnaponisikiliza sasa"

**shangazwa na maneno ya neema ambayo yalikuwa yanatoka katika kinywa chake**
"lipigwa butwaa na vitu vya neema alivyokuwa akivisema." Hapa "aneema" inaweza kuerejea 1) ubora au jinsi ya ushawishi aliozungumza Yesu, au 2) kwamba Yesu alizungumza maneno kuhusu neema ya Mungu.

**Huyu si ni mwana wa Yusufu?**
Watu walifikiri kwamba Yusufu alikuwa baba wa Yesu. Yusufu hakuwa kiongozi wa dini, hivyo walishangaa kwamba mtoto wake atahubiri kiasi hicho. NI: "Huyu ni mwana wa Yusufu tu!" au "Baba yake ni Yusufu tu!"

## Luke 4:23

**Maelezo kwa Ujumla**
Nazarethi ni mji ambao ndimo Yesu alikulia

**Kwa hakika**
"Kwa hakika" au "bila shaka." Huu ni uthibitisho wa nguvu.

**Daktari, jiponye mwenyewe!**
Kama daktari haonekani kuwa ana afya, hakuna sababu kumwamini kuwa kweli ni daktari. Wakati watu wanasema mithali hii kwa Yesu, watamaanisha hawakuamini kwamba yeye ni nabii sababu hafanani.

**lolote tulilosikia ... fanya hivyo hivyo kwenye miji ya kwenu.**
Watu wa Nazarethi hawakuamini Yesu kuwa nabii sababu ya sifa yake ya chini kama mtoto wa yusufu. Hawataamini isipokuwa waone wao wenyewe akifanya miujiza.

**Ukweli nasema kwenu**
"Hii kweli ni hakika." Hii ni kauli ya msisitizo kuhusu kile kinachofuata.

**hakuna nabii anayepokelewa kwenye mji wa kwao**
Yesu anaitengeneza kauli hii kwa ujulma ili kwmba awakemee watu. Yeye anamaanisha kwamba wanakataa kuamini taarifa za miujiza yake Kapernaumu. Wao walifikiri tayari walijua yote yanayomhusu yeye.

**mji wa kwao**
"ardhi yao" au "wenyeji wa mji" au "nchi ambayo alikulia"

## Luke 4:25

**Sentensi kwa Ujumla**
Yesu anawakumbusha watu, wanaomsikiliza kwenye sinagogi, kuhusu Eliya na Elisha waliokuwa manabii ambao waliwafahamu.

**Lakini nawaambia ukweli**
"Nawaambia ukweli kabisa." Kauli hii ilitumika kusisitiza umhimu, ukweli na usahihi wa kauli zinazofuata.

**wajane**
mjane ni mwanamke aliyefiwa na mume wake.

**wakati wa Eliya**
Watu wale aliokuwa anawahutubia walijua kwamba Eliya alikuwa mmoja wa manabii wa Mungu. Kama wasomaji wako hawatajua hilo, unaweza ukafanya taarifa zisizowazi kuwa wazi kma UDB. AT: "Eliya alipokuwa anatoa unabii Israel"

**wakati wingu lilipofungwa**
Hii ni sitiari. Anga limefananishwa na dari iliyofungwa, na hivyo hakuna mvua itakayonyysha toka huko. NI: "ambapo hakuna mvua inashuka chini kutoka angani" au "wakati ilikuwa hakuna mvua kabisa"

**njaa kubwa**
"tatizo kubwa la kupungua chakula." Njaa ni kipindi kirefu ambapo hakuna uzalishaji wa mazo ya kutosha chakula kwa watu.

**mpaka Sarepta ... kwa mjane anayeishi huko**
Watu walioishi Sarepta walikuwa Wamataifa, siyo Wayahudi. Watu wanaomsikiliza Yesu wangeelewa kwamaba watu wa Sarepta walikuwa Wamataifa. Mjane mmataifa anaishi Sarepta.

**Naamani Msiria**
Msiria ni mtu kutoka nchi ya Siria. Watu wa Siria ni siyo Wayahudi. NI: "Mmataifa Naamani kutoka Siria"

## Luke 4:28

**Watu wote kwenye sinagogi walijaa hasira waliposikia mambo haya**
Watu wa Nazarethi walikosewa sana kwamba Yesu alidondoa maandiko ambayo Mungu aliwasaidia wamataifa badala ya Wayahudi.

**walimlazimisha yeye atoke nje ya mji**
"walimlazimisha yeye kuuacha mji" au "alisukumwa nje ya mji" (UDB)

**jabali la kilimani**
"ncha ya jabali"

**yeye alipitia katikati yao**
"kupita katikati ya mkutano" au "kati ya watu ambao wanajaribu kumuua yeye." Neno "haki" hapa ni sawa na neno "rahisi." Linaashiria kwamba hakuna kilichomzuia yeye kuweza kutembea kupitia mkutano wenye hasira.

**alikwenda sehemu nyingine**
"alikwenda mbali" au "alikwenda kwa njia yake" Yesu alikwenda ambako alikuwa kapanga kwenda badala ya ambako watu walijaribu kumlazimisha aende.

## Luke 4:31

**Sentensi Unganishi**
Yesu anakwenda Kapernaumu, anafundisha watu katika Sinagogi huko, na anaamuru mapepo kuondoka kwa mtu.

**Ndipo yeye**
"ndipo Yesu." Hii inaashiria tukio jipya.

**alishuka Kapernaumu**
Kirai hiki "shuka chini" ilitumika hapa sababu Kapernaumu ni chini kuliko Nazarethi.

**Kapernaumu, ni mji katiaka Galilaya**
"Kapernaumu, mji mwingine katika Galilaya"

**liostaajabisha**
"lishangaa sana" au "liovutia sana" au "lioshangaza "

**alizungumza kwa mamlaka**
"alizungumza kama mtu mwenye mamlaka" au "maneno yake yalikuwa na nguvu kubwa"

## Luke 4:33

**Sasa ... alikuwepo mtu**
Kirai hiki kinatumika kudokeza utangulizi wa mhusika mpya ndani ya simulizi; katika suala hili, mtu aliyepagawa pepo.

**ambaye alikuwa na pepo mchafu**
"ambaye alipagawa na pepo mchafu" au "ambaye alitawaliwa na na roho mchafu" (UDB)

**alilia kwasauti ya juu**
"yeye alipiga kelele"

**Tunanini cha kufanya na wewe**
Hili jibu la kichokozi ni nahau ambayo inamaana: "Nini tulichonacho cha kufanana?" au "unahaki gani ya kutusumbua sisi?"

**Nini cha kufanya na wewe, Yesu wa Nazarethi?**
Swali hili lingeandikwa kama sentensi. NI: "Nini wewe, Yesu wa Nazarethi, unataka kutufanyia" au Hakuna chochote cha kufanya na wewe, Yesu wa nazarethi!" au "Huna haki kutusumbua sisi, Yesu wa Nazarethi!"

### Luke 4:35

**Yesu alikemea pepo, akisema**
"Yesu alikemea pepo akisema," au "Yesu bila huruma alisema kwa pepo"

**toka nje yake**
Yeye alimwamuru pepo kutokumtawala mtu. NI: "mwache peke yake" au "usiishi ndani ya mtu huyu tena"

**Haya ni maneno ya aina gani?**
Watu wanadhihirisha jinsi walivyoshangazwa kwamba Yesu anamamlaka kuamuru pepo kumwacha mtu. Hii inaweza kuandikwa kama sentensi. NI: "Haya maneno yanashangaza!" au "maneno yake ya ajabu"

**Anaamuru roho wachafu kwa mamlaka na nguvu**
"Yeye anamamlaka na nguvu kuamuru roho wachafu"

**Habari kumhusu zilianza kuenea ... kanda inayozunguka**
Hii ni amri kuhusu kile kilichotokea baada ya simulizi ambacho kilisababishwa na matukio ndani ya hadithi yenyewe.

**habari kumhusu yeye zilianza kuenea**
"taarifa kuhusu Yesu zilianza kuenea" au "watu walianza kueneza habari kuhusu Yesu"

### Luke 4:38

**Sentensi Unganishi**
Yesu bado yuko Kapernaumu, lakini sasa yuko katika nyumba ya Simoni, alipomponya mama mkwe wa Simoni na watu wengi.

**Ndipo Yesu akaondoka**
Hii inaanzisha tukio jipya

**Mama mkwe wa Simoni**
Mkwe - "mama yake mke wa Simoni"

**Alikuwa anaumwa**
Hii ni nahau inayomaanisha "alikuwa anaugua"

**homa kali**
"mwili wake ulikuwa na joto kali"

**kusihi badala yake**
Maana yake walimwomba Yesu amponye homa yake. Hii inaweza kusemwa wazi. NI: "kumwomba Yesu amponye homa"

**Hivyo alisimama**
Neno "Hivyo" linaweka wazi kwamba alifanya hivi kwa sababu watu walimsihi badala ya mama mkwe wa Simoni.

**alisimama kwake**
"alikwenda kwake na aliegama kwake"

**liikemea homa**
"alisema kwa kuikaripia homa" au "aliamuru homa kumwacha" UDB. Itakuwa ni msaada kusema wazi alichoiambia homa kufanya. NI: "aliiamuru ngozi kupoa" "aliuamuru ugonjwa kumwacha"

**alianza kuwahudumia**
Hapa hii inamaana alianza kuandaa chakula kwaajili ya Yesu na watu wengine ndani ya nyumba.

### Luke 4:40

**alilaza mkono wake juu**
"aliweka mkono wake juu" au "aligusa"

**Pepo pia yakatoka nje**
Hii ilimaanisha kwamba Yesu aliyafanya mapepo yaondoke kwa watu yaliokuwa yamewatawala. Hii inaweza kusemwa wazi. NI: "Yesu pia aliyalazimisha mapepo yatoke"

**analia kwa sauti na akisema**
inamaanisha kitu kilekile, na huenda inarejea kulia kwa hofu au hasira. Baadhi ya tafsiri inatumia neno moja. NI: "paza sauti"

**Mwana wa Mungu**
Hiki ni cheo mhimu kwa Yesu.

**alikemea pepo**
"aliwaambia pepo kwa ukali"

**usingeliwaruhusu**
"Wao hapana kuwaruhusu"

### Luke 4:42

**Sentensi Unganishi:**
Ingawa watu walitaka Yesu abaki Kapernaumu, anakwenda kuhubiri kwenye masinagogi mengine Uyahudi.

**ilipofika mapambazuko**
"wakati wa jua kuchomoza"

**mahali palipo jitenga**
"mahali pa pekee" au "mahali pasipokuwa na watu"

**kwa miji mingi mingine**
"kwa watu katika miji mingine mingi"

**hii ni sababu nilikuwa nimetumwa hapa**
Hii inaweza ikawekwa kwenye kauli tendaji, NI: "hii ni sababu Mungu alinituma hapa mimi"

**Uyahudi**
Tangu Yesu awe Galilaya, neno "Uyahudi" hapa huenda linarejea kwenye ukanda wote ambako Wayahudi waliishi wakati huo, NI: "ambapo waliishi Wayahudi"

---

## Chapter 5

1 Basi ilitokea wakati watu walipomkusanyikia na kumzunguka Yesu na kusikiliza neno la Mungu, ambapo
alikuwa amesimama kando ya ziwa Genesareti. 2 Aliona mashua mbili zimetia nanga pembeni mwa ziwa.
Wavuvi walikuwa wametoka na walikuwa wakiosha nyavu zao. 3 Yesu akaingia katika mojawapo ya zile
mashua, ambayo ilikuwa ya Simoni na kumwomba aipeleke majini mbali kidogo na nchi kavu. Kisha
akakaa na kufundisha kutokea kwenye mashua. 4 kuongea, akamwambia Simoni, "Ipeleke mashua yako
mpaka kwenye kilindi cha maji nakushusha nyavu zako ili kuvua samaki." 5 Simon akajibu na kusema,
Bwana, tumefanya kazi usiku wote, na hatukukamata chochote, lakini kwa neno lako, nitazishusha nyavu.
6 Walipofanya hivyo walikusanya kiasi kikubwa cha samaki na nyavu zao zikaanza kukatika. 7 Hivyo
wakawaashiria washirika wao kwenye mashua nyingine ili waja na kuwasaidia. Walikuja wakazijaza
mashua zote, kiasi kwamba zikaanza kuzama. 8 Lakini Simoni Petro, alipoona hivyo, alianguka magotini
pa Yesu akisema,"Ondoka kwangu, kwa sababu mimi ni mtu mwenye dhambi Bwana." 9 Kwa sababu
alishangazwa, na wote waliokuwa pamoja naye, kwa uvuvi wa samaki waliokuwa wameufanya. 10 Hili
liliwajumuisha Yakobo na Yohana wana wa Zebedayo, ambao walikuwa washirika wa Simoni. Na Yesu
akamwambia Simoni, "Usiogope, kwa sababu kuanzia sasa na kuendelea utavua watu." 11
Walipokwishazileta mashua zao nchi kavu, waliacha kila kitu na kumfuata yeye. 12 Ilitokea kwamba
alipokuwa katika mji mmojawapo, mtu aliyekuwa amejaa ukoma alikuwa huko. Wakati alipomuona Yesu,
alianguka akiinamisha uso kwake mpaka chini na kumuomba, akisema, "Bwana, ikiwa unataka, waweza
kunitakasa." 13 Kisha Yesu alinyoosha mkono wake na kumgusa, akisema, "Nataka. Takasika." Na saa
ileile ukoma ukamwacha. 14 "Alimwagiza asimwambie mtu yeyote, lakini alimwambia, "Nenda zako, na
ukajionyeshe kwa makuhani na utoe sadaka ya utakaso wako, sawasawa na kile Musa alichokiamuru, kwa
ushuhuda kwao." 15 Lakini habari kumuhusu yeye zikaenea mbali zaidi, na umati mkubwa wa watu ukaja
pamoja kumsikiliza akifundisha na kuponywa magonjwa yao. 16 Lakini mara kwa mara alijitenga
faraghani na kuomba. 17 Ilitokea siku moja kati ya hizo siku alikuwa akifundisha, na walikuwapo
Mafarisayo na waalimu wa sheria wamekaa hapo ambao walikuja wakitokea vijiji vingi tofauti katika mkoa
wa Galilaya na Yudea, na pia kutokea katika mji wa Yerusalemu. Nguvu ya Bwana ilikuwa pamoja naye
kuponya. 18 watu kadhaa walikuja, wamembeba kwenye mkeka mtu aliyepooza, na wakatafuta njia ya
kumwingiza ndani ili kumlaza chini mbele ya Yesu. 19 Hawakupata njia ya kumwingiza ndani kwa sababu
ya umati, hivyo walipanda juu ya paa la nyumba na kumshusha yule mtu chini kupitia kwenye vigae, juu
mkeka wake katikati ya watu, mbele kabisa ya Yesu. 20 Akiangalia imani yao, Yesu alisema, "Rafiki,
dhambi zako umesamehewa." 21 Waandishi na Mafarisayo waliaanza kuhoji hilo, wakisema, "Huyu ni nani
anayeongea makufuru? Ni nani anaweza kusamehe dhambi ila Mungu pekee yake?" 22 Lakini Yesu,
akitambua nini walichokuwa wakifikiri, aliwajibu na kuwaambia, "Kwa nini mnaulizana hili mioyoni
mwenu? 23 Kipi ni rahisi kusema, 'Dhambi zako zimesamehewa' au kusema 'Simama utembee?' 24 Lakini
mjue ya kwamba Mwana wa Adamu anayo mamlaka duniani ya kusamehe dhambi, Nakwambia wewe,
'Amka, chukua mkeka wako na uende nyumbani kwako.'" 25 Wakati huo huo akaamka mbele yao na
akachukua mkeka wake aliokuwa ameulalia. Kisha akariudi nyumbani kwake akimtukuza Mungu. 26 Kila
mmoja alishangazwa na wakamtukuza Mungu. Walijawa na hofu, wakisema, "Tumeona mambo yasiyo ya
kawaida leo." 27 Baada ya mambo haya kutokea, Yesu alitoka huko na akamwona mtoza ushuru aliyeitwa
Lawi amekaa eneo la kukusanyia kodi. Akamwambia, "Nifuate." 28 Hivyo Lawi akanyanyuka na kumfuata,
akiacha kila kitu nyuma. 29 Kisha Lawi akaandaa nyumbani kwake karamu kubwa kwa ajili ya Yesu.
Walikuwapo watozaushuru wengi kule na watu wengi walioketi mezani wakila pamoja nao. 30 Lakini
Mafarisayo na waandishi wao walikuwa wakiwanung'unikia wanafunzi, wakisema, "Kwa nini mnakula na
kunywa na watoza ushuru pamoja na watu wengine wenye dhambi?" 31 Yesu akawajibu, "Watu walio
katika afya njema hawahitaji tabibu, ni wale tu wanaoumwa ndiyo watakao mhitaji mmoja. 32 Sikuja
kuwaita watu wenye haki haki wapate kutubu, bali kuwaita wenye dhambi wapate kutubu." 33
Wakamwambia, "Wanafunzi wa Yohana mara nyingi hufunga na kuomba, na wanafunzi wa Mafarisayo nao
hufanya vivyo hivyo. Lakini wanafunzi wako hula na kunywa." 34 Yesu akawaambia, "Inawezekana mtu
yeyote akawafanya waliohudhuria harusi ya Bwana Arusi kufunga wakati Bwana Arusi bado yu pamoja
nao? 35 Lakini siku zitakuja wakati Bwana Arusi atakapoondolewa kwao, ndipo katika siku hizo
watafunga." 36 Kisha Yesu aliongea pia kwao kwa mfano. "Hakuna anayechana kipande cha nguo kutoka
kwenye vazi jipya na kukitumia kurekebisha vazi la zamani. Kama akifanya hivyo, ataichana nguo mpya,
na kipande cha nguo kutoka vazi jipya kisengefaa kutumika na nguo ya vazi la zamani. 37 pia, hakuna mtu
ambaye huweka divai mpya kwenye viriba vikuukuu. Kama akifanya hivyo, divai mpya ingepasua kile
chombo, na divai ingemwagika, na viriba vingeharibika. 38 Lakini divai mpya lazima iwekwe kwenye


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

viriba vipya. 39 Na hakuna mtu baada ya kunywa divai ya zamani, hutataka mpya, kwa sababu husema, 'Ya zamani ni bora."'

---

## Luka 05 Maelezo ya Jumla

### Dhana maalum katika sura hii

#### "Utavua watu"

Agano Jipya mara nyingi huzungumzia juu ya kufanya wanafunzi au wafuasi wa Kristo. Hii ni huduma kuu ya kanisa. Kuna takwimu nyingi tofauti zinazotumiwa kuelezea hii katika Agano Jipya. Katika sura hii, Yesu anatumia mfano wa uvuvi kueleza kuwa wanafunzi wa Kristo wanapaswa kukusanyika watu wengine wawe wanafunzi wa Kristo. Yesu anamsaidia mvuvi Simoni kuvua samaki wengi sana ili kuonyesha kwamba Yesu atawawezesha Simoni na wanafunzi wengine kukusanyika wau wengi kumfuata Kristo. and

#### "Watu wenye dhambi"

Mafarisayo hutaja kundi la watu kuwa "wenye dhambi." Walikuwa wanamaanisha ni watu ambao hawakuwa na nia ya kufuata Sheria ya Musa. Hata hivyo, Luka anatumia neno "wenye dhambi" kama maneno ya kuzihaka, kwa sababu Yesu anasema kwamba alikuja kuwaita wenye dhambi kutubu. Kwa kutaja "wenye dhambi," Yesu alikuwa akimaanisha mtu yeyote mwenye hatia ya dhambi. and

#### Kufunga na Karamu

Kufunga mara nyingi kulifanyika wakati wa toba. Hakukufanyika wakati wa furaha. Kwa kuwa wakati ambapo Yesu alikuwa pamoja na wanafunzi wake ilikuwa wakati wa furaha, aliwaambia kama watafunga kwa wakati hayuko pamoja na wao tena.

### Takwimu muhimu za matamshi katika sura hii

#### Hali ya Kufikiri

Yesu anatumia hali ya kufikiri kuwahukumu Mafarisayo. Kifungu hiki kinajumuisha "watu wenye afya njema" na "watu wenye haki." Hii haimaanishi kwamba kuna watu ambao hawahitaji Yesu. Hakuna "watu wenye haki," kila mtu anahitaji Yesu. (See: and Luke 5:31-32)

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

#### Maelezo yaliyodokezwa

Katika sehemu kadhaa za sura hii mwandishi alidokezea habari fulani ambayo wasomaji wake wa awali wangeelewa na kuwazia. Wasomaji wa kisasa labda hawajui mambo hayo yote, hivyo wanaweza kuwa na shida kuelewa mambo yote yaliyoandikwa na mwandishi. UDB mara nyingi huonyesha jinsi habari hiyo inaweza kutolewa ili wasomaji wa kisasa waweze kuelewa vifungu hivi.

#### Matukio ya zamani

Sehemu za sura hii ni mfululizo wa matukio ambayo tayari yametokea. Katika kifungu fulani, wakati mwingine Luka anaandika kana kwamba matukio yamekwisha kutokea wakati matukio mengine bado yanaendelea (ingawa yamekamilika wakati anaandika). Hii inaweza kusababisha shida katika kutafsiri kwa kuunda utaratibu wa matukio usiofaa. Inaweza kuwa muhimu kufanya haya thabiti kwa kuandika kana kwamba matukio yote yamekwisha kutokea.

#### "Mwana wa Binadamu"

Yesu anajiita mwenyewe kama "Mwana wa Binadamu." Lugha zingine haziwezi kuruhusu mtu kujitaja mwenyewe kama 'mtu wa tatu.'

---

### Luke 5:1

**Kauli Unganishi:**
Yesu anahubiri kutoka katika mtumbwi wa Simoni Petro katika ziwa Genesareti

**Sasa ilitokea**
Kauli hii inatumika hapa kuweka alama kwenye mwanzo wa sehemu mpya ya simulizi. Kama lugha yako inanamna ya kufanya hivi, ungefikiri kutumia hapa.

**ziwa Genesareti**
Hili ni jina lingine la ziwa Galilaya. Galilaya ulikuwa upande magharibi wa ziwa, na na nchi ya Genesareti ulikuwa upande wa mashariki, hivyo ulikuwa unaitwa kwa majina yote.

**kuosha nyavu zao**
Walikuwa wanasafisha nyavu za kuvuvia ili wazitumia tena kupata samaki.

**mitumbwi mmoja ambao ulikuwa wa Simoni**
"mtumbwi unaomilikiwa na simoni"

**akamwambia kuweka kwenye maji mbali kidogo kutoka kwenye ardhi**
"alimwambia Petro kuusukuma mtumbwi zaidi kutoka ufuoni"

**aliketi na akawafundisha watu**
kuketi ilikuwa ni mfumo wa kawaida kwa mwalimu.

**aliwafundisha watu tokea kwenye mtumbwi**
"aliwafundisha watu akiwa amekaa kwenye mtumbwi." Yesu alikuwa katika mtumbwi mbali kidogo kutoka ufuoni na alikuwa anaongea na watu ambao walikuwa kwenye ufuo.

### Luke 5:4

**Alipokwisha kumaliza kuzungumza**
"Yesu alipomaliza kuwafundisha watu"

**ya maneno yako**
"kwa sababu ya maneno yako" au "kwa sababu umeniambia kufanya hivi"

**walipunga**
walikuwa mbali sana kutoka ufuoni hivyo walifanya ishara, huenda kupunga mikono.

**walianza kuzama**
"mtumbwi ulianza kuzama." "mtumbwi ulianza kuzama kwa sababu samaki walikuwa wazito sana."

### Luke 5:8

**alianguka chini magotini pa Yesu**
Maana zinazowezekana ni 1) "kuinama chini magotini pa Yesu" au 2) kulala chini miguuni ya ardhi miguuni pa Yesu" 3) "kupiga magoti mbele ya Yesu." Yesu hakuanguka kwa bahati mbaya. Yeye alifanya hivi kama ishara ya unyenyekevu na heshima kwa Yesu.

**mtu mwenye dhambi**
Neno hapa kwa "mtu" linamaanisha "mtu mzima mwanaume" na kwa ujumla zaidi "binadamu."

**kamata samaki**
"idadi kubwa ya samaki"

**washirika pamoja na Simoni**
"Wadau wa Simoni katika biashara ya uvuvi"

**utakamata watu**
Sura ya kukamata samaki imekuwa ikitumika kama sitiari kwa kukusanya watu kumfuata Kristo. NI: "utavua watu" au "mtakusanya watu kwaajili yangu" au "mtaleta watu kuwa wanafunzi"

### Luke 5:12

**Sentensi Unganishi**
Yesu anamponya mkoma katika mji tofauti ambao hautajwi jina.

**Ikawa**
Kauli hii inaonesha tukio jipya katika simulizi.

**mtu aliyejaa ukoma**
"mtu alikuwa anaukoma." Hii inatambulisha mhusika mpya kwenye simulizi.

**akaangukia kichwa**
"alipiga magoti na kichwa kikagusa chini" au "aliinama mpaka chini" (UDB)

**kama uko tayari**
"kama unataka"

**unaweza ukanifanya msafi**
ilifahamika kwamba yeye alikuwa anamuuliza Yesu aponywe. Hii inaweza ikasemwa wazi. NI: tafadhali nisafishe, sababu unaweza

**nifanye msafi ... uwe safi**
Hii inarejea kwenye usafi wa ibada, lakini ilifahamika kwamba yeye si msafi kwasababu ya ukoma. Yeye hasa anamuuliza Yesu amponye maradhi yake. Hii inaweza kusemwa wazi. NI: "niponye ukoma hivyo nitakuwa msafi ... upone"

**ukoma ukamwacha**
"hakuwa naukoma tena" (UDB)

### Luke 5:14

**kutomwambia mtu**
Hii tafsiri inaweza ikanukuiwa moja kwa moja. "kutomwambia mtu kwamba wewe umeponywa." Ni "Kutokusema kwa yeyote."

**dhabihu kwa utakaso wako**
Sheria inamtaka mtu kufanya dhabihu maalumu baada ya utakaso wao. Hii ilimruhusu mtu kuwa safi

kitaratibu, na kuweza tena kushiriki katika desturi kidini.

**kwa ushuhuda**
"Hii inathibitisha uponyaji wako""

**Kwao**
Maana zinazowezekana 1) "kwa makuhani" 2) "kwa watu wote"

### Luke 5:15

**Taarifa kumhusu yeye**
"habari kuhusu Yesu." Hii pengine ingemaanisha "taarifa kuhusu uponyaji mtu kwa Yesu" au "taarifa kuhusu Yesu kuponya watu."

**taarifa kuhusu yeye zilisambaa zaidi na zaidi**
"taarifa kuhusu yeye zilizagaa sana" au "watu waliendelea kuzisema habari kuhusu yeye katika maeneo mengine"

**maeneo yaliyotengwa**
"maeneo ya pekee" au "maeneo ambapo hapakuwa na watu wengine"

### Luke 5:17

**Kauli Unganishi:**
Siku moja Yesu alipokuwa akifundisha katika jengo, baadhi ya watu walimleta mtu aliyepooza kwaajili Yesu kumponywa.

**Ilitokea**
Kauli hii inaonesha mwanzo wa sehemu mpya katika simulizi.

### Luke 5:18

**Sasa baadhi ya watu wakaja**
Hawa ni watu wapya katika simulizi. Lugha yako inaweza kuwa na njia ya kuonesha kwamba hawa ni watu wapya. "kulikuwa na watu ambao walikuja."

**godoro**
"kitu cha kulalia" au "kitu cha kuunyosha mwili"

**alikuwa amepooza**
"hangeweza kuondoka mwenyewe"

**Wasingeweza kupata njia ya kumleta ndani kwa sababu ya kusanyiko, hivyo**
Katika baadhi ya lugha inaweza inaweza ikawa kiasili ukirekebishwa. "Lakini kwa sababu ya mkutano wa watu, wasingepata njia kumleta mtu ndani"

**kwasababu ya mkutano**
Ni wazi kwamba sababu iliyowafanya wasiweze kuingia ilikuwa hadhara kubwa sana pale hapakuwa na nafasi kwaajili yao.

**walikwenda juu hadi juu kabisa ya nyumba**
Nyumba zilikuwa na dari, na baadhi ya nyumba zilikuwa na ngazi au kipandio (daraja) cha kurahisisha kupanda kule juu.

**mbele ya Yesu kabisa**
"mbele ya Yesu moja kwa moja" au "kwa haraka mbele ya Yesu"

### Luke 5:20

**angalia imani yao, Yesu alisema**
ilieleweka kwamba walimwamini Yesu anaponya mtu aliyepooza. NI: "Yesu alipotazama kwamba wanaamini kwamba anaweza kumponya mtu, alimwambia "

**Mwanadamu**
Hili ni neno lililotumika kwa ujumla ambalo watu walitumia walipokuwa wakizungumza mtu na ambaye jina lake hawakulijua. ilikuwa siadabu, lakini pia haikuonesha heshima maalumu. Baadhi ya lugha ziliweza kutumia neno kama "rafiki" au "mkuu."

**dhambi zako zimesamehewa**
"umesamehewa" au "nasamehe dhambi zako"

**hoji hiki**
"jadili hili" au "toa hoja kuhusiana na hili." NI: "pengine jadili hata siyo Yesu alikuwa na mamlaka ya kusamehe dhambi."

**Nani huyu ambaye anasema kufuru?**
Swali hili linaonesha jinsi walivyoshituka na kukasirika kwa kile ambacho Yesu alisema. "Mtu huyu anamkufuru Mungu" au "Yeye anamkufuru Mungu kwa kusema hivyo"

**Nani anayeweza kusamehe dhambi, lakini Mungu pekee?**
Inachodokeza taarifa ni kwamba kama mtu anadai kusamehe dhambi anasema ni Mungu. "Hakuna anayeweza kusamehe dhambi lakini Mungu pekee" au "ni Mungu pekee ambaye anaweza kusamehe dhambi."

### Luke 5:22

**kutambua walichokuwa wanafikiri**
Kirai hiki kinaashiria kwamba walikuwa wanahojiana kimya kimya, hivyo kwamba Yesu alitambua zaidi na alisikia walichokuwa wanfikiri.

**Kwa nini mnaulizana hili mioyoni mwenu**
Msingepaswa kusema hivi mioyoni mwenu " au"Msingepaswa kutia shaka kwamba nina mamlaka ya kusamehe dhambi"

**Mioyoni mwenu**
Hii inarejea sehemu ya mtu ambayo hufikiri au huamini.

**rahisi kusema**
Kitu ambacho hakipo wazi ni kimoja. "Ni rahisi kusema, sababu hakuna mmoja atakayejua, lakini kitu kingine ni "kigtumu kusema sababu kila mmoja atajua". watu wasione kama mtu dhambi zako zimesamehewa, 'lakini Mungu pekee anaweza sababisha huyu mlemavu kusimama na kutembea."

**mnaweza kujua**
Yesu alikuwa akiongea kwa Waandishi na Mafarisayo. Neno "enyi" ni wingi.

**Mwana wa Adam**
Yesu alikuwa akirejea yeye peke yake

**Nasema kwenu**
Yesu alikuwa akisema haya kwa mtu aliyepooza .Neno "wewe" ni umoja

### Luke 5:25

**kwa haraka**
"mara moja"njia sahihi"

**akainuka**
Inaweza kusaidia kusema kwa wazi kwamba aliponywa. NI: "mtu aliponywa! akainuka."

**kujawa na hofu**
"hofu sana"au" kujawa na utisho"

**vitu vinavyozidi vya kawaida**
"vitu vya kushangaza "au" vitu vigeni"

### Luke 5:27

**Sentensi Unganishi:**
Yesu alipoondoka nyumbani, anamwita Lawi, Myahudi mtoza ushuru amfuate. Lawi anaandaa mlo kwaajili ya Yesu uliowakera mafarisayo na waandishi.

**Baada ya mambo hayo kutokea**
Kirai "vitu hivi" kinamaanisha kilichotokea kwenye mistari iliyopita. Ishara hii ni tukio jipya.

**akamwona mtoza ushuru**
"akamwangalia mtoza ushuru kwa umakini "au" alimwangalia mtoza ushuru kwa uangalifu"

**Nifuate**
Kufuata mtu ilikuwa ni kauli imaanishayo kuwa mwanafunzi. NI: "Kuwa mwanafunzi wangu "au" njoo, nifuate kama mwalimu wako"

**Acha vyote nyuma**
"akaacha kazi yake kama mtoza ushuru"

### Luke 5:29

**Sentensi Unganishi**
Chakulani, Yesu anazungumza na Mafarisayo na waandishi.

**Nyumbani mwake**
"kwenye nyumba ya Lawi"

**walioketi mezani**
Aina ya Kigiriki ya kula kwenye karamu ilikuwa kuegemea kochi na kujihimili peke yako kwa mkono wa kushoto kwenye baadhi ya mito ." au " "kwenye meza"kukaa mezani"

**kwa wanafunzi wake**
"kwa wanafunzi wa Yesu"

**Kwa nini unakula ... kwa mtu mwenye dhambi?**
Mafarisayo na Waandishi waliuliza haya kudhihirisha kutoridhishwa kwao kwamba Yesu na wanafunzi wake walikuwa wanakula na wenye dhambi. NI: "Huwezi kula na wenye dhambi!"

**mnakula na kunywa pamoja ... watu wenye dhambi**
Mafarisayo na waandishi waliamini kwamba watu wa dini wanapaswa kujitenga na watu waliowaona kuwa ni wenye dhambi. Neno "wewe" ni wingi.

**Watu ambao ni wazima ... wagonjwa**
Yesu anadhihirisha hii kama mithali.

**Tabibu**
daktari atibuye " au" daktari"

**ni ambao wanaumwa tu**
Maneno "inahitaji" yanaeleweka kutoka kirai kilichotangulia. NI: "ni wale wagojwa tu wanamwitaji"

**watu wenye haki**
Baadhi ya watu walifikiri wanahaki. Yesu anarejea kwa hao kwa namna walivyofikiri kuhusu wao wenyewe ingawaje alijua kwamba hawakuwa wenye haki. NI: "watu wafikirio wanahaki"

### Luke 5:33

**Akawaambia**
"Viongozi wa dini wakasema kwa Yesu"

**inawezekana yeyote akafanya ... pamoja nao?**
Yesu alitumia swali kusababisha watu kufikiri kuhusu hali ambayo tayari wanaijua."Hakuna mmoja wenu anawaambia waliohudhuria harusini kufunga wakati bado Bwana arusi yupo nao."

**waliohudhuria harusini**
"wageni" au "marafiki. "Hawa ni marafiki ambao husherehekea na mtu ambaye anafunga ndoa.

**waalikwa wa bwana arusi wanafunga**
kufunga ni ishara ya huzuni. Viongozi wa dini walielewa kwamba waalikwa arusini hawawezi kufunga wakati bwana arusi akiwa pamoja nao.

**siku zitakuja**
"upesi" au siku hizo" (UDB)


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**Bwana Arusi atakapoondolewa kwao.**
Yesu anajifananisha yeye mwenyewe na bwana arusi, wanafunzi wake ni waalikwa arusini. Hakufafanua sitiari, hivyo tafsiri ieleze kama ni lazima tu.

## Luke 5:36

**Taarifa kwa ujumla**
Yesu anasema habari kwa waandishi na mafarisayo waliokuwa nyumbani kwa Lawi.

**Hakuna mtu huchana**
"Hakuna mmoja hupasua " au" mtu hachani kamwe"

**kama alifanya hivyo**
Kauli hii tete inaelezea sababu kwa nini mtu hatarekebisha vazi kwa njia hiyo.

**kurekebisha**
"karabati"

**kisingefaa**
"kisingeweza kukubaliana " au" kisingekuwa sawa"

## Luke 5:37

**Hakuna mtu awekae**
"Mtu hawezi kuweka "au" hakuna hata mmoja huweka"

**Divai mpya**
"juisi ya dhabibu."Hii inamaanisha divai ambayo bado hajachachishwa."

**Kiriba**
Hii ni mifuko iliyotengenezwa kwa ngozi ya mnyama. Ingeweza kuitwa mifuko ya divai "au "mifuko iliyotengenezwa kwa ngozi."

**kiriba kipya kingepasua ngozi**
Kipindi divai mpya inachana na kuvutika, inapasua ngozi ya zamani kwa sababu hata hivyo hunyooka. Wasikilizaji wa Yesu walielewa taarifa zihusuzo divai iliyochachishwa na kuvutika.

**Divai ingevuja**
"Divai ingevuja nje ya mifuko"

**viriba vipya**
"viriba vipya " au "mifuko mipya ya divai."Hii inamaanisha viriba vipya vya divai, visivyotumika.

**kunywa divai ya zamani ... anataka mpya**
Sitiari hii inakanusha mafundisho ya zamani ya viongozi wa dini ni kinyume na mafundisho mapya ya Yesu. Dokezo ni kwamba watu ambao walizoea mafundisho ya zamani hawako tayari kusikiliza vitu vipya ambavyo Yesu anafundisha.

**Divai ya zamani**
"divai ambayo imechachishwa"

**Anasema cha zamani ni bora**
Itasaidia kwa kuongeza: na "hata hivyo tayari kujaribu divai mpya.

## Chapter 6

1 Sasa ilitokea kwenye Sabato kwamba Yesu alikuwa akipita katika ya shamba la nafaka na wanafunzi
wake walikuwa wakichuma masuke, wakayasuguasugua kati ya mikono yao wakala nafaka. 2 Lakini
baadhi ya Mafarisayo wakasema, "Kwa nini mnafanya kitu ambacho si halali kisheria kukifanya siku ya
sabato"? 3 Yesu, akawajibu, akisema, "Hamkuwahi kusoma kile Daudi alifanya alipokuwa na njaa, yeye na
wanaume waliokuwa pamoja naye? 4 Alikwenda katika nyumba ya Mungu, na akachukuwa mikate
mitakatifu na kuila baadhi, na kuitoa baadhi kwa watu aliokuwa nao kuila, hatakama ilikuwa halali kwa
makuhani kuila." 5 Kisha akawaambia, "Mwana wa Adamu ni Bwana wa Sabato." 6 Ilitokea katika Sabato
nyingine kwamba alikwenda ndani ya sinagogi na kuwafundisha watu huko. Palikuwa na mtu ambaye
mkono wake wa kulia ulikuwa umepooza. 7 Waandishi na Mafarisayo walikuwa wanamwangalia kwa
makini kuona kama angemponya mtu siku ya Sabato, ili waweze kupata sababu ya kumshtaki kwa
kufanya kosa. 8 Lakini alijua nini walikuwa wanafikiri na akasema kwa mtu aliyekuwa amepooza mkono,
"Amka, simama hapa katikati ya kila mmoja." Hivyo huyo mtu akanyanyuka na kusimama pale. 9 Yesu
akasema kwao, "Nawauliza ninyi, ni halali siku ya Sabato kufanya mema au kufanya madhara, kuokoa
maisha au kuyaharibu?" Kisha aliwaangalia wote na kumwambia yule mtu, 10 "Nyoosha mkono wako."
Akafanya hivyo, na mkono wake ulikuwa umeponywa. 11 Lakini walijawa na hasira, wakaongeleshana wao
kwa wao kuhusu nini wanapaswa wafanye kwa Yesu. 12 Ilitokea siku hizo kwamba alikwenda mlimani
kuomba. Aliendelea usiku mzima kumuomba Mungu. 13 Ilipokuwa asubuhi, aliwaita wanafunzi wake
kwake, na akawachagua kumi na wawili kati yao, ambao pia aliwaita "mitume." 14 Majina ya wale mitume
yalikuwa Simoni (ambaye pia alimwita Petro) na Andrea ndugu yake, Yakobo, Yohana, Filipo,
Bartolomayo, 15 Mathayo, Tomaso na Yakobo mwana wa Alfayo, Simoni, ambaye aliitwa Zelote, 16 Yuda
mwana Yakobo na Yuda Iskariote, ambaye alikuwa msaliti msaliti. 17 Kisha Yesu alitelemka pamoja nao
toka mlimani na kusimama mahali tambarare. Idadi kubwa ya wanafunzi wake walikuwa huko, pamoja na
idadi kubwa ya watu kutoka Uyahudi na Yerusalemu, na kutoka pwani ya Tiro na Sidoni. 18 Walikuja
kumsikiliza na kuponywa magonjwa yao. Watu waliokuwa wakisumbuliwa na pepo wachafu waliponywa
pia. 19 Kila mmoja kwenye hilo kusanyiko alijaribu kumgusa kwa sababu nguvu za uponyaji zilikuwa
zikitokea ndani yake, na aliwaponya wote. 20 Kisha akawaangalia wanafunzi wake, na kusema,
"Mmebarikiwa ninyi mlio maskini, kwa maana ufalme wa Mungu ni wenu. 21 Mmebarikiwa ninyi mlio na
njaa sasa, kwa maana mtashibishwa. Mmebarikiwa ninyi mliao sasa, kwa maana mtacheka. 22
Mmebarikiwa ninyi ambao watu watakapowachukia na kuwatenga na kuwashutumu ninyi kwamba ni
waovu, kwa ajili ya Mwana Adamu. 23 Furahini katika siku hiyo na kurukaruka kwa furaha, kwa sababu
hakika mtakuwa na thawabu kubwa mbinguni, kwa maana baba zao waliwatendea vivyohivyo manabii. 24
Lakini ole wenu mlio matajiri! Kwa maana mmekwisha pata faraja yenu. 25 Ole wenu mlio shiba sasa!
Kwa maana mtaona njaa baadaye. Ole wenu mnaocheka sasa! Kwa maana mtaomboleza na kulia baadaye.
26 Ole wenu, mtakaposifiwa na watu wote! Kwa maana baba zao waliwatendea manabii wa uongo
vivyohivyo. 27 Lakini nasema kwenu ninyi mnaonisikiliza, wapendeni adui zenu na kufanya mema kwa
wanao wachukieni. 28 Wabarikini wale wanao walaani ninyi na waombeeni wale wanaowaonea. 29 Kwake
yeye akupigaye shavu moja, mgeuzie na la pili. Kama mtu akikunyang'anya joho lako usimzuilie na kanzu.
30 Mpe kila akuombaye. Kama mtu akikunyang'anya kitu ambacho ni mali yako, usimuombe akurudishie.
31 Kama mpendavyo watu wawatendee, nanyi watendeeni vivyo hivyo. 32 Kama mkiwapenda watu
wawapendao ninyi tu, hiyo ni thawabu gani kwenu? Kwamaana hata wenye dhambi huwapenda wale
wawapendao. 33 Kama mkiwatendea mema wale wanaowatendea ninyi mema, hiyo ni thawabu gani
kwenu? Kwa maana hata wenye dhambi hufanya vivyo hivyo. 34 Kama mkikopesha vitu kwa watu ambao
mnategemea watawarudishia, hiyo ni thawabu gani kwenu? Hata wenye dhambi huwakopesha wenye
dhambi, na hutegemea kupokea kiasi hicho hicho tena. 35 Lakini wapendeni adui zenu na watendeeni
mema. Wakopesheni na msihofu kuhusu kurudishiwa, na thawabu yenu itakuwa kubwa. Mtakuwa wana
wa Aliye Juu, kwasababu yeye mwenyewe ni mwema kwa watu wasio na shukurani na waovu. 36 Iweni na
huruma, kama Baba yenu alivyo na huruma. 37 Msihukumu, nanyi hamta hukumiwa. Msilaani, nanyi
hamtalaaniwa. Sameheni wengine, nanyi mtasamehewa. 38 Wapeni wengine, nanyi mtapewa. Kiasi cha
ukarimu - kilichoshindiliwa, kusukwasukwa na kumwagika - kitamwagika magotini penu. Kwa sababu kwa
kipimo chochote mnachotumia kupimia, kipimo hicho hicho kitatumika kuwapimia ninyi." 39 Kisha
akawaambia mfano pia. "Je mtu aliye kipofu aweza kumwongoza mtu mwingine kipofu? Kama alifanya
hivyo, basi wote wangalitumbukia shimoni, je wasingetumbukia? 40 Mwanafunzi hawi mkubwa kuliko
mwalimu wake, lakini kila mtu akiisha kufundishwa kwa ukamilifu atakuwa kama mwalimu wake. 41 Na
kwa nini basi wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti lililo ndani ya jicho lako

huliangalii? 42 Utawezaje kumwambia ndugu yako, 'Ndugu, naomba nikitoe kibanzi kilicho ndani ya jicho
lako,' nawe huangalii boriti iliyo katika jicho lako mwenyewe? Mnafiki wewe! Kwanza itoe boriti katika
jicho lako mwenyewe, ndipo utaona vizuri kutoa kibanzi katika jicho la ndugu yako. 43 Kwa sababu
hakuna mti mzuri uzaao matunda mabaya, wala hakuna mti mbaya uzaao matunda mazuri. 44 Kwa sababu
kila mti hutambulika kwa matunda yake. Kwa sababu watu hawachumi tini kutoka kwenye miba, wala
hawachumi zabibu kutoka kwenye michongoma. 45 Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa
yaliyo mema, na mtu mwovu katika hazina mbovu ya moyo wake hutoa yaliyo maovu. Kwa sababu kinywa
chake husema yale yaujazayo moyo wake. 46 Kwanini mnaniita, 'Bwana, Bwana', na bado hamyatendi yale
nisemayo? 47 Kila mtu ajaye kwangu na kuyasikia maneno yangu na kuyatendea kazi, nitawaonyesha jinsi
alivyo. 48 Anafanana na mtu ajengae nyumba yake, ambaye huchimba chini sana, na kujenga msingi wa
nyumba juu ya mwamba imara. Mafuriko yalipokuja, maporomoko ya maji yaliipiga nyumba, lakini
hayakuweza kuitikisa, kwa sababu ilikuwa imejengwa vizuri. 49 Lakini yeyote asikiaye neno langu na
hakulitii; mfano wake ni mtu aliyejenga nyumba juu ya ardhi pasipokuwa na msingi, mto ulipoishukia kwa
nguvu, nyumba ile ilitopata maangamizi makubwa.

---

## Luka 06 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

Luka 6:20-49 ina baraka na ole nyingi ambazo zinaonekana kuwa sawa na Mathayo 5-7. Sehemu hii ya Mathayo kwa kawaida inaitwa "Mahubiri ya Mlimani." Katika Luka, hayashikamani na mafundisho juu ya ufalme wa Mungu kama katika injili ya Mathayo.

### Dhana maalum katika sura hii

#### "Kula nafaka"

Ilikuwa nazoezi yaliokubaliwa kwa wasafiri kuchuma na kula kiasi kidogo cha nafaka kutoka kwa mimea katika mashamba waliyoyapitia. Sheria ya Musa ililazimisha walimaji waruhusu wasafiri hivyoo. Wafarisay waliwaza kama kuchuma nafaka ni kazi ya "kukusanya masuke yaiyobaki" na sheria ya Musa inazuia kufanya kazi kwa siku ya Sabato. , and )

### Takwimu muhimu za matamshi katika sura hii

#### Maneno yanayoonyesha mfano

Ilikuwa kawaida kwa Yesu kutumia maneno ya mifano kwa kufundisha watu ukweli usiyo rahisi wa kiroho.

#### Maswali ya uhuishaji

Yesu alitumia maswali ya uhuishaji ili kuwafundisha watu na kuwahukumu.

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

#### Maelezo yaliyodokezwa

Mara nyingi Luka anaandika habari yaliyoelewa kabisa na watu wa kale wa inchi za Mashariki ya Karibu lakini labda watu wa leo wa mazoezi tofauti hawaelewi. kwa mfano watu wanatarajia siku ya hukumu ya mwisho au labda hukumu kwa siku ya mwisho ya maisha yao

#### Wanafunzi kumi na wawili

Yafuatayo ni orodha ya wanafunzi kumi na wawili: Katika Mathayo: Simoni (Petro), Andrea, Yakobo mwana wa Zebedayo, Yohana mwana wa Zebedayo, Filipo, Bartholomayo, Tomasi, Mathayo, Yakobo mwana wa Alfayo, Thadayo, Simoni mzeloti na Yuda Iskarioti.

Katika Marko: Simoni (Petro), Andrea, Yakobo mwana wa Zebedayo na Yohana mwana wa Zebedayo (ambaye aliwaita Boanerge, yaani, wana wangurumo), Filipo, Bartholomayo, Mathayo, Tomasi, Yakobo mwana wa Alfayo, Thadayo, Simoni mzeloti, na Yuda Isikarioti.

Katika Luka: Simoni (Petro), Andrea, Yakobo, Yohana, Filipo, Bartholomayo, Mathayo, Tomasi, Yakobo mwana wa Alfayo, Simoni (aitwaye mzeloti, Yuda mwana wa Yakobo, na Yuda Isikarioti.

Inawezekana kuwa Thadayo na Yuda, mwana wa Yakobo, ni majina mawili ya mtu mmoja.

---

## Luke 6:1

**Sentensi Unganishi:**
Sasa Yesu na wanafunzi wake wanatembea kupitia kwenye shamba la ngano wakati baadhi ya mafarisayo wanaanza kuwauliza wanafunzi kuhusu walichokuwa wanafanya siku ya sabato ambayo katika sheria ya Mungu imetengwa kwaajili ya Mungu.

**Taarifa kwa Ujumla**
Neno "wewe" hapa ni wingi, na linarejea kwa wanafunzi.

**sasa ikatokea**
Kirai hiki kilitumika hapakuzingatia mwanzo wa sehemu mpya ya masimulizi. Ikiwa lugha yako ni njia ya kufanya hivi, ingeweza kutumika hapa.

**masuke**
Kwa suala hili, hizi ni sehemu kubwa za nchi ambapo watu walikuwa wametawanya mbegu pawe na ngano nyingi.

**juu ya ngano**
Hii ni sehemu ya juu ya mmea wa ngano, ambao ni aina jani kubwa. inashikilia mbegu inayoota ya mmea.

**kufikicha katikati ya mikono yao**
Walifanya hivi kutenganisha ngano. NI: "Walifikicha ngano katika mikono yao kutenganisha ngano na ganda" (UDB)

**Kwa nini mnafanya vitu ambavyo ni kinyume kufanya siku ya sabato?**
Hili ni swali linalowatuhumu wanafunzi kwa kuvunja sheria. NI: "Kuchuma nafaka siku ya sabato ni kinyume na sheria ya Mungu!"

**kufanya kitu fulani**
Mafarisayo waliona hata kitendo kidogo cha kufikicha ngano kuwa ni kazi ivunjayo sheria. NI: "kufanya kazi"

## Luke 6:3

**Hamkuwahi hata kusoma ... yeye?**
Yesu anawakemea mafarisayo kwaajili ya kutojifunza maandiko. Hii inaweza kuandikwa kama sentensi NI: "Mtajifunze kutokana na yale mliyo soma .... yeye"

**Mkate wa wonyesho**
"Mkate mtakatifu " au "mkate ambao uliokuwa ukitolewa sadaka kwa Mungu"

**Mwana wa Adam**
Yesu alikuwa anarejea yeye peke yake. 'Mimi' Mwana wa Adam. NI: "Mimi, Mwana wa Adamu"

**ni Bwana wa Sabato**
Cheo "Bwana" hapa inasisitiza mamlaka juu ya Sabato. NI: "ana mamlaka kutambua kipi ni sahihi kwa mtu kufanya siku ya sabato!"

## Luke 6:6

**Sentensi Unganishi:**
Waandishi na Mafarisayo wanatazama Yesu anaponya mtu siku ya Sabato

**Taarifa kwa Ujumla**
Hapa sasa ni siku ya Sabato nyingine na Yesu yuko kwenye Sinagogi.

**Ilitokea**
Kirai hiki kimetumika hapa kuzibgatia mwanzo wa tukio jipya katika masimulizi.

**Mtu alikuwa pale**
Hii inatambulisha mhusika mpya kwenye simulizi.

**mkono wake umepooza**
mkono wa mtu ambaye umepata umeadhirika kiasi ambachomhawezi kuunyoosha. Ulikuwa umejikunja kwenye eneo la ngumi, ikaufanya uonekane mdogo na wenye kupinda.

**walikuwa wanamuangalia kwa karibu**
"walikuwa wanamuangalia Yesu kwa makini"

**ili waweze kupata**
"kwa sababu walitaka kutafuta"

**katikati ya kila mmoja**
"mbele ya kila mtu" (UDB). Yesu alimtaka yule mtu kusimama ambapo kila mmoja angemuona.

## Luke 6:9

**Kwao**
"kwa Mafarisayo"

**ni halali ... okoa maisha ... iharibu?**
Yesu alitaka kuwasahihisha Mafarisayo wajuao kwamba ni kosa kuponya siku ya Sabato. Aliuliza swali kama kupinga kati ya kufanya wema au uovu ili kwamba iwe wazi kipi ni sahihi na kipi ni kibaya. NI: "tendo lipi ambalo sheria inaruhusu - kufanya wema na kuponya, au kuumiza na kuharibu maisha?"

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**kufanya mema au kufanya madhara**
"kusaidia mtu au kumdhuru mtu"

**Nyoosha mkono wako**
"Shikilia mkono wako" au" panua mkono wako"

**alirejeshwa**
"aliponywa"

### Luke 6:12

**taarifa kwa Ujumla**
Yesu anachagua mitume kumi na wawili baada ya kuomba usiku mzima.

**Ikatokea katika siku hizo**
kirai hiki kimetumika hapa kuashiria mwanzo wa kipande kipya cha masimulizi.

**katika siku hizo**
"katika wakati huo" au"sio mbali baada ya hapo " au" siku moja katikati ya hapo"

**alikwenda nje**
"Yesu alikwenda nje"

**ilipokuwa siku**
"ilipokuwa asubuhi" au "siku iliyofuata"

**Aliwachagua kumi na wawili miongoni mwao**
"aliwachagua kumi na wawili kati ya wanafunzi"

**"ambao pia aliwaita mitume"**
"ambao aliwafanya mitume" au "na alipowateua wao kuwa mitume."

### Luke 6:14

**majina ya mitume yalikuwa**
Hizi ni taarifa zimeongezwa kwenye mstari wa ULB

**ndugu yake Andrea**
"kaka yake Simoni, Andrea"

**Zelote**
inawezekana maana 1) "Zelote" ni cheo kinacho onesha alikuwa sehemu ya kundi la watu waliotaka kuwaacha huru Wayahudi kutoka utawala wa Rumi NI: "mzalendo" au "mtaifa" au 2) "mwenye bidii" ni maelezo yanayoashiria alikuwa na bidii kwaajili ya Mungu kuheshimiwa. NI: "shauku"

**kuwa msaliti**
Inaweza kuwa lazima kueleza nini maana ya "msaliti" katika mkutadha huu. NI: "aliwasaliti rafiki zake" au "aliwageuka rafiki zake mbele ya maadui" (kawaida kwa kurudisha fedha alizolipwa" au "kumweka rafiki katika hatari kwa kuwaambia maadui kuhusu yeye"

### Luke 6:17

**Sentensi Unganishi:**
Ingawa Yesu akiwaelekea hasa wanafunzi wake, walikuwapo watu wengi karibu ambao wanasikiliza.

**pamoja nao**
"pamoja na kumi na wawili aliowachagua" au "pamoja na mitume wake kumi na wawili"

**waliponywa**
Hii inaweza kusema katika kauli tendaji "kwa Yesu kuwaponya wao"

**waliokuwa wakisumbuliwa na roho wachafu pia walipona**
Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji. NI: "Yesu pia aliwaponya watu walisumbuliwa na roho wachafu."

**waliosumbuliwa na roho wachafu**
"sumbuliwa na roho chafu" au waliotawaliwa na roho chafu"

**nguvu za kuponya zilikuwa zikimtoka**
Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji NI: "alikuwa na nguvu kuponya watu" au "alitumia nguvu zake kuponya watu"

### Luke 6:20

**Ninyi mmebarikiwa**
Kirai hiki kimerudia mara tatu. Kila mara ,kinaashiria kwamba Mungu huwapa neema watu fulani au kwamba hali zao ni chanya au nzuri.

**Mmebarikiwa ninyi mlio maskini**
"Wale ambao ni maskini hupokea neema ya Mungu" au " ambao ni maskini hunufaika"

**Kwa maana ufalme wa Mungu ni wenu**
Lugha ambazo hazina neno ufalme laweza sema, "Mungu ni mfalme wako" au "kwa sababu Mungu ni mtwala wako."

**Ufalme wako ni wa Mungu**
"ufalme wa Mungu ni wako." Hii ingeweza kumaanisha 1) "umetokana na ufalme wa Mungu" au 2) Utakuwa na mamlaka katika ufalme wa Mungu."

**Mtacheka**
"Mtacheka na kufurahia" au "Mtakuwa na furaha"

### Luke 6:22

**Mmebarikiwa ninyi**
"Mmepokea neema ya Mungu" au "Mnanufaika" au "Ni kwa namna gani ni nzuri kwenu"

**Kuwatenga ninyi**
"kuwakataa ninyi"

**Kwa ajili wa Mwana wa Adam**
"kwa sababu mnajumuika na Mwana wa Adam" au" kwa sababu walimkataa Mwana wa Adam "

**Siku hiyo**
"Kipindi wanafanya mambo hayo" au "kipindi yanatokea"

**vuna kwa furaha**
Nahau hii inamaanisha "kuwa na furaha zaidi"

**dhawabu kubwa**
"malipo makubwa" au "zawadi nzuri"

### Luke 6:24

**Ole wenu**
"jinsi gani kwenu ni hatari." Kirai hiki kimerudia mara tatu. Ni kinyume cha "mmebarikiwa ninyi" Kila mara, kinaashiria kwamba hasira ya Mungu ni moja kwa moja kwa watu, au kwamba kitu hasi au kibaya kinawasubiri.

**ole wenu ninyi mlio matajiri**
namna gani balaa ni wale ambao ni matajiri" au "shida zitakuja kwa wale ambao ni matajiri"

**Mfariji wenu**
"mfariji wenu" au "kinacho waridhisha ninyi" au "kinacho wafanya mwe na furaha"

**Mlio shiba sasa**
"ambao matumbo yao yameshiba sasa" au "ambaye hula kingi sasa"

**wanao cheka sasa**
"ambaoana furaha sasa."

### Luke 6:26

**Ole wenu**
"ni gani balaa gani litakuwa kwenu" au "jinsi mtakavyo kuwa na huzuni"

**Kipindi wanadamu wote**
kipindi watu wote" au "kipindi kila mmoja"

**hivyo ndivyo wahenga waliwafanya manabii wa uongo**
"walinena vizuri juu ya manabii wa uongo"

### Luke 6:27

**Sentensi Unganishi:**
Yesu anaendelea kuzungumza kwa wanafunzi wake na vile vile na mkutano wanao msikiliza yeye.

**kwenu mnaosikiliza**
Yesu sasa anaaza kuzungumza kwa hadhara yote, zaidi kuliko kwa wanafunzi wake tu.

**penda ... fanya mema ... Bariki ... omba**
Katika kila amri hizi hufanyika kwa mwendelezo, siyo tu kwa mara moja.

**penda adui zako**
Hii hainamaana unawapenda tu adui na siyo marafiki. Hii inaweza kusemwa. NI: "Wapende adui, siyo tu rafiki!" (UDB)

**penda ... fanya mema kwa**
Virai viwili hivi vinamaana sawa, na kwa pamoja vinasisitiza hoja.

**Bariki ambao**
Mungu ndiye abarikie. Hii inaweza ikadhihirisha. NI: "Omba Mungu kubariki hao" (UDB)

**ambao wanakulaani**
"ambao wanatabia ya kukulaani"

**wale ambao wanakutendea mabaya**
"wale ambao wanatabia ya kukutenda mabaya"

### Luke 6:29

**Kwa yeye akupigaye**
"kama yeyote akupigaye"

**katika shavu moja**
"kwenye upande mmoja wa uso"

**Mpe pia upande mwingine**
Inasaidia kusema ambacho mshambuliaji atafanya kwa mtu. NI: "geuza uso wako kwamba aweza kupiga na shavu jingine pia"

**Usizuie**
"hapana kumzuia kuchukua"

**Mpe kila mmoja akuombaye**
"Ikiwa yeyote anakuomba kitu, mptie"

**usimuulize**
"usimwombe" au "usihitaji"

### Luke 6:31

**Kama unavyotaka watu wakufanyie, ufanye hivyo kwao**
Kwa baadhi ya lugha zingine inaweza kuwa uasilia zaidi kubadili amri: NI: "Uwafanyie watu sawasawa na unavyotaka watu wakufanyie."

**Ni ujira gani kwenu?**
"Ni dhawabu gani mtapokea?" au "Mtapokea sifa gani kwa kufanya hivyo?" Hii inaweza kuandikwa kama sentensi. NI: "Hamtapokea thawabu yeyote kwa hilo" au "Mungu hatawazawadia kwa hilo"

**kurudisha kiasi kile kile**
Sheria ya Musa iliamuru Wayahudi wasipokee riba kwa pesa waliyokopeshana.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

### Luke 6:35

**Dhawabu yenu itakuwa kubwa**
"mtapokea dhawabu kubwa" au "mtapokea malipo mazuri" au "mtapata zawadi nzuri kwa sababu ya hilo"

**Mtakuwa wana wa aliye juu**
Ni vizuri sana kutafsiri "wana" kwa maneno ambayo lugha yako itayatumia kwa asili kurejea kwa mwana wa kibinadamu.

**wana wa aliye juu**
Hakikisha kwamba neno "wana" ni wingi lisichanganywe na cheo cha Yesu "Mwana wa aliye Juu Sana"

**Wasio na shukrani na ni watu waovu**
"Watu ambao hawamshukuru yeye na ambao ni waovu"

**Baba yako**
Hii inamrejea Mungu. Ni bora kutafsiri "Baba" kwa neno ambalo lugha ambayo kwa asili hutumika kurejea kwa baba binadamu.

### Luke 6:37

**Msihukumu**
"Msihukumu watu" au "usimkosoe mtu"

**na wewe**
"na kama matokeo yako"

**hamtahukumiwa**
Yesu hakusema ambao wasingehukumu. Inawezekana maana ni 1) "Mungu hatakuhukumu wewe" au 2) "hakuna wa kukuhukumu wewe."

**Msishutumu**
"Msishutumu watu"

**Hamtashutumiwa**
Yesu hakusema ambaye angehukumu. inawezekana inamaanisha 1) "Mungu hatakushutumu wewe" au 2) "hakuna hata mmoja atakaye washutumu."

**Nanyi mtasamehewa**
Yesu hakusema ambaye angesamehe. Inawezekana inamaanisha 1) "Mungu atakusamehe" au 2 ) "watu watakusamehe."

### Luke 6:38

**Nanyi mtapewa**
Yesu hakusema kwa hakika ambaye angetoa. Inawezekana inaanisha 1) "yeyote atakupa wewe 2) "Mungu atakupa wewe?

**kiasi cha ukarimu ....magotini penu**
Amri ya sentensi hii inaweza kurudiwa. NI: "kitamwagwa magotini penu kiasi cha ukarimu kilichosindiliwa na kumwagika. "Yesu alitumia mfano wa mfanya biashara wa nafaka kupata kiasi cha ukarimu. NI: "Ni kama mfayabiashara wa nafaka ambaye hushindilia nafaka na kuzitikisa pamoja na hutoka nafaka nyingi ambazo humwagika, watakupatia wewe kwa ukarimu.

**Kiasi cha ukarimu**
"kiasi kingi"

**Itapimwa hivyo hivyo kwako**
Yesu hakusema kwa hakika nani atapima. Maana zinazowezekana 1)"watatumia kipimo hicho hicho kupima vitu vyako" au 2) Mungu atakupimia pia vitu wewe

### Luke 6:39

**Sentensi Unganishi**
Yesu anahusisha baadhi ya mifano kujenga hoja yake.

**mtu kipofu anaweza kumuongoza kipofu mwingine?**
Yesu alitumia swali ili kupata watu wa kufikiri kitu ambacho tayari wanajua. Hii inaweza kuandikwa kama sentensi. NI: "Mtu kipofu hawezi kumuongoza mtu mwingine kipofu.

**mtu kipofu**
mtu ambaye ni "kipofu" ni sitiari kwa mtu ambaye hajafundishwa kama mwanafunzi.

**Ikiwa alifanya**
Baadhi ya lugha zinaweza kupendelea, "kama mmoja alifanya" Hii ni hali upuuzi kwamba haiwezi kabisa kutokea.

**wote wataangukia shimoni, je hawawezi?**
Hii inaweza kuandikwa kama sentensi. NI: wawili wote wataangukia shimoni"

**Mwanafunzi siyo mkubwa kuliko mwalimu mwalimu wake**
"Mwanafunzi hawezi kumzidi mwalimu wake." Maana zinazowezekana ni 1) "Mwanafunzi hana maarifa kuliko mwalimu wake" au 2) Mwanafunzi hana mamlaka kuliko mwalimu"

**Mwanafunzi hawi mkubwa kuliko mwalimu wake**
Hii inaweza kumaanisha kuwa 1)"mwanafunzi hawezi kuwa na ufahamu mkubwa kuliko mwalimu "au 2) " Mwanafunzi hana mamlaka zaidi ya mwalimu ."Mwanafunzi hawezi kumzidi mwalimu."

**kila mmoja akishamaliza kufundishwa**
"Kila mwanafunzi aliyefundishwa vizuri" au "kila mwanafunzi ambaye amejazwa mafundisho na mwalimu."

### Luke 6:41

**kwanini unaangalia ... lakini huzingatii kijiti ambacho kimo kwenye jicho lako?**
Yesu anatumia swali hili kuwapa watu changamoto kuzingatia dhambi zao wenyewe kabla

hawajafuatilia dhambi za watu wengine. NI: "usiangalie ... lakini puuza kitiji ambacho kimo kwenye jicho lako"

**kibanzi kilichomo kwenye jicho la ndugu yako**
Hii ni sitiari ambayo inarejea kwenye kosa dogo alilofanya muumini mwenzako.

**kipande cha kijiti**
"doa" (UDB) au "kibanzi." Tumia neno kwa kitu kidogo ambacho kwa kawaida kinaingia kwenye jicho la mtu.

**ndugu**
Hapa "ndugu" inanarejea kwa myahudi au muumini mfuasi wa Yesu.

**kijiti ambacho kimo kwenye jicho lako**
Hii ni sitiari kwa kosa la mtu maarufu. kijiti hakiwezi kuingia kwenye kwenye jicho la mtu kilivyo. Yesu anasisitiza kwamba mtu awe makini kwa makosa yake mwenyewe kabla hajashughulikia makosa madogo ya mwingine.

**kijiti**
"boriti " au "kigogo"

**Unawezaje kusema ... jicho?**
Yesu anauliza swali hili kukosoa watu wazingatie dhambi zao kabla ya kufuatilia dhambi za wengine. NI: "Usiseme ... jicho"

## Luke 6:43

**Taarifa kwa Ujumla:**
watu wanaweza wakasema kama mti ni mzuri au mbaya, na ni aina gani ya mti, kwa matunda yake unayozaa. Yesu anatumia hii kama sitiari isiyo elezewa - tunajua mtu wa aina gani kwa ya kuona mtendo yao.

**kwa kuwa ipo**
"sababu ipo" Hii inaashiria kwamba kinachofuata ni sababu ni sababu ya kwanini hatupaswi kuwahukumu ndugu zetu

**mti mzuri**
mti wenye afya

**haribika**
"liooza" au "baya" au "siofaa"

**Kila mti hujulikana**
watu hutambua aina ya mti kwa matunda yake unayozaa. Hii inaweza kusemwa kwa kauli tendaji. NI: "watu wanajua aina ya mti" au "watu wanatambua mti"

**Mchongoma**
Mmea au kichaka chenye miiba

**waridi mwitu**
mzabibu au kichaka kilicho na miiba

## Luke 6:45

**Taarifa kwa Ujumla:**
Yesu analinganisha mawazo ya mtu kwa hazina nzura au mbaya. Mawazo mazuri ya mtu mzuri yanasababisha matendo mazuri. Mawazo maovu ya mtu mwovu husababisha matendo mabaya.

**Mtu mwema**
Neno "mwema" hapa linahusu mwenye haki au maadili mema.

**mtu mwema**
Neno "mtu" linarejea kwa mtu, mwanaume au mwanamke. NI: "mtu mwema"

**Hazina njema ya moyo wake**
"vitu vizuri hutunza moyoni mwake" au "vitu vizuri huvithamini"

**huzaa kilicho kizuri**
Kutoa kilicho kizuri ni sitiari kwa kufanya mema. NI: "kufanya kilicho kizuri"

**hazina mbaya ya moyo wake**
"mambo mabaya anayotunza moyoni mwake" au "mambo mabaya anayothamini"

**katika utajiri wa moyo wake mdomo huzungumza**
Kirai "kinywa chake" kinawakilisha yeye kutumian mkinywa chake. NI: "anachofikiri moyoni mwake kinaathiri anachosema kwa mdomo wake" au anachokithamini moyoni mwake huamua kinachosemwa na kinywa.

## Luke 6:46

**Taarifa kwa Ujumla:**
Yesu anamlinganisha mtu ambaye anatii na mtu anayejenga nyumba juu ya mwamba ambapo itakuwa na uimara na gharika.

**Bwana, Bwana**
Urudiaji wa maneno haya huashiria kwamba walimwita Yesu kwa kawaida "Bwana."

**Kila mtu ajaye kwangu ... nitakwambia anacho kifanana**
Itakuwa wazi zaidi kubadili mfumo wa sentensi hii. NI: "Nitakuambia jinsi kila mtu anayekuja kwangu akasikia na kuyatii maneno yangu anavyofanana "

**jenga msingi wa nyumba kwenye mwamba imara**
"Kuchimba msingi wa nyumba kwa kina kufikia mwamba imara" Baadhi ya tamaduni hawajengi juu ya mwamba, wanaweza kuhitaji kutumia kitu kingine kwa msingi imara.

**Msingi**
"msingi" au "saidia"

**mwamba imara**
Huu ni mwamba mgumu ambao upo chini ya udongo.

**Maporomoko ya maji**
"maji yaendayo kasi" au "mto "

**Yakatokea dhidi**
"Yakagonga dhidi yake"

**tikisa**
Maana zinazowezekana ni 1) "sababisha kutikisika" au 2) "iharibu."

**Kwa sababu ilikuwa imejengwa vizuri**
"kwa sababu mtu alikuwa ameijenga vizuri"

### Luke 6:49

**Taarifa kwa Ujumla:**
Yesu anamlinganisha mtu asikiaye hatii mafundisho na mtu ambaye kajenga nyumba bila msingi hivyo itaanguka wakati wa mafuriko.

**lakini mtu**
"Lakini" inaonesha utofauti mkubwa kwa mtu aliyetangulia ambaye alijenga kwenye msingi.

**juu ya ardhi pasipo msingi**
Baadhi ya tamaduni nymba yenye msingi ni imara. Taarifa za kuongeza zinaweza zikawa msaada NI: "lakini hakuchimba chini na kujenga kwanza msingi"

**Msingi**
"msingi" au "msaada imara"

**mafuriko ya maji**
"maji -yanayotembea kwa kasi"

**Maporomoka**
"maji yanakwenda kwa kasi" au "mto"

**tiririka kinyume**
"iliyogonga"

**poromoka**
"anguka chini" au "ikagawanyika"

**kifusi cha nyumba hiyo kilikuwa kamili**
"nyumba hiyo ilikuwa imeharibika kabisa"

---


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 7

1 Baada ya Yesu kumaliza kila kitu alichokuwa anasema kwa watu waliomsikiliza, akaingia Kapernaumu. 2
Mtumwa fulani wa akida, aliyekuwa wa thamani sana kwake, alikuwa mgonjwa sana na alikuwa karibu ya
kufa. 3 Lakini akiwa amesikia kuhusu Yesu, yule Akida alimtuma kiongozi wa kiyahudi, kumwomba aje
kumwokoa mtumwa wake ili asife. 4 Walipofika karibu na Yesu, walimsihi kwa bidii na kusema, "anastahili
kwamba unapaswa kufanya hivi kwa ajili yake, 5 kwa sababu analipenda taifa letu, na ndiye aliyejenga
sinagogi kwa ajili yetu". 6 Yesu akaendelea na safari yake pamoja nao. lakini kabla hajaenda mbali na
nyumba, afisa mmoja aliwatuma marafiki zake kuzungumza naye. "Bwana, usijichoshe mwenyewe kwa
sababu mimi sistahili wewe kuingia kwenye dari yangu. 7 Kwa sababu hii sikufikiria hata mimi mwenyewe
kuwa ninafaa kuja kwako, lakini sema neno tu na mtumishi wangu atapona. 8 Kwani mimi pia ni mtu
niliyewekwa kwenye mamlaka na nina askari chini yangu. Husema kwa huyu "Nenda" na huenda, na kwa
mwingine, "Njoo" naye huja, na kwa mtumishi wangu 'Fanya hiki', na yeye hufanya". 9 Yesu aliposikia
haya alishangaa, na kuwageukia makutano waliokuwa wanamfuata na kusema."Nawaambia, hata katika
Israeli, sijawahi kuona mtu mwenye imani kuu kama huyu. 10 Kisha wale waliokuwa wametumwa walirudi
nyumbani na kumkuta mtumishi akiwa mzima. 11 fulani baada ya haya, ilitokea kuwa Yesu alikuwa
anasafiri kwenda mji ulioitwa Naini. wanafunzi wake wakaenda pamoja naye wakiambana na umati wa
watu. 12 Alipofika karibu na Lango la jiji tazama, mtu aliyekufa alikuwa amebebwa, na ni mtoto wa pekee
kwa mama yake. aliyekuwa mjane, na umati wa wawakilishi kutoka kwenye jiji walikuwa pamoja naye. 13
Alipomwona, Bwana akamsogelea kwa huruma kubwa sana juu yake na akamwambia, "Usilie". 14 Kisha
akasogea mbele akaligusa jeneza ambalo walibebea mwili, na wale waliobeba wakasimama akasema
"Kijana nasema amka" 15 Mfu akainuka na kukaa chini na akaanza kuongea. Kisha Yesu akamkabidhi kwa
mama yake. 16 Kisha hofu ikawajaa wote. wakaendelea kumtukuza Mungu wakisema "Nabii mkuu
ameinuliwa miongoni mwetu" na "Mungu amewaangalia watu wake" 17 Hizi habari njema za Yesu zilienea
Yudea yote na kwa mikoa yote ya jirani. 18 Wanafunzi wa Yohana walimwamwambia mambo haya yote. 19
Ndipo Yohana akawaita wawili wa wanafunzi wake na kuwatuma kwa Bwana kusema "Wewe ndiye yule
ajaye, au kuna mtu mwingine tumtazamie? 20 Walipofika karibu na Yesu hawa wakasema, "Yohana
mbatizaji ametutuma kwako kusema, 'Wewe ni yule ajaye au kuna mtu mwingine tumtazamie?" 21 kwa
wakati huo aliowaponya watu wengi kutoka katika magonjwa na mateso, kutoka kwa roho wachafu, na
kwa watu wenye upofu aliwapa kuona. 22 Yesu akajibu na kusema kwao. "Baada ya kuwa mmekwenda
mlikotoka mtamjulisha Yohana mlichokiona na kukisikia. Wenye upofu wanapokea kuona na viwete
wanatembea, wenye ukoma wanatakasika, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa na kuwa hai tena,
masikini wanaambiwa habari njema. 23 Na mtu ambaye hataacha kuniamini mimi kwa sababu ya matendo
yangu amebarikiwa". 24 Baada ya wale waliotumwa na Yohana kurudi walikotoka, Yesu akaanza kusema
kwa makutano juu ya Yohana, "Mlikwenda nje kuona nini, mwanzi ukiwa unatikiswa na upepo? 25 lakini
mlikwenda nje kuona nini, mtu aliyevaa vizuri? tazama watu wale wanaovaa mavazi ya kifalme na kuishi
maisha ya starehe wako kwenye nafasi za wafalme. 26 lakini mnakwenda nje kuona nini, Nabii? Ndiyo,
ninasema kwenu na zaidi sana kuliko nabii. 27 Huyu ndiye aliyeandikiwa, "Tazama, namtuma mjumbe
wangu mbele ya macho yenu, atakeyeandaa njia kwa ajili yangu, 28 Nasema kwenu, kati ya wale
waliozaliwa na mwanamke, hakuna mkuu kama Yohana, lakini mtu asiye muhimu sana atakayeishi na
Mungu mahali alipo yeye, atakuwa mkuu kuliko Yohana." 29 Na watu wote waliposikia haya pamoja na
watoza ushuru, walitangaza kuwa Mungu ni mwenye Haki. Walikuwepo kati yao wale waliobatizwa kwa
ubatizo wa Yohana. 30 Lakini mafarisayo na wataalamu wa sheria za kiyahudi, ambao hawakubatizwa na
yeye walikataa hekima za Mungu kwa ajili yao wenyewe. 31 Tena naweza kuwalinganisha na nini watu wa
kizazi hiki? Wakoje hasai? 32 Wanafanana na watoto wanaocheza kwenye eneo la soko, wanaokaa na
kuitana mmoja baada wa mwingine wakisema, 'Tumepuliza filimbi kwa ajili yenu, na hamkucheza.
tumeomboleza na hamkulia.' 33 Yohana mbatizaji alikuja hakula mkate wala hakunywa divai, na mkasema
"Ana pepo. 34 Mwana wa Mtu amekuja amekula na kunywa na mkasema, "Angali ni mlafi na mlevi, rafiki
wa watoza ushuru na wenye dhambi! 35 Lakini hekima imetambulika kuwa ina haki kwa watoto wake
wote." 36 Mmoja wa mafarisayo alimwomba Yesu aende kula pamoja naye. Baada ya Yesu kuingia kwenye
nyumba ya farisayo, aliegemea kwenye meza ili ale. 37 Tazama kulikuwa na mwanamke mmoja katika jiji
hilo aliyekuwa na dhambi. Akagundua kuwa alikuwa amekaa kwa Farisayo, akaleta chupa ya manukato. 38
Alisimama nyuma yake karibu na miguu yake huku akilia. Tena alianza kulowanisha miguu yake kwa
machozi, na kuifuta kwa nywele za kichwa chake, akiibusu miguu yake na kuipaka manukato. 39 Na yule
farisayo aliyekuwa amemwalika Yesu alipoona hivyo, akawaza mwenyewe akisema, "Kama huyu mtu
angekuwa nabii, angejua huyu ni nani na ni aina gani ya mwanamke anayemgusa, ya kuwa ni mwenye


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

dhambi. **40** Yesu akajibu na kumwambia, "Simoni nina kitu cha kukuambia. "Akasema" "Kiseme tu
mwalimu!" **41** Yesu akasema "Kulikuwa na wadaiwa wawili kwa mkopeshaji mmoja. Mmoja alikuwa
anadaiwa dinari mia tano na wa pili alidaiwa dinari hamsini. **42** Na walipokuwa hawana pesa ya kumlipa
aliwasamehe wote. Sasa ni nani atampenda zaidi? **43** Simoni akamjibu na kusema, "Nadhani
aliyesamehewa zaidi."Yesu akamwambia, "Umehukumu kwa usahihi." **44** Yesu akamgeukia mwanamke na
kusema kwa Simoni, "Unamwona huyu mwanamke. Nimeingia kwenye Nyumba yako. Hukunipa maji kwa
ajili ya miguu yangu, lakini huyu, kwa machozi yake, alilowanisha miguu yangu na kuifuta kwa nywele
zake. **45** Hukunibusu, lakini yeye, tangu alipoingia humu hakuacha kunibusu miguu yangu. **46** Hukuipaka
miguu yangu kwa mafuta, lakini ameipaka miguu yangu kwa manukato. **47** Kwa jambo hili, nakwambia
kwamba alikuwa na dhambi nyingi na amesamehewa zaidi, na pia alipenda zaidi. Lakini aliyesamehewa
kidogo, hupenda kidogo tu." **48** Baadaye akamwambia mwanamke, "Dhambi zako zimesamehewa" **49** Wale
waliokaa mezani pamoja naye wakaanza kusemezana wao kwa wao, "Huyu ni nani mpaka anasamehe
dhambi?" **50** Na Yesu akamwambia mwanamke, "Imani yako imekuokoa. Enenda kwa amani"

---

## Luka 07 Maelezo ya Jumla

#### Muundo na upangiliaji

Baadhi ya tafsiri hupendelea kuweka mbele kidogo nukuu za Agano la Kale. ULB na tafsiri nyingine nyingi za Kiingereza huingiza mistari yote ya 7:27, ambayo ni nukuu kutoka Agano la Kale.

Kuna nyakati katika maelezo ya sura hii ambapo kuna mabadiliko ya ghafla katika mada. Mtafsiri hapaswi kulainisha mabadiliko haya.

#### Dhana maalum katika sura hii

#### Jemadari

Hali hii haikuwa jambo la kawaida sana katika Israeli ya kale. Haikuwa kawaida kwa askari wa Kirumi kuhitaji chochote kwa Waisraeli kwani hawakuwa wa maana kwa Warumi na hawangehitaji uponyaji kutoka kwa Myahudi. Haikuwa pia kawaida kwa tajiri kujali maslahi ya mtumwa wake. Hii inaonyesha imani kuu.

#### Ubatizo wa Yohana

Ubatizo ambao Yohana alifanya ulikuwa tofauti na ubatizo ambao kanisa linafanya. Ubatizo wa Yohana ulikuwa unaashiria kuwa wale waliopokea walikuwa wametubu dhambi zao. Ndio maana Mafarisayo hawakuhusika katika ubatizo wa Yohana. and ).

#### "Wenye dhambi"

Luka anaashiria kundi la watu kuwa "wenye dhambi." Viongozi wa Kiyahudi waliona watu hawa kuwa hawaelewi Sheria ya Musa, na hivyo wakawaita "wenye dhambi." Kwa kweli, viongozi wenyewe ndio walikuwa wenye dhambi. Hali hii inaweza kuchukuliwa kama kinaya.

#### "Miguu"

Miguu ilionekana kuwa ni chafu sana katika inchi za Mashariki ya Karibu ya Kale. Ingekuwa tendo la unyenyekevu sana kwa mwanamke huyu kuosha miguu ya Yesu na ilikuwa njia ya kumheshimu Yesu.

#### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

#### "Mwana wa Binadamu"

Yesu anajiita mwenyewe kama "Mwana wa Binadamu." Lugha zingine haziwezi kuruhusu mtu kujitaja mwenyewe kama 'mtu wa tatu.'

---


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

### Luke 7:1

**Taarifa kwa ujumla**
Yesu anaingia Kapernaumu pale alipomponya mtumishi wa akida.

**watu wakiwa wanasikiliza**
Nahau "wakati watu wanasikiliza" anasisitiza anataka watu wasikie anchosema. NI: "ni kwa watu ambao walikuwa wanamsikiliza" au "kwa watu waliohudhuria" au "kwaajili ya watu kusikia"

**Aliingia Kapernaumu**
Hii inaanzisha tukio jipya katika simulizi

### Luke 7:2

**Nani alikuwa wa thamani kwake**
"ambaye akida alimthamini" au "ambaye alimweshimu"

**alimuuliza kwa uaminifu**
"sihi pamoja" au "alimwomba"

**anayestahili**
"akida anastahili"

**Taifa letu**
"Watu wetu" hii inarejea kwa wayahudi.

### Luke 7:6

**aliendelea kwenye njia yake**
"alienda"

**siyo mbali kutoka kwenye nyumba**
kauli hasi hizi zinaweza kubadilishwa. NI: "karibu na nyumba"

**Usijisumbue mwenyewe**
Akida alikuwa anaongea kwa upole kwa Yesu. NI: "Usijisumbue mwenyewe kwa kuja nyumbani kwangu" au "Sitaki kukuudhi"

**Ingia chini ya dari yangu**
Kirai hiki ni nahau inayo maanisha "Njoo ndani ya nyumba yangu." Kama lugha yako ina nahau inayomaanisha "Njoo kwenye nyumba yangu" fikiri kama ina weza kuwa nzuri kuweka hapa."

**sema neno tu**
Mtumishi alijua kuwa Yesu atamponya yule mtumishi kwa kusema tu. Hapa "neno" linarejea kuamuru. NI: "toa tu agizo"

**Mtumishi wangu atapona**
Neno lililotumiwa kutafsiri hapa kama "Mtumishi" mara nyingi limetafsiriwa kama "Mvulana" inaweza kuonyesha ishara kuwa mtumishi alikuwa kijana mdogo au inaonyesha ufanisi wa akida kwake.

**kwa mtumishi wangu**
Neno lililotafsiriwa hapa kama "mtumishi" ni neno la kawaida kwa mtumishi.

### Luke 7:9

**Alimshangaa**
"alimshanga akida"

**nawaambia**
Yesu alisema haya kusisitiza maajabu ambayo anataka kuwaambia.

**hata katika Israel sijawahi kuona imani kubwa hivi**
maana yake ni kuwa Yesu alitarajia wayahudi kuwa na imani kama hii, lakini hawakuwa hivyo. Hakuwatajia wamataifa kuwa na imani ya namna hii, lakini huyu mtu amekuwa na imani hiyo. Unaweza kuongeza taarifa iliyofichika. NI: "sijaona mwisraeli yeyote anaye niamini kwa kiasi kama mmataifa huyu!" (UDB)

**wale waliokuwa wametumwa**
Ilifahamika kwamba hawa walikuwa watu waliotumwa na akida. Hii inaweza kusemwa NI: "watu ambao watawala wa Rumi waliowatuma kwa Yesu"

### Luke 7:11

**Sentensi Unganishi**
Yesu anaenda katika mji wa Naini, pale alipomponya mtu aliyekuwa amekufa.

**Naini**
ni jina la Mji

**tazama, mtu aliyekufa alikuwa kafa**
Neno "Tazama" linatuashiria utangulizi wa simulizi ya mtu aliyekufa kwenye habari. Lugha yako inaweza kuwa na njia ya kufanya hivi. NI: "Kulikuwa na mtu aliyekufa"

**mtu ambaye alikuwa amekufa alikuwa kabebwa**
Hii inaweza ikasemwa katika kauli tendaji. NI: watu walikuwa wanapeleka nje ya mji mtu aliyekufa"

**mwana pekee wa mama yake (ambaye alikuwa mjane)**
"alikuwa mwana pekee wa mamaye, na alikuwa mjane" Hii ni taarifa iliyotangulia kuhusu aliyekufa na mama yake.

**ilitokea kuwa**
hii sentensi inatumika hapa kuonyesha mwanzo wa habari mpya. kama Lugha yako ina njia nyingine ya kufanya hivi unaweza kutumia hapa.

**mjane**
mwanamke ambaye mumewe amesha kufa

**alisukumwa na huruma kwa ajili yake**
"aliona huruma kwa ajili yake"

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**akaja mbele**
"akaenda mbele" au "akamsogelea aliyekufa"

**jeneza lililokuwa limebeba mwili**
Hiyo ilikuwa ni machela au kitanda kilitumika kubeba mwili kwenda maeneo ya kuzika. kisingeweza kuwa kitu cha kuzikia. Tafsiri nyingine inapunguza uthamani "Jeneza" au "Kiti cha msiba"

**nasema kwako**
Yesu alisema hili kuonyesha mamlaka yake "Nisikilize!"

**maiti**
mtu alikuwa bado amekufa; sasa alikuwa hai. Itakuwa lazima kusema hili wazi. NI: "ni mtu aliyekuwa amekufa."

## Luke 7:16

**Sentensi Unganishi**
Hii inatumabia jinsi ilivyotokea kama matokeo ya uponyaji wa Yesu kwa mtu aliyekuwa amekufa.

**hofu ikawajaa wote**
"Hofu huwajaa wote." Hii inaweza katika kauli tendaji. NI: "wate wakawa na hofu sana."

**Nabii mkuu**
Walikuwa wanarejea kwa Yesu, siyo kwa yule nabii asiyejulikana.

**Ameinuliwa kati yetu**
"Amekuja kuwa nasi" au "Ameonekana kwetu." Mungu ameinua nabii mkuu katikati yetu." Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji. NI: "Mungu ameinua nabii mkuu kati yetu"

**amengalia juu ya**
Nahau hii inamaana "ajali"

**Habari hizi njema kuhusu Yesu zikaenea**
"Habari hizi njema" inarejea kwa vitu ambavyo watu walikuwa wanasema katika mstari wa 16. Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji "Watu wakaeneza hizi taarifa kuhusu Yesu" au "Watu waliwaambia wengine hii taarifa ya kuhusu Yesu."

**Habari hizi**
"Hili neno" au "Huu ujumbe"

## Luke 7:18

**Taarifa Unganishi :**
Yohana anatuma wawili wa wanafunzi wake kumuuliza Yesu.

**Wanafunzi wa Yohana walimwambia kuhusu mambo yote**
Hii inatambulisha tukio jingine kwenye habari

**akamwambia**
"akamwambia Yohana"

**mambo yote haya**
"mambo yote alikuwa anafanya"

**watu walisema, "Yohana mbatizaji ametutuma kwako kusema 'ni wewe ... au tumtazamie mwingine?"**
Sentensi hii inaweza kuandikwa hivyo kwamba ikawa na nukuu ya moja kwa moja tu. NI: "watu walisema kwamba Yohana mbatizaji aliwatuma wao kwake kuuliza 'wewe ni yule ajaye, au tumtazamie mwingine?" au "watu walisema, '"Yohana katutuma sisi kwako kuuliza kama ni yule ambaye anakuja, au kama tutazamie mwingine."

**tumtazamie mwingine**
"tusubiri mwingine" au "tumtazamie mtu fulani"

## Luke 7:21

**Kwa saa hiyo**
"kwa wakati huo"

**kutoka kwa roho wachafu**
Itakuwa msaada kusema tena uponyaji. NI: "aliwaponya na roho chafu"au "na aliwaweka huru watu kutoka katika roho chafu"

**aliwaambia**
"aliwaambia wajumbe wa Yohana" au "alisema kwa wajumbe aliowatuma Yohana"

**Toa taarifa kwa Yohana**
"Mwambie Yohana"

**watu wahitaji**
"watu masikini"

**Mtu asiyeacha kuniamini kwa sababu ya matendo yangu amebarikiwa**
Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji. NI: "Mungu atambariki mtu ambaye haachi kuamini kwake sababu ya matendo yake"

**Mtu**
"Watu" au "yeyote" Huyu si mtu maalumu.

**usisitishe**
maana mbili hasi "Hendelea"

## Luke 7:24

**Sentensi Unganishi**
Yesu anaanza kuzungumza katika makutano kuhusu Yohana mbatizaji. anauliza maswli balagha kuwasaidia kufikiri kuhusu ambacho Yohana mbatizaji hasa anavyofanana.

**Nini ... mwanzi ukutikiswa na upepo?**
Hii inategemea jibu hasi. "milikwenda nje kuona mwanzi ukitikiswa na upepo? siyo hivyo" Inaweza pia ikaandikwa kama sentensi. NI: "Kwa hakika hamkwenda kuona mwanzi ukitikiswa na upepo!"

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**Mwanzi umetikiswa na upepo**
Maana zinazowekeana kwa sitiari hii ni (1) mtu anaye badili mawazo yake, kama mwanzi ni rahisi kugeuzwa na upepo, au 2) mtu anayeongea sana lakini hasemi chochote cha mhimu, kama mwanzi ugeuzwavyo wakati upepo unapovuma.

**Lakini nini ... mtu aliyevaa mavazi laini?**
Hii pia inatazamia jibu hasi, sababu Yohana alivaa vazi gumu. "mlikenda huangalia mtu amevaa nguo laini? siyo hivy!" Hii pia inaweza kuandikwa kama sentensi. NI: Hakika hamkwenda kuona mtu amevaa nguo laini!"

**liyevaa nguo laini**
Hii inarejea nguo za gharama. Nguo za kawaida zilikuwa chakavu. NI "vaa nguo za gharama"

**Ikulu ya mfalme**
Ikulu ni kubwa, nyumba ya gharama anayoishi mfale.

**Lakini ... Nabii?**
Hii inaelekea kwenye jibu chanya. "Mlikwenda nje kuona nabii?" Ndivyo mlivyofanya!" Hii pia inaweza ikaandikwa kama sentensi. NI: "Lakini mlienda kweli kuona nabii!"

**Ndiyo, asema kwenu**
Yesu alisema kusisitiza umhimu wa vile ambavyo angesema badaye

**zaidi ya nabii**
Kirai hiki kinamaanisha kwamba Yohana alikuwa kabisa nabii, lakini kwamba alikuwa hata zaidi ya nabii halisi. NI: ""siyo nabii wa kawaida" au "ni muhimu zaidi ya nabii wa kawida"

## Luke 7:27

**Huyu ndiye aliyeandikiwa**
"Nabii huyo ni yule manabii waliyeandika kumhusu" au "Yohana ni yule manabii walimwandika wakati mrefu uliopita"

**Tazama, mimi namtuma**
katika mstari huu, Yesu anamnukuu nabii Malaki na kusema kuwa Yohana ni mjumbe wa kile Malaki alisema.

**Mbele ya uso wako**
Nahau inamaana "Mbele yako" or "kwenda mbele yako"

**yako**
Neno "Yako" ni umoja kwa sababu Mungu aliongea kwa masihi katika nukuu.

**Nasema kwako**
Yesu alikuwa anaongea na makutano hivyo "Ninyi" ni wingi. Yesu alitumia kirai hiki kusisitiza ukweli wa vitu vya kushangaza aliokuwa anaenda kuusema.

**kati ya waliozaliwa na mwanamke**
"baadhi ya wale mwanamke amewazaa" hii ni sitiari lakini inalenga kwa watu wote. NI: "watu wote waliowahi kuishi."

**Hakuna aliye mkuu kuliko John**
"Yohana ni mkuu zaidi"

**angalau mtu mhimu katika ufalme wa Mungu**
Hii inahusiana na kila mtu ambaye ni sehemu ya ufalme ambao Mungu atauanzisha.

**Ni mkuu kuliko alivyo**
kiwango cha kiroho cha watu katika ufalme wa Mungu kitakuwa cha juu kuliko cha watu kabla ya ufalme uliokuwa umeanzishwa. NI: "kiwango cha kiroho cha juu kuliko Yohana"

## Luke 7:29

**Taarifa kwa Ujumla**
Luka, mwandishi wa kitabu, alichangia juu ya mwitikio wa watu kwa Yohana na Yesu.

**Wakati watu wote ... ubatizo wa Yohana**
Mstari huu unaweza kurekebishwa wazi zaidi. NI: "wakati watu wote waliokuwa wamebatizwa na Yohana, wakiwemo watoza ushuru, walisikia hiki, wakatangaza kwamba Mungu ni mwenye haki.

**walitangaza kuwa Mungu ni mwenye haki**
"Walisema kwamba Mungu amejionyesha mwenyewe kuwa ni mwenye haki" au "walitangaza kuwa Mungu alitenda kwa haki

**sababu walibatizwa na ubatizo wa Yohana**
Hii inaweza ikasemwa katika kauli tendaji NI: "sababu walikubali Yohana awabatize" au "sababu Yohana aliwabatiza wao."

**walikataa kusudi la Mungu kwa ajili yao wenyewe**
"walikataa ambacho Mungu alitaka wao wafanye" au "chagua kutotii ambacho Mungu aliwaambia"

**wao hawakubatizwa na Yohana**
Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji NI: "ambao Yohana hakuwabatiza" au "ambao walikataa kubatizwa na Yohana" au " wale waliokataa ubatizo wa Yohana."

## Luke 7:31

**Taarifa Unganishi:**
Yesu aliendelea kusema kwa watu Kuhusu Yohana mbatizaji.

**Tena, naweza kuwalinganisha na nini ... wanafanana?**
Yesu alitumia maswali kutambulisha mlinganisho.Yawaeza kuandikwa kama sentensi. NI: "Hivi ndivyo nitawafananisha kizazi hiki., na ndivyo wanavyofanana.

**Watu wa kizazi hiki**
Watu wanalioishi wakati wa Yesu anasema

**Wanafanana**
Haya maneno ni mwanzo wa kulinganisha kwa Yesu. Yesu anasema kwamba watu wa kizazi hiki wanafanana na watoto ambao hawaridhiki na njia mbazo watoto wengine wanafanya

**Eneo la soko**
Kubwa, eneo la wazi ambapo watu huja kuuza bidhaa zao.

**na hamkucheza**
"Lakini hamkucheza kwenye mziki"

**Na hamkuomboleza**
"Lakini hamkuomboleza na sisi"

### Luke 7:33

**hakula mkate**
Maana zinazowezekana ni 1) "Kufunga mfululizo" au 2) kutokula chakula cha kawaida

**mnasema, 'Ana pepo'**
Yesu alikuwa ananukuu kile watu walikuwa wanasema kuhusu Yohana. Hii inaweza ikasemwa bila nukuu ya moja kwa moja. NI: "Mlisema kuwa ana pepo" au "Mlimtuhumu kuwa ana Pepo"

**Mwana wa Mtu**
Yesu alitarajia watu pale kujua kuwa alikuwa anajisemea mwenyewe. NI: "Mimi" mwana wa mtu.

**Mkasema, "Angali ... mdhambi"**
Yesu alikuwa ananukuu kile watu walikuwa wanasema kuhusu mwana wa Mtu. Hii inaweza kusemwa moja kwa moja. NI: "mmesema kwamba mimi ni mtu Mlafi na mlevi, rafiki wa watoza ushuru na wenye dhambi"

**Mtu mlafi**
Ni yule kitabia ya hula chakula kingi zaidi ya uhitaji wake.

**hekima imetambulika kuwa ina haki kwa watoto wake wote**
Hii inaonekana kabisa kuwa ni mithali ambayo Yesu aliihusisha na hali hii. Hii huenda inamaana kwamba watu wenye hekima wangeelewa watu hawangemkataa Yesu na Yohana.

### Luke 7:36

**Sentensi Unganishi:**
Mfarisayo alimwalika Yesu kula nyumbani kwake.

**Taarifa kwa Ujumla**
Ilikuwa ni desturi ya wakati huo mtazamaji kuhudhuria chakula cha jioni bila kula.

**Sasa mmoja wa mafarisayo**
Alama ya mwanzo mpya wa habari na inatambulisha mfarisayo kwenye habari.

**aliegemea kwenye meza ili ale**
"Alikaa kuzunguka kwenye meza kwa ajili ya chakula." Ilikuwa ni desturi kwa chakula cha starehe kama hiki chakula cha jioni kwa wanaume kula huku wakiwa wamejilaza kwa raha wakizunguka meza.

**Tazama kulikuwa na mwanamke mmoja**
Neno "Tazama" linatutazamisha sisi kwa mtu mwigine katika hadithi. Lugha yako inaweza ikawa na namna ya kufanya hivi.

**aliyekuwa na dhambi**
Yawezekana alikuwa kahaba. "Aliyeishi maisha ya dhambi" au "Ambaye alikuwa na sifa za kuishi maisha ya dhambi."

**chupa ya manukato**
"chupa hii ilitengenezwa kwa jiwe laini." Chupa ni laini, mwamba mweupe. watu walihifadhi vitu vya thamani katika hiyo chupa.

**mafuta ya manukato**
"na manukato ndani yake." manukato yalikuwa ni mafuta yaliyokuwa yanatoa harufu nzuri ndani yake. watu walijipaka wao wenyewe au kunyunyizia nguo zao ili wanukie vizuri.

**kwa nywele za kichwa chake**
"Kwa nywele zake"

**kuwalowanisha kwa manukato**
"mwaga manukato juu yao"

### Luke 7:39

**akawaza mwenyewe akisema**
"alisema yeye mwenyewe"

**Kama huyu mtu angekuwa nabii, angejua ... mdhambi**
Farisayo aliwaza kuwa Yesu hakuwa nabii kwa sababu amemruhusu mwanamke mwenye dhambi kumgusa. NI: "Inaonekana Yesu siyo nabii, sababu nabii angejua kwamba mwanamke anayemgusa ni mwenye dhambi."

**ni mdhambi**
Simoni kimakosa alihisi kwamba nabii asingeruhusu kuguswa. Ukweli huu ungeongezwa. NI: "ni mdhambi na asingeruhusiwa kugusa"

**Simoni**
Hili lilikuwa ni jina la Farisayo aliyemwalika Yesu katika nyumba yake. Huyu hakuwa Simoni Petro.

### Luke 7:41

**Taarifa kwa Ujumla:**
Kusisitiza nini anaenda kumwambia Simoni Farisayo, Yesu alimwambia hadithi.

**Kulikuwa na wadaiwa wawili kwa mkopeshaji mmoja**
"mkopeshaji fulani alikuwa na wadeni wawili"

**dinari mia tano**
"posho ya siku 500. " Dinari" ni wingi wa dinarius." Dinari ilikuwa ni sarafu ya fedha.

**hamsini**
"posho ya siku 50"

**aliwasamehe wote**
"aliwasamehe madeni yao" au "aliyafuta madeni yao"

**Nadhani**
Simoni alikuwa na tahadhari ya jibu hili. NI: "Huenda"

**Umehukumu kwa usahihi**
"Uko sahihi"

### Luke 7:44

**Yesu akamgeukia mwanamke**
"Yesu akamwangalia mwanamke. "Yesu akaelekeza uamkini wa Simoni kwa mwanamke kwa kumgeukia"

**hukunipa maji kwaajili ya miguu yangu**
Huu ni wajibu wa msingi kwa mwenyeji kuleta maji na taulo kwaajili ya wageni kuoshwa na kukausha miguu yao baada ya kutembea kwenye njia ya vumbi.

**wewe ... lakini yeye**
Yesu mara mbili anatumia virai hivi kupinga upungufu wa heshima ya Simoni kwa kile kitendo cha ziada cha mwanamke.

**kailowanisha miguu yangu kwa machozi yake**
Mwanamke alitumia machozi yake kwa maji yaliyokosekana.

**aliifuta kwa nywele zake**
Mwanamke alitumia nywele zake badala ya taulo iliyokosekana.

**hukunipa busu**
"Mwenyeji mzuri kwenye huo utamaduni aliwasalimia wageni wake kwa busu kwenye shavu. Simono hakufanya."

**hakuacha kunibusu miguu yangu**
"ameendelea kunibusu miguu yangu"

### Luke 7:46

**Hukufanya ... lakini yeye**
Yesu anaendelea kupinga wema hafifu wa Simoni na kitendo cha mwanamke

**tia kichwani pangu mafuta**
"paka kichwa changu kwa mafuta" Hii ilikuwa ni desturi ya kumkaribisha mgeni aliyeheshimika. NI: "nikaribisha kwa kunitia mafuta kichwani"

**tia mafuta miguu yangu**
Mwanamke alimweshimu sana Yesu kwa kufanya hivi. Alitoa kielelezo cha unyenyekevu kwa kutia mafuta miguuni badala ya kichwani.

**Nawaambia**
Hii inasisitiza umhimu wa sentensi inayofuata.

**dhambi zake, ambazo zilizo nyingi, zimesamehewa**
Hii inaweza kusemwa katika kauli tendaji. NI: "Mungu kasamehe dhambi zake nyingi"

**yeye alipenda zaidi**
upendo wake ulikuwa ulikuwa ushahidi kwamba dhambi zake zimesamehewa. Baadhi ya lugha zinahitaji kitu cha "Upendo" Kusema. "alipenda zaidi ambaye amemsamehe" au " alimpenda sana Mungu."

**Lakini aliyesamehewa kidogo**
"Mtu yeyote anasamehewa vitu vichache." Katika sentensi hii Yesu anaonyesha kanuni za jumla. Hata hivyo, Simon alikuwa anatarajia kuelewa kuwa Yesu anazungumzia kuwa Simoni ameonesha upendo kidogo.

### Luke 7:48

**Ndipo akamwambia**
"ndipo akamwabia mwanamke" (UDB)

**Dhambi zako zimesamehewa**
"umesamehewa." Hii inaweza ikasemwa katika kauli tendaji NI: "Nasamehe dhambi zako"

**kaa pamoja**
"kaa pamoja kuzunguka meza" au "kula pamoja"

**Nani huyo hata anasamehe dhambi**
Viongizi wa dini walijua kwamba Mungu tu anayesamehe dhambi, na hawakuamini kwamba Yesu alikuwa Mungu, Swali hili huenda lilikusudiwa kuwa tuhuma. NI: "Huyu mtu anafikiri kuwa yeye ni nani?" Ni Mungu pekee anaye samehe dhambi!" au "Kwanini huyu mtu anajifanya kuwa Mungu awezaye kusamehe dhambi?"

**Imani yako imekuponya wewe**
"Kwa sababu ya imani, umeokoka" "imani" inaweza ikatazamwa kama kitendo. NI: "kwa sababu umeamini, umeokoka"

**Nenda katika amani**
Hii ni namna ya kusema kwaheri wakati huohuo unatoa baraka. NI: "Unapokwenda, usiwe na wasi wasi kabisa" au "Mungu akupe amani unapoenda"

---

## Chapter 8

[1] Ilitokea muda mfupi baadaye kwamba Yesu alianza kusafiri katika miji na jiji mbalimbali, akihubiri na
kutangaza habari njema ya ufalme wa Mungu na wale kumi wawili walikwenda pamoja naye, [2] vilevile
wanawake fulani waliokuwa wameponywa kutoka kwa roho wachafu na magonjwa mbalimbali. Walikuwa
ni Mariamu aliyeitwa Magdalena ambaye alikuwa ametolewa pepo saba. [3] Yoana mke wa Kuza na meneja
wa Herode, Susana, na wanawake wengine wengi, waliotoa mali vyao kwa ajili yao wenyewe. [4] Nabaada
ya umati wa watu kukusanyika pamoja, wakiwemo na watu waliokuja kwake kutoka miji mbalimbali,
akazungumza nao kwa kutumia mifano. [5] "mpandaji alienda kupanda mbegu, alipokuwa apanda, baadhi
ya mbegu hizo ziliangukia kando ya njia zikakanyagwa chini ya miguu, na ndege wa angani wakazila. [6]
Mbegu zingine zilianguka juu ya udongo wa miamba na zilipoota na kuwa miche zilipooza kwa sababu
hakukuwa na unyevunyevu. [7] Mbegu zingine ziliangukia kwenye miti ya miiba, nayo hiyo miti ya miiba
ikakua pamoja na zile mbegu na zikasongwa. [8] Lakini mbegu zingine ziliangukia kwenye udongo unaofaa
na zikazaa mazao mara mia zaidi. "Baada ya Yesu kusema mambo haya, alipaza sauti,"Yeyote aliye na
masikio ya kusikia na asikie." [9] Tena wanafunzi wake wakamuuliza maana ya mfano huo, [10] Yesu
akawaambia, "Mmepewa upendeleo wa kujua siri ya ufalme wa Mungu, lakini watu wengine
watafundishwa tu kwa mifano, ili kwamba 'wakiona wasione na wakisikia wasielewe.' [11] Na hii ndiyo
maana ya mfano huu. Mbegu ni neno la Mungu. [12] Mbegu zile zilizoanguka kando kando ya njia ndiyo
wale watu wanaolisikia neno, na baadaye mwovu shetani hulichukua mbali kutoka moyoni, ili kwamba
wasiamini na kuokolewa. [13] Kisha na zile zilizoangukia kwenye mwamba ni watu wale wanaosikia neno na
kulipokea kwa furaha lakini hawana mizizi yeyote, wanaamini tu kwa muda mfupi, na wakati wa majaribu
huanguka. [14] Na mbegu zile zilizoangukia kwenye miiba ni watu wanaosikia neno, lakini wanapoendelea
kukua husongwa na huduma na utajiri na ubora wa maisha haya na hawazai matunda. [15] Lakini zile
mbegu zilizoangukia kwenye udongo mzuri ni wale watu, ambao ni wanyeyekevu na mioyo mizuri, baada
ya kulisikia neno hulishikilia na likawa salama na kuazaa matunda ya uvumilivu. [16] Sasa, hakuna hata
mmoja, anayewasha taa na kuifunika kwa bakuli au kuiweka chini ya kitanda. Badala ya kuiweka kwenye
kinara cha taa ili kwamba kila mmoja anayeingia apate kuiona. [17] Kwa kuwa hakuna kitakachojificha
ambacho hakitajulikana, au chochote kilicho sirini ambacho hakitajulikana kikiwa kwenye mwanga. [18]
kwa hiyo kuwa makini unapokuwa unasikiliza. Kwa sababu aliye nacho, kwake ataongezewa zaidi, lakini
asiye nacho hata kile kidogo alicho nacho kitachukuliwa." [19] baadaye mama yake Yesu na ndugu zake
wakaja kwake hawakaribia kwa sababu ya umati wa watu. [20] Na akataarifiwa, "Mama yako na ndugu
zako wako pale nje wanahitaji kukuona wewe. [21] Lakini, Yesu akajibu akasema "Mama yangu na ndugu
zangu ni wale wanaolisikia neno la Mungu na kulitii." [22] Ilitokea siku moja kati ya siku zile Yesu na
wanafunzi wake alipanda kwenye mtumbwi, na akawaambia, "Na tuvuke ng'ambo ya pili ya ziwa."
Wakaandaa mashua yao. [23] Lakini walipoanza kuondoka, Yesu akalala usingizi, na dhoruba kali yenye
upepo, na mashua yao ikaanza kujaa maji na walikuwa kwenye katika kubwa sana. [24] baadaye wanafunzi
wake wakaja kwake na kumwamsha, wakisema, "Bwana mkubwa! Bwana mkubwa! tuko karibu kufa!"
Akaamka na akaukemea upepo na mawimbi ya maji vikatulia na kukawa na utulivu. [25] Tena akawaambia,
"Imani yenu iko wapi?" Wakaogopa, Walishangaa, wakasemezana kia mmoja na mwenzake,"Huyu ni nani,
kiasi kwamba anaamuru hata upepo, na maji na humtii?" [26] Wakafika kwenye mji wa Gerasini iliyo
upande wa nyuma ya Galilaya. [27] Yesu aliposhuka na kukanya kwenye ardhi, mtu fulani kutoka mjini,
akakutana naye, na huyu mtu alikuwa na nguvu za giza. Kwa muda mrefu alikuwa havai nguo, na alikuwa
haishi kwenye Nyumba, lakini aliishi kwenye makaburi. [28] Alipomwona Yesu akalia kwa sauti, na
akaanguka chini mbele yake. kwa sauti kubwa akisema, Nimefanya nini kwako, Yesu mwana wa Mungu
aliye juu? Nakusihi, Usiniadhibu mimi" [29] Yesu akaamuru roho chafu imtoke mtu yule, kwa kuwa mara
nyingi amepamgaa. hata kama alikuwa amefungwa minyororo na kubanwa na kuwekwa chini ya ulinzi,
alivunja vifungo na kuendeshwa na mapepo mpaka jangwani. [30] Yesu akamwuliza, "Jina lako nani?"
akajibu akisema, "Legioni" Kwa maana mapepo mengi yameingia kwake. [31] Wakaendelea kumsihi
usituamuru twende kwenye shimo. [32] Kundi la Nguruwe lilikuwa likichunga juu ya kilima, wakamsihi
awaruhusu wakaingie kwa hao nguruwe. Na akawaruhusu kufanya hivyo. [33] kwa hiyo wale mapepo
wakamtoka mtu yule na kuingia kwa wale nguruwe, na lile kundi likakimbia kwenye mwinuko wa mlima
mpaka ziwani na wakazama humo. [34] wale watu waliokuwa wanachunga wale nguruwe walipoona
kilichotokea, wakakimbia na wakatoa taarifa pale mjini na nje katika miji iliyowazunguka. [35] Watu
waliposikia hayo walienda kuona kilichotokea, na wakaja kwa Yesu na wakamwona mtu ambaye mapepo
yalikuwa yamemtoka. alikuwa amevaa vizuri na mwenye akili timamu, amekaa kwenye miguu ya Yesu, na
waliogopa. [36] ndipo mmoja wao aliyeona kilichotokea alianza kuwasimlia wengine jinsi huyu mtu

aliyekuwa anaongozwa na mapepo alivyoponywa. **37** Watu wote wa mkoa wa Wagerasi na maeneo
yaliyozunguka walimwomba Yesu aondoke kwao kwa sababu walikuwa na hofu kuu. Na aliingia kwenye
mtumbwi ili arudi. **38** Mtu yule aliyetokwa na pepo alimsihi Yesu kwenda naye, lakini Yesu alimwambia
aende na kusema, **39** "Rudi kwenye nyumba yako na uhesabu yale yote ambayo Mungu amekutendea"
Huyu mtu aliondoka, akitangaza pote katika mji wote yale yote ambayo Yesu aliyofanya kwa ajili yake. **40**
Na Yesu akarudi, makutano wakamkaribisha, kwa sababu wote walikuwa wanamngoja. **41** Tazama akaja
mtu mmoja anaitwa Yairo ni mmoja kati ya viongozi katika sinagogi. Yairo akaanguka miguuni pa Yesu na
kumsihi aende nyumbani kwake, **42** kwa sababu alikuwa na mtoto msichana mmoja tu, mwenye umri wa
miaka kumi na wibili, na alikuwa katika hali ya kufa. Na alipokuwa akienda, makutano walikuwa
wakisongama dhidi yake. **43** Mwanamke mwenye kutokwa damu kwa miaka kumi na miwili alikuwa pale
na alitumia pesa zote kwa waganga, lakini hakuna aliyemponya hata mmoja, **44** alikuja nyuma ya yesu na
kugusa pindo la vazi lake, na ghafla kutokwa damu kukakoma. **45** Yesu akasema, "Nani ambaye
kanigusa?" Walipokataa wote, Petro akasema, Bwana Mkubwa, umati wa watu wanakusukuma na
wanakusonga." **46** Lakini Yesu akasema, "Mtu mmoja alinigusa, maana nilijua nguvu zimetoka kwangu."
**47** Mwanamke alipoona ya kuwa hawezi kuficha alichokifanya, akaanza kutetemeka, akaanguka chini
mbele za Yesu alitangaza mbele ya watu wote sababu zilizofanya amguse na vile alivyoponywa gafla. **48**
Kisha akasema kwake, "Binti, imani yako imekufanya uwe mzima. Enenda kwa Amani." **49** Alipokuwa
akiendelea kusema, mtu mmoja akaja kutoka kwenye nyumba ya kiongozi wa sinagogi, akisema, "Binti
yako amefariki. Usimsumbue mwalimu." **50** Lakini Yesu aliposikia hivyo, alimjibu, "Usiogope. Amini tu, na
ataokolewa." **51** Kisha alipoingia kwenye hiyo nyumba, hakuruhusu mtu yeyote kuingia pamoja naye,
isipokuwa Petro, Yohana na Yakobo, baba yake binti, na mama yake. **52** Sasa watu wote walikuwa
wanaomboleza na kutoa sauti kwa ajili yake, lakini akasema, "Msipige kelele, hajafa, lakini amelala tu." **53**
Lakini wakamcheka kwa dharau, wakijua kuwa amekufa. **54** Lakini Yeye, akimshika binti mkono, akaita
kwa sauti, akisema, "Mtoto, inuka" **55** roho yake ikamrudia, na akainuka wakati huohuo. Akaamrisha
kwamba, apewe kitu furani kwa ili ale. **56** Wazazi wake wakashangaa, lakini aliwaamuru wasimwambie
mtu kilichokuwa kimetokea.

---

## Luka 08 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

Kuna nyakati katika maelezo ya sura hii ambapo kuna mabadiliko ya ghafla katika mada. Mtafsiri hapaswi kulainisha mabadiliko haya.

### Dhana maalum katika sura hii

### Miujiza

Miujiza ya Yesu katika sura hii inaonyesha kwamba alikuwa na mamblaka juu ya mambo yanayozidi udhibiti wa binadamu. Inaonyesha pia kwamba kumwabudu Yesu ni jibu sahihi kwa matendo yake.

### Takwimu muhimu za matamshi katika sura hii

### Mifano

Mfano ni hadithi fupi inayotumikiwa kwa kuonyesha fundisho ya maadili au wa kidini. Sura hii ina mfano mrefu, unaofunua ukweli kwa wale wanaomwamini Yesu. Pia yanaficha ukweli huo huo kutoka kwa wale wanaomkataa Yesu. Mifano kwa kawaida huchukua fomu ya hadithi.

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

### Kaka na Dada

Sura hii inaanzisha dhana ya kaka na dada "wa kiroho". Maandiko hutumia maneno haya kwa kutaja uhusiano kati ya Waisraeli. Hapa, wale wanaomfuata Yesu sasa wanajulikana kama kaka na dada. and )

---

### Luke 8:1

**Taarifa ya jumla:**
mistari hii inatoa mrejesho wa habari za Yesu kuhusu kuhubiri wakati anasafiri.

**Ilitokea**
Hiki kipande cha maneno kimetumika hapa kuweka alama ya sehemu ya habari mpya.

**waliokuwa wameponywa na roho wachafu na magonjwa mbalimbali**
"Ambao Yesu amewaweka huru kutokana na roho chafu na kuwaponya na magonjwa"

**Mary... na wanawake wengi.**
"Wanawake watatu waliokuwa wanaitwa: Mariam, Yoana, na Susana.

**Yoana, mke Kuza, Meneja wa Herode.**
Yoana alikuwa mke wa Kuza, na Kuza alikuja meneja wa Herode. "Yoana, Mke wa meneja wa Herode."

### Luke 8:4

**Taarifa ya yumla:**
Yesu aliwaambia mfano wa mpandaji kwa makutano. Alieleza maana ya ke kwa wanafunzi wake.

**Sasa**
Hili neno linaonyesha mwanzo wa kitendo katika habari.

**mpandaji alienda kupanda mbegu**
"mkiulima alienda kupanda baadhi ya mbegu shambani"

**zikakanyagwa chini ya miguu**
"Zilikanyagwa pia mara zilipoota"

**wakazila**
"Walizila zote"

**Zilipooza**
"Miche ikakauka na kupooza"

**hazikuwa na unyevunyevu**
"ardhi ilikuwa kavu"

### Luke 8:7

**taarifa unganishi**
Yesu anamaliza kuwaambia mfano makutano

**zikasongwa**
Miti ya miiba ikachukua madini, maji, na mwanga, kwa hiyo miche ya mkulima haikukua vizuri.

**zikazaa mazao**
"Kuzaa mavuno" au "Kuzaa mbegu zaidi"

**Yeyote mwenye masikio ya kusikia na asikie.**
inaweza kuwa ni kiasili sana kwa baadhi ya lugha kutumia nafsi ya pili: "Wewe mwenye sikio la kusikia, sikia."

**Yeyotemwenye sikio la kusikia**
" Anayeweza kusikia" au "Yeyote anayenisikia mimi"

**na asikie**
"Na asikilize vizuri" au "na awe makini kwa kile ninachokisema"

### Luke 8:9

**Ujumbe wa kuunganisha**
Yesu anaanza kusema kwa wanafunzi wake.

**Mmepewa upendeleo wa kujua**
"MUngu amewapa ninyi zawadi ya kuelewa" au "Mungu amewafanya watu kuelewa"

**siri ya ufalme wa Mungu**
Hizi ni kweli kwamba zimejificha lakini Yesu aliwafunulia.

**wakiona wasione**
"kupitia wanachoona, hawatajua." "kupitia wanavyoona vitu, hawatavielewa" au "kupitia wanavyoona vitu vikitokea, hawataelewa vina maanisha nini."

**wakisikia wasielewe**
"Kupitia wanavyosikia hawatelewa." "kupitia wanavyosikia maelekezo, hawataelewa ukweli."

### Luke 8:11

**Ujumbe wa kuunganisha:**
Yesu anaaza kuelezea maana ya mfano wa udongo kwa wanafunzi wake.

**mwovu shetani hulichukua neno mbali kutoka moyoni**
Hii inamaanisha kuwa anawafanya kusahau neno la Mungu ambalo wamelisikia.

**hulichukua mbali**
Kwenye mfano hii ilikuwa kama fumbo la ndege anayedaka mbegu. jaribu kutumia maneno kwa lugha yako ambayo hutunza picha hii.

**kutoka moyoni mwao**
Hii ina maana kuwa shetani hukichukua neno mbali mbali na hamu zao za kuliamini neno la Mungu.

**ili kwamba wasiamini na kuokolewa**
Tangu mwanzo hili lilikuwa kusudi la mwovu, inaweza kutafsiriwa kama. "Kwa sababu mwovu amezama, 'Hawataamini na hawataokolewa"' au "'Hawataweza kuamini kwa matokeo ambayo Mungu atawaokoa."

**wakati wa majaribu huanguka**
"Wakikutana na magumu wanaanguka mbali na Imani" au "Wanapokutana na magumu wanaacha kuamini"

## Luke 8:14

**husongwa na huduma na utajiri**
"huduma na utajiri na ubora wa maisha huwasonga." "kama palizi huzuia miche mizuri kukua, huduma, utajiri, na ubora wa maisha haya zinawabana hawa watu kukua."

**huduma**
"vitu ambavyo watu huogopa"

**ubora wa maisha haya**
"vitu ambavyo kwenye maisha watu hufurahia"

**hawazai matunda**
"hawazai kuzaa matunda." "kama mche ambao haukui na kuzaa matunda, hawawezi kukua na na kufanya kazi njema."

**kuazaa matunda ya uvumilivu**
"Kuzaa matunda ya Uvumilivu." Ni kama miche yenye afya inavyozaa matunda mazuri, wanatoa kazi njema kwa uvumilivu"

## Luke 8:16

**Ujumbe wa kuunganisha:**
Yesu aliendelea na mfano mwingine kisha akahitimisha kwa wanafunzi wake kwa kusisitiza jukumu la familia yake katika kazi yake.

**Sasa**
Hili neno limetumika hapa kuweka alama ya kuanza kwa mfano mwingine.

**kinara cha taa**
"meza" au "rafu"

**hakuna kitakachojificha ambacho hakitajulikana**
"kita kitu kilichojificha kitajulikana"

**au chochote kilicho sirini ambacho hakitajulikana kikiwa kwenye mwanga**
"na kila kitu ambacho ni siri kitajulikana na kuja kwenye mwanga"

**unapokuwa unasikiliza**
"jinsi gani unasikiliza katika kile ninawaambia" au "Jinsi unavyosikiliza neno la Mungu"

**aliye nacho**
"yeyote anayesikiliza" au "yeyote anayepokea ninachokifundisha"

**kwake ataongezewa zaidi**
"vingi atapewa." "Mungu atampa vingi"

**asiye nacho**
"yeyote ambaye hataaelewa" au "yeyote ambaye hatapokea kile ninachofundisha"

## Luke 8:19

**Ndugu**
Hawa walikuwa wadogo zake Yesu nusu ndugu.

**ikaelezwa kwake**
"watu wakamwambia" au "mtu fulani akamwambia"

**wanahitaji kukuona**
"wanasubiri kukuona" au " na wanataka kukuona"

**Mama yangu na ndugu zangu ni wale wanaolisikia neno la Mungu na kulitii**
"Wale wanaolisikia neno la Mungu na kulitii wanafanana na mam yangu na ndugu zangu kwangu" au "Wale wanaosikia neno la Mungu na kulitii ni mhimu sana kwangu kama mama yangu na ndugu zangu"

## Luke 8:22

**ujumbe wa kuunganisha**
Yesu na wanafunzi wake kisha wakatumia mashua kuvuka ziwa Genasareti. wanafunzi wakajifunza megi kuhusu nguvu ya Yesu kupitia dhoruba iliyotokea.

**Sasa ilitokea**
Neno hili limetumika hapa kuonyesha alama wa mwanzo wa kipande kipya cha kile kilichotekea.

**ziwa**
Hili ni ziwa Genesareti ambalo liliitwa ziwa la Galilaya.

**walipoanza kuondoka**
"walipotoka"

**akalala usingizi**
"Alilala"

**dhoruba kali yenye upepo ikaja**
"upepo wenye nguvu ghafla ukaanza kupiga"

## Luke 8:24

**Bwana mkubwa**
Neno la kigriki ambalo limetafsiriwa hapa kama "Bwana mkubwa" siyo neno la kawaida kwa "Bwana mkubwa" hili linahisiana na mtu mwenye mamlaka, na si kwa mtu ambaye anamiliki mtu mwingine. "Bosi" au "Msimamizi" au na neno ambalo linamlenga mtu mwenye mamlaka, kama "Mheshimiwa"

**akaukemea**
"alizungumza kwa kasi"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**vikatulia**
"upepo na mawimbi wakakoma"

**Imani yenu iko wapi?**
Yesu alikuwa anawakemea kwa upole kwa sababu walikuwa hawamwamini kuwa atawajali. "Mlipaswa kuwa na imani" au "Mlipaswa kuniamini"

**Huyu ni nani**
"Ni mtu wa namna gani huyu."

**kwamba anaamuru**
Hii inaweza ikawa mwanzo wa sentensi chache: "Anaamuru"

### Luke 8:26

**ujumbe wa kuunganisha**
Yesu na wanafunzi wake wakaja pwani kwa Wagerasi ambapo Yesu aliondoa mapepo mengi kutoka kwa mwanaume.

**Mkoa wa Gerasini**
Wagerasini walikuwa ni watu kutoka mji ulioitwa Gerasa.

**usawa wa Galilaya**
"Upande mwingine wa Galilalya"

**mtu fulani kutoka mjini**
"mtu kutoka mji wa Gerasa"

**na huyu mtu alikuwa na nguvu za giza**
"mtu ambaye nguvu za giza zilimwendesha" au "huyu mtu alikuwa anaendeshwa na nguvu za giza"

**Kwa muda mrefu alikuwa havai nguo.... lakini aliishi kwenye makaburi**
Hii ni taarifa ya nyuma kuhusu huyu mtu aliyekuwa na mapepo.

**alikuwa havai nguo**
"hakuwa anavaa nguo"

**Makaburini**
Hizi ni sehemu ambazo watu huwa wanaweka miili ya watu waliokufa, yawezekana ni mapango. ukweli kwamba mtu huyu alikuwa anaishi humo inaashiria kuwa haya hayakuwa mashimo yaliyochimbwa chini ya ardhi.

### Luke 8:28

**Alipomwona Yesu**
"yule mwenye pepo alipomwona Yesu"

**akalia kwa sauti**
"alipiga kelele" au "alipiga yowe"

**akaanguka chini mbele yake**
"alilala chini ya ardhi mbele ya Yesu." Hakuanguka kwa ajali kama ajali.

**kwa sauti kubwa akisema**
"Alisema kwa sauti ya juu" au "Alipiga kelele"

**Nimefanya nini kwako**
"Kwa nini unanitesa mimi"

**mwana wa Mungu aliye juu**
Hiki ni cheo kikubwa sana kwa ajili ya Yesu.

**mara nyingi amepagawa**
"mara nyingi walikuwa wanamshika mtu huyu" au "mara nyingi huenda ndani mwake." Hii inatuambia jinsi Pepo alivyofanya mara ya nyingi kabla ya Yesu kukutana naye.

**hata kama alikuwa amefungwa.... na kuwekwa chini ya ulinzi**
"Hata kama watu walimfunga... na kumbana na kumlinda"

### Luke 8:30

**Jeshi**
imetafsiriwa hii na neno ambalo linahusu kikundi kikubwa cha maaskari au watu. Katika tafsiri zingine zinasema "Legioni." "Kikosi cha" au Brigedia"

**twende kwenye shimo**
"Kumtoka mtu na kwenda kwenye shimo"

### Luke 8:32

**Kundi la Nguruwe lilikuwa likichunga juu ya kilima**
ona

**lilikuwa likichunga juu ya kilima**
"lilikuwa karibu linakula majani juu ya kilima"

**iyo wale mapepo**
Neno "Hivyo" limetumika hapa kuweka alama ya tukio lililotokea kwa sababu ya kitu fulai kingine kilichotokea huko nyuma. kwa jambo hili. Yesu akayaambia mapepo kwamba yaweza kwenda kwa nguruwe.

**likakimbia**
"Kimbia kwa haraka sana"

### Luke 8:34

**wakakimbia**
"kwa haraka wakakimbia mbali"

**wakamwona mtu ambaye mapepo yalikuwa yamemtoka**
"walimwona mtu ambaye mapepo yamemtoka"

**alikuwa amevaa vizuri**
"Alikuwa amevaa nguo"

**mwenye akili timamu**
"alikuwa na akili timamu" au "alikuwa anaishi kawaida"

**amekaa kwenye miguu ya Yesu**
"amekaa chini, akimsikiliza Yesu"

**na waliogopa**
"walimwogopa Yesu"

## Luke 8:36

**mmoja wao aliyeona kilichotokea**
Hawa walikuwa watu waliokuwa na mtu yule wakati Yesu alifanya mapepo yaondoke.

**mtu aliyekuwa anaongozwa na mapepo alivyoponywa**
Yesu amemwokoa mtu aliyekuwa na mapepo yakimwongoza" au "Yesu alimponya mtu alikuwa na mapepo yakimwongoza"

**mkoa wa Gelasini**
"Eneo hilo la Gerasini" au "eneo ambapo watu wa wagerasini waliishi"

**walikuwa na hofu kuu**
"wakajawa na hofu." au "hofu kubwa iliwajaa."

## Luke 8:38

**Mtu yule**
wakati mwingine unapaswa kuaza na hii. "Kabla ya Yesu ana wanafunzi wake kuondoka, yule mtu" au "Kabla ya Yesu na wanafunzi wake hawajawasha mashua yao, mtu"

**Nyumba yako**
"kaya yako" au "familia yako"

## Luke 8:40

**Ujumbe wa kuunganisha:**
wakati Yesu na wanafunzi wake waliporudi Galilaya upande mwingine wa ziwa, alimponya binti wa mtawala wa sinagogi mwenye miaka 12 na pia mwnamke aliyekuwa akitokwa na damu miaka 12.

**taarifa za jumla**
Mistari hii inatupa taarifa za nyuma kuhusu Yairo.

**makutano wakamkaribisha**
"Kwa furaha ya makutano wakamsalimia"

**Tazama akaja mtu mmoja anaitwa Yairo**
Neno "Tazama" linatutazamisha sis kwa Yairo kama mtu mpya katika habari hii. lugha yako inaweza kukawa na njia nyingine ya kufanya hivi. "Kulikuwa na mtu aliyeitwa Yairo."

**mmoja kati ya viongozi katika sinagogi**
"mmoja wa viongozi katika sinagogi la mtaa" au "'kiongozi wa watu walikutana kwenye sinagogi katika eneo hilo"

**akaanguka miguuni pa Yesu**
(1) "Alianguka kwenye miguu ya Yesu" au (2) "alilala chini kwenye ardhi katika miguu ya Yesu." Yairo akuanguka kwa ajali. alifanya vile kama ishara ya ubinadamu na heshima kwa Yesu.

**alikuwa katika hali ya kufa**
"alikuwa katika hali ya kufa" au "alikuwa karibu na kifo"

**Na alipokuwa akienda**
Watafsiri wengine wanaweza kusema kwanza, "Hivyo Yesu alikubali kwenda na yule mtu."

**makutano walikuwa wakimsukuma dhidi yake**
"makutano walikuwa wakijaa kwa kubanana kumzunguka Yesu"

## Luke 8:43

**mwenye kutokwa damu**
"alikuwa anatokwa na damu nyingi" alikuwa akitokwa damu kutoka na tumbo lake hata kama haikuwa kawaida ya wakati wake. kwa kabila baadhi wanaweza wakawa na njia ya upole kuhusiana na hali hii.

**hakuna aliyemponya hata mmoja**
"lakini hakuna hata mmoja wao wa kumtibu" au "hakuna hata mmoja wao aliweza kumponya"

**kugusa pindo la vazi lake**
"aligusa pindo la vazi lake" Wanaume wa kiyahudi walivaa Taso juu ya makunjo ya nguo zao kama sehemu ya mavazi ya sherehe zao kama amri katika amri za Mungu. Hii inaonyesha ndiyo alichogusa.

## Luke 8:45

**Bwana Mkubwa**
Neno liliotafsiriwa hapa kama "Bwana mkubwa" siyo neno la kawaida kwa "Bwana mkubwa." Hii inaenda kwa mtu mwenye mamlaka, lakini si kwa mtu mwingine yeyote. "Bosi" au "Msimamizi" au na neno ambalo ni la kawaida limetumika kuelezea mtu aliye kwenye mamlaka, kama vile "Mheshimiwa"

**umati wa watu wanakusukuma na wanakusonga**
Kwa kusema hiv, Petro alikuwa akihusisha kila mmoja anaweza kumgusa Yesu. hii ni taarifa thabiti inaweza kufanywa kwa wazi kama ni mhimu katika UDB

**nilijua nguvu zimetoka kwangu**
"Nimesikia uponyaji nguvu zimetoka kwangu." Yesu hakupotwza nguvu au kuwa mdhaifu, lakini nguvu yake inamponya mwanamke.

## Luke 8:47

**hawezi kuficha alichokifanya**
"hawezi kutunza siri ya kile alichokifanya." "kwamba asingeweza kuendelea kutunza kama siri maana yeye ni yule aliyemgusa Yesu."

**akaanza kutetemeka**
"akatetemeka kwa hofu"

**akaanguka chini mbele za Yesu**
yawezekana maana ni 1). "aliinama chini mbele za Yesu" au 2) alilala chini kweye ardhi katika miguu ya Yesu. "hakuanguka kiajali. alifanya hivi kama ishara ya ubinadamu na heshima kwa ajili ya Yesu.

**mbele ya**
"Kwenye sehemu ya" au "Mbele"

**Binti**
Hii ilikuwa ni aina ya kusema kwa mwanamke. Kabila lako linaweza kuwa na njia nyingine ya kuonyesha huu wema.

**imani yako imekufanya uwe vizuri**
"Kwa sababu ya Imani yako, umekuwa vizuri." "Kwa sababu umeamini, umeponywa"

**Enenda kwa Amani**
Hii ni njia ya kusema, ""Kwa heri" na kutoa baraka kwa wakati mmoja. "Unapokwenda, Usiogope hata kidogo" au "Mungu akupe amani unapoenda"

## Luke 8:49

**Alipokuwa akiendelea kusema**
"wakati Yesu alipokuwa akiongea kwa mwanamke"

**kiongozi wa sinagogi**
Hii inarudi kwa Yairo.

**alimjibu**
"Yesu alimjibu Yairo"

**ataokolewa**
"Nitamponya"

## Luke 8:51

**Kisha alipokuja kwenye nyumba**
"Kisha walipokuja katika nyumba, Yesu"

**isipokuwa Petro, Yohana na Yakobo, baba yake binti, na mama yake**
"aliwaruhusu Petro, Yohana, Yakobo, baba yake binti, na mama yake kuingia ndani"

**watu wote walikuwa wanaomboleza na kutoa sauti kwa ajili yake**
"watu wote walikuwa wanaonyesha huzuni zao na kulia kwa sauti kwa sababu binti amekufa"

## Luke 8:54

**Mtoto, inuka**
"Binti mdogo, amka"

**roho yake ikarudi**
"akawa mzima" au "akawa hai tena"

**roho**
"pumzi" au "Uhai"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 9

1 Akawaita wale kumi na wawili pamoja, akawapa uwezo na mamlaka juu ya mapepo yote na kuponya
magonjwa. 2 Akawatuma waende kuhubiri ufalme wa Mungu na kuponya wagonjwa. 3 Akawaambia,
"Msichukue chochote kwa ajili ya safari yenu wala fimbo, wala mkoba, wala mkate, wala pesa wala
msichukue kanzu mbili. 4 Nyumba yoyote mtakayo iingia, kaeni humo mpaka mtakapo ondoka mahali
hapo. 5 Na kwa wale wasio wapokea, mtakapo ondoka mji huo, jikung'uteni vumbi katika miguu yenu kwa
ushuhuda juu yao". 6 Wakaondoka na kwenda kupitia vijijini, wakitangaza habari njema na kuponya watu
kila mahali. 7 Sasa Herode, mtawala, alisikia yote yaliyo kuwa yakitokea alitaabika sana, kwa sababuu
ilisemekana na baadhi kwamba Yohana mbatizaji amefufuka kutoka wafu, 8 na baathi kwamba Elia
amekwisha tokea, na kwa wengine kwamba mmoja wa manabii wa zamani amefufuka katika wafu tena. 9
Herode alisema, "nilimchinja Yohana, lakini huyu ni nani ninae sikia habari zake? Na Herode alitafuta njia
ya kumwona Yesu. 10 Wakati waliporudi wale waliotumwa, wakamwamwambia kila kitu walicho fanya.
Akawachukua pamoja naye, akaenda peke yake katika mji uitwao Bethsadia. 11 Lakini makutano
wakasikia kuhusu hili wakamfuata, na aliwakaribisha, na akaongea nao kuhusu ufalme wa Mungu, na
aliwaponya wale waliohitaji uponyaji. 12 Siku ikaanza kuisha, na wale kumi na wawili wakaenda kwake na
kusema, "Watawanye makutano kwamba waende katika vijiji vya karibu na mijini wakatafute mapumziko
na chakula, kwa sababu tupo eneo la nyikani." 13 Lakini akawaambia, "Nyie wapeni kitu cha kula."
Wakasema "Hatuna zaidi ya vipande vitano vya mikate na samaki wawili, isipokuwa tungeenda na
kununua chakula kwa ajili ya kusanyiko hili la watu." 14 Kulikua na wanaume wapatao elfu tano pale.
Akawambia wanafunzi wake. "Wakalisheni chini katika makundi ya watu wapatao hamsini kwa kila kundi.
15 Kwa hiyo wakafanya hivyo na watu wa wakaketi chini. 16 Akachukua mikate mitano na samaki wawili
na akatazama mbinguni, akavibariki, na kuvimega katika vipande, akawapa wanafunzi wake ili waviweke
mbele ya makutano. 17 Wote wakala na wakashiba, na vipande vya chakula vilivyo baki viliokotwa na
kujaza vikapu kumi na viwili. 18 Nayo ikawa kwamba, alipokuwa akiomba peke yake, wanafunzi wake
walikuwa pamoja naye, na akawauliza akisema, "watu husema mimi ni nani?" 19 Wakijibu, wakasema,
"Yohana mbatizaji, lakini wengine husema Eliya, na wengine husema mmoja wa manabii wa nyakati za
zamani amefufuka tena." 20 Akawambia, "Lakini ninyi mwasema mimi ni nani?" Akijibu Petro akasema,
"Kristo kutoka kwa Mungu." 21 Lakini kwa kuwaonya, Yesu akawaelekeza kutomwambia yeyote juu ya hili,
22 akasema kwamba mwana wa Adamu lazma ateseke kwa mambo mengi na kukataliwa na wazee na
Makuhani wakuu na waandishi, na atauawa, na siku ya tatu atafufuka. 23 Akawambia wote, "kama mtu
yeyote akitaka kunifuata, lazima ajikane mwenyewe, achukue msalaba wake kila siku, na anifuate. 24
Yeyote ajaribuye kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini yeyote apotezae maisha yake kwa faida yangu,
atayaokoa. 25 Je kitamfaidia nini mwanadamu, kama akiupata ulimwengu wote, lakini akapoteza au
akapata hasara ya nafsi yake? 26 Yeyote atakaye nionea aibu mimi na maneno yangu, kwake yeye mwana
wa Adam atamuonea aibu atakapo kuwa katika utukufu wake, na utukufu wa Baba na malaika watakatifu.
27 Lakini ninawaambia ukweli, kuna baadhi yenu wasimamao hapa, hawata onja umauti mpaka wauone
ufalme wa Mungu." 28 Ikatokea yapata siku nane baada ya Yesu kusema maneno haya kwamba
akawachukua pamoja nae Petro, Yohana na, Yakobo, wakapanda mlimani kuomba. 29 Na alipokuwa katika
kuomba, muonekano wa uso wake ulibadilika, na mavazi yake yakawa meupe na ya kung'aa. 30 Na
tazama, walikuwepo wanaume wawili wakiongea naye! Walikuwa Musa na Elia, 31 walionekana katika
utukufu. Waliongea kuhusu kuondoka kwake, jambo ambalo alikaribia kulitimiza Yerusalem. 32 Sasa Petro
na wale waliokua pamoja naye walikuwa katika usingizi mzito. Lakini walipokuamka, waliuona utukufu
wake na wanaume wawili waliokuwa wamesimama pamoja nae. 33 Ikatokea kwamba, walipokuwa
wakiondoka kwa Yesu, Petro akamwambia, "Bwana, ni vizuri kwetu kukaa hapa na inatupasa tutengeneze
makazi ya watu watatu. Tutengeneze moja kwa ajili yako, moja kwa ajili ya Musa, na moja kwa ajili ya
Eliya." Hakuelewa alichokuwa akiongelea. 34 Alipokuwa akisema hayo, likaja wingu na likawafunika; na
waliogopa walipoona wamezunguwa na wamezungukwa na wingu. 35 Sauti ikatoka kwenye wingu
ikasema, "Huyu ni Mwanangu mteule. Msikilizeni yeye." 36 Sauti iliponyamaza, Yesu alikuwa peke yake.
walikaa kimya, na katika siku hizo hawakumwambia yeyote lolote miongoni mwa waliyoyaona. 37 Siku
iliyofuata, baada ya kutoka mlimani, kusanyiko kubwa la watu lilikutana naye. 38 Tazama, mwanaume
kutoka kwenye kusanyiko alilia kwa sauti, akisema, "Mwalimu ninakuomba umtazame mwanangu, kwa
kuwa ni mwanangu wa pekee. 39 Unaona roho chafu humshika, na mara hupiga kelele, na pia humfanya
achanganyikiwe na kutokwa povu kinywani. Nayo humtoka kwa shida, ikimsababshia maumivu makali. 40
Naliwasihi wanafunzi wako kuikea itoke. lakini hawakuweza." 41 Yesu akajibu akasema, "Enyi kizazi
kisichoamini na kilichopotoka, mpaka lini nitkaa nanyi na kuchukuliana nanyi? Mlete mwanao hapa." 42


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

Kijana aliokuwa anakuja, roho cha ikamuangusha chini na kumtikisa kwa fujo. Lakini Yesu aliikemea ile
roho chafu, alimponya mvulana, na kamkabidhi kwa baba yake. 43 Wote walishangazwa na ukuu wa
Mungu. Lakini walipokuwa wakistaajabu wote kwa mambo yote aliyo yaliyotedeka, akasema kwa
wanafunzi wake, 44 "Maneno yawakae masikioni mwenu, kwa kuwa Mwana wa Adamu atatolewa
mikononi mwa wanadamu." 45 Lakni hawakuelewa maana ya maneno hayo, na yalifichwa machoni pao, ili
wasije wakalielewa. Waliogopa kumuuliza kuhusu neno hilo. 46 Kisha mgogoro ulianza ulizuka miongoni
mwao i juu ya nani angekuwa mkuu. 47 Lakini Yesu alipotambua walichokuwa wakihojiana mioyoni mwao,
alimchukua mtoto mdogo, na kumuweka upande wake, 48 na akasema, " kama mtu yeyote akimpokea
mtoto mdogo kama huyu kwa jina langu, anipokea mimi pia, na yeyote akinipokea mimi, ampokea pia
aliyenituma, kwa kuwa aliye mdogo kati yenu wote ndiye alie mkuu" 49 Yohana akajibu akasema, "Bwana,
tulimuona mtu akifukuza pepo kwa jina lako na tukamzuia, kwa sababu haambatani na sisi." 50 Lakini
Yesu akamwambia, "Msimzuie, kwa kuwa asiye kinyume na ninyi ni wa kwenu" 51 Ikatokea kwamba,
kulinga na siku zilivyokua zikikaribia zsiku zake za kwenda mbinguni, kwa uimara alielekeza uso wake
Yerusalemu. 52 Akatuma wajumbe mbele yake, nao wakaenda na kuingia katika kijiji cha Wasamaria ili
wamtayarishie mahali. 53 Lakini watu huko hawakumpokea, kwasababu alikua ameelekeza uso wake
Yerusalemu. 54 Wanafunzi wake Yakobo na Yohana walipo liona hili, wakasema, "Bwana unahitaji tuamuru
moto ushuke chini kutoka mbinguni uwateketeze?" 55 Lakini aliwageukia akawakemea. 56 Kisha
walikwenda kijiji kingine. 57 Walipokuwa wakienda katika njia yao, mtu mmoja akamwambia,
"Nitakufuata popote uendapo." 58 Yesu akamwambia, "Mbweha wanamashimo, ndege wa angani wana
viota, lakini mwana wa Adamu hana pakulaza kichwa chake." 59 Ndipo akamwambia mtu mwingine,
"Nifuate." Lakini yeye akasema, "Bwana, niruhusu kwanza niende nikamzika baba yangu," 60 Lakini yeye
akamwambia, "Waache wafu wawazike wafu wao, lakini wewe nenda ukautangaze ufalme wa Mungu kila
mahali." 61 Pia mtu mwingine akasema. "Nitakufuata, Bwana, lakini niruhusu kwanza nikawaage walio
katika nyumba yangu." 62 Laki Yesu akamwambia hakuna mtu, atiaye mkono wake kulima na kuangalia
nyuma atakayefaa kwa ufalme wa Mungu."

---

## Luka 09 Maelezo ya Jumla

#### Dhana maalum katika sura hii

#### "Kuhubiri ufalme wa Mungu"

Kuna mzozo kati ya wasomi kuhusu maana ya ufalme we Mungu hapa unamaanisha utawala wa Mungu duniani au ujumbe wa injili

#### Eliya

Nabii Malaki alitabiri kwamba siku moja Eliya angerudi kabla Masihi hajaja. Yesu anaelezea kwamba Yohana Mbatizaji alitimiza unabii huu kwa kumtumikia Mungu kwa namna ileile kama Eliya. Eliya ametajwa kwa njia mbili tofauti katika sura hii, kama mtu halisi na kurudi kimfano kwa Eliya. and )

#### "Ufalme wa Mungu"

Maneno 'ufalme wa Mungu' katika sura hii yalitumikiwa kwa kutaja ufalme utakapokuja wakati maneno haya yaliyosemwa.

#### "Waliona utukufu [wa Yesu]"

Katika Maandiko utukufu wa Mungu unaonekana kama mwanga wa kunga'a sana. Utukufu wa Mungu Katika Maandiko utukufu wa Mungu unaonekana kama mwanga wa kunga'a sana kwa mtu anayeuona. Tukio hilo, iliyoandikwa katika sura hii, linaitwa "kugeuka sura," asababu Yesu aligeuka sura na kubadilika sura ili aonyeshe utukufu wake wa kiungu. and )

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

### Kitendawili

Kitendawili ni taarifa inayoonekana kuwa ya ajabu, ambayo ni kana kwamba inajikana yenyewe, lakini kwa hakika sio ya ajabu. Mfano wa kitendawili katika sura hii: "Yeyote anayetaka kuokoa maisha yake ataipoteza, na yeyote anayepoteza maisha yake kwa ajili yangu ataipata." (Luka 9:24).

### "Mwana wa Binadamu"

Yesu anajiita mwenyewe kama "Mwana wa Binadamu." Lugha zingine haziwezi kuruhusu mtu kujitaja mwenyewe kama 'mtu wa tatu.'

### "Kupokea"

ULB inatumia neno hili mara kadhaa katika sura hii kwa maana mbalimbali. Yesu anasema, "Yeyote akipokea mtoto mdogo kama huyu kwa jina langu, yeye ananipokea pia, na yeyote akinipokea mimi, anapokea pia yeye aliyenituma"

---

## Luke 9:1

**Sentensi Unganishi**
Yesu anawakumbusha wanafunzi wake waasitegemee pesa na vitu nyao, anawapa nguvu, na pia awatuma waende sehemu mbalimbali.

**nguvu na mamlaka**
Maneno haya mawili yametumika pamoja kuonesha kwamba wale kumi na wawili walikuwa na uwezo na haki ya kuponya watu.

**magonjwa**
"ugonjwa"

**aliwatuma nje**
"aliwatuma sehemu mbalimnbali" au "aliwambia waende"

## Luke 9:3

**Akawaambia**
"Yesu akawaambia wale thenashara"

**Usichukue chochote**
AT." usichukue chochote" au "usije na chochote"

**Kwaajili ya safari yako**
"kwa ajili ya safari yako" au "wakati unasafiri." Wasichukue chochote kwaajili ya safiri yao yote, watapita kijiji kwa kijiji mpaka warudi kwa yesu.

**fimbo**
"fimbo" au "fimbo ya kutembelea." ilikuwa ni fimbo kubwa iliyotumika kumsaidia mtu wakati wa kupanda au kwenye barabara mbovu. ilikuwa ikitumika pia kujilinda dhidi ya watekaji.

**Mkoba**
ni mfano wa kibebeo(begi) ambalo wasafiri hutumia kwa kubebea kile anachokitaka safarini.

**Mkate**
AT: "Chakula"

**Nyumba yeyote mtakayoingia**
"Nyumba yoyote mtakayoingia"

**Kaeni humo**
"Bakieni humo" au "muishi kwa mda ndani ya ile nyumba kama wageni"

**Kutoka mahali hapo**
"kutoka mjini" au "kutoka katika sehemu ile"

## Luke 9:5

**Na kwa wale watakao kataa kuwapokea**
AT: " hiki ndo mtakachofanya kwa watu watakao kataa kuwapokea"

**mtakapo ondoka**
"waliondoka sehemu ambayo yesu alikuwepo"

**kila mahali**
"walienda kila mahali"

## Luke 9:7

**Taarifa kamili**
Mistarin hii inapingan kutoa taarifa kuhusu Herode

**sasa**
hili neno limetumika kuonesha pumziko katika story kamili. Hapa Luka anasimulia taarifa za msingi za Herode.

**Herode, mkuu wa mkoa**
Inamwakilisha Herod ambae alikuwamtawala wa moja ya nne ya Israel.

**alitaabika sana**
"alikasirika sana" au "alikuwa anashangaa"

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**Nilimkata kichwa Yohana**
AT: "niliwaamlisha wanajeshi wangu wamkate kichwa Yohana"

## Luke 9:10

**Sentensi unganishi**
Ingawa wafuasi walirudi kwea yesu na wakaenda Bethadia kupumzika, makutano walimfata yesu awaponye na kusikiliza mafundisho yake. Aliwasaidia kugawanyisha mkate na samaki wakati wanarudi nyumbani.

**wale waliotiumwa**
AT: " wale mitume kumi na mbili aliowatuma yesu"

**walirudi**
"walirudi pale alipokuwa yesu"

**wakamuambia**
"mitume wakamuambia yesu"

**kila kitu walichofanya**
Hii ina wakilisha mafundisho na uponyaji waliofanya walipoenda kwenye miji.

**aliwachukua , aliondoka mwenyewe**
Yesu na mitume wake waliondoka wenyewe. AT: "aliwachukua wakaondoka pamoja"

**Bethadia**
Hili ni jina la mji.

## Luke 9:12

**Siku ikaanza kuisha**
"jua lilivyoanza kuzama" au " siku ilivyoanza kuisha"

**Watawanye makutano**
"kuwaambia makutano waondoke"

**labda twende tukanunua chakula**
AT: " labda tutaenda kununa chakula" au " labda kama twende kununua chakula" au unaweza kuanza sentyensi mpya "kama wewe unataka tuwalishe, tutatakiwa kwenda kununua chakula."

**kama wanaume elfu tano**
"kama wanaume elfu tano." hii number haijumuishi wanwake na watoto ambao yaweza kuwa walikuwepo.

**wakalisheni**
"waambieni wakae"

**"hamsini kila "**
"50 kila "

## Luke 9:15

**Wakafanya hivyo**
wanfunzi wakawakalisha makutano kwenye makundi ya watu hamsini hamsini.

**akachukua**
"yesu akachukua"

**mkate**
kiwango maarumu cha mkate wa kuokwa. AT: "mkate mzima"

**na akiangalia**
"wakati anaangalia" au " baada ya kuangalia"

**juu mbinguni**
Hii inawakilisha kuangalia juu, kuelekea mawinguni. Wayahudi waliamini kuwa mbingu iko juu mawinguni.

**watenge mbele ya**
"kuwagawia" au " kuwapa"

**wakashiba**
AT: "walikula kama walivyotaka"

## Luke 9:18

**Sentesi kiunganishi:**
Yesu akisali, pekee yake na wanfunzi wake, na kuanza kuongelea kuhusu yesu ni nani. Yesu anawaambia kuhus kifo chake na ufufuo utakao fata na kuwataka wamfate yeye hata iweje.

**Nayo ikawa kwamba**
Hii sentensi inaashiria mwanzo wa tukio jipya.

**alipokuwa akiomba**
"yesu alipokuwa akiomba"

**kusali pekee**
Wanfunzi walikuwa na yesu, lakini alikuwa anasali pekee yake na yeye mwenyewe kwa siri.

**kujibu, wakasema**
"walimjibu wakisema"

**Yohana mbatizaji**
AT: "wengine wanasema wewe ni Yohana mbatizaji"

**kutoka nyakati za zamani**
"ambae aliishi muda mrefu uliopita"

**amefufuka tena**
"alifufuka"

## Luke 9:20

**Akawaambia**
"yesu akawaambia wanafunzi wake"

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**kujibu, Petro akasema**
"Petro alijibu na kusema" au "Petro alijibu kwa kusema"

**Lakini kwa kuwaonya, Yesu akawaelekeza**
AT: "Lakini yesu waliwaonya na kuwaelekeza" au '"Ndipo yesu waliwapa onyo kali"

**kutomwambia yoyote**
"kutokumwambia mtu yoyote" au " wasimwambie mtu yoyote." Hii inaashiria msemo. AT: "lakini kuwaaonya, yesu aliwaambia, "msimwambie mtu yoyote"

**kwamba mwana wa Adamu atateseka kwa vingi**
AT: "kwamba watu wanweza msababishia mwana wa Adamu kuteseka sana." Hii pia inaweza kutafasiriwa kama msemo wa moja kwa moja kwa sababu ipo kwenye UBS.

**na kukataliwa na wazee na wakuu wa Makuhani na waandishi**
AT: "na wazee, wakuu wa makuhani, na waandishi watamkataa"

**na atauliwa**
AT: " na watu watamuua"

**kwenye siku ya tatu**
"siku tatu baada ya kufa" au "kwenye siku ya taut baada ya kifo chake"

**atafufuka**
"atawekwa hai." AT: "Mungu atamfanya hai tena" au "atafufuka"

### Luke 9:23

**akawambia**
yesu akawaambia

**wote**
Hii inamaanisha wanafunzi wake wote waliokuwa na yesu.

**kunifata mimi**
"kunifata mimi" au "kuongozana na mimi kama mwanafunzi"

**ajikane**
AT: "kujijitoa kwa nfasi yake mwenywe," au "na aache tamaa yake mwenyewe"

**achukue msalaba wake kila siku**
"auchukue na aubebe msalaba wake kila siku." Hii haimaanishi aubebe msalaba kila siku. Inamaanisha wafuasi wake wakatae vitu wanavyovitakana wawe tayari kuteseka na kufa ili kumtii yesu.

**anifuate**
"kenda pamoja na mimi" au "kuanza kunifuata na kuendelea kunifuata"

**kitamfaidia nini mwanadamu...binafsi?**
Yesu anatumia swali kuwafundisha wanafunzi wake. AT: "mwanadamu hapati kitu chochote kizuri...binafsi."

**kama akiupata ulimwengu wote**
"kama atapata kila kitu ulimwenguni"

**akapoteza au akapata hasara yake binafsi**
AT: "yeye mwenyewe atapotea"

### Luke 9:26

**na maneno yangu**
AT: "na nilichosema" au "na nilichofundisha"

**yeye mwana wa Adam atamuonea aibu**
"mwana wa Adam atamuonea aibu"

**mwana wa Adam**
Yesu alikuwa anajiongelea yeye mwenyewe. AT: "mimi, mwana wa Adam"

**atakapo kuwa katika utukufu wake**
Yesu anajiongelea yeye mwenyewe kupitia nafsi ya tatu. AT: "nitakapokuja kwenye utukufu wangu"

**baadhi yenu wasimamao hapa**
"baadhi yenu mliosimama na mimi hapa"

**hawata ionja mauti mpaka wauone ufalme wa Mungu**
AT: "watauona ufalme wa Mungu kabla hawajafa" au "utauona ufalme wa Mungu kabla huja"

### Luke 9:28

**Sentensi kiunganishi**
Siku nane baada ya Yesu kuwaambia kuwa baadhi hawatakufa kabla ya kuuona ufalme wa Mungu, Yese anaenda mlimani kuomba pamoja na Petro na Yohana ambao walilala wakati Yesu anabadilika muonekano .

**Ikatokea**
Hii sentenso imetumika hapa kuashiria tukio muhimu katika hadithi. Kama lugha yako ina namna nzuri ya kufanya hivi, unaweza kufikria kuitumia hapo.

**siku nane**
"siku 8"

**maneno haya**
Hii inaashiria Yesu alisema kwa wanafunzi wake kwenye mistari inayoendelea.

**juu ya mlima**
Haiko wazi ni juu kiasi gani walienda. AT: "pembeni mwa mlima"

**meupe na ya kung'aa**
"nyeupe ya kungaa na kali" au "nyeupe kali na ya kungaa"

### Luke 9:30

**Tazama, walikuwepo wanaume wawili wanaongea**
Neno "tazama" hapa liaashiria tuwe makini kwa taarifa ya kushangaza inayofata. AT: "ghafla kulikuwa na wanaume wawili wanaongea" au "ghafla wanaume wawili walikuwa wanaongea."

**walionekana katika utukufu**
Hii sentensi ya kuoanaisha inatoa taarifa kuhusu Musa na Elisha. AT: "na walionekana wenye utukufu"

**kuondoka kwake**
"kuondoka kwake" au "atakavyooondoka." AT: "kifo chake."

### Luke 9:32

**sasa**
Hii sentensi ya imetumika kuashiria pumziko kwenye hadithi wenyewe inayotolewa, Hapa Luka anasimuili taarifa kuhusu Musa na Yakobo, na Yohana.

**waliuona utukufu wake**
Hii inamaanisha mwanga uliowaka kuwazunguka. AT: "Aliona mwanga mkali unawaka kwa yesu" au "waliona mwanga mkali unatokea ndani ya Yesu"

**wanaume waili walikuwa wamesimama nae**
Inamaanisha Musa na Elisha.

**Ikatokea kwamba**
Hii sentensi imetumika hapa kuonesha matukio yananza. Kama lugha yako ina maana nzuri zaidi , unaweza fikiria kuitumia hapa.

**Bwana**
Neno lililotafasiriwa hapa kama "Bwana" sio neno la kwawaida kumaanisha " Bwana." Hili linamaanisha mtu mwenye mamlaka na sio mtu anaemmiliki mtu mwingine. AT: "Bosi"au "kiongozi" au neno huwa linatumika kueleza mtu mwenye mamlaka, mfano kama "Sir"

**malazi**
"hema" au "kibanda"

### Luke 9:34

**Alipokuwa akisema vitu hivi**
"Wakati Petro alikuwa akisema viotu hivi"

**waliogopa**
Hawa wanafunzi wazima hawakuogopa mawingu. Msitari unaashiria woga usio wa kawaida ulitokea juu yao kupitia mawing. AT: "walishitushwa"

**walivyokuwa wamezungukwa na wingu**
AT: "kama mawingu yalivyo wazunguka"

**Sauti ikatoka winguni, ikisema**
AT: "Mungu akaongea nao kupitia mawinguni akisema"

**mwanangu uliyechaguliwa**
Neno "kuchaguliwa" linatoa taarifa kuhusu mtoto wa Mungu. Haisemi kuwa Mungu alikuwa na mtoto zaidi ya mmoja. AT: "mwanangu niliuyekuchagua" (UDB) au "mwanangu,uliyechaguliwa"

**walikaa kimya, na katika siku hizo... vitu walivyoona**
Hii ni taarifa inayosema kilichotokea baada ya hadithi kama matokeo ya hadithi yenyewe.

**siku hizo**
Hizi zinaweza kuwakirisha siku ambazo mpaka Yesu anachukuliwa mawinguni baada ya ufufuo au yaweza kuwa baada ya siku ambazo Yesu alitoa kauli.

### Luke 9:37

**Sentensi unganishi**
Siku ya pili baada ya Yesu kubali muonekano, Yesu alitoa pepo lililokuwa limemuingia kijana ambae wanafunzi walishindwa kumponya.

**Ikatokea**
Hii tungo inaashiria mwanzo wa sehemu nyingine ya hadithi, Kama lugha yako ina maana nzuri zaidi , unaweza fikiria kuitumia hapa.

**Tazama, mwanaume kutoka kwenye kusanyiko**
Neno "tazama" linatujulisha juu ya mtu mpya anaetokea kwenye hadithi. lugha yako ina maana nzuri zaidi. Kiingereza kinatumia "kulikuwa na mwanaume kwenye kusanyikao"

**unaona, roho**
Tungo "unaona" inatutambulisha kwa pepo kwenye hadithi ya mwanadamu. lugha yako ina maana nzuri zaidi. Kiingereza kinatumia "kulikuwa na pepo"

**Lilitoka kwa tabu**
inaweza kuwa na maana hizi 1) "vigumu kumuacha kamwe mwanangu" (UDB) au 2) "ni ngumu kwa mwanangu wakati linatoka"

**povu mdomoni**
Wakati mtu anamshituko, wanaweza kupata shida kupimua au kumeza. Hii inasababisha povu jeupe kutokea kwenye midomo yao. Kama lugha yako inaweza elezea vizuri, itumie.

### Luke 9:41

**Yesu akajibu akasema**
"kwenye jibu Yesu akasema"

**Enyi kizazi kisicho amini na wachafu**
Hii ilielezwa kwenye umati uliokuwa limekusanyika, na sio kwa wanafunzi.

**mpaka lini nitazidi kuwabeba**
Hapa "nita" ni wingi. Yesu anatumia swali kukemea umati. AT: "nimefanya merngi na bado hamuamini!"

**Mlete mwanao hapa**
Hapa "wako" ni umoja. Yesu snaongea moja kwa moja na baba wa anaemshughulikia.

**aliokuwa anakuja**
"anakuja" au "yuko anakuja"

**aliikemea**
"alizungumza kwa ukali kwa"

### Luke 9:43

**Wote walishangazwa kwa ukuu wa Mungu**
Yesu alifanya miujiza , lakini umati haukutambua nguvu za Mungu zilitumika kuponya.

**aliyo yafanya**
"kwamba Yesu alifanya"

**Maneno haya yazame kwa undani masikioni mwenu**
AT: "sikizia kwa makini na ukumbuke" au "usisahau hili"

**kwa kuwa mwana wa Adamu atatolewa kwenye mikoni ya wanadamu**
Hapa " mikono" inamaanisha nguvu au utawala. AT : "wanadamu watamkabidhisha mwan wa Adamu kwenye mamlaka."

**mwana wa Adamu**
Yesu anajiongelea mwenyewe kwenye nafsi ya tatu. AT: "mimi, mwana wa Adamu"

**Lakni hawakuelewa maana ya neno hili**
AT: "wahakujua anaongelea kifo chake"

**na lilifichwa juu yao**
AT: "Mungu aliwafichia maana yake"

### Luke 9:46

**Taarifa kamili**
Mzozo kuhusu madarsks ukanza kati ya wanafunzi.

**kati yao**
"kati ya wanafunzi"

**wakihojiana mioyoni mwao**
AT: "kufikiria juu ya mtu mmoja mmoja" au "kufikilia kimoyoni"

**jina langu**
Hii inawakilisha mtu anaefanya jambo au an kama muwakirishi wa Yesu. AT: "kwa sababu yangu

**anampokea pia**
AT: "ni kama amenipokea mimi"

**aliyenituma mimi**
"Mungu, aliyenituma"

### Luke 9:49

**Petro akajibu akasema**
Yohana alikuwa anajibu juu ya kile Yesu alichosema kuhusu ukuu. Hakuwa anajibu swali. alitaka kujua mtu aliye yalhimiza mapepo kutoka atakuwa na nafasi gani kati ya wanafunzi. AT : "kwenye kujibu, Yohana akasema" au "Yohana alijibu kwa Yesu"

**Bwana**
Neno lililotafasiriwa hapa kama "Bwana" sio neno la kwawaida kumaanisha " Bwana." Hapa linamaanisha mtu mwenye mamlaka na sio mtu anaemmiliki mtu mwingine. AT: "Bosi"au "mweshimiwa"

**jina lako**
Hii inamaanisha mtualiyekuwa anaongea alikuwa na nguvu na mamlaka ya Yesu.

**Msimzuie**
AT: "mruhusu aendelee"

**kwa kuwa asiye kinyume na ninyi ni wa kwenu**
Baadhi ya lugha ina misemo inayomaanisha kitu kile kile. AT: "kama mtu asipokuzuia , ni kama anakusaidia" au "kama mtu hatendi kinyume na wewe, anafanya sawa sawa na matakwa yako."

### Luke 9:51

**Taarifa kwa ujumla**
Na sas ni dhahili kuwa Yesu ameamua kwenda Yerusalem.

**Ikatokea kwamba**
Hii tungo imetumika hapa kuashiri mwanzo wa sehemu mpya ya hadithi

**siku zake za kwenda juu zilikaribia**
"muda ulikuwa unafika wa yeye kwenda juu" au " muda ulikaribia wa yeye kwenda juu"

**aliazimia**
"kudhamilia" au "kukusudia"

**weka uso wake**
AT: "alifikiria akilini mwake" au "aliamua"

**kumuandalia**
Hii inamaanisha kufanya mipango ya kufika katika eneo, inawezekana kuunganisha eneo la kuongealea, anaeo la kukaa, na chakula.

**Hawakumpokea**
"hawakumkaribisha" au au hawakutaka abaki"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

### Luke 9:54

**liona hili**
"aliona kwamba wasamaria hawakumpokea Yesu"

**tuamuru moto ushuke chini kutoka mbinguni uwateketeze**
Yakobo na Yohana walipendekeza njia hii ya hukumu kwa sababu walijua kwamba hivi ndivyo manabii kama Elia walivyo hukumu watu waliomkataa Mungu.

**aliwageukia akawakemea**
"Yesu aligeuka na kuwakemea Yakobo na Yohana." Yesu hakuwahukumu Wasamaria , kama wanafunzi walivyo tegemea.

### Luke 9:57

**mtu mmoja**
Huyu hakuwa moja ya wanafunzi

**Mbweha wanamashimo**
Yesu anajibu kwa mithali ili kufundisha watu kuhusu kuwa mwanafunzi wa Yesu. Yesu anajibu kwamba kama mtu atahitaji kumfuata, kwamba mtu huyo anaweza asiwe na nyumba. AT: "Mbeha wana mashimo...wala sehemu ya kulaza kichwa. Hivyo usitegemee kama utakuwa na nyumba"

**Mbweha**
Hawa ni wanyama wa nchi sawa na mbwa. Wanalala katika mapango au shimo katika arthi.

**ndege wa angani**
"ndege wanaoruka angani"

**mwana wa Adamu**
"Yesu anaongea kuhusu yeye mwenyewe katika nafsi ya tatu"

**hana pakulaza kichwa chake**
"sina sehemu ya kulaza kichwa changu" or "wala sehemu ya kulala." Yesu anakuza ili kujenga hoja kwambaalikuwa hakalibishwi popote kuishi.

### Luke 9:59

**Sentensi Unganishi**
Yesu anaendelea kuongea na wanafunzi wake akiwa pembezoni mwa barabara.

**Mnifuate mimi.**
Hii ina maanisha kuwa mfuasi wa Yesu na kwenda pamoja naye.

**Mniruhusu kwanza niondoke**
"Kabla sijafanya hivyo, mniache niende."

**Waache wafu wawazike wafu wa kwao**
Kwa sababu watu waliokwisha kufa hawawezi kumzika mtu yeyote, Maana inayokusudiwa hapa ni ya kwamba watu walio wafu katika roho wawazike watu walio wafu katika mwili.

### Luke 9:61

**Nitakufata**
"nitaungana nawe kama mwanafynzi" au " niko tayari kukufata"

**kwanza ni ruhusu nikuagae**
"kabla sijafanya hivyo, niruhusu niseme kwaheri" au "niruhusu kwanza niwaambie naondoka"

**walio katika nyumba yangu**
"nyumba yangu" au "watu wa nyumabani kwangu"

**Hakuna anaefaa kwa ajili ya ufalme wa Mungu**
Yesu anajibu mithari kumfundisha mwandamu kwa mwanafunzi wake, Yesu anamaanisha mtu hafai kwa ajili ya ufalme wa Mungu kama anafata watu wa nyuma badala ya kumfata Yesu

**"Atiae mkono wake kwenye jembe**
AT: " baada ya kuanza kulima shamba lake" au "baada ya kuanza kuandaa shamba lake"

**akaangalia nyuma**
Mtu anaangalia nyuma wakati analima hawezi kuliongoza vizuri jembe pale linapotakiwa kwenda. Wanatakiwa kuwa makini kuangalia mbele ili walime vizuri.

**kufaa kwa**
"kufaa kwa" au " kizuri kwaajili ya"

---


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 10

1 Baada ya mambo hayo, Bwana akachagua sabini wengine, na kuwatuma wawili wawili wamtangulie
katika kila mji na eneo alilotarajia kwenda. 2 Akawaambia, "Mavuno ni mengi, lakini wafanyakazi ni
wachache. Hivyo basi muombeni Bwana wa mavuno, ili kwamba atume haraka wafanyakazi katika
mavuno yake. 3 Enendeni katika miji. Angalieni, ninawatuma kama kondoo katikati ya mbwa mwitu. 4
Msibebe mfuko wa pesa, wala mikoba ya wasafiri, wala viatu, wala msimsalimie yeyote njiani. 5 Katika
nyumba yeyote mtakayo ingia, kwanza semeni, 'Amani iwe katika nyumba hii.' 6 kama mtu wa amani yupo
pale, amani yenu itabaki juu yake, lakini kama sivyo, itarudi kwenu. 7 Bakini katika nyumba hiyo, kuleni
na mnywe watakachokitoa, kwa maana mfanyakazi anastahili mshahara wake. Msihame kutoka nyumba
hii kwenda nyingine. 8 Mji wowote muuingiao, na wakawapokea, kuleni chochote kitakachowekwa mbele
yenu, 9 na ponyeni wagonjwa waliomo humo. Semeni kwao, 'Ufalme wa Mungu umekuja karibu yanu' 10
Lakini katika mji wowote mtakaoingia, na wasiwapokee, nendeni nje katika barabara na semeni, 11 'Hata
vumbi katika mji wenu lililonata miguu mwetu tunalikung'uta dhidi yenu! Lakini tambueni hili, Ufalme wa
Mungu umekaribia.' 12 Ninawambieni kwamba siku ya hukumu itakuwa ni usitahamilivu zaidi kwa
Sodoma kuliko mji huo. 13 Ole kwako Korazini, Ole kwako Bethsaida! Kama kazi kuu zilizo fanyika ndani
yako ingalifanyika Tiro na Sidoni, Wangelitubu zamani sana, wakikaa ndani ya nguo za gunia na majivu.
14 Lakini itakuwa usitahamilivu zaidi siku ya hukumu kwa Tiro na Sidoni zaidi yenu. 15 Wewe
Kapernaumu, Unafikiri utainuliwa mpaka Mbinguni? Hapana, utashushwa chini mpaka kuzimu 16 Atakaye
wasikiliza ninyi anisikiliza mimi, na yeyote atakaye wakataa anikataa mimi, na yeyote anikataaye mimi
anmtakaa aliyenituma" 17 Wale sabini walirudi kwa furaha, wakisema, "Bwana, hata mapepo wanatutii
katika jina lako." 18 Yesu akawaambia, "Nilimwona Shetani akianguka kutoka mbinguni kama radi. 19
Tazama, nimewapa mamlaka ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za adui, na hapana chochote kwa
njia yoyote kitakachowadhuru. 20 Hata hivyo msifurahi tu katika hili, kwamba roho zinawatii, lakini
furahini zaidi kwamba majina yenu yameandikwa mbinguni." 21 Katika mda uleule alifurahi sana katika
Roho Mtakatifu, na kusema, "Ninakusifu wewe, Baba, Bwana wa mbingu na dunia, kwa sababu
umeyaficha mambo haya kutoka kwa wenye hekima na akili, na kuyafunua kwa wasio fundishwa, kama
watoto wadogo. Ndio, Baba, kwa kuwa ilipendeza katika machoni pako." 22 "Kila kitu kimekabidhiwa
kwangu na Baba yangu, na hakuna afahamuye Mwana ni nani ila Baba, na hakuna afahamuye Baba ni
nani ila Mwana, na ye yote ambaye Mwana hutamani kujifunua kwake." 23 Akawageukia wanafunzi,
akasema faraghani, "Wamebarikiwa wayaonayo haya ambayo ninyi mnayaona. 24 Ninawambia ninyi,
kwamba manabii wengi na wafalme walitamani kuona mambo myaonayo, na hawakuyaona, na kusikia
kusikia mnayoyaikia, na hawakuyasikia." 25 Tazama, mwalimu fulani wa sheria ya Kiyahudi alisimama na
kumjaribu, akisema, "Mwalimu, nifanye nini niurithi izima wa milele?" 26 Yesu akamwambia,
"Kimeandikwa nini katika sheria? Unaisoma je?" 27 Akajibu akasema, "Utampenda Bwana Mungu wako
kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote, na jirani yako
kama nafsi yako mwenyewe." 28 Yesu akasema, "Umejibu kwa usahihi. Fanya hivi na utaishi." 29 Lakini
mwalimu, akitamani kujihesabia haki mwenyewe, Akamwambia Yesu, "Na jirani yangu ni nani?" 30 Yesu
akijibu akasema, "Mtu fulani alikuwa akitelemka kutoka Yerusalem kwenda Yeriko. Akaangukia kati ya
wanyang'anyi, waliomnyang'anya mali yake, na kumpiga na kumuacha karibu akiwa nusu mfu.. 31 Kwa
bahati kuhani fulani alikuwa akishuka katika njia hiyo, alipo muona alipita upande mwingine. 32 Vivyo
hivyo Mlawi pia, alipofika mahali pale na kumuona, akapita upande mwingine. 33 Lakini Msamaria mmoja,
alipokuwa akisafiri, alipita pale alipokuwa mtu huyo. alipomuona, alisukumwa kwa huruma. 34
Alimkaribia na kumfunga vidonda vyake, akimwiga mafuta na divai juu yake. Alimpandisha juu ya
mnyama wake, na kumpeleka katika nyumba ya wageni na kumhudumia. 35 Siku ilyofuata alichukua
dinari mbili, na akampatia mmiliki wa nyumba ya wageni na kumwambia, 'Muhudumie na chochote cha
ziada utakacho tumia, nitakulipa nitakaporudi.' 36 Ni yupi kati ya hawa watatu, unafikiri, alikuwa ni jirani
kwake yeye aliyeangukia kati ya wanyang'anyi?" 37 Mwalimu alisema, "Ni yule aliyeonesha huruma
kwake." Yesu akamwambia, "Nenda na ukafanye vivyo hivyo" 38 Sasa walipokuwa wakisafiri, waliingia
katika kijiji fulani, na mwanamke mmoja jina lake Martha alimkaribisha nyumbani kwake. 39 Alikuwa na
dada aliyeitwa Mariamu, aliekaa miguuni pa Bwana na kusikiliza neno lake. 40 Lakini Martha alijipa
shughuli nyingi za kuandaa mlo. Alikwenda kwa Yesu, na kusema, "Bwana, haujali kwamba dada yangu
ameniacha nihudumu peke yangu? Hivyo basi mwambie anisaidie." 41 Lakini Bwana alimjibu na
kumwambia, "Martha, Martha, una sumbuka juu ya mambo mengi, 42 lakini ni kitu kimoja tu cha muhimu.
Mariamu amechagua kilicho chema, ambacho hakitaondolewa kutoka kwake."

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

# Luka 10 Maelezo ya Jumla

### Dhana maalum katika sura hii

### Mavuno

Mavuno ni picha ya kawaida inayotumiwa katika Agano Jipya. Wakati watu wanakuja kwa Yesu na kumwamini inajulikana kama mavuno.

### "Alikuwa jirani"

Dhana ya "kuwa jirani" ilikuwa muhimu katika desturi ya inchi za kale za Mashariki ya Karibu, ambayo kukaribisha wageni ilikuwa heshimu sana. Katika sura hii, "jirani ina maana ya mtu anayesihi karibu au labda mtu mwingine ye yote. "Alikuwa jirani" pia hutumiwa kumaanisha "alikuwa jirani mwema."

---

## Luke 10:1

**Taarifa kwa ujumla**
Yesu anawatuma zaidi ya watu sabini mbele yake. Hao sabini wanarudi na furaha , na Yesu anawajibu kwa kumuabudu baba wa mbinguni.

**sasa**
Neno hili limetumika kuashiria tukio jipya katika hadithi.

**sabini**
"70." matoleo mengine yanasema "sabini na mbili" au "72." utatakiwa kuweka maezezo yanayosema ivyo.

**Aliwatuma huko, wawili wawili**
"Aliwatuma huko katika makundi ya wawili wawili" au "Aliwatuma huko wawili wawili katika kila kundi"

**Akawaambia**
Hii iikuwa kabla hawajaondoka. AT: "Hiki ndo alichowaambia" au "kabla hajaondok aliwaambia."

**Mavuno ni mengi, lakini wafanyakazi ni wachache**
"kulikuwa kuna mazao mengi, lakini

## Luke 10:3

**enendeni katika njia zenu**
"enendeni kwenye majiji" au "enendeni kwa watu"

**ninawatuma nje kama kondoo katikati ya mbwa mwitu**
Hii inamaana ya kuwa kuna watu wangewadhuru wale ambao Yesu aliwatuma. Majina ya wanyama wengine yangeweza kuwakilishwa. AT;"Nitakapowatuma huko nje watu watawadhuru kama ambavyo mbwa mwitu huwaingilia kondoo"

**Mbwa mwitu**
Hii imetafasiriwa na maana halisi ya "mbwa wa mwituni" au "mbwa wakali" au jina la mnyama wa pekee kama mbwa ambaye watu huwa wanamfaham.

**Musibebe mfuko/mikoba yenye pesa.**
"Musichukue Mikoba yenye pesa ndani yake"

**Msimusalimie yeyote muwapo njiani.**
Yesu alikuwa anasisitiza ya kuwa waende kwa haraka huko mjini na wafanye hii kazi. Hakuwambia wawe wakorofi au watu wabaya.

## Luke 10:5

**Amani iwe katika nyumba hii**
Hii ilikuwa ni salamu na baraka. Hapa "nyumba" inawakilisha watu wanaoishi ndani ya nyumba. AT: "watu wa nyumba hii na wapokee amani."

**mtu wa amani**
"mtu mwenye amani." Huyu ni mtu anaetaka kuwa na amani na Mungu na watu.

**amani yenu itabaki juu yake**
AT: "atakuwa na amani aliyombarikia"

**kama sivyo**
AT: "kama hakuna mtu mwenye amani huko" au "mwenye nyumba sio mtu wa amani"

**itarudi kwenu**
"hatokuwa na hiyo amani" au "hatoipokea hiyo amani uliyombarikia"

**Mbakie katika nyumba ile ile.**
Yesu hakumaanisha waendelee kubakia ndani ya nyumba kwa siku nzima, ila wapate kulala katika nyumba mojakila usiku. AT:" Kuendelea kulala katika nyumba"

**Mfanya kazi anasitahili mshahara wake**
Yesu alikuwa alikuwa akizungumzia wale watu aliowatuma huko nje. Kwa sababu wangekuwa wakiwafundisha na kuwaponya watu, hivyo watu wangewapatia mahali pa kukaa pamoja na chakula.

**Msiende nyumba kwa nyumba**
AT:" Msilale sehemu/nyumba tofauti tofauti katika kila usiku"

## Luke 10:8

**Na wakawapokea ninyi.**
" Kama wakiwakaribisha"

**Kuleni chochote kitakachowekwa mbele yenu**
AT " kuleni chakula chochote watakacho wapeni"

**Ufalme wa Mungu umekaribia kwenu,**
Hii inarejea ya kuwa kazi ya ufalme wa Mungu ilikuwa ikifanyika mahali pale kupitia uponyaji kwa wanafunzi wake na mafundisho ya Yesu. AT:" Munaweza kuuona ufalme wa Mungu ukiwazunguka ninyi".

## Luke 10:10

**Na wasiwapokee**
"kama wakiwakataa"

**Hata vumbi lililonatia miguu yetu kutoka katika mji wenu tunalikung'uta thidi yenu**
Kwa sababu Yesu alikuwa akiwatuma watu hawa huko nje katika makundi ya watu wawili wawili, hivyo watu wawili wawili walikuwa wasemaji kwa kila kundi. kwa hiyo lugha zenye tafasiri ya neno "sisi" ndo ilikuwa hivyo. AT: "Kama ambavyo mlitukana sisi, na ndivyo tutakavyo wakana ninyi. Na hata tumekataa vumbi linalo toka katika mji wenu linalonata katika miguu yetu".

**Lakini tambueni hili, Ufalme wa Mungu umekaribia.**
Neno "Lakini tambueni hiii" linatambulisha onyo. Linamaanisha "hata kama mkitukana sisi, haibadilishi maana ya ufalme wa Mungu kuwepo hapa".

**Ufalme wa Mungu umekaribia.**
"Ufalme wa Mungu upo kati yenu"

**Ninasema kwenu**
Yesu alikuwa akiyasema haya kwa watu sabini(70) ambao alikuwa akiwatuma huko nje, Alisema haya ili kuonesha ya kuwa alikuwa aseme kitu cha muhimu zaidi"

**Siku ya hukumu**
kwa kawaida neno linasema "siku ile"Lakini wanafunzi wake walielewa ya kuwa, alimanisha siku ya mwisho ya hukumu kwa wenye dhambi.

**Itakuwa ni usitahamilivu zaidi kwa Sodoma kuliko mji huo.**
"Mungu hataihukumu Sodoma kwa nguvu kama atakavyouhukumu ule mji" AT "Mungu atawahukumu watu wa ule mji kwa nguvu zaidi ya atakavyo wahukumu watu wa Sodoma".

## Luke 10:13

**Ole kwako Korazini, Ole kwako Bethadia!**
Yesu aliongea kana kwamba watu wa Korazini na Bethadai walikuwepo, lakini hawakuwepo.

**Kama kazi kuu zilizo fanyika ndani yako ingali fanyika Tire na Sidoni.**
Yesu anaelezea hali ambayo ingetokea hapo nyuma lakini haikutokea. AT: " Kama mtu angelitenda miujiza kwa watu wa Tire na Sidoni ambayo ningetenda kwenu"

**Wangeli tubu zamani sana,**
"Watu wanyonge walioishi huko wangelionesha huzuni ya dhambi zao".

**wakikaa ndani ya nguo za gunia na majivu.**
"Wakivaa nguo za magunia na kukaa kwenye majivu"

**Lakini itakuwa usitahamilivu zaidi siku ya hukumu kwa Tire na Sidoni zaidi yenu.**
AT: "Lakini kwa sababu hamkutubu na kuniamini mimi hata kama mliniona nikitenda miujiza, Mungu atawaadhibu zaidi ya jinsi ambavyo atawadhibu Tire na Sidoni"

**Katika hukumu**
"Siku ya mwisho ambapo amaungu atamuhukumu kila mmoja.

**Wewe Kaperanaum,**
Yesu anaongea na watu wa mji wa Kaperanaum, kama vile walikuwa wakisikiliza kumbe ndivyo sivyo.

**Unafikiri utainuliwa mpaka Mbinguni?**
Yesu anatumia swali kuwakalipia watu wa Kaperanaum kwa kujisifu kwao. AT : "Hautakaamufikie juu mpka mbinguni" au "Mungu hatakuheshimu"

**Utashushwa chini mpaka kuzimu**
AT: "Utaenda chini kuzimu" au " Mungu atakupeleka kuzimu".

## Luke 10:16

**Atakaye wasikiliza ninyi anisikiliza mimi**
AT: "Mtu akiwasikiliza, ni kama ananisikiliza mimi"

**Yeyote awakataapo anikataa mim**
"Atakaye wakataa ninyi, amenikataa mimi".

**Yeyote anikataaye mimi amtakaa aliyenituma"**
Atakaye nikataa mimi, itakuwa kama anamkataa yeye aliyenituma".

**Aliyenituma mimi.**
Hii inarejea Mungu Baba aliemuteuwa Yesu kwa ajili ya kazi Maalumu. AT: " Mungu, alienituma".

## Luke 10:17

**Wale sabini walirudi**
Lugha zingine zinaweza sema ya kuwa wale sabini walienda kwanza huko nje kama ambavyo UDB

inasema. Hii ni taarifa ya mwanzo inayoweza fanya ya mwisho.

**Sabini**
Unawezataka kuongeza idadi, kwa maana ya kwamba, "Andishi mbalimbali wana 72 badala ya 70.

**Katika jina lako**
kwa hapa, "Jina" lina rejea Nguvu na mamulaka ya Yesu".

**Nilimtazanma Shetani akianguka kutoka mbinguni kama radi.**
Yesu alitumia mfano hai, kuonesha jinsi ambavyo Mungu alikuwa akimshinda shetani pale ambapo wanafunzi wake 70 walikuwa wakihubiri mjini".

**Mamlaka ya kukanyaga nyoka na nge**
"Mamlaka ya kukanyaga nyoka na kusaga n'ge" Maana zinazotambulika ni kama, 1)Hii inarejea uhalisia wa nyoka na n'ge. au 2) Nyoka na nge ni vielelezi wa roho chafu. UDB inatoa tafasiri ya kuwa hizi ni roho chafu. "Nimewapa haki na mamlaka ya kuteka roho chafu"

**Mamlaka juu ya pepo wabaya na n'ge**
Hii inamaana ya kuwa watafanya haya na hawatadhurika. AT:Watatembea juu ya nyoka na n'ge na hawatawadhuru".

**N'ge**
Mnyama mdogo mwenye sehemu mbili za kushikia mfano wa pembe, na kitolea sumu mfano wa sindano kali kwenye mkia wake.

**Na nguvu zote dhidi ya adui**
Nimewapa mamlaka kuzishinda nguvu za adui" au " Nimewapa mamlaka ya kumshinda adui" na adui ni Shetani.

**Msifurahi tu katika hili,kwamba roho wanawatii**
" Msifurahi tu kwa sababu wanawatii"'

**majina yenu yameandikwa mbinguni.**
AT: "Mungu ameyaandika majina yenu mbinguni" au "Majina yenu yapo katika orodha ya watu ambao ni ufalme wa mbinguni".

## Luke 10:21

**Bwana wa mbingu na dunia**
AT: "Mtawala juu ya kilammoja na kilakitu mbinguni na duniani"

**Vitu hivi**
Hii inarejea mafundisho ya nyuma ya Yesu juu ya mamlaka ya wanafunzi wake. Inaweza kuwa rahisi kusema " vitu hivi" na msomi aweze kuielewa maana.

**Wenye hekima na ufahamu**
" kutoka kwa watu wenye hekima na ufahamu". AT: "kutoka kwa watu wanaofikiri kuwa waoni wenye hekima na ufahamu".

**kwa wasio fundishwa**
Hii inamaanisha wale watu wasio waza kuwa wao ni wenye hekima na wanawiwa kuyapokea mafundisho ya Yesu.

**Kama watoto wadogo**
"kama watoto wadogo". hii inawakilisha watu wanaojua ya kuwa si wenye hekima na maarifa.

**kwa kuwa ilikuwa nzuri na kupendeza katika macho yako.**
SAT: "kwa nyie mkiyafanya haya, yanawapendeza ninyi".

## Luke 10:22

**Kila kitu kimekabithiwa kwangu kutoka kwa Baba yangu**
AT: " Baba yangu amekabidhi kila kitu kwangu".

**Baba... Mwana.**
Hivi ni vichwa vikuu vya muhimu vinavyoelezea uhusiano kati ya Mungu na Yesu.

**Mwana**
Yesu alikuwa akijizungumzia yeye katika nafasi ya tatu.

**afahamuye Mwana ni nani**
Neno ambalo limetafasiriwa kama "Afahamuye" linamaanisha kujua kutokana na kumwelewa mtu. Mungu Baba anamjua Yesu kwa namna hiyo.

**Ila Baba**
Hii inamaanisha ni Baba peke yake anajua Mwana ni nani.

**na yeyote ambaye mwana anatamani kujifunua kwake**
AT: "na watu watajua Baba ni nani endapo Mwana atataka kuwadhihirishia Baba kwao".

## Luke 10:23

**Akawageukia wanafunzi, akasema kwa siri,**
Yawezekana hii ilikuwa katika wakati fulani. AT: "badaye, ambapo wanafunzi wakewalikuwa peke yao pamoja naye, akasema"

**Wamebarikiwa wavionavyo vitu mvionavyo**
Pengine hii ilikuwa na maana kwa watu wote waliokuwa wamekuja kumsikiliza Yesu AT: "Ni jinsi gani ilivyo vyema kwa wale wanaoona vitu mnavyoviona".

**Vitu hivi mvionavyo**
"Vitu ambavyo mmeniona mimi nikivifanya"

**Vitu hivi mvisikiavyo**
"Vitu ambavyo mmenisikia mimi nikiviongea".

## Luke 10:25

**Sentensi unganishi**
Yesu anajibu kwa kutumia simuilizi kwa mwalimu wa kiyahudi ambaye alitaka kumujaribu Yesu.

**Tazama, mwalimu fulani**
Hii pia ilitokea kwa wakati fulani, AT: "Siku moja Yesu alipokuwa akiwafundisha watu, Mwalimu fulani"(UDB)

**Tazama**
Hii inatupeleka moja kwa moja kwa mtu mpya katika simulizi. Pengine lugha yako ikawa ina namna ya kufanya hivi.

**Alimujaribu**
"Kumchanganya"

**Kimeandikwa nini katika sheria?**
Yesu anatumia mfano kumfundisha huyu Mwalimu wa kiyahudi. AT: "niambie ni nini Musa aliandika kwenye sheria"

**Unaisoma je?**
"Umesoma nini ndani yake?" au "Unaelewa nini ambacho unaweza sema?"

**Lazima umpende.... jirani kama wewe mwenyewe**
Mtu yule(myahudi) ananukuu kile Musa alichoandika kwenye sheria.

**Moyo wako.....roho yako....nguvu zako...akili yako**
Yote hii inamaanisha ya kuwa mtu lazima ampende Mungu kikamilifu na kila kitu chake

**Jirani yako**
Hii inamaanisha mtu aliepo katika jamii yako. AT: "raia mwenzako" au "watu wa jamii yako".

## Luke 10:29

**Lakini mwalimu, akitamani kujibibitisha kuwa**
Lakini alijaribu kutafuta njia ya kujisafisha yeye mwenyewe, hivyo akasema" au " lakini akataka kuonekana kuwa ni mwenye haki, akasema"

**Akajibu, Yesu akasema**
Yesu akamjibu yule mtu kwa kumwambia fumbo AT: " kwa kumjibu Yesu akamwambia simulizi hii"

**Akaangukia kati ya wanyang'anyi,**
" Alizungukwa na wanyang'anyi" au "wanyang'anyi wakamteka".

**Wakamvuaa na kumnyang'anya vya kwake**
"Walimchukulia vyote alivyokuwa navyo" au "Wakamuibia vitu vyake vyote"

## Luke 10:31

**Kwa bahati**
Hiki ni kitu ambacho hakuna alikuwa amepanga.

**kuhani fulani**
Maelezo haya yanatambulisha mtu mpya katika simuilizi, lakini haimutaji kwa jina lake.

**Na alipomuona**
"Na baada ya kuhani kumuona yule mtu aliekuwa amejeruhiwa".Kuhani ni mtu wa dini, hivyo watu walihisi ya kuwa angemsaidia yule mtu.Kwa sababu hakumsaidia aya hii ingeweza kutafasiriwa kama "lakini baaada ya kumuona" kuleta umakini kwa hii hali ambayo haikutokea kama ilivyokuwa ikitarajiwa.

**Akapita uapende mwingine wa barabara**
Inaonesha dhahiri ya kuwa hakumsaidia yule mtu mwenye majeraha. AT:"hakumsaidia yule mwenye majeraha badala yake alimpita".

## Luke 10:33

**Lakini msamaria mmoja**
Hii inatambulisha mtu mpya kwenye simulizi bila ya kutaja jina lake. Tunajua tu ya kuwa alikuwa msamaria . Wayahudi walikuwa wakiwadharau wasamaria na walikuwa wakimudhania ya kuwa hatamsaidia yule myahudi aliekuwa ameumizwa.

**Alipomuona**
"Baada ya msamaria kumuona yule mtu aliekuwa ameumizwa"

**Alisukumwa kwa huruma**
"Akamuonea huruma"

**Akamfunga vidonda vyake, akavimwagia mafuta na divai.**
Angekuwa ameweka yale mafuta na divai kwenye vidonda vyake, AT:" akaweka divai na mafuta kwenye vidonda na akavisokota kwenye nguo"

**Akavimwagia mafuta na divai**
Divai ilitumika kusafisha vidonda na mafuta yalitumika kuzuia kudhuriwa kwa vidonda

**Mnyaama wake**
"Mnyama wake mwenyewe". Huyu alikuwa mnyamaambaye alitumika kubeba mizigo mizito. inasemekana alikuwa punda.

**Dinari mbili**
"Mshahara wa siku mbili". Denari ni umoja wa denari.

**Mwenyeji wake.**
" Mwangalizi wake" au "mtu ambaye alimtunza na kuwa akribu naye"

## Luke 10:36

**Ni yupi kati ya hawa watatu unafikiri.**
AT:" Unafikiri nini? ni nani kati ya hawa watatu"

**Alikuwa jirani**
"Alijionesha mwenyewe kuwa jirani mwema"

**Yeye alieangukia kati ya wanyang'anyi.**
" Kakwe yeye ambaye wanyang'anyi walimteka"

### Luke 10:38

**Taarifa kamili**
Yesu anakuja kwenye nyumba ya Matha ambapo dada yake Mariam akawa akimsikiliza Yesu kwa umakini mkubwa.

**sasa**
Neno hili limetumika mahali hapa kuonesha tukio jipya

**walipokuwa wakisafiri,**
"Kama ambavyo Yesu na wanafunzi wake walikuwa wakisafiri"

**kijiji fulani**
Hii inatambulisha kijiji kama sehemu mpya,lakini hapakupewa jina.

**mwanamke mmoja jina lake Matha**
Hii inamtambulisha Matha kama mhusika mpya. Pengine lugha yako ikawa na namna nyingine ya kumtambulisha mtu mpya.

**alikaa miguuni mwa Bwana**
Hii ilikuwa kawaida na yenye heshima kwa mtu anayetaka kujifunza kwa mda ule. AT:" alikaa kwenye sakafu"

**na kusikiliza neno lake**
AT: "Na akasikiliza Mafundisho ya Bwana"

### Luke 10:40

**haujali...peke yangu?**
Martha alaikuwa analalamika kuwa Bwana alimruhusu Mariamu aketi amsikilize wakati kulikuwa na kazi nyingi za kufanya. Alimuheshimu Bwana, ndo maana alitumia swali la kejeli kufanya malaliko yake kuwa ya upole.AT: "inaonekana hujali..pekeyangu."

**Martha, Martha**
Yesu arudia rudia jian la martha kuonesha msisitizo. AT: "Mpendwa Martha" au "wewe Martha."

**ambacho hakitachukuliwa kutoka kwake**
Inaweza maanisha 1) " Sitachukua fursa yake" au "2) "Hatapoteza alichopatakwa sababu ananisikiliza."

---


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 11

1 Ilitokea wakati Yesu alipokuwa anaomba mahali fulani, mmoja wa mwanafunzi wake alimwambia,
"Bwana, tufundishe sisi kuomba kama Yohana alivyo wafundisha wanafunzi wake'. 2 Yesu akawaambia,
Msalipo, semeni, 'Baba, Jina lako litakazwe. Ufalme wako uje. 3 Utupe mkate wetu wa kila siku. 4
Utusamehe makosa yetu, kama nasi tunavyowasamehe wote waliotukosea. Usituongoze katika majaribu."
5 Yesu akawaambia, "Ni nani kwenu atakuwa na rafiki, ambaye atamuendea usiku, na kumwambia, Rafiki
niazime mikate mitatu. 6 Kwa sababu rafiki yangu amenijia sasa hivi kutoka safarini, nami sina cha
kumuandalia.' 7 Na yule aliyeko ndani akamjibu, usinitaabishe, Mlango umekwisha kufungwa, na watoto
wangu, pamoja nami tumekwisha kulala kitandani. Siwezi kuamka na kukupa wewe mikate. 8
Nawaambia, japo kuwa haamki na kukupatia mikate kama rafiki yake, kwa sababu ya kuendelea
kumgongea bila aibu, ataamka na kukupatia vipande vingi vya mikate kulingana na mahitaji yako. 9 Nami
pia nawaambieni, Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata, pigeni hodi nanyi mtafunguliwa. 10
Kwa kuwa kila mtu aombaye atapokea, na kila mtu atafutaye atapata, na kila mtu apigaye hodi, mlango
utafunguliwa kwake. 11 Ni baba yupi miongoni mwenu, mwanaye akimuomba samaki atampa nyoka
badala yake.? 12 Au akimuomba yai atampa nge badala yake?. 13 Kwa hiyo, ikiwa ninyi mlio waovu
mnajuwa kuwapa watoto wenu zawadi nzuri, je si zaidi sana Baba yenu wa mbinguni kwamba atawapa
Roho Mtakatifu hao wamuombao?" 14 Baadaye, Yesu akawa anakemea pepo, na mtu mwenye pepo
alikuwa bubu. Ikawa pepo lilipomtoka, mtu huyo aliweza kuongea. Umati wakastaajabu sana. 15 Lakii
watu wengine wakasema, huyu anaondo mapepo kwa Beelzebul, mkuu wa mapepo 16 Wengine
walimjaribu na kumtaka awaonyeshe ishara kutoka mbinguni. 17 Lakini Yesu aliyatambua mawazo yao na
kuwaambia, "Kila ufalme utakaogawanyika itakuwa ukiwa, na nyumba iliyo gawanyika itaanguka. 18
Kama Shetani atakuwa amegawanyika, ufalme wake utasimamaje? Kwa sababu mwasema natoa mapepo
kwa Belzebuli 19 Kama mimi natoa mapepo kwa Belzebuli, je wenzenu wanatoa mapepo kwa njia gani?
Kwa sababu hii, wao watawahukumu ninyi. 20 Lakini, kama natoa mapepo kwa kidole cha Mungu, basi
uflame wa Mungu umewajia. 21 Mtu mwenye nguvu aliye na silaha akilinda nyumba yake, vitu vyake
vitakaa salama. 22 Lakini akivamiwa na mtu mwenye nguvu zaidi, Yule mtu mwenye nguvu
atamnyang'anya silaha zake, na kuzichukua mali zake zote. 23 Yeye asiye pamoja nami yuko kinyume
nami, na yeye asiyekusanya pamoja nami hutapanya. 24 Pepo mchafu amtokapo mtu, huenda na kutafuta
mahali pasipo na maji ili ajipumzishe. Atakapokuwa amekosa, husema, 'nitarudi nilipotoka. 25 Akirudi na
kukuta nyumba imefagiliwa na imekaa vizuri. 26 Hivyo huenda na kutafuta mapepo saba walio waovu
kuliko yeye mwenyewe na kuwaleta waje wakae mahali pale. Na hali ya mtu huyo huwa mbaya kuliko
ilivyokuwa mara ya kwanza." 27 Ilitokea kwamba alipokuwa akisema maneno hayo, mwanamke fulani
alipasa sauti yake zaidi ya wote kwanye mkutano wa watu na kusema " Limebarikiwa tumbo lililo kuzaa
na matiti uliyoyanyonya" 28 Lakini yeye akasema, wamebarikiwa wale wasikio neno la Mungu na
kulitunza. 29 Wakati umati wa watu wanakusanyika na kuongezeka, Yesu akaanza kusema " Kizazi hiki ni
kizazi cha uovu. Hutafuta ishara, na hakuna ishara watayopewa zaidi ya ile ishara ya Yona. 30 Maana
kama Yona alivyokuwa ishara kwa watu wa Ninawi, ndivyo na Mwana wa Adamu atakavyokuwa ishara
kwa kizazi hiki 31 Malkia wa Kusini atasimama siku ya hukumu na watu wa kizazi hiki na kuwahukumu
wao, kwani yeye alitoka katika mwisho wa nchi ili aje asikilize hekima za Solomoni, na hapa yuko aliye
mkuu kuliko Solomoni. 32 Watu wa Ninawi watasimama katika hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki
siku ya hukumu watakihukumu, kwani wao walitubu kwa mahubiri ya Yona, na tazama, hapa yuko aliye
mkuu kuliko Yona. 33 Hakuna Mtu yeyote, awashaye taa na kuiweka sehemu ya chini yenye giza
isiyoonekana au chini ya kikapu, ila huwasha na kuweka juu ya kitu ili kila mtu aingiaye aweze kuona
mwanga. 34 Jicho lako ni taa ya mwili. Jicho lako likiwa zuri basi mwili wako wote utakuwa kwenye
mwanga. Lakini jicho lako likiwa baya basi mwili wako wote utakuwa kwenye giza. 35 Kwa hiyo,
mjihadhari ili mwanga ulio ndani yenu usitiwe giza. 36 Hivyo basi, kama mwili wako wote uko kwenye
mwanga, na hakuna sehemu iliyo katika giza, basi mwili wako utakuwa sawa na taa iwakayo na kutoa
mwanga kwenu." 37 Alipomaliza kuongea, Farisayo alimwalika akale chakula nyumbani kwake, naye Yesu
akaingia ndani na kuwa pamoja nao. 38 Na Mafarisayo wakashangaa kwa jinsi ambavyo hakunawa
kwanza kabla ya chakula cha jioni. 39 Lakini Bwana akawaambia, "Ninyi Mafarisayo mnaosha nje ya
vikombe na bakuli, lakini ndani yenu mmejaa tamaa na uovu. 40 Ninyi watu msio na ufahamu, Je yeye
aliyeumba nje hakuumba na ndani pia? 41 Wapeni masikini yaliyo ndani, na mambo yote yatakuwa safi
kwenu. 42 Lakini ole wenu Mafarisayo, kwani mnatoa zaka ya mnanaa na mchicha na kila aina ya mboga
ya bustani. Lakini mmeacha mambo ya haki na kumpenda Mungu. Ni muhimu zaidi kufanya yaliyo ya haki

na kumpenda Mungu, bila kuacha kufanya na hayo mengine pia. 43 Ole wenu Mafarisayo, kwa kuwa
mnapenda kukaa katika viti vya mbele kwenye masinagogi na kuamkiwa kwa salamu za heshima sokoni.
44 Ole wenu, kwani mnafanana na makaburi yasiyo na alama ambayo watu hutembea juu yake
pasipokujua." 45 Mwalimu mmoja wa sheria za Kiyahudi akamjibu na kumwambia, "Mwalimu,
unachokisema kinatuudhi pia sisi." 46 Yesu akasema, "Ole wenu, waalimu wa sheria! kwani mnawapa
watu mizigo mikubwa wasiyoweza kuibeba, walakini ninyi hamgusi mizigo hiyo hata kwa moja ya vidole
vyenu. 47 Ole wenu, kwa sababu mnajenga na kuweka kumbukumbu kwenye makaburi ya manabii' ambao
waliuwawa na mababu zenu. 48 Hivyo ninyi mwashuhudia na kukubaliana na kazi walizozifanya mababu
zenu, kwa sababu hakika waliwauwa manabii ambao mnajenga kumbukumbu katika makaburi yao. 49
Kwa sababu hiyo pia, hekima ya Mungu inasema, 'Nitawatumia manabii na mitume nao watawatesa na
kuwaua baadhi yao. 50 Kizazi hiki kitawajibika kwa damu ya manabii waliouawa tangu kuanza kwa dunia,
51 Kutoka damu ya Abeli hadi damu ya Zakaria, aliyeuawa katikati ya madhabahu na patakatifu. Ndiyo,
nawaambia ninyi, kizazi hiki kitawajibika. 52 Ole wenu waalimu wa sheria za Kiyahudi, kwa sababu
mmechukua funguo za ufahamu; nyie wenyewe hamuingii, na wale wanaotaka kuingia mnawazuia." 53
Baada ya Yesu kuondoka pale, Waandishi na Mafarisayo walimpinga na kubishana naye juu ya mambo
mengi. 54 wakijaribu kumnsana kwa maneno yake.

---

## Luka 11 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

Baadhi ya tafsiri hupendelea kuweka mbele kidogo mashairi au sala maalum. ULB na tafsiri nyingine nyingi za Kiingereza huingiza mistari ya 11: 2-4, ambayo ni sala maalum, inayoitwa "Sala ya Bwana." Sala hii katika Mathayo 6 kuweka mbele kidogo."

### Dhana maalum katika sura hii

### Sala ya Bwana

Huu sio maombi ya kurudiwa mara kwa mara, ingawa sala hii inaweza kutumika kwa njia hiyo. Badala yake, hutoa mfano wa jinsi Wakristo wanapaswa kuomba.

### Yona

Yona alikuwa nabii wa Agano la Kale wa muhimu fulani lakini sio umuhimu mkubwa. Aliita taifa la Wayunani kutubu dhambi zao na walitii. Matukio haya husababisha nabii wa Kiyahudi kuwa na hasira juu ya neema ya Mungu inayoonyeshwa kwa Mataifa. Sura hii inalinganisha na mtazamo wa baadaye wa Wayahudi, sababu ya ukosefu wao wa toba na baadaye kuwa na hasira juu ya Mungu kwa neema anayowaonyesha Wayunani. , and )

### Mwanga

Mwangazi ni picha ya kawaida katika Maandiko iliyotumiwa kuonyesha haki. Mwanga pia hutumiwa kuonyesha njia ya haki na kuonyesha kuishi kwa haki. Giza mara nyingi hutumiwa kama picha ya kuonyesha dhambi au uovu. and )

### Kuosha

Hii ilikuwa zoezi lililofanywa na Mafarisayo, lakini haikuwa wajibu kulingana na sheria ya Musa. Mafarisayo walikuwa na ibada nyingi zinazohusisha kuosha kwa kujaribu kujiweka safi. Hii ni ajabu kwa sababu hakuna kiasi cha maji kinachoweza kuwafanya kuwa safi kiroho. , and

---

### Luke 11:1

**Habari za jumla**
Hii ni mwanzo wa sehemu inayofuata ya hadidhi.
Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuomba

**Ilitokea**
Neno hili lilitumika kuonyesha mwanzo wa...

## Luke 11:2

**Yesu akawaambia, "msalipo mseme, "Baba Jina lako litakaswe**
Yesu, mwana wa Mungu, Aliwaamuru wanfunzi kuheshimu Jina la Mungu "Baba", kwa kulitamka jina la Mungu kama "Baba" wakati wa kuomba

**Yesu akawaambia**
Yesu aliwaambia wanafunzi wake

**Baba**
Hii ni cheo muhimu kwa Mungu

**Jina lako litakaswe**
"Watu wote wakuheshimu wewe" au "mfanye kila mmoja aliheshimu Jina lako"

**Ufalme wako uje**
"Uizimamishe ufalme wako" Tunataka utawale watu wako.

## Luke 11:3

**Maneno yenye kuunganisha**
Yesu aliendelea kuwafundisha wanafunzi wake namna ya kuomba.

**mkate wetu wa kila siku**
Mkate ni chakula cha gharama ambacho huliwa na watu kila siku

**Utusamehe makosa yetu**
"Utusamehe kwa kufanya dhambi kinyume na wewe" au "Tusamehe dhambi zetu"

**Kama nasi tunavyo wasamehe**
Kwasbabu nasi tunawasamehe

**Waliotukosea**
wale waliofanya makosa juu yetu au waliotutendea mambo mabaya

**Usituongoze katika Majaribu**
Tuongoze mbali na majaribu

## Luke 11:5

**Maneno yenye kuunganisha**
Yesu aliendelea kufundisha wanafunzi wake juu ya maombi

**Ni nani kati yenu mwenye**
Yesu alitumia maswali kuwafundisha wanafunzi wake . "Fikiria mmoja wenu anayo" au "Fikiria unayo"

**Niazime mikate mitatu**
Nikopeshe mkate mitatu au nipe mikate mitatu na nitakupilia baadaye . Mwenyeji hana chakula chochote kilicho tayari cha kumpa mgeni wake.

**amenijia sasa hivi kutoka njiani**
alikuwa akisafiri na sasa hivi akaja nyumbani mwangu

**sina cha kumuandalia yeye**
"chakula chochote kilicho tayari cha kumpa"

**Siwezi kuamuka**
"Siyo rahisi kwangu mimi kuamka"

**Nawaambia**
Yesu alikuwa akiongea na wanafunzi, Neno ninyi ni wingi

**akupe mkate kwasababu wewe ni rafiki yake**
Yesu aliongea na wanafunzi wake kana kwamba wao ndiyo waliokwenda kuomba mkate.

**kuendelea bila aibu**
Hii inamaanisha ile hali ambayo yule mtu aliendelea kuomba mkate bila kujali kama ni wakati mwafaka wa rafiki wake kuamka katikati ya usiku na kumpa mkate

## Luke 11:9

**Omba..tafuta....bisha**
Yesu alitoa hizi amri kuwatia moyo wanafunzi wake kuomba bila kukoma. Lugha nyingine huitaji maelezo zaidi. "waweza kuelezea kama ifuatavyo: endelea kuomba kwa kile unachokihitaji....endelea kutafuta kile unachohitaji kwa Mungu...endelea kubisha hodi kwenye mlango"

**Nanyi mtapewa**
"Mungu atakupatia " au "Utapokea"

**Bisha/kugonga**
Kugonga katika mlango ni kupiga mara kadhaa kumfanya yule aliyeko ndani ajue kuwa unasimama je. Inaweza pia kutafsiriwa kwa kutumia njia ambayo watu wa kabila lenu huonyesha kuwa wamefika. Mfano "Kuita" au "kukohoa" au "Kupiga makofi" . Hapa inamaana mtu anendelee kuomba kwa Mungu hadi amjibu

**itafunguliwa kwenu**
"Mungu atafungua Mlango kwa ajili yako" au "Mungu atakukaribisha Ndani"

## Luke 11:11

**kauli inayounganisha**
Yesu alimaliza kufundisha wanafunzi wake kuhusu maombi.

**Nani kati yenu...nyoka?**
Yesu alitumia maswali kufundisha wanafunzi wake. " Hamna kati yenu...nyoka"

**Mkate**
"Mkate" au "Kiasi cha cakula"

**au badalaya samaki, nyoka?**
Hii inaweza kutafsiriwa kama sentensi mpya. "Au, kama akiomba samaki, hutampa nyoka"

**Nnge**
Nge ni kama buibui , lakini ana mkia wenye sumu unao choma. Kama Nnge hafahamiki sehemu unayoishi, waweza kutafsiri kama "buibui mwenye sumu" au "Buibu anayechoma"

**kama ninyi mlio waovu mnajua**
"kwa kuwa ninyi mlio waovu mnajua " au "hata japokuwa ninyi ni watenda dhambi , mnajua"

**Je si zaidi Baba yenu wa mbinguni atawapa na kuzidi Roho Mtakatifu ... wamuombao?**
Je si zaidi na kwa uhakika Baba yenu wa mbinguni atawapa Roho Mtakatifu ...Yeye? Yesu alitumia maswali tena kuwafundisha wanafunzi wake. "Uwe na uhakika kuwa Baba yenu wa Mbinguni atawapatia Roho Mtakatifu...yeye"

### Luke 11:14

**Habari ya Jumla**
Hii ni sehemu nyingine ya hadithi iliyofuata. Yesu alihojiwa baada ya kukemea pepo limtoke kwa mtu aliyekuwa bubu.

**Yesu alikuwa akimuondoa pepo**
"Yesu alikuwa akimuondoa pepo nje ya mtu" Au " Yesu alimuamuru pepo kumuacha mtu"

**alikuwa bubu**
hunda yule pepo haongei. Huenda msomaji alifahamu kuwa huyo pepo alikuwa na nguvu ya kuwafanya watu wasiongee. " pepo alimsababishia yule mtu asiweze kuongea"

**ikawa**
kifungu hiki inatumika kuonyesha tendo lilipoanza. Kama lugha yenu ina namna ya kufanya hili, unaweza kutumia hapa. Pepo alipomtoka mtu yule, na hivyo ikampelekea Yesu kufundisha habari za roho mbaya.

**ikawa pepo lilipomtoka**
"wakati pepo lilipo mtoka mtu" au "wakati pepo lilipo muacha mtu"

**yule mtu aliyekuwa bubu akazungumza**
"mtu ambaye alikuwa hawezi kuzungumza sasa akazungumza"

**Kwa Beelzebul, mkuu wa mapepo, anatoa mapepo**
"anatoa mapepo kwa nguvu ya Beelzebul, mkuu wa mapepo"

### Luke 11:16

**Habari ya jumla**
Yesu alianza kujibu umati waliojikusanya

**Wengine wakamjaribu**
"Watu wngine walimjaribu Yesu". Walimtaka awathibitishie kuwa mamlaka yake yanatoka kwa Mungu.

**na kumtaka awaonyeshe ishara kutoka mbinguni**
"na kumuambia awape ishara kutoka mbinguni" au "kwa kutaka awaonyeshe ishara kutoka mbinguni". Ni kwa njia hii walimtaka yeye athibitishe kuwa mamlaka yake yanatoka kwa Mungu.

**Kila ufalme utakaogawanyika itakuwa ukiwa**
"Kama watu katika ufalime watapigana wenyewe kwa wenyewe, wataingamiza ufalme wao. "

**Nyumba iliyogawanyika itaanguka**
Hapa "Nyumba" inamaanisha ni familia, "Kama watu wa familia moja wakipigana wenyewe kwa wenyewe wataiharibu familia yao"

**kuanguka**
"Kuangushwa chini na kuharibiwa" Taswira hii ya nyumba kuanguka chini inafananishwa na uharibifu utakaotokea pale watu wa familia moja wakipigana wenyewe kwa wenyewe.

### Luke 11:18

**kama shetani takuwa amegawanyika**
"Shetani" hapa inawakilisha wale mapepo waliojiunga na Shetani kumuasi Mungu. "Kama shetani na washirika wa ufalme wake wanapigan a wao kwa wao"

**ufalme wake utasimamaje?**
Yesu alitumia maswali kufundisha watu. "Ufalme wa Shetani hautadumu" au "Ufalme wa shetani utaanguka na kusambaratika"

**Kwasababu mwasema natoa mapepo kwa Belzebuli**
Kwa sababu mwasema ni kwa nguvu ya Belzebuli nawafanya mapepo kuwaacha watu . sehemu iliyofuata ya majibu yake inaweza kutamkwa kirahisi: "hii inamaana Shetani amegawachika juu yake"

**Je wenzenu wanatoa mapepo kwa njia gani?**
"ni kwa nguvu ya nani wenzenu wanawaamurisha mapepo kuwaacha watu. " Yesu alitumia swali kufundisha watu.Swali la Yesu inaweza kurahisishwa, "basi ni lazima tukubaliane kuwa wenzenu pia hutumia nguvu ya Beelzebuli kuondoa mapepo". "Lakini tunajua kuwa hiyo si kweli".

**wao watawahukumu ninyi**
wenzenu wanao watoa mapepo kwa nguvu ya Mungu watawahukumu ninyi kwa kusema kuwa mimi natoa mapepo kwa nguvu ya Beelzebuli.

**kwa kidole cha Mungu**
"Kidole cha Mungu" inamaanisha ni Nguvu ya Mungu

**Basi ufalme wa Mungu umewajia**
"Hii inaonyesha kuwa ufalme wa Mungu umekuja kwenu"

## Luke 11:21

**mtu mwenye nguvu ...akilinda nyumba yake**
Hii inaongelea Yesu ambaye anamshinda Shetani na mapepo wake kama mtu mwenye nguvu zaidi ananyo chukua vitu vya mtu mwenye nguvu

**vitu vyake vitakaa salama**
"hakuna awezaye kuiba vitu vyake"

**na kuzichukua mali zake zote**
"Kuiba mali zake" au kuchukua kila kitu alichokitaka"

**yeye asiye pamoja nami**
"yeye asiyenisaidia " au "yeye asitenda kazi pamoja nami"

**yuko kinyume nami**
"anafanya kazi kinyume nami". Hii inamaanisha wale watu waliosema kuwa Yesu anafanya kazi pamoja na Shetani.

## Luke 11:24

**mahali pasipo maji**
"Hii inamaanisha "sehemu ya ukiwa", mahali ambapo roho mbaya hurandaranda .

**akikosa**
"kama roho hakupata sehemu ya kupumzika"

**nyumba yangu nilikotokea**
Hii inamaanisha mtu yule ambaye alikuwa anakaa kwake. "mtu ambaye nilikuwa nikikaa kwake"

**na kukuta nyumba imefagiliwa na imekaa vizuri**
"akaikuta mtu alifagia nyumba na kuwa safi na kuweka kila kitu mahali pake " au " kumkuta mtu kama nyumba iliyosafishwa na kupangiliwa vizuri"

**imefagiliwa**
"tupu" Mfano huu inamaanisha hali ambayo mtu hakujazwa Roho wa Mungu baada ya mapepo kuondoka.

## Luke 11:27

**Habari ya Jumla**
Huu ni mkatizo wa mafindisho wa Yesu. Mwanamke aliongea baraka na Yesu akajibu.

**Ilitokea**
Kifungu hiki kinatumika kuonyesha tukio muhimu katika historia. Kama lugha yako ina njia ya kufanya hii, unaweza ukatumia hapa.

**aliyepasa sauti yake kwenye mkutano**
"aliongea kwa sauti iliyozidi kelele za umati"

**Limebarikiwa tumbo lililo kuzaa na matiti ulioyanyonya**
Sehemu ya mwili wa mwanamke ilitumika kuwakilisha mwanamke. " Ana heri kiasi gani yule mama aliyekuzaa na kukunyonyesha kwenye matiti yake" au " Ana furaha iliyoje yule mwanamke aliyekuzaa na kukunyonyesha kwenye matiti yake"

**lakini, wamebarikiwa wale**
" Ni vizuri zaidi kwa wale "

## Luke 11:29

**Kauli inayounganisha**
Yesu aliendelea kufundisha umati

**Kizazi hiki ni kizazi cha uovu**
Watu wanaoishi katika nyaka hii ni watu waovu

**Hutafuta ishara**
"Wanataka mimi niwape ishara " au "Wengi wenu mnataka mimi niwape ishara" . Habari ya aina ya ishara wanayotaka inaweza kufaywa rahisi kama ilivyo katika UDB

**na hakuna ishara watakao pewa**
"Mungu hatawapa ishara "

**Ishara wa Yona**
"kile kilichotokea kwa Yona" au "muujiza ambao Mungu alifanya kwa Yona"

**Maana kama Yona alivyokuwa ishara...ndivyo**
Hii inamaana kuwa Yesu atatumika kama ishara kutoka kwa Mungu kwa ajili ya Wayahudi wa wakati huo kama ilivyokuwa kwa Yona alivyotumika kama ishara kutoka kwa Mungu kwa watu wa Ninawi.

**Mwana wa Adamu**
Yesu alikuwa akijisemea mwenyewe

## Luke 11:31

**Malkia wa Kusini**
Hii ilimaanisha malkia wa wa Sheba. Sheba ilikuwa ni ufalme wa kusini mwa Israeli

**atasimama siku ya hukumu na watu wa kizazi hiki**
"Atasima pia na kuwahukumu watu wa kizazi hiki"

**kalitoka katika mwisho wa nchi**
"alikuja tokae umbali mrefu" au " Alikuja kutoka sehemu ya mbali"

**Yuko mkuu kuliko Sulemani**
Yesu alikuwa akiongelea juu yake. "Mimi ni mkuu kuliko Sulemani lakini hamnisikilizi"

## Luke 11:32

**Watu wa Ninawi watasimama katika hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki na kuwahukumu**
"Watu wa Ninawi watasimama na kuwahukumu watu wa nyakati na kuwalaani."

**kwani walitubu**
"watu wa Ninawi walitubu"

**Yuko aliye mkuu kuliko Yona**
Yesu alijiongelea mwenyewe. "Mimi ni mkuu kuliko Yona lakini hamkutubu"

## Luke 11:33

**Kauli unayounganisha**
Yesu alimaliza kuwafundisha makutano

**Kuweka sehemu ya chini yenye giza**
"kuficha kwenye sehemu iliyofichika"

**Ila Juu ya kitu**
"ila wanaweka juu ya meza" au " Ila wanaweka juu ya kabati"

**Jicho lako ni taa ya mwili**
Hii imewasilishwa na mafumbo tofauti. Jicho hufananishwa na Maono, ambayo ni mfano wa kuelewa. Mwili ni kiwakilishi cha maisha ya Mwanadamu. " Jicho lako ni taa ya maisha yako" au "Maono yako ni taa ya maisha yako" Kwasababu Yesu alikuwa anaongea kitu ambacho ni kweli kwa kila mtu, inaweza ikatafsiriwa kama " Jicho ni taa ya mwili wa mwanadamu"

**Jicho lako likiwa zuri**
" Maono yako yakiwa mazuri" au "ukiona vema"

**mwili wako wote utakuwa kwenye mwanga**
Yesu aliongelea kweli kama mwanga . "mwanga wa kweli utakuwa maishani mwako" Au "Maisha yako yote utakuwa na mwanga"

**jicho lako likiwa baya , mwili wako wote utakuwa kwenye giza.**
Yesu aliongelea habari ya kuwa katika uongo kama vile ni kuwa katika giza. " Maono yako yakiwa mabaya, basi maisha yako yote yanajawa na giza"

**mwili wako wote utakuwa sawa na mwanga utouo mwango kwenu.**
Yesu aliongea watu ambao wamejawa na kweli kama vile taa iwakavyo na kutoa mwanga wote.

## Luke 11:37

**Habari ya Jumla**
Huu ni mwanzo wa sehemu iliyofuata ya hadithi. Yesu alikaribishwa kula nyumbani mwa Mfarisayo

**akawa pamoja nao**
"kukaa katika meza". " ilikuwa ni desturi kwa chakula kama hii wanaume kula wakiwa wamekaa vizuri kwa kustarehe kwenye meza"

**kunawa**
Mafarisayo wana sheria ya kuwa watu ni lazima wanawe mikono yao ili waonekane kuwa wasafi mbele za Mungu. "kunawa mikono" au "kunawa mikono ili kuwa msafi kiibada"

## Luke 11:39

**Habari ya jumla**
Yesu alianza kuongea na mafarisayo

**nje ya vikombe na bakuli**
Kuoasha nje ya vyombo ilikuwa ni sehemu ya mazoea ya ibada kwa Wafarisayo

**lakini ndani yenu mmejaa tamaa na uovu.**
Hii inafananishwa na njinzi wanavyosahau ndani ya vyombo na wanavyosahau maisha yao ya ndani.

**Je yeye aliyeumba nje hakuumba na ndani pia?**
Yesu alitumia swali kuwakemea Mafarisayo kwa kutojua ya kuwa kile kilichoko ndani ya miyoyo yao inajalisha kwa Mungu.

**Wapeni maskini yaliyo ndani**
"Wapeni Maskini kile kilichoko ndani ya vikombe na bakuli" au " Muwe wakarimu kwa watu maskini"

## Luke 11:42

**mnatoza zaka ya mnanaa na kila aina ya mboga ya bustani**
" mnatoa moja ya kumi ya mnanaa na mchicha na kila aina ya mboga ya bustani", Yesu alikuwa anatoa mfano wa njinzi mafarisaya walivyo makini katika kutoa moja ya kumi ya mapato yao.

**mnanaa na mchicha**
hizi ni kama dawa. Watu huweka kidogo kwenye chakula ili kuipa utamu fulani. Kama watu hawafahamu mnanaa na mchicha, unaweza kutumia majina ya viungo wanayoijua au ufahamu wa jumla wa "viungo."

**na kila aina ya viungo vya bustani**
Tafsiri yake inaweza kuwa 1) Kila aina nyingine ya mbogamboga" 2) "Kila aina ya viungo vya bustani" 3) Kila aina ya mimea ya bustani

**bila kuyaacha kuyafanya na hayo mengine pia**
"na kila wakati myafanye na hayo mengine pia"

## Luke 11:43

**kauli inayounganisha**
Yesu alimaliza kuongea na mafarisayo

**viti vya mbele**
"viti vizuri sana"

**ole wenu, kwani mnafanana na makaburi yasiyo na alama ambayo watu hutembea juu yake pasipokujua"**
Mafarisayo ni kama makaburi yasiyo na alama kwasababu wanaonekana kama waasafi, lakini huwafanya watu waliokaribu nao kuwa siyo wasafi.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**makaburi yaliyofichika**
Makaburi hayo yalikuwa mashimo kuchimbwa katika ardhi ambapo maiti kuzikwa. Wao hawakuwa na mawe nyeupe kwamba watu kawaida kuweka juu ya makaburi ili kwamba watu wengine kuona kwao. Wakati watu kutembea juu ya kaburi, wangeweza kuwa najisi.

## Luke 11:45

**Habari ya Jumla**
Yesu alianza kumjibu mwalimu wa Kiyahudi

**kwani mnawapa watu mizigomikubwa wasiyoweza kuibeba**
"munaweka mizigo juu ya watu ambayo ni mizito kubebeka" . Yesu aliongea kuhusu mtu fulani kuwapa watu sheria nyingi kama mtu kuwapa mizigo mizito kubeba. "Mnawapa watu mizigo mizito kwa kuwapa sheria nyingi za kufuata"

**walakini ninyi hamgusi mizigo hiyo hata kwa moja ya vidole vyenu.**
"lakini hamtumii hata moja ya kidole chenu kuwasaidia kubeba mizigo hiyo. "Lakini hamfanyi kitu chochote kabisa kuwasaidia waitii sheria zenu"

## Luke 11:47

**ambao**
Hii huwafanya kuona utofauti kati yao kwa namna wanavyo waheshimu manabii wakati wakipuuza ukweli kuwa wababu zao ndio waliowauwa.

**hivyo ninyi mwashuhudia na kukubaliana**
Yesu aliwakemea Mafarisayo na waalimu wa sheria . Walijua mauwaji ya manabii, lakini hawakushutumu wala kuwalaani wababu zao kwa kuwauwa. " kwahiyo, badala ya kuwakana wao, ninyi mwashuhudia na kukubaliana "

## Luke 11:49

**Kwasababu hiyo**
Hii inarejea sentensi iliyofuata, Mungu atawatuma manabii wengi ili kuonesha kuwa kizazi hiki kitawauwa, kama walivyofanya baba zao.

**Hekima ya Mungu inasema**
"Mungu kwa hekima yake alisema" au "Mungu alisema kwa hekima"

**Nitawatumia manabii na mitume**
"Nitawatumia manabii na mitume watu wangu"

**watawatesa na kuwauwa baadhi yao**
"watu wangu watawatesa na kuwauwa baadhi ya manabii na mitume"

**Kizazi hiki, kitawajibika na damu iliyomwagwa ya manabi wote.**
Damu iliyomwagwa inamaanisha mauwaji ya manabii. "Kwa hiyo Mungu atawajibisha kizazi hiki kwa kifo cha manabii wote ambao watu wamewauwa"

**Zakaria**
Huyu ni kuhani wakati wa Agano la kale aliyewakemea watu wa israeli kwa habari ya usinzi. Huyu siye Baba wa Yohana Mbatizaji.

**ambaye ameuwawa**
"ambaye watu walimuuwa"

## Luke 11:52

**Kauli ya kuunganisha**
Yesu alimaliza kumjibu mwalimu wa Kiyahudi

**mmechukuwa funguo za ufahamu ...na mnawazuia wale wanaotaka kuingia**
Yesu aliongea kuhusu ukweli wa Mungu kama vile ilikuwa ndani ya nyumba ambayo waalimu walikataa kuingia na hawaruhusu wengine kuingia. Hii ina maanisha waalimu hawamjui Mungu , na pia wanawazuia wengine kumjua Yeye pia.

**Ufunguo**
Hii inawakilisha maana ya ruhusa, kama kwenye nyumba au kwenye chumba cha stoo.

**nyie wenyewe hamuingii**
" ninyi wenyewe hamuingii ndani kupata ufahamu"

## Luke 11:53

**Habari za jumla**
Huu ni mwisho wa sehemu ya hadithi ambapo Yesu alikula katika nyumba ya mfarisayo. Hii mistari inamweleza msomaji nini kilifanyika baada ya sehemu ya habari kuu ya hadithi kuisha "

**Baada ya Yesu kuondoka pale**
" Baada ya Yesu kuondoka katika nyumba ya mfarisayo"

**wakijaribu kumtega kwa maneno yake**
Hii inamaanisha walihitaji Yesu kusema kitu kibaya ili waweze kumshitaki

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 12

1 Kwa wakati huo, maelfu mengi ya watu walikusanyika pamoja, kiasi cha kuanza kukanyagana, akaanza
kusema na wanafunzi wake kwanza, "Jihadharini na chachu ya Mafarisayo ambayo ni unafiki" 2 Na
hapatakuwepo na siri iliyofichika ambayo haitafunuliwa, wala jambo lililofichwa ambalo halitajulikana. 3
Na lolote mlilolisema katika giza, litasikiwa katika mwanga. Na yoyote mliyoyasema kwenye sikio ndani
ya vyumba vyenu vya ndani vilivyofungwa yatatangazwa juu ya paa la nyumba. 4 Nawaambieni rafiki
zangu, msiwaogope wale wauao mwili na kisha hawana kitu kingine cha kufanya, 5 Lakini nitawaonya
mtakaye mwogopa. Mwogopeni yule ambaye baada ya kuwa ameua, ana mamlaka ya kutupa jehanamu.
Ndiyo, nawaambiani ninyi, mwogopeni huyo. 6 Je shomoro watano hawauzwi kwa sarafu mbili? hata hivyo
hakuna hata mmoja wao atakayesahaulika mbele za Mungu. 7 Lakini mjue kuwa, nywele za vichwa vyenu
vimehesabiwa. Msiogope. Ninyi ni wa thamani kubwa kuliko shomoro wengi. 8 Ninawaambia, yeyote
atakayenikiri Mimi mbele za watu, Mwana wa Adamu atamkiri mbele za malaika wa Mungu. 9 Lakini
yeyeyote atakayenikana mbele za watu naye atakanwa mbele ya Malaika wa Mungu. 10 Yeyote
atakayesema neno baya juu ya Mwana wa Adamu, atasamehewa, lakini yeyote atakayemkufuru Roho
Mtakatifu, hatasamehewa. 11 Watakapowapeleka mbele za wakuu wa masinagogi, watawala, na wanye
mamlaka, msiogope juu na namna ya kuongea katika kujitetea au nini mtakachosema, 12 kwa kuwa Roho
Mtakatifu atawafundisha namna mtakavyosema kwa wakati huo." 13 Mtu mmoja katika kusanyiko
akamwambia, "Mwalimu, mwambie ndugu yangu anigawie sehemu ya uruthi wangu." 14 Yesu akamjibu,
ni nani aliye niweka kuwa mwamuzi na mpatanishi kati yenu.? 15 Ndipo akawaambia, Jihadharini na kila
namna ya tamaa, kwa sababu uzima wa mtu hauko katika wingi wa vitu alivyo navyo." 16 Yesu
akawaambia mfano, akisema, Shamba la mtu mmoja tajiri lilizaa sana, 17 na akajiuliza ndani yake,
akisema, nitafanyaje kwani sina mahali pa kuhifadhi mazao yangu? 18 Akasema, nitafanya hivi. Nitavunja
ghala zangu ndogo na kujenga iliyo kubwa, na kuyahifadhi mazao yangu yote na vitu vingine. 19
Nitaiambia nafsi yangu, "Nafsi, umejiwekea akiba ya vitu vingi kwa miaka mingi. Pumzika, ule, unywe na
kustarehe." 20 Lakini Mungu akamwambia, ewe mtu mpumbavu, usiku wa leo wanahitaji roho kutoka
kwako, na vitu vyote ulivyoviandaa vitakuwa vya nini? 21 Ndivyo itakavyokuwa kwa kila mtu anayejiwekea
mali na si kujitajirisha kwa ajili ya Bwana. 22 Yesu akawaambia wanafunzi wake, Kwa hiyo nawaambia
msihofu juu ya maisha yenu__ya kuwa mtakula nini au juu ya miili yenu __ya kuwa mtavaa nini 23 Kwa
kuwa maisha ni zaidi ya chakula, na mwili ni zaidi ya mavazi. 24 Angalieni ndege wa angani, hawalimi
wala hawavuni. Hawana chumba wala ghala ya kuhifadhia, lakini Baba yenu huwalisha. Ninyi si bora zaidi
kuliko ndege! 25 Ni yupi kati yenu ambaye akijisumbua ataweza kuongeza dhiraa moja katika maisha
yake? 26 Ikiwa basi hamuwezi kufanya hicho kitu kidogo kilicho rahisi kwa nini basi kusumbukia hayo
mengine?. 27 Angalieni maua -yanavyomea. Hayafanyi kazi wala hayasokoti. Lakini nawaambia, hata
Sulemani katika utukufu wake wote hakuvikwa kama mojawapo ya haya, 28 Kama Mungu huyavika vizuri
majani ya kondeni, ambayo leo yapo, na kesho hutupwa kwenye moto. Je si zaidi atawavika ninyi? enyi wa
imani haba! 29 Msisumbukie juu ya kuwa mtakula nini au mtakunywa nini, wala msiwe na hofu. 30 Kwa
kuwa Mataifa yote ya dunia husumbukia mambao yao. Na Baba yenu anajua ya kuwa mnahitaji hayo. 31
Lakini tafuteni ufalme wake kwanza, na hayo mengine mtazidishiwa, 32 msiogope, enyi kundi dogo, kwa
sababu Baba yenu anafurahia kuwapa ninyi huo ufalme. 33 Uzeni mali zenu na mkawape maskini,
mjifanyie mifuko isiyoishiwa__hazina ya mbinguni isiyokoma, sehemu ambapo wezi hawatakaribia wala
nondo haitaweza kuharibu. 34 Kwa kuwa palipo na hazina yako, ndipo na roho yako itakapokuwepo. 35
Nguo zenu ndefu ziwe zimefungwa kwa mkanda, na taa zenu zihakikishwe kuwa zinaendelee kuwaka, 36
na muwe kama watu wanaomtazamia Bwana wao kutoka kwenye sherehe ya harusi, ili kwamba akija na
kupiga hodi, wataweze kumfungulia mlango kwa haraka. 37 Wamebarikiwa wale watumishi, ambao Bwana
atawakuta wako macho. Hakika atafunga nguo yake ndefu kwa mkanda, kisha atawaketisha chini kwa
chakula, na kisha kuwahudumia. 38 Kama Bwana atakuja kwa zamu ya pili ya ulinzi ya usiku, au hata
zamu ya tatu ya ulinzi, na kuwakuta wakiwa tayari, itakuwa ni heri kwa hao watumishi. 39 Zaidi ya hayo,
mjue hili, kama bwana mwenye nyumba angelijua saa ambayo mwivi anakuja, asingeliruhusu nyumba
yake ifunjwe. 40 Iweni tayari pia kwani hamjui ni wakati gani mwana wa Adamu atarudi. 41 Petro
akasema, "Bwana, watuambia sisi wenyewe hii mifano, au unamwambia kila mtu.? 42 Bwana akawaambia,
"Ni nani mtumwa mwaminifu au mwenye hekima ambaye bwana wake atamweka juu ya watumishi
wengine, ili awagawie chakula chao kwa wakati mwafaka? 43 Amebarikiwa mtumishi yule, ambaye bwana
wake akija atamkuta akifanya yale aliyoagizwa. 44 Hakika nawaambia ninyi ya kuwa atamweka juu ya
mali yake yote. 45 Lakini Mtumishi yule akisema moyoni mwake, "bwana wangu anachelewa kurudi; hivyo

akaanza kuwapiga wale watumishi wa kiume na wa kike, kisha akaanza kula, kunywa na kulewa, **46**
bwana wake yule mtumwa atakuja katika siku asiyotegemea na saa asiyoijua, naye atamkata vipande
vipande na kumuweka katika sehemu pamoja na wasiokuwawaaminifu' **47** Mtumishi, anayejua mapenzi ya
bwana wake, naye hakujiandaaa wala hakufanya sawa sawa na mapenzi yake, atapigwa viboko vingi. **48**
Lakini mtumishi asiyejua mapenzi ya bwana wake, lakini akafanya yanayostahili adhabu, atapigwa viboko
vichache. Kwa kuwa yeye aliyepewa vingi, vingi hudaiwa kutoka kwake, na yeye aliyeaminiwa kwa vingi,
kwake vitadaiwa vingi zaidi. **49** Nimekuja kuwasha moto duniani, na natamani iwe umekwishawaka, **50**
Lakini nina ubatizo ambao nitabatizwa, na nina huzuni mpaka utkapokamilika! **51** Je mnafikiri kuwa
nimekuja kuleta amani duniani? Hapana, Nawaambieni, badala yake nimeleta mgawanyiko. **52** Tangu sasa
na kuendelea kutakuwa na watu watano katika nyumba moja wamegawanyika, na watatu watakuwa
kinyume na wawili, na wawili watakuwa kinyume na watatu. **53** Watagawanyika, baba atakuwa kinyume
na mwanae, na mwanae atakuwa kinyume na babaye, mama atakuwa kinyume na binti yake, na binti
atakuwa kinyume na mama yake, Mama mkwe atakuwa kinyume na mkwe wake naye mkwe atakuwa
kinyume na mama mkwe wake. **54** Yesu akawa anawaambia makutano pia, "Mara muonapo mawingu
yakitokea magharibi, mnasema nyakati za mvua zimewadia; na ndivyo inavyo kuwa, **55** Na upepo wa
kusini ukivuma, mnasema, Patakuwepo na joto kali, na ndivyo inavyokuwa. **56** Enyi wanafiki, mnaweza
kutafsiri mwonekano wa nchi na anga, lakini inakuwaje hamuwezi kuutafsiri wakati uliopo? **57** Ni kwa nini
kila mmoja wenu asipambanue lililo sahihi kwake kulifanya wakati ambapo angali na nafasi ya kufanya
hivyo? **58** Maana mkienda na mshitaki wako mbele ya hakimu, jitahidi kupatana na mshitaki wako mungali
bado mko njiani asije akakupeleka kwa hakimu, na hakimu akupeleka kwa ofisa, na ofisa akakutupa
gerezani. **59** Nakuambia, hutatoka huko hadi umelipa mpaka senti ya mwisho.

---

## Luka 12 Maelezo ya Jumla

### Dhana maalum katika sura hii

#### "Kukufuru Roho"

Kuna matatizo mengi juu ya kutambua vizuri dhambi hii maalum. Hata hivyo, inaonekana kuwa inahusisha kumtukana Roho Mtakatifu na kazi yake. Kwa kuwa sehemu ya kazi yake ni kuwashawishi watu juu ya dhambi zao na kwamba wanahitaji kusamehewa na Mungu, yeyote anayezarau ukweli huu, atakataa kuja kwa Mungu kwa toba. Kwa sababu hii, hangeweza kusamehewa.

#### Usimamizi

Ingawa neno "msimamizi" haitumiwi katika sura hii, uwakilishi, ambao ni kazi ya msimamizi, ni neno kubwa katika mafundisho haya. Msimamizi mwema ni mtu ambaye wengine wanaweza kumwamini kushughulika juu ya vitu vyao. Kwa sababu kila kitu ni cha Mungu daima, kila kitu anachompa kila mtu bado ni cha Mungu, na mtu anayepokea zawadi kutoka kwa Mungu ni mwendeshaji wa kile ambacho ni cha Mungu. zawadi kwa Mungu" instead of "zawadi kutoka kwa kwa Mungu" or "Hivi sivyo vitu vinavyoonekana tu, vitu ambavyo Mungu aliwaruhusu mtu kuchunga, lakini ni mambo pia kama uwezo wa asili wa mtu huyo. Mungu anatumaini kama watumishi wake watakumbuka kama ataweza kila mara kuwaomba ripoti ya vitu alivyowapatia.

#### Mgawanyiko

Kuna fundisho muhimu juu ya mgawanyiko katika sura hii (Luka 12:51-56). Mgawanyiko huu haukusudi kuwa na maana ya kusema kama watu wangekuwa adui. Lakini, ina maana ya kusema kama katika ulimwengu kuna mgawanyiko wazi kati ya watu Wakristo na watu wasio Wakristo na wale wasio Wakristo. Kuonekan kama mfuasi wa Yesu ni muhimu kuliko uhusiano nyingine wowote wa familia.

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

#### "Mwana wa Binadamu"

Yesu anajiita mwenyewe kama "Mwana wa Binadamu." Lugha zingine haziwezi kuruhusu mtu kujitaja mwenyewe kama 'mtu wa tatu.'

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

### Maelekezo ya jumla na Maalum

Mara na mara Agano Jipya hutoa maagizo au amri maalum kuhusu Wakristo wote. Wakati mwingine, maagizo yake yanafikiriwa kuwa maagizo ya ujumla na yanapaswa kuchukuliwa kama "mawazo mazuri." Kwa mfano, "usiwe na wasiwasi" au "uza vitu vyako" sio maagizo kwa Wakristo wote.

---

## Luke 12:1

**Habari za Jumla**
Hii ni sehemu iliyofuata ya hadithi. Yesu alianza kuwafundisha wanafunzi wake mbele ya maelfu ya watu.

**kwa wakati huo**
"wakati wakifanya hayo "

**wakati maelfu ya watu ..walikanyagana**
Hii ni habari ya nyuma inayoelezea mpangilio wa hadithi

**watu wengi maelfu**
"ni kusanyiko kubwa"

**walikanyagana**
Hii ni kivumishi kinachoelezea wingi wa watu waliokuwepo

**Alianza kusema na wanafunzi wake kwanza**
"Yesu alianza kwanza kuongea na wannafunzi wake, na kuwaambia"

**Mjihadhari na chachu ya Mafarisayo ambayo ni unafiki.**
Kama vile chachu inavyoenea kwa donge la unga wa mkate, unafiki wao huenea kwa jamii nzima. "Mjitunze na unafiki ya Mafarisayo ambayo ni sawa na chachu" au " Mjihadhari msije mkawa wanafiki kama Mapharisayo. Hii tabia ya uovu hushawishi kila mmoja kama ambavyo chachu huharibu donge la unga"

## Luke 12:2

**Lakini hapatakuwepo na siri iliyofichika ambayo haitafunuliwa**
"Lakini kila kitu kilichofichwa kitaonyeshwa" Neno "lakini" ni neno la kiunganishi" Lakini watu watajua mambo yote wafanyayo watu kwa siri"

**wala jambo lililo fichwa ambalo halitajulikana**
Hii ina maana sawa na sehemu ya kwanza ya sentensi ili kuzizitiza ukweli. " na watu watajifunza kuhusu kile ambacho watu wengine wanajaribu kuficha"

**itasikiwa katika mwanga**
" watu watasikia katika mwanga"

**mliyoyasema kwenye sikio**
"Kumnong'onezea mtu mwingine"

**ndani ya vyumba vyenu vya ndani**
"kwenye chumba iliyofungwa". "Kwa sehemu ya faragha" au "Kwa siri"

**vitatangazwa**
"itasemwa kwa sauti ya juu". "Watu watatangaza"

**juu ya nyumba**
Nyumba katika Israeli zlikuwa na paa gorofa, hivyo watu wanaweza kwenda na kusimama juu yao. Kama viongozi wanavyokuwa na wasiwasi kujaribu kufikiria jinsi watu wanavyoweza kupanda juu ya zile nyumba, hii inaweza pia kutafsiriwa na usemi zaidi kwaa jumla, kama vile "kutoka mahali pa juu ambapo kila mmoja atakuwa na uwezo wa kusikia."

## Luke 12:4

**Nawaambia rafiki zangu**
Yesu anawaanda wasikilizaji wake kutambua kuhamia kwenye mada nyingine, kwa hili, kuongelea kuhusu kutokuogopa.

**hawana kitu kingine cha kufanya**
"hawawezi kusababisha maumivu mengine zaidi" au "hawawezi kukuzuru zaidi"

**Muogopeni yule**
"Mwogopeni Mungu ambaye" au "Muogopeni Mungu kwa sababu"

**akisha kuua**
"baada ya kukua" au "baada ya kumuua mtu"

**ana mamlaka ya kutupa kwenye jehanamu**
"ana mamlaka ya kuwatupa watu kwenye jehanamu"

## Luke 12:6

**Je shomoro watano hawauzwi kwa senti mbili?**
Yesu anatumia swali kuwafundisha wanafunzi

**Shomoro**
Ni ndege wadogo sana wenye kula mbegu

**hakuna mmoja wao atakayesahaulika mbele za Mungu**
"Mungu hajawahi kusahau mmoja wao". "Mungu kwa uhakika anakumbuka kila shomoro"

**hata nywele za vichwa vyenu vimehesabiwa**
"Mungu anajua hata idadi ya nywele zilizoko kichwani mwako"

**Msiogope**
"Msiwaogope watu" au "Msiwaogope watu watakao waujeruhi ninyi"

**Ninyi ni wa thamani kubwa kuliko shomoro wengi.**
"Mungu anawathamini ninyi kuliko mashomoro wengi"

## Luke 12:8

**Nawaambia Ninyi**
Yesu alikuwa anawaanda wasikilizaji wake kutambua kuhamia kwa mada nyingine, kwa hili, anaongelea kuhusu kukiri.

**yeyote atakayenikiri mbele za watu**
"yeye atakaye waambia wengine kuwa yeye nimwanafunzi wangu" au " yeyote atakaye nitambulisha mbele ya wengine kwamba ni mwaminifu kwangu"

**Mwana wa Adamu**
Yesu alikuwa akirejea Yeye mwenyewe. Mimi Mwana wa Adamu

**yeyote atakaye nikana mbele za watu**
"Yeyote atakaye nikataa mbele za watu" " Yeyote atakaye kataa kunitambulisha kwa wengine kuwa yeye ni mwanafunzi wangu" au " yeyote atakaye kataa kusema yeye ni mwaminifu kwangu"

**naye atakanwa**
"Atakanwa" Mwana wa Adamu atamkana yeye " au " Nitamkana kuwa si mwanafunzi wangu"

**Yeyote atakayesema neno baya juu ya Mwana wa Adamu,**
"Yeyote atakayesema jambo baya juu ya Mwana wa Adamu "

**atasamehewa**
"atasamehewa". "Mungu atamsamehe yeye kwa hilo"

**atakayemkufuru Roho Mtakatifu**
"atakayeongea maovu juu ya Roho Mtakatifu " au "Kusema kuwa Roho Mtakatifu ni mwovu"

**Hatasamehewa**
"Mungu atamuhesabu kuwa na hatia milele"

## Luke 12:11

**mbele ya wakuu wa masinagogi**
" Ndani ya masinagogi ili wawaulize maswali kwa viongozi wa kidini"

**wenye mamlaka**
"watu wengine wenye nguvu ndani ya nchi"

**kwa wakati huo**
"kwa muda huo" au "Kisha"

## Luke 12:13

**Habari za Jumla**
Hii ni katizo kwa mafundisho ya Yesu. Mtu mmoja alimuomba Yesu amfanyie kitu na Yesu akamjibu.

**Mtu**
Maana inayowezekani ni 1) Hii ni namna ya kuongea na mtu mgeni au 2) Yesu anamkemea yule mtu. Labda lugha yenu ina njia mbadala ya kuongea na watu kwa namna ya njia hizi mbili. Watu wengine hawatafsiri neno hili kabisa.

**Ni nani aliyeniweka kuwa mwamuzi au mpatanishi kati yenu?**
Yesu alitumia swali kumfundisha huyo mtu. " Mimi siyo mwamuzi wenu au mpatanishi" . Lugha zingine hutumia wingi wa maneno ya "Yenu" au "Wenu"

**Ndipo akawaambia**
Neno "akawaambia" hapa huenda inarejea umati wote wa watu.

**jihadharini na kila namna ya tamaa**
"Jichungei na kila aina ya uchoyo". "Msijiruhusu kupenda kuwa vitu"au " Msiruhusu tamaa ya kuwa na vitu vingi iwatawale"

**uzima wa mtu**
Hii ni kauli ya jumla za ukweli. Haimrejei mtu yeyote maalum. Lugha nyingine zina jinsi ya kuelezea .

**wingi wa vitu alivyo navyo**
"Ni kiasi gani vya vitu anavyomiliki" au "kiasi gani ya mali anayomiliki"

## Luke 12:16

**Kauli inayounganisha**
Yesu aliendeleza mafundisho yake kwa kuwaeleza mfano

**Kisha Yesu akawaambia**
Huenda Yesu alikuwa bado anaongea na mkutano wote.

**ilizaa sana**
"imezaa mavuno mengi"

**ghala**
jengo ambalo wakulima huhifadhi mazao na chakula wanachopanda baada ya kuvunwa

**vitu**
"Mali"

**Nitaiambia nafsi yangu**
"Nitajiambia mwenyewe"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Luke 12:20

**kauli inayounganisha**
Yesu alinukuu jinsi Mungu alivyomjibu mtu tajiri, alipokuwa anamalizia hadithi yake.

**usiku wa leo wanahitaji roho kutoka kwako**
"utakufa usiku wa leo" au " Nitaichukuwa uhai wako kutoka kwako leo"

**na vitu vyote ulivyoviandaa vitakuwa vya nani?**
"nani atamiliki vitu ulivyo hifadhi?" au " ni nani atakayekuwa nayo vitu ulivyoviandaa?" Mungu alitumia swali kumfanya mtu atambue kuwa hatamiliki tena vitu hivyo.

**anayejiwekea mali**
"kuhifadhi vitu vya dhamani"

**na si tajiri**
"maskini"

**kwa ajili ya Mungu**
Maana yake ni kwamba mtu huyu hakuwa anajali vitu vilivyo muhimu kwa Mungu, au kuwa Mungu atamlipa. "kwa mtazamo wa Mungu" au "kulingana na Mungu"

## Luke 12:22

**Kauli inayounganisha**
Yesu aliendelea kuwafundisha wanafunzi wake mbele ya umati.

**Kwahiyo**
"kwasababu hiyo" au " kwasababu ya mafundisho ya hadihi hii"

**Nawaambia**
"Nataka niwaambie kitu muhimu"au "Inabidi msikilize kwa umakini juu ya hili"

**juu ya maisha yenu-ya kuwa mtakula nini**
"kuhusu maisha yenu na nini mtakula" au " kuhusu kuwa na chakula cha kutosha ili muweze kuishi"

**juu ya miili yenu -ya kuwa mtavaa nini**
"kuhusu miili yenu na nini mtavaa" au " kuhusu kuwa na nguo za kutosha za kuvisha miili yenu"

## Luke 12:24

**ndege wa angani (Rivens)**
(Rivens) hii inamaanisha 1) Ni aina ya ndege wanaokula mbegu zaidi, au 2) aina ya ndenge wanaokula nyama ya wanyama waliokufa. Wasikilizaji wa Yesu watakuwa wameidharau hao ndege kuwa si kutu (rivens) kwani Wayahudi hawali aina hiyo ya ndege.

**Ninyi si bora zadi kuliko hao ndege**
Hii ni tahamaki na siyo swali. Yesu alisisitiza ukweli kwamba watu ni wa muhimu sana kwa Mungu kuliko ndege.

**Ni yupi kati yenu ...maisha yake?**
Yesu alitumia swali kufundisha wanafunzi wake

**kuongeza dhiraa moja katika maisha yake**
Huu ni mfano kwasababu dhiraa hutumika kupima urefu, na siyo muda. Taswira ya maisha ya mtu kufutwa kama vile ubao, au kamba , au kitu chochote kigumu.

**ikiwa basi hamuwezi kufanya....hayo mengine ?**
Yesu alitumia swali lingine kuwafundisha wanafunzi wake.

## Luke 12:27

**maua**
(Lilies), haya ni mauwa mazuri yanayojiotea yenyewe shambani. Kama lugha yako haina jina la mauwa ya aina ya (lily) unaweza kutumia jina lingie la maua yanayofanana na hilo au tafsiri kama "maua"

**wala hayajisokoti**
"haitengenezi uzi ili yajivike" au "hawatengenezi uzi"

**Sulemani katika utukufu wake**
"Sulemani aliyekuwa na mali nyingi" au "Sulemani aliyevikwa vizuri"

**Kama Mungu huyavika vizuri majani ya kondeni**
"Kama Mungu huyavika majani ya kondeni namna hiyo " au "Kama Mungu huwapa mauwa ya kondeni mavazi mazuri hivyo" Kama Mungu hufanya majani ya kondoni kuwa mazuri kama hivi"

**hutupwa kwenye moto**
"mtu huzitupa kwenye moto"

**Je si zaidi atawavika ninyi**
"Hii ni mshangao na siyo swali. Yesu alitilia mkazo kuwa atawatunza na kuwajali watu zaidi kuliko anavyojali majani.

## Luke 12:29

**Msisumbukie juu ya kuwa mtakula nini au mtakunywa nini**
"usitazame zaidi juu ya kula na kunywa" au "Msiwe na tamaa zaidi ya kula na kunywa"

**mataifa yote ya dunia**
Hapa "mataifa" inamaanisha "wasio amnini" "Watu wote wa mataifa mengine" au "watu wote wasio amini duniani"

**Baba yenu anajua ya kuwa mnahitaji vitu hivyo**
Baba wa Yesu, Mungu Baba, pia hufanyika Baba wa wote watakao muamini Yesu.

**Baba**
Hii ni sifa muhimu sana kwa Mungu.

### Luke 12:31

**tafuteni ufalme**
"kushughulika na ufalme wa Mungu" au "Kutamani sana ufalme wa Mungu"

**na hayo mengine mtazidishiwa**
"hayo mambo mengine pia mtapewa". "Hayo mengine" ina maanisha chakula na mavazi. "Mungu atawapa ninyi hizo vitu"

**kundi dogo**
Yesu aliwaita wanafunzi wake kundi. Kundi ni mkusanyiko wa kondoo au mbuzi ambayo mchungaji anawatunza. Kama vile mchungaji anvyowajali kondoo, Mungu atawajali wanafunzi wa Yesu. "kundi dogo"au "kundi linalopendwa"

### Luke 12:33

**na mkawape maskini**
"na wapeni watu maskini fedha mlizopata kwa mauzo"

**mjifanyie mifuko ...hazina ya mbinguni**
mifuko na hazina mbinguni zinamaanisha kitu kimoja. Vyote vinawakilisha baraka za Mungu mbinguni.

**mjifanyie**
"kwa namna hii mtajifanyia wenyewe"

**mifuko isiyoishiwa**
"mifuko ya fedha ambazo hazitoboki"

**isiyokoma**
'"ambazo haiishiwi" au "haipungui"

**Moyo wako**
Hapa "moyo" una maanisha mawazo ya mtu.

### Luke 12:35

**Kauli ya jumla**
Yesu alianza kuelezea mfano

**nguo zenu refu zifungwe na mkanda**
Watu walivaa mavazi marefu. Walikuwa wakifunga na mkanda ili kuwafanya waweze kutembea njiani . " Funga nguo zako na mkanda ili uweze kuhudumia" au Uvae na uwe tayari kuhudumia"

**taa zenu zihakikishwe kuwa zinaendelea kuwaka**
"Fanyeni taa zenu ziendelee kuwaka"

**muwe kama watu wanaomtazamia Bwana wao**
Hii unafananishwa na jinsi wanafunzi wanavyotakiwa kuwa tayari kwa Yesu kurudi kama watumishi walio tayari kwa bwana wao kurudi.

**kutoka kwenye karamu ya harusi**
"kurudi nyumbani kutoka kwenye karamu ya harusi"

### Luke 12:37

**Wamebarikiwa**
"Ni vizuri kama nini"

**ambao bwana atawakuta wako macho akirudi**
"wale ambao bwana wao atawakuta wakimngoja atakapo rudi" au "Walio tayari bwana akirudi"

**atafunga ..atawaketisha chini**
Kwasabu watumishi wamekuwa waaminifu na wako tayari kumuhudumia bwana wao, bwana atawalipa kwa kuwahudumia wao.

**atafunga nguo yake refu na mkanda**
'atajiandaa kuwahudumia wao kwa kufunga nguo yake na mkanda" au " atavaa tayari kuwahudumia"

**kwa zamu ya pili ya ulinzi ya usiku**
zamu ya pili ya ulinzi ni kati ya saa 3:00 usiku na saa 6:00 usiku. "karibu na usiku wa manane" au "kabla ya usiku wa manane"

**au kwa zamu ta tatu ya ulinzi**
zamu ya tatu ya ulinzi ni kuanzia saa 6:00 usiku na na saa 9:00 usiku. Au "akija akiwa amechelewa sana usiku"

### Luke 12:39

**asingeruhusu nyumba yake ifunjwe**
"asingeruhusu mwizi aivunje nyumba yake"

**kwani hamjui ni saa ngapi mwana wa Adamu atarudi**
Kitu pekee kinacho wafananishwa kati ya mwizi na Mwana wa Adamu ni kwamba watu hawajui ni wakati gani wanakuja, hivyo wanatakiwa kuwa tayari.

**wakati gani Mwana wa Adamu atarudi**
Yesu alikuwa akiongelea habari zake mwenyewe. "wakati Mimi, Mwana wa Adamu, nitakapo kuja"

### Luke 12:41

**Kauli inayounganisha**
Katika mstari wa 42, Yesu aliendelea kuelezea mfano

**Kauli ya jumla**
Katika mstari wa 41, kuna katizo katika kuelezea mfano kwani Petro alimuuliza Yesu swali kuhusu mfano.

**Ni nani...kwa wakati mwafaka**
Yesu alitumia swali kufundisha watu. Yesu hakujibu swali la Petro moja kwa moja, lakini alitegemea wale wanaotaka kuwa watumwa waaminifu kuwa mfano huo inawahusu wao. " Nimesema kwa kila mmoja ambaye ..kwa wakati mwafaka.

**Mtumwa mwaminifu na mwenye hekima**
Yesu alielezea mfano mwingine wa jinsi watumishi wanavyotakiwa kuwa waaminifu wakati wanamngoja bwana wao arudi.

**ambaye bwana wake atamuweka juu ya watumishi wengine**
"ambaye bwana wake atamuweka kuwa mtawala wa wengine"

**Amebarikiwa mtumishi yule**
"Itakuwa heri kwa mtumishi yule"

**ambaye bwana wake akija atamkuta akifanya**
"kama bwana wake akirudi atamkuta akifanya kazi hiyo"

### Luke 12:45

**Mtumishi yule**
Hii ina maanisha yule mtumishi ambaye bwana alimuweka juu ya wengine

**akisema moyoni mwake**
"akafikiri ndani yake"

**bwana wangu anakawia kurudi**
"bwana wangu hatarudi mapema"

**watumishi wa kiume na wa kike**
Neno lililotafsiriwa hapa kama "watumishi wa kiume na Kike" mara nyingi hutafsiriwa kama "wavulana" na "wasichana". Inaweza kuashiri kuwa watumishi walikuwa vijana au wanao pendwa sana na bwana wao.

**katika siku asiyotegemea**
"wakati mtumishi hamtegemei"

**kumuweka katika sehemu pamoja na wasio waaminifu**
Inaweza kuwa na maana zifuatazo: 1) Ile hali ya bwana kutoa adhabu kali kwa mtumishi wake. 2) Hii inaelezea jinsi ambavyo mtumishi atakavyo vyongwa kama adhabu.

### Luke 12:47

**Kauli inayounganisha**
Yesu alimaliza kuelezea mfano

**atapigwa viboko vingi**
"atapigwa mara nyingi" au "atachapwa mara nyingi" ."bwana wake atampiga mara nyingi"au "bwana wake atamuadhibu sana"

**kwa kuwa yeye aliyepewa vingi, vingi hudaiwa kutoka kwake**
"watahitaji vingi kwa yeyote aliyepokea vingi" au " bwana atahitaji vingi kwa kila mmoja aliyempa vingi"

**na yeye aliyeaminiwa kwa vingi**
"Kwa yule waliyempatia vitu vingi avitunze" au "kwa yule aliyepewa wajibu mkubwa"

**aliyeaminiwa ...vitadaiwa**
"bwana alimkabidhi ..bwana atataka"

### Luke 12:49

**Kauli inayounganisha**
Yesu aliendelea kufundisha wanafunzi wake

**Nimekuja kuwasha moto duniani**
"Nimekuja kutupa moto duniani" au "Nimekuja kuwasha moto duniani" . Inawsza kuwa na maama zifuatazo: 1) Yesu alikuja kuwahukumu watu 2) Yesu alikuja kuwatakasa wanaomuamini 3) Yesu alikuja kusababisha kugawanyika kwa watu.

**natamani iwe imekwisha kuwaka**
Kuna msisitizo wa njisi alivyotaka hayo yatokee. " Natamani sana kuwa imeshawaka" au "Ni jinsi gani ninavyotamani iwe imeshaanza"

**Lakini nina ubatizo ambao nitabatizwa kwayo**
"Ubatizo" ina maanisha aina ya mateso ambayo Yesu atapata. Kama maji yamfinikavyo mtu wakati wa ubatizo, mateso yatamkabili na kumpata Yesu. " Ni lazima nipitie mateso mabaya" au "Nitapitia katika mateso makubwa kama vile mtu anavyofunikwa na maji wakati wa ubatizo"

**Lakini**
Neno "Lakini" linatumika kuonyesha kuwa hatawasha moto duniani mpaka kwanza apitie hayo mateso"

**nina huzuni hadi ikamilike**
Mshangao inasisitiza jinsi alivyo na huzuni. "Nina huzuni sana na itaendelea kuwepo hadi nimalize ubatizo huu wa mateso"

### Luke 12:51

**Je mnafikiri kuwa nimekuja kuleta amani duniani?**
Yesu alitumia swali kufundisha wanafunzi wake. Watu walimtegemea Masiha awaletee amani kwa maadui wao. "Msifikiri kuwa nimekuja kuleta amani duniani"

**lakini badala yake mgawanyiko**
" lakini nimekuja kuleta mgawanyiko" au "watu watakuwa wakigawanyika miongoni mwao kwa sababu nimekuja"

**mgawaniko**
"uadui" au "kutoelewana"

**kutakuwa na watu watano katika nyumba moja wamegawanyika**
Hii ni mfano wa aina ya mgawanyiko utakao kuwepo kwenye familia.

**kutakuwa na watano katika nyumba moja**
kutakuwepo na watu watano katika nyumba moja

## Luke 12:54

**Kauli ya Jumla**
Yesu alianza kuonge na umati

**Nyakati za mvua zimewadia**
"Mvua inakuja" au "Inaenda kunyesha"

**nchi na anga**
"nchi na anga" au " hali ya hewa"

**inakuwaje hamuwezi kutafsiri nyakati za leo?**
Yesu alitumia swali kukemea umati. "Mnatakiwa kujua namna ya kutafsiri nyakati za leo"

## Luke 12:57

**kwanini msihukumu yaliyo sahihi wenyewe?**
Yesu anatumia swali kukemea umati. Anafundisha namna ya kufanya jambo jema kabila ya kuchelewa. Ninyi wenyewe mwatakiwa kutambua yaliyo mema"

**wenyewe**
"kwa utashi wenu" au "wakati bado mna muda wa kufanya hivyo"

**Maana mkienda**
Japo Yesu alikuwa akiongea na umati, hali aliyokuwa anaiwasilisha ni ya mtu kupitia mwenyewe..

**kukubaliana na mshitaki wako**
"mkubaliane juu ya jambo na mshitaki wako"

**hakimu**
Hili lina maanisha hakimu mkazi, lakini neno hili hap ni maalum zaidi na linatisha.

**hatakutoa huko**
"hatakuruhusu wewe utoke huko"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 13

1 Kwa wakataihuo huo, kulikuwa na baadhi watu waliomtaarifu juu ya Wagalilaya ambao Pilato aliwaua na
kuchanganya damu yao na sadaka zao. 2 Yesu akajibu na kuwaambia, "Je mwadhani kuwa Wagalilaya hao
walikuwa na dhambi kuliko Wagalilaya wengine wote ndiyo maana wamepatwa na mabaya hayo? 3
Hapana, nawaambia, lakini msipotubu, nanyi mtaangamia vivyo hivyo. 4 Au wale watu kumi na nane
katika Siloamu ambao mnara ulianguka na kuwaua, mnafikiri wao walikuwa wenye dhambi zaidi kuliko
watu wengine katika Yerusalemu? 5 Hapana, mimi nasema, lakini kama msipotubu, ninyi nyote pia
mtaangamia. 6 Yesu aliwaambia mfano huu, "Mtu mmoja alikuwa na mtini umepandwa katika shamba
lake na alikwenda kutafuta matunda juu yake lakini hakupata. 7 Akamwambia mtunza bustani, 'Tazama,
kwa miaka mitatu nimekuja na kujaribu kutafuta matunda kwenye mtini huu lakini sikupata. Uukate.
Kwani ulete uharibifu wa ardhi? 8 Mtunza bustani akajibu na kusema, 'uache mwaka huu ili niupalilie na
kuweka mbolea juu yake. 9 Kama ukizaa matunda mwaka ujao, ni vema; lakini kama hautazaa, uukate.!"'
10 Sasa Yesu alikuwa akifundisha katika mojawapo ya Masinagogi wakati wa Sabato. 11 Tazama,
alikuwepo mama mmoja ambaye kwa miaka kumi na minane alikuwa na rohomchafu wa udhaifu, na yeye
alikuwa amepinda na hana uwezo kabisa wa kusimama. 12 Yesu alipomwona, alimwita, akamwambia,
"Mama, umewekwa huru kutoka kwenye udhaifu wako." 13 Akaweka mikono yake juu yake, na mara mwili
wake akajinyoosha na akamtukuza Mungu. 14 Lakini mkuu wa sinagogi alikasirika kwa sababu Yesu
alikuwa amemponya siku ya Sabato. Hivyo mtawala akajibu akawambia makutano, "Kuna siku sita
ambazo ni lazima kufanya kazi. Njoni kuponywa basi, si katika siku ya Sabato. ' 15 Bwana akamjibu na
akasema, "wanafiki! Hakuna kila mmoja wenu kufungua punda wako au ng'ombe kutoka zizini na
kuwaongoza kumpeleka kunywa siku ya Sabato? 16 Hivyo pia binti wa Abrahamu, ambaye Shetani
amemfunga kwa miaka kumi na minane, je haikumpasa kifungo chake kisifunguliwe siku ya sabato?" 17
Alipokuwa akisema maneno hayo, wale wote waliompinga waliona aibu, bali makutano wote wa wengine
walishangilia kwa ajili ya mambo ya ajabu aliyotenda. 18 Yesu akasema, "Ufalme wa Mungu unafanana na
nini, na naweza kuulinganisha na nini? 19 Ni kama mbegu ya haradari aliyoitwaa mtu mmoja na kuipanda
shambani mwake, na ikamea ikawa mti mkubwa, na ndege wa mbinguni wakajenga viota vyao katika
matawi yake. 20 Tena akasema, "Niufananishe na nini ufalme wa Mungu? 21 Ni kama chachu ambayo
mwanamke aliichukua na kuchanganyakwenye vipimo vitatu vya unga hata ukaumuka." 22 Yesu
alitembelea kila mji na kijiji njiani akielekea Yerusalemu na kuwafundisha. 23 Mtu mmoja akauliza,
"Bwana, ni watu wachache tu watakaookolewa?" Hivyo akawaambia, 24 "Jitahidi kuingia kwa kupitia
mlango mwembamba, kwa sababu wengi watajaribu na hawataweza kuingia. 25 Mara baada ya mmiliki
wa nyumba kusimama na kufunga mlango, basi mtasimama nje na kupiga hodi mlangoni na kusema,
Bwana, Bwana, tufungulie yeye atajibu na kuwaambia, siwajui ninyi wala mtokako.' 26 Ndipo mtasema,
Tulikula na kunywa mbele yako na wewe ulifundisha katika mitaa yetu." 27 Lakini yeye atawajibu,
`nawaambia, siwajui mtokako, ondokeni kwangu, ninyi watenda maovu!' 28 Kutakuwa na kilio na kusaga
meno wakati mtakapowaona Abrahamu, Isaka, Yakobo na manabii wote katika ufalme wa Mungu, lakini
ninyi wenyewe mumetupwa nje. 29 Watafika kutoka Mashariki, Magharibi, Kaskazini na Kusini, na
kupumzika katika meza ya chakula cha jioni katika ufalme wa Mungu. 30 Na tambua hili, wa mwisho ni
wa kwanza na wa kwanza atakuwa wa mwisho." 31 Muda mfupi baadaye, baadhi ya Mafarisayo walikuja
na kumwambia, "Nenda na ondoka hapa kwa sababu Herode anataka kukuua." 32 Yesu akasema,
"Nendeni mkamwambie yule mbweha, `Tazama, ninawafukuza pepo na kufanya uponyaji leo na kesho, na
siku ya tatu nitatimiza lengo langu. 33 Katika hali yoyote, ni muhimu kwa ajili yangu kuendelea leo, kesho,
na siku iliyofuata, kwa vile haikubaliki kumuua nabii mbali na Yerusalemu. 34 Yerusalemu, Yerusalemu,
nani anawaua manabii na kuwapiga mawe wale waliotumwa kwenu. Mara ngapi nimetaka kuwakusanya
watoto wenu kama vile kuku anavyokusanya vifaranga vyake chini ya mbawa zake, lakini humkulitaka hili.
35 Tazama, nyumba yako imetelekezwa. Nami nawaambia, hamuwezi kuniona hata mtakaposema
'Amebarikiwa huyo ajaye kwa jina la Bwana.'"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

# Luka 13 Maelezo ya Jumla

### Takwimu muhimu za matamshi katika sura hii

### Maarifa ya Kudhaniwa

Sura hii inaanza na kurejelea ya matukio mawili, ambayo maelezo yake hayajahifadhiwa (Luka 13:1-5).

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

### Matumizi ya kitendawili

Kitendawili ni taarifa inayoonekana kuwa ya ajabu, ambayo ni kana kwamba inajikana yenyewe, lakini kwa hakika sio ya ajabu. Mfano wa kitendawili katika sura hii: "wale ambao hawana muhimu zaidi watakuwa wa kwanza, na wale ambao ni muhimu zaidi watakuwa wa mwisho" (Luka 13:30).

---

## Luke 13:1

**Unganisha maelezo:**
Yesu bado akizungumza mbele ya umati wa watu. Hii ni sehemu moja ya hadithi aliyoanza

**Habari kwa ujumla:**
Katika aya hizi, baadhi ya watu katika umati walimuuliza Yesu swali na anaanza kujibu.

**Wakati huo**
Msemo huu unajumuisha tukio hili hadi mwisho wa sura ya 12 wakati Yesu alikuwa akifundisha umati wa watu.

**ambao damu Pilato kuchanganywa na sadaka yao wenyewe**
Hapa 'damu' inahusu kifo cha Wagalilaya. pengine Pilato akaamuru askari wake kuua watu badala ya kufanya hivyo mwenyewe. AT "ambaye askari wa Pilato waliuawa wakati Wagalilaya walipokuwa wakitoa dhabihu."

**Unafikiri kwamba hawa Wagalilaya ni wenye dhambi**
.......

**Hapana nawaaambia**
Hapa 'Nawaambia' nasisitiza 'hapana.' AT "Kwa hakika walikuwa si wenye dhambi" au "wewe unakosea kufikiri kwamba mateso yao yanathibitisha kwamba walikuwa wenye dhambi."

**Nyinyi nyote mtaangamia kwa njia sawa**
"nyinyi nyote pia mtakufa. "Msemo" katika njia hiyo hiyo' ina maana wao watakuwa na uzoefu wa matokeo sawa, si kwamba watakufa kwa njia sawa.

**kuangamia**
"kupoteza maisha yako " au "kufa"

## Luke 13:4

**Au wale**
Huu ni mfano wa pili wa Yesu kuhusu watu ambao walioteseka. AT "Au kuhusisha wale" au "Fikiria kuhusu wale."

**watu kumi na nane**
"18 watu"

**Siloamu**
Hili ni jina la eneo la Yerusalemu

**unathani walikuwa wamepotelea dhambini**
'Walikuwa wenye dhambi zaidi' au "gani hii kuthibitisha kwamba walikuwa zaidi wenye dhambi?' Yesu anatumia swali kufundisha watu. AT 'sidhani kwamba walikuwa zaidi wenye dhambi

**watu wengine**
"watu wengine"

**Hapana nasema**
Hapa "Nasema" inasisitiza "Hapana" AT "Kwa hakika walikuwa si zaidi wenye dhambi" au 'Wewe ni unakosea kufikiri kwamba mateso yao yanathibitisha kwamba walikuwa zaidi wenye dhambi."

**angamia**
"Kupoteza maisha yako" au "kufa"

## Luke 13:6

**Habari za jumla**
Yesu anaanza kwa kuwaambia mfano kueleza kauli yake ya mwisho, "Lakini kama hamta tubu, nyote pia mtangamia."

**Mtu mmoja alikuwa amepanda mti**
Mtu alikuwa amepanda mti

**Miaka mitatu**
3 miaka

**Kwani unaleta unaharibifu wa ardhi?**
mtu anatumia swali kusisitiza kwamba mti haina maana na mtunza bustan lazima aukata. AT "Je, si basi unaharibu ardhi".

### Luke 13:8

**kuunganisha maelezo**
Yesu alimaliza kusimulia mfano wake. Huu ni mwisho wa sehemu ya hadithi ambayo ilianza

**Uache**
AT '"usiufanyie kitu chochote huu mti" au " usiukate"

**na weka mbolea juu yake**
"na weka mbolea kwenye udongo." Mbolea ni kinyesi cha wanyama. Watu huiweka kwenye ardhi kufanya udongo kuwa mzuri kwa mimea na miti.

**Ukate**
Mtumishi alitoa pendekezo; yeye hakuwa anatoa amri kwa mmiliki. AT "Ngoja niukate" au "Niambie niukata."

### Luke 13:10

**Habari za jumla**
Hii ni sehemu ya pili ya hadithi. aya hizi hutoa taarifa ziliyopita kuhusu mazingira ya sehemu hii ya hadithi na kuhusu mwanamke mlemavu aliyetambulishwa kwenye hadithi

**Sasa**
neno hili ni alama ya sehemu mpya ya hadithi.

**wakati wa Sabato**
"Siku ya Sabato." Baadhi ya lugha husema "Sabato" kwa sababu hatujui ambavyo hasa siku ya Sabato ilikuwa.

**Tazama, mwanamke alikuwa huko**
Neno "tazama" hapa alerts sisi mtu mpya katika hadithi.

**Miaka kumi na nane**
18 miaka

**roho mbaya ya udhaifu**
"Roho mbaya kwamba ilimfanya yeye awe dhaifu"

### Luke 13:12

**Umeponywa udhaifu wako**
"Wewe umeponywa kutokana na ugonjwa wako." Kwa kusema hivyo, Yesu alikuwa akifanya na kutokea.

**Aliweka mikono yake juu yake**
Yeye alimgusa

**yeye aliweza kujiinua**
AT "yeye alisimama moja kwa moja"

**alichukizwa kwa sababu Yesu alikuwa amemponya**
AT "alikuwa na hasira kwa sababu Yesu amemponya"

**akajibu na kusema**
"Alisema" au "alijibu"

**Mje na muponywe kisha**
AT "njooni basi huponya wakati wa siku hizo sita"

### Luke 13:15

**Bwana akamjibu**
"Bwana alijibu kwa mtawala wa sinagogi"

**sio kila mmoja wenu kufungua punda wako ... Sabato?**
Yesu anatumia swali kuwafanya wao kufikiri juu ya kitu tayari walijua. AT 'Wewe kufungua punda wako ... Sabato."

**Punda au Ng'ombe**
Hawa ni wanyama ambao watu kuwatunza kwa kuwapa maji.

**Mtoto wa Ibrahimu**
AT "uzao wa Ibrahimu"

**ambaye Shetani alimfunga**
AT "ambaye Shetani alimfanya kilema" au "ambaye Shetani alimfunga kwa ugonjwa huu"

**miaka kumi na nane miaka mingi**
18 kwa miaka mingi. "neno "mrefu" hapa inasisitiza kuwa miaka kumi na minane ilikuwa muda mrefu sana kwa mwanamke kuteseka. Lugha nyingine wanaweza kuwa na njia nyingine ya kusisitiza hili.

**lazima vifungo vyake asifunguliwe ... siku?**
Yesu anazungumza kuhusu ugonjwa wa wanawake kana kwamba ni kana kwamba amefungwa. AT "ni haki ya kumfungua yeye kutoka kwa Shetani ... siku" au "ni haki ya kutolewa yeye kutoka vifungo vya ugonjwa huu ... siku."

### Luke 13:17

**Kama alivyosema mambo hayo**
"'Wakati Yesu aliposema mambo hayo"

**mambo ya ukufu aliyofanya**
"Mambo ya ukufu Yesu alikuwa akifanya"

### Luke 13:18

**Kuunganisha maelezo**
Yesu alianza kwa kuwaambia mfano kwa watu katika sinagogi.

**Ufalme wa Mungu unafanana na nini**
Yesu anatumia swali kutambulisha kile yeye kitamhusu kufundisha. AT "Mimi nitawaambia ufalme wa Mungu ni kama nini"

**nini naweza kuulinganisha nacho**
Hii kimsingi ni sawa na swali lililopita. Yesu alitumia hilo kutambulisha nini ataweza kukizungumzia . Baadhi ya lugha wanaweza kutumia yote kwa ujumla, na baadhi kutumia moja tu.

**Ni kama mbegu ya Haradali**
Mbegu ya haradali ni mbegu ndogo sana ambayo hukua katika mimea kubwa. Kama hii haijulikani, inaweza kutafsiriwa kwa jina la mbegu nyingine kama hiyo au rahisi kama "mbegu ndogo."

**na huipanda Bustanini mwake**
na hupandwa katika bustani zao. ' Watu hupanda aina ya baadhi ya mbegu kwa kuzitupa ili waweze kuzitawanya katika bustani.

**mti mkubwa**
Hii ni exaggeration ya kufanya hatua. AT 'kichaka kubwa sana.'

**"Ndege wa angani"**
"Ndege wa angani." AT "ndege warukao angani" au "ndege".

## Luke 13:20

**Unganisha maelezo**
Yesu alimaliza kuzungumza na watu katika sinagogi. Huu ni mwisho wa sehemu hii ya hadithi.

**Kwa nini naweza kulinganisha Ufalme wa Mungu?**
Yesu anatumia swali jingine kutambulisha kile yeye ataweza kufundisha.

**Ni kama chachu**
Kiasi kidogo tu cha chachu kilikua kinahitajika ili kufanya kiasi cha unga kuumuka . Hii inaweza kufanya wazi kama ilivyo katika UDB.

**vipimo vitatu vya unga**
"kiasi kikubwa cha unga" au kwa muda kwamba utamaduni wako unatumia kwa kupima kiasi kikubwa cha unga.

## Luke 13:22

**Habari za jumla:**
Hii ni sehemu ya nyingine ya hadithi. Yesu anajibu swali kwa kuwaeleza mfano kuhusu kuingia ufalme wa Mungu

**Yesu alitembelea kila mji na kijiji ... na kuwafundisha**
Hii ni taarifa zilizopita kwamba kutuambia nini Yesu alikuwa akifanya wakati tukio hili lilipotokea.

**ni watu wachache tu watakao okolewa**
Mungu ataokoa watu wachache tu

**pPmbana kuingia kwa kupitia mlango mwembamba**
"Fanya Kazi kwa bidii ili kupita njia ya mlango mwembamba." Yesu anazungumza kuhusu ufalme wa Mungu kana kwamba ni nyumba. Yesu anazungumza na kundi, "wewe" alisema katika amri hii ni wingi

## Luke 13:25

**mmiliki wa nyumba**
Hii ina maana ya Mungu. AT "Mungu."

**utakuwa umesimama nje**
Yesu alikuwa akizungumza na mkuta. mfumo wa "ninyi" ni wingi. Yeye aliwashughulikia wao kama vile hawataingia kwa kupitia mlango katika ufalme

**Pound mlango**
"Kugonga kwenye mlango"

**Ondokeni kwangu**
"Nenda mbali na mimi"

**watenda maovu**
"watu wanaofanya uovu "

## Luke 13:28

**Unganisha maelezo**
Yesu anaendelea kuzungumzia kuingia katika ufalme wa Mungu. Huu ni mwisho wa mazungumzo haya.

**lakini nyinyi-nyinyi mulikuwa mutupwe nje**
"lakini ninyi wenyewe mulikuwa mutupwe nje." AT "Lakini Mungu atawafukuza nyinyi nje"

**Wao watafika**
"Watu watakuja"

**wa mwisho ni wakwanza**
Hii ni kuhusu heshima au umuhimu. AT "baadhi ambao ni muhimu angalau watakuwa muhimu zaidi'"au "baadhi ambaye watu hawata mheshima, Mungu atamheshimu."

## Luke 13:31

**Kuunganisha Maelezo**
Kuunganisha Maelezo Hili ni tukio la lingine katika sehemu hii ya hadithi. Yesu bado yupo njia kuelekea Yerusalemu, wakati baadhi ya Mafarisayo wakizungumza naye kuhusu Herode.

**Muda mfupi baadae**
'"Muda mfupi baada ya Yesu alipomaliza kusema"

**Nenda na ondoka hapa kwa sababu Herode anataka kukuua**
Tafsiri hii kama onyo kwa Yesu. Walikuwa wakitoa ushauri aende mahali pengine na kuwa salama.

**Herode anataka kukuua**
Herode ataagiza watu kumuua Yesu. AT "Herode anataka kupeleka watu wake kuua wewe."

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**yule mbweha**
Yesu alimuita Herode mbweha. Mbweha ni mbwa porini mdogo. Maana inawezekana ni 1) Herode hakuwa tishio kubwa wakati wote 2) Herode alikuwa mdanganyifu

**siku ya tatu**
Angalia:

**haikubaliki kumuua nabii mbali na Yerusalemu**
Viongozi wa Wayahudi waliua manabii wengi wa Mungu katika Yerusalemu na Yesu alijua kwamba wangeweza kumuua huko pia. AT "ni katika Jerusalem kwamba viongozi wa Wayahudi huwaua wajumbe wa Mungu."

### Luke 13:34

**Kuunganisha maelezo:**
Yesu alimaliza kukabiliana na Mafarisayo. Hii ni mwisho wa sehemu hii ya hadithi.

**Yerusalemu, Yerusalemu**
esu anazungumza kana kwamba watu wa Yerusalemu walikuwa huko kumsikiliza. Yesu alisema hii mara mbili ili kuonyesha jinsi alikuwa akisikitisha kwa ajili yao

**mnawaua manabii na kuwapiga mawe wale waliotumwa kwenu**
Kama itakuwa ni ajabu kushughulikia mji, unaweza kufanya wazi kwamba Yesu kwa kweli akihutubia watu katika mji "wewe watu wanaowaua manabii na kuwapiga mawe wale Mungu aliwatumwa kwenu"

**kuwakusanya watoto wako**
"Kukusanya watu wako" au 'kukusanya wewe"

**kwa jinsi kuku anavyokusanya vifaranga vyake chini ya mbawa zake**
Hii inaelezea jinsi kuku inalinda vifaranga wake kutokana na madhara kwa kufunika wao kwa mbawa zake

**nyumba yenu imetelekezwa**
Hii inaelezea jinsi kuku inalinda vifaranga wake kutokana na madhara kwa kuwafunika wao kwa mbawa zake.Maana inawezekana ni 1) "Mungu amekuacha" au 2) "mji yako ni tupu." Inamaana kwamba Mungu ameacha kulinda watu wa Yerusalemu, hata maadui wanaweza kuwashambulia na kuwafukuza. Huu ni unabii kuhusu jambo ambalo lingetokea hivi karibuni. AT "nyumba yako itakuwa imetelekezwa' au 'Mungu atawaacha ninyi."

**huwezi kuniona mimi hadi mtakaposema**
"Huwezi kuniona mpaka wakati unakuja wakati utasema" au "wakati mwingine utakaponiona, utasema"

**JIna la bwana**
Hapa "jina" inahusu nguvu na mamlaka ya Bwana

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 14

1 Iltokea siku ya Sabato, alipokua akienda nyumbani kwa mmoja wa viongozi wa Mafarisayo kula mkate,
nao walikuwa wakimchunguza kwa karibu. 2 Tazama, pale mbele yake alikuwa mtu ambaye
anasumbuliwa na uvimbe. 3 Yesu aliuliza wataalam katika sheria ya Wayahudi na Mafarisayo, "Je, ni halali
kumponya siku ya Sabato, au sivyo?" 4 Lakini wao walikuwa kimya, kwahiyo Yesu akamshika, akamponya
na kumruhusu aende zake. 5 Naye akawaambia, "Ni nani kati yenu ambaye ana mtoto au ng'ombe
anatumbukia kisimani siku ya Sabato hata mvuta nje mara moja?" 6 Wao hawakuwa na uwezo wa kutoa
jibu kwa mambo haya. 7 Wakati Yesu alipogundua jinsi wale walioalikwa kwamba wamechagua viti vya
heshima, akawaambia mfano, akiwaambia, 8 "Wakati mnapoalikwa na mtu harusini, usiketi katika nafasi
za heshima, kwa sababu inawezekana amealikwa mtu ambaye ni wakuheshimiwa zaidi kuliko wewe. 9
Wakati mtu aliyewaalika ninyi wawili akifika, atakuambia wewe, "mpishe mtu huyu nafasi yako," na kisha
kwa aibu utaanza kuchukua nafasi ya mwisho. 10 Lakini wewe ukialikwa, nenda ukakae mahali pa
mwisho, ili wakati yule aliyekualika akija, aweze kukuambia wewe, `Rafiki, nenda mbele zaidi." ndipo
utakuwa umeheshimika mbele ya wote walioketi pamoja nawe mezani. 11 Kwa maana kila ajikwezaye
atashushwa, na yeye ajishushae atakwezwa. ' 12 Yesu pia alimwambia mtu aliyemwalika, 'Unapotoa
chakula cha mchana au cha jioni, usiwaalike rafiki zako au ndugu zako au jamaa zako au majirani zako
matajiri, ili kwamba wao wasije wakakualika wewe ukapata malipo. 13 Badala yake, unapofanya sherehe,
waalike maskini, vilema, viwete na vipofu, 14 na wewe utabarikiwa, kwa sababu hawawezi kukulipa. Kwa
maana utalipwa katika ufufuo wa wenye haki." 15 Wakati mmoja wa wale walioketi mezani pamoja na
Yesu aliposikia hayo, naye akamwambia, "Amebarikiwe yule atakayekula mkate katika Ufalme wa
Mungu!" 16 Lakini Yesu akamwambia, "Mtu mmoja aliandaa sherehe kubwa, akaalika watu wengi. 17
Wakati sherehe ilipokuwa tayari, alimtuma mtumishi wake kuwaambia wale walioalikwa, `'Njooni, kwa
sababu vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari.' 18 Wote, wakaanza kuomba radhi. Wa kwanza
akamwambia mtumishi, 'Nimenunua shamba, lazima niende kuliona. Tafadhali unisamehe.' 19 Na
mwingine akasema, `'Nimenunua jozi tano za ng'ombe, na mimi naenda kuwajaribu. Tafadhali uniwie
radhi.' 20 Na mtu mwingine akasema, 'Nimeoa mke, kwa hiyo siwezi kuja.' 21 Mtumishi akarudi na
kumwambia bwana wake mambo hayo. Yule mwenye nyumba alikasirika akamwambia mtumishi wake,
`'Nenda upesi mitaani na katika vichochoro vya mji ukawalete hapa maskini, vilema, vipofu na
walemavu." 22 Mtumimishi akasema, `Bwana, hayo uliyoagiza yamekwisha tendeka, na hata sasa bado
kuna nafasi.' 23 Bwana akamwambia mtumishi, 'Nenda katika njia kuu na vichochoro na uwashurutishe
watu waingie, ili nyumba yangu ijae. 24 Kwamaana nawaambia, katika wale walioalikwa wa kwanza
hapana atakayeonja sherehe yangu. ' 25 Sasa umati mkubwa walikuwa wanakwenda pamoja naye, naye
akageuka na akawaambia, 26 'Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, mama yake, mke wake,
watoto wake, ndugu zake waume na wanawake- ndio, na hata maisha yake pia -hawezi kuwa mwanafunzi
wangu. 27 Mtu asipochukua msalaba wake na kuja nyuma yangu hawezi kuwa mwanafunzi wangu. 28
Maana ni nani kati yenu, ambaye anatamani kujenga mnara hataketi kwanza akadirie gharama kwa
mahesabu kama ana kile anachohitaji ili kukamilisha hilo? 29 Vinginevyo, baada ya kuweka msingi na
kushindwa kumaliza, wote walioona wataanza kumdhihaki, 30 wakisema, Mtu huyu alianza kujenga,
akawa hana nguvu za kumaliza.' 31 Au mfalme gani, akitaka kwenda kupigana na mfalme mwingine katika
vita, ambae hatakaa chini kwanza na kuchukua ushauri kuhusu kama ataweza, pamoja na watu elfu kumi
kupigana na mfalme mwingine anayekuja juu yake na watu elfu ishirini? 32 Na kama sivyo, wakati jeshi la
wengine bado liko mbali, hutuma balozi kutaka masharti ya amani. 33 Kwa hiyo basi, yeyote kati yenu
ambaye hataacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu. 34 Chumvi ni nzuri, lakini ikiwa
Chumvi imepoteza ladha yake, jinsi gani inaweza kuwa chumvi tena? 35 Haina matumizi kwa udongo au
hata kwa mbolea. hutupwa mbali. Yeye aliye na masikio ya kusikia, na asikie."

---

## Luka 14 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

Mstari wa 3 unasema, "Yesu aliwauliza wataalam wa sheria ya Kiyahudi na Mafarisayo, 'Je, ni halali kuponya siku ya Sabato, au la?'" Mara nyingi, Mafarisayo walimkasirikia Yesu kwa kuponya siku ya Sabato. Katika kifungu hiki, Yesu awashangaza Mafarisayo. Ilikuwa kawaida Mafarisayo ambao walijaribu kumtega Yesu.

### Mabadiliko ya ghafla

Sura hii inabadilika kwa kasi kutoka kwenye mada moja hadi nyingine. Kuna sehemu kadhaa kubwa zilizo na mistari nyingi na mafundisho mengine mafupi yaliyomo katika mstari mmoja.

### Takwimu muhimu za matamshi katika sura hii

### Mfano

Luka 14:15-24 ni kama mfano uliopanuliwa. Ufalme wa Mungu unaweza kuwasilishwa kama sikukuu ya harusi au chakula cha jioni. Mfano huu ungeweza kuonyesha kuwa watu wanamkataa Yesu kwa sababu mbalimbali zisizo muhimu na kwa sababu ya hii kukosa kupokea baraka kubwa za Yesu.

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

### Matumizi ya kitendawili

Kitendawili ni taarifa inayoonekana kuwa ya ajabu, ambayo ni kana kwamba inajikana yenyewe, lakini kwa hakika sio ya ajabu. Mfano wa kitendawili katika sura hii: "kwa maana kila mtu atakayejikuza atanyenyekezwa, na yeye atakayejinyenyekeza atainuliwa" (Luka 14:11).

---

## Luke 14:1

**Taarifa kwa ujumla**
Hii ni sehemu ya pili ya hadithi. Leo ni Sabato na Yesu yuko nyumbani kwa Mfarisayo. Mstari wa 1 huwapa kutumia taarifa za msingi kuhusu mazingira ya hadithi.

**kula mkate**
"Kula" au "kwa ajili ya chakula." Mkate ilikuwa ni sehemu ya mlo na hutumiwa katika adhabu hii kwa kutaja mlo.

**kumuangali yeye kwa karibu**
Walitaka kuona kama wangeweza kumshtaki kufanya kitu chochote kibaya.

**Tazama, kuna mbele yake alikuwa ni mtu**
Neno "tazama" hutahadharisha sisi kwa mtu mpya katika hadithi. lugha yako inaweza kuwa njia ya kufanya hili. kiingeleza anatumia "Kuna mbele yake alikuwa mtu."

**alikuwa akisumbuliwa na uvimbe**
Uvimbe ni uvimbe unaotokana na ujenzi wa maji hadi katika sehemu za mwili. Baadhi ya lugha inaweza kuwa na jina kwa hali hii. AT "alikuwa akisumbuliwa kwa sababu sehemu ya mwili wake ilikuwa na uvimbe wa maji"

**Je, ni halali kumponya... siyo?**
"Je, sheria kibali chetu sio kuponya...?

## Luke 14:4

**Lakini wao wakanyamaza**
viongozi wa dini walikataa kujibu swali la Yesu.

**Ni nani kati yenu ambaye ana mwana au ng'ombe ... haitakua mara moja kumvuta yeye nje?**
Yesu anatumia swali kwa sababu yeye aliwataka kukubali kwamba wao wangemsaidia mtoto wao au ng'ombe, hata siku ya Sabato. Kwa hiyo, ilikuwa haki kwa yaye kuponya watu hata siku ya Sabato. AT "Kama mmoja wenu ana mwana au ng'ombe ... wewe bila ya shaka utamvuta yeye nje mara moja."

**Wao hawakuwa na uwezo wa kutoa jibu**
Walijua jibu na kwamba Yesu alikuwa sahihi, lakini hawakutaka kusema chochote kuhusu hilo. AT "Walikuwa hawana kitu cha kusema."

## Luke 14:7

**wale walioalikwa**
AT "wale ambao ni viongozi wa Mafarisayo walikuwa wamelikwa kwenye mlo"

**viti vya heshima**
"Viti kwa ajili ya watu wakuheshimiwa" au"'viti kwa ajili ya watu muhimu"

**Wakati wewe umealikwa na mtu**
AT "Wakati mtu anapokualika"

**kwa sababu mtu anaweza kuwa amemualika ambaye ni wakuheshimiwa zaidi kuliko wewe**
AT "kwa sababu mtu anaweza kuwa amamualika mtu ambaye ni muhimu zaidi kuliko wewe"

**na kisha kwa aibu**
"Basi utajisikia aibu na"

## Luke 14:10

**Kuunganisha maelezo**
Jesus continues speaking to the people at the Pharisee's house.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**Unapoalikwa**
AT "wakati mtu anakualika kwenye mlo"

**mahali pa chini zaidi**
"Kiti maana ya mtu angalau muhimu"

**kwenda juu zaidi**
"sogea kwenye kiti kwaajiri ya watu muhimu zaidi"

**Basi utakuwa wakuheshimiwa**
AT "Kisha mmoja ambaye aliyekualika wewe atakuheshimu"

**ambae anajiinu nafsi yake**
"Anajaribu kuangalia muhimu" au "ambaye anachukua nafasi muhimu"

**anayejinyenyekeza**
"atakuwa ameonyesha kuwa duni" au "atapewa nafasi isiyomuhimu." au "Mungu atakayejinyenyekeza.'

**anayejinyenyekeza**
"Ambaye amechagua kuangalia isiyo muhimu" au "ambaye amechukua nafasi isiyo muhimu"

**atainuliwa**
"Itakuwa inaonyesha kuwa muhimu" au "atapewa nafasi muhimu." AT 'Mungu atawainua."

## Luke 14:12

**kama wao wanaweza**
"Kwa sababu wao wanaweza"

**na wewe atalipwa**
AT "na kwa njia hii kukulipa"

## Luke 14:13

**Unganisha maelezo**
Yesu anaendelea kuzungumza na Mfarisayo aliyemwalika nyumbani kwake.

**nawe utakuwa heri**
AT"'Mungu atakubariki"

**hawawezi kukulipa**
AT "hawawezi kuwakaribisha karamu katika kurudi"

**maana utalipwa katika ufufuo wa wenye haki**
AT "Mungu atakulipa wakati yeye huleta watu wema nyuma ya maisha"

## Luke 14:15

**Habari za jumla**
Mmoja wa watu katika meza anaongea na Yesu na Yesu anajibu kwa kuwaeleza mfano

**Heri yeye**
mtu alikuwa si akizungumza juu ya mtu fulani. AT "Amebarikiwa mtu yeyote ambaye" au" Jinsi nzuri ni kwa kila mtu. "

**yeyeto atakae kula mkate**
neno "mkate" hutumika kwa kutaja mlo mzima" AT "ambao kula katika mlo."

**Lakini Yesu akamuambia**
Yesu akaanza kuelezea mfano

**Wakati chakula cha jioni kikiwa kimeandaliwa**
AT "Wakati huo kwa chakula cha jioni" au "Wakati chakula cha jioni kikiwa tayari kuanza"

**wale walioalikwa**
AT "wale waliokuwa wamealikwa"

## Luke 14:18

**kuunganisha maelezo**
Yesu anaendelea kusema mfano wake.

**Habari za jumla**
Watu wote ambao walialikwa na mtumishi wakampa udhuru kuhusu ni kwanini hawakuweza kuja kwenye karamu

**kufanya udhuru**
"Kusema kwa nini hawakuweza kuja chakula cha jioni"

**Tafadhali udhuru kwangu**
"Tafadhali nisamehe' au 'Tafadhali kubali msamaha wangu"

**jozi tano za ng'ombe**
AT "10 ng'ombe kufanya kazi katika mashamba yangu"

**Kuoa mke**
tumizi kujieleza ambako ni asili katika lugha yako. Baadhi ya lugha wanaweza kusema "wamezipata ndoa'"au "kuchukuliwa mke."

## Luke 14:21

**alikasirika**
"Akawa na hasira na watu waliokuwa wamealikwa"

**mtumishi akasema**
Inaweza kuwa muhimu na hali wazi kulisema taarifa ambazo mtumishi alifanya nini bwana amemwagiza. AT "Baada mtumishi akatoka na alifanya hivyo, yeye akarudi na kusema."

**nini uliamuli kimekuwa**
AT "Nimefanya nini aliamuru"

 

### Luke 14:23

**Kuunganisha maelezo**
Yesu alimaliza mfano wake.

**barabarani na mipakani**
Hii ina maana ya barabara na njia nje ya mji. AT "barabara kuu na njia nje ya mji."

**kuwatawalia**
Aliwadai

**ile nyumba yangu inaweza kujaa**
"Ili watu wanaweza kuijaza nyumba yangu"

**kwa nilicho waambia**
Neno "wewe" linamhusu mtumishi.

**wale watu**
neno hapa kwa "watu" linamaanisha "wanaume watu wazima" na si tu watu kwa ujumla

**ambao walikuwa wa kwanza kualikwa**
"Ambaye mimi nilimulika wakwanza"

**utaonja chakula changu cha jioni**
"Kufurahia chakula cha jioni Nimetengeneza"

### Luke 14:25

**Habari za ujumla**
Yesu anaanza kufundisha umati wa watu ambao walikuwa safarini pamoja naye.

**Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake mwenyewe ... hawezi kuwa mwanafunzi wangu**
Hapa, "chuki' ni exaggeration kuonyesha jinsi muhimu ni kumpenda Yesu zaidi kuliko mtu mwingine. AT "Kama mtu akija kwangu na hanipenda mimi zaidi kuliko yeye anavyompenda baba yake ... hawezi kuwa mwanafunzi wangu" au "Tu kama mtu ananipenda mimi zaidi kuliko yeye anayempenda baba yake mwenyewe ... hawezi kuwa mwanafunzi wangu"

**ndiyo, na nafsi yake mwenyewe**
"Na hata nafsi yake mwenyewe"

**Mtu asipochukua msalaba wake na kunifuata hawezi kuwa mwanafunzi wangu**
AT "Kama mtu anataka kuwa mwanafunzi wangu, ni lazima kubeba msalaba wake na kunifuata"

**kubeba msalaba wake mwenyewe**
Warumi mara nyingi walimfanya mtu kubeba msalaba wake kabla walipomsulubisha. Yesu hamaanishi kila Mkristo ni lazima asulubiwe. Yeye anamaana wao lazima kuwa tayari kuteseka kwa njia yoyote kuwa wanafunzi wake.

### Luke 14:28

**Maana ni nani katika ninyi, ambaye anatamani kujenga mnara, hatakaa chini kwanza akadirie gharama kwa mahesabu kama ana kile anachohitaji ili kukamilisha hilo?**
Yesu anatumia swali kupata watu kufikiri juu ya nini wangeweza kufanya katika hali fulani. AT "Kama mtu alitaka kujenga mnara, bila ya shaka kwanza kukaa chini na kuamua kama alikuwa na fedha za kutosha kukamilisha hilo."

**Mnara**
Hii inaweza kuwa mnara katika shamba lake. AT "jengo refu" au "sehemu ya juu ya jukwaa."

**baada ya kuweka msingi**
"Wakati yeye imejenga msingi." AT "wakati yeye anaanza kujenga"

### Luke 14:31

**Au**
Yesu alitumia neno hili kuanzisha hali nyingine ambapo watu kuhesabu gharama kabla ya kufanya uamuzi.

**nini mfalme ... si kukaa chini kwanza na kuchukua ushauri ... wanaume?**
Yesu anatumia swali jingine kufundisha umati wa watu. AT "unajua kwamba mfalme ... bila kukaa chini kwanza na kuchukua shauri ... wanaume."

**kuchukua ushauri**
Maana inawezekana ni 1) "kufikiri kwa makini kuhusu" au 2) "kumsikiliza washauri wake."

**Kumi elfu ... Ishirini elfu**
"10,000...20,000"

**Na kama si**
"Na kama yeye anatambua kwamba yeye hakuwa na uwezo wa kumshinda mfalme wengine"

**yeyote kati yenu ambaye hataacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu**
wale tu kati yenu ambao wataacha vyote walivyo navyo wanaweza kuwa wanafunzi wangu

**Kuacha vyote alivyo navyo**
Kuacha nyuma vyote alivyo navyo

### Luke 14:34

**Kuunganisha maelezo**
Yesu anamalizia kufundisha umati wa watu.

**Chumvi ni nzuri**
"Chumvi ni muhimu." Yesu anafundisha somo juu ya wale ambao wanataka kuwa wanafunzi wake.

**vipi inaweza kufanyika kuwa chumvi tena?**
Yesu anatumia swali kufundisha umati wa watu. AT "hawezi kuwa chumvi tena" au " hakuna anaeweza kuifanya kuwa chumvi tena"

**mbolea**
Watu kutumia mbolea ku rutubisha bustani na mashamba. Chumvi bila ladha ni haina maana ni haina hata thamani ya kuchanganywa na mbolea. AT "lundo la mbolea' au 'mbolea."

**Ni kutupwa mbali**
AT "Mtu kuitupilia mbali"

**Yeye aliye na masikio ya kusikia, na asikie**
AT "Kama una masikio ya kusikia, kusikiliza vizuri" au "Kama unasikia ninachosema, kuwa makini"

**Yeye aliye na masikio ya kusikia**
"Yeyote anaweza kusikia" au "Mtu anikisikia mimi"

**basi naye asikie**
"basi naye asikilize vizuri" au "basi naye awe makini kwa kile nisemacho"

---

## Chapter 15

1 Basi watoza ushuru wote na wengine wenye dhambi walikuja kwa Yesu na kumsikiliza. 2
Mafarisayowaote na waandishi wakanung'unika wakisema, "Mtu huyu huwakaribisha wenye dhambi na
hata hula nao." 3 Yesu akasema mfano huu kwao, akisema 4 "Nani kwenu, kama ana kondoo mia moja na
akipotelewa na mmoja wao, hatawaacha wale tisini na tisa nyikani, na aende akamtafute yule aliyepotea
hadi amwone? 5 Naye akisha kumpata humweka mabegani pake na kufurahia. 6 Afikapo kwenye nyumba,
huwaita rafiki zake na jirani zake akawaambia furahini pamoja nami, kwa kuwa nimempata kondoo wangu
aliyepotea.' 7 nawaambia vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja
atubuye, zaidi ya wenye haki tisini na tisa ambao hawana haja ya kutubu 8 Au kuna mwanamke gani
mwenye sarafu kumi za fedha, akipotewa na sarafua moja, hata washa taa na kufagia nyumba na kutafuta
kwa bidii hadi atakapoipata? 9 Na akiisha kuiona huwaita rafiki zake na jirani zake akawaambia furahini
pamoja nami, kwa kuwa nimeipata tena sarafu yangu niliyokua nimeipoteza. 10 Hata hivyo nawaambia
kuna furaha mbele ya malaika wa Mungu kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye." 11 Na Yesu
akasema, "Mtu mmoja alikua na wana wawili 12 yule mdogo akamwambia babaye, Baba nipe sehemu ya
mali inayonistali kuirithi. Hivyo akagawanya mali zake kati yao. 13 Siku si nyingi yule mdogo akakusanya
vyote anavyomiliki akaenda nchi ya mbali, na huko akatapanya hela zake, kwa kununua vitu asivyo
vihitaji, na kutapanya fedha zake kwa anasa. 14 Nae alipokua amekwisha tumia vyote njaa kuu iliingia
nchi ile naye akaanza kuwa katika uhitaji. 15 Akaenda na kujiajiri mwenyewe kwa mmoja wa raia wa nchi
ile, naye alimpeleka shambani kwake kulisha nguruwe. 16 Na akawa akitamani kujishibisha kwa maganda
waliyokula nguruwe kwa sababu hakuna mtu aliempa kitu chochote apate kula. 17 Ila yule mwana mdogo
alipozingatia moyoni mwake, alisema 'ni watumishi wangapi wa baba yangu wanachakula kingi cha
kutosha na mimi niko hapa, ninakufa na njaa! 18 Nitaondoka na kwenda kwa baba yangu, na kumwambia,
"Baba nimekosa juu ya mbingu na mbele ya macho yako. 19 Sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye
kama mmoja wa watumishi wako." 20 Ndipo akaondoka akaenda kwa baba yake. Alipokua angali mbali
baba yake alimuona akamwonea huruma akaenda mbio na kumkumbatia na kumbusu. 21 Yule mwana
akamwambia, 'baba nimekosa juu ya mbingu na mbele ya macho yako sistahili kuitwa mwana wako.' 22
Yule baba aliwaambia watumishi wake, 'lileteni upesi vazi lililo bora, mkamvike mtieni na pete kidoleni na
viatu miguuni. 23 Kisha mleteni ndama yule alienona mkamchinje tule na kufurai. 24 Kwa kuwa
mwanangu alikua amekufa naye yu hai. Alikua amepotea nae ameonekana wakaanza kushangilia. 25 Basi
yule mwanae mkubwa alikuwako shamba. Alipokuwa akija na kuikaribia nyumba alisikia sauti ya nyimbo
na michezo. 26 Akaita mtumishi mmoja akamuuliza mambo haya maana yake nini? 27 Mtumishi
akamwambia mdogo wako amekuja na baba yako amemchinjia ndama aliyenona kwa sababu amerudi
salama.' 28 Mwana mkubwa akakasirika akakataa kuingia ndani na babaye alitoka nje kumsihi. 29 Ila
akamjibu babayake akisema, 'Tazama mimi nimekutumikia miaka mingi, wala sijakosa amri yako, lakini
hujanipa mwana mbuzi, ili niweze kusherehekea na rafiki zangu. 30 Lakini alipokuja huyu mwana wako
aliyetapanya mali yako yote pamoja na makahaba umemchinjia ndama alienona. 31 Baba akamwambia,
'Mwanangu, wewe u pamoja nami siku zote na vyote nilivyo navyo ni vyako. 32 Ila ilikua vyema kwetu
kufanya sherehe na kufurahi, huyu ndugu yako alikua amekufa, na sasa yu hai; alikua amepotea naye
ameonekana."

---

## Luka 15 Maelezo ya Jumla

#### Muundo na upangiliaji

#### Mfano wa mwana mpotevu

Luka 15:13-32 ni mfano mmoja, unaojulikana kama mfano wa mwana mpotevu. Kuna takwimu tatu katika hadithi. Kwa ujumla inakubaliwa kuwa baba anaonyesha mfano wa Mungu and )

### Dhana maalum katika sura hii

### "Wenye dhambi"

Mafarisayo hutaja kundi la watu kuwa "wenye dhambi." Viongozi wa Kiyahudi walidhani watu hawa walikuwa wenye dhambi, lakini kwa kweli viongozi wenyewe walikuwa pia wenye dhambi. Hali hii inaweza kuchukuliwa kama kinaya.

---

## Luke 15:1

**Habari kwa ujumla**
Hii ni sehemu ya pili ya hadithi. Hatujui sehemu ambapo haya yalijir; ni tu siku moja wakati Yesu alikuwa akifundisha.

**Sasa**
hii ni mwanzo wa sehemu mpya ya hadithi.

**Mtu huyu anakaribisha wenye dhambi**
"Mtu huyu amaleta wenye dhambi mbele yake" au "Mtu huyu ameshiriki na wenye dhambi"

**Mtu huyu**
Walikuwa wakizungumza kuhusu Yesu.

**hata anakula nao**
neno "hata" inaonyesha kwamba wao walidhani ilikuwa mbaya kwamba Yesu kuruhusu wenye dhambi kuja kwake, lakini ilikuwa mbaya zaidi kwamba angeweza kula pamoja nao.

**Watoza ushuru wote.**
Hii ni kusisitiza kuwa kulikuwa na watu wengi sana. "watoza ushuru wengi"

## Luke 15:3

**Taarifa kwa ujumla**
Yesu anaanza kwa kuwaambia mifano kadhaa. mfano wa kwanza ni kuhusu mtu na kondoo wake.

**kwao**
Hapa "wao" inamaanisha viongozi wa dini.

**Nani kati yenu ... mpaka ampate?**
Yesu anatumia swali kuwakumbusha watu kwamba kama yeyote kati yao akipoteza mmoja wa kondoo wake, wataenda kumtafuta. Baadhi ya lugha na njia za kuonyesha kwamba hii ni hali dhahania na si hadithi kuhusu mtu fulani ambaye amepoteza kondoo.

**Nani kati yenu, kama ana kondoo mia**
Kwakua mfano umeanza na "Nani kati yenu," baadhi ya lugha zingeendeleza mfano katika mtu wa pili. "Tuseme mmoja wenu, kama ana kondoo mia"

**mia ... tisini na tisa**
tisa "100 ... 99"

**Nani kati yenu ... hata waacha... mpaka ampate?**
Yesu anatumia swali kuwakumbusha watu kwamba kama mmoja kati yao wamepoteza mmoja wa kondoo zao, wao bila ya shaka huenda kumtafuta. "Kila mtu ... bila ya shaka huondoka ... mpaka ampate." Baadhi ya lugha na njia za kuonyesha kwamba hii ni hali dhahania na si hadithi kuhusu mtu fulani ambaye amepoteza kondoo.

**mia ... tisini na tisa**
tisa "100 ... 99"

**kumlaza mabegani mwake**
Hii ilikuwa njia ambayo wachungaji walibeba kondoo. Hii inaweza kusemwa "kumlaza mabegani mwake na kumbeba nyumbani"

## Luke 15:6

**Wakati anakuja nyumbani**
"Wakati mmiliki wa kondoo anakuja nyumbani" au "Wakati umefika nyumbani". Rejea mmiliki wa kondoo kama alivyofanya katika mstari uliopita.

**hata hivyo**
"katika njia sawa" au "kama mchungaji na marafiki na majirani wangefurahia"

**kutakuwa na furaha mbinguni**
"kila mtu mbinguni atafurahi"

**wenye haki tisini na tisa wasio hitaji kutubu**
wenye haki tisini na tisa wasio hitaji kutubu. Yesu hakuwa akisema kwamba kweli kuna watu wenye haki. Anamaanisha watu ambao wanadhani ni wenye haki, ila sio. "Watu 99 ambao wanadhani kwamba wao ni wenye haki na hawana haja ya kutubu."

**watu tisini na tisa wenye haki**
watu tisini na tisa wenye haki "watu 99 wema"

**zaidi ya watu wenye haki tisini na tisa wasio hitaji kutubu.**
watu wenye haki tisini na tisa wasio hitaji kutubu Hii haina maana kwamba Mungu hana radhi kwa wale wanaomtii anachukua furaha kubwa ndani yao. Lakini furaha mbinguni kwa wakati mtu anaokolewa kutoka dhambini ni hata furaha zaidi!

**hawana haja ya kutubu**
Hii haina maana kwamba waumini hawana haja ya kutubu wote wanahitaji kufanya.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

### Luke 15:8

**Kuunganisha kauli:**
Yesu anaanza kuwaambia mfano mwingine. Ni kuhusu mwanamke na shilingi kumi.

**Au mwanamke gani ... hatawasha taa ... na kutafuta kwa bidii hata aipate?**
Yesu anatumia swali kuwakumbusha watu kwamba yeyote kati yao akipoteza safara ya fedha, bila shaka ataanza kuitafuta kwa bidii.

**Mwanamke gan.**
Hii ni hali dhahania na si hadithi kuhusu mwanamke halisi. Baadhi ya lugha ina njia ya kuonesha hili.

**Hata hivyo**
"Kwa njia hiyo hiyo" au "Kama vile watu hushangilia pamoja na mwanamke"

**mwenye dhambi mmoja anayetubu**
"wakati mwenye dhambi mmoja akitubu"

**Au mwanamke gani ... hatawasha taa ... na kutafuta kwa bidii hata aipate?**
Yesu anatumia swali kuwakumbusha watu kwamba yeyote kati yao akipoteza safara ya fedha, bila shaka ataanza kuitafuta kwa bidii. "Mwanamke yeyote ... bila ya shaka atawasha taa ... na kutafuta kwa bidii hata aipate"

**Kama alikua apoteze**
Hii ni hali dhahania na si hadithi kuhusu mwanamke halisi. Baadhi ya lugha na njia ya kuonesha hili.

### Luke 15:11

**Kuunganisha kauli:**
Yesu anaanza kuwaambia mfano mwingine. Ni kuhusu kijana ambaye anamuomba baba yake sehemu ya urithi wake.

**Mtu mmoja**
hii ni utangulizi wa mtu mwingine katika mfano. Baadhi ya lugha zinaweza kusema "Kulikuwa na mtu ambaye"

**nipe saiv**
mwana alitaka baba yake ampe haraka. Lugha ambazo zina njia ya amri hiyo ina maana kwamba wanataka iyo ifanyike mara moja unapaswa kutumia njia hiyo.

**mali ninayo takiwa kurithi**
"sehemu ya mali yako kwamba ulipanga kunipa mimi wakati wewe ukifa"

**nipe**
mwana alitaka baba yake ampe haraka. Lugha ambazo zina njia ya amri hiyo ina maana kwamba wanataka iyo ifanyike mara moja unapaswa kutumia njia hiyo.

**sehemu ya mali ambayo inaniangukia mimi**
"sehemu ya mali yako kwamba ulipanga kunipa mimi wakati wewe ukifa"

**kati yao**
"kati ya wanawe wawili"

### Luke 15:13

**wakakusanya wote aliokua anawadai**
"akakusanya vitu vyake" au "kuweka mambo yake katika mfuko wake"

**kununua vitu asivyo vihitaji, na kupoteza pesa yake juu ya maisha ya anasa**
"kwa kutumia fedha yake yote juu ya vitu asivyo vihitaji"

**njaa kali ikaenea nchini kote**
"ukame ukatokea huko na nchi nzima haikuwa na chakula cha kutosha"

**Sasa**
Neno hili limetumika hapa kuadhimisha mapumziko katika hadithi kuu. Hapa Yesu anaeleza jinsi yule mdogo akaenda kutoka kuwa na mengi hadi kuwa katika uhitaji.

**kuwa katika mahitaji**
"kukosa kile anachokihitaji" au "kutokua na yakutosha"

**maisha ya anasa**
"kuishi bila kufikiria"

### Luke 15:15

**Alikwenda**
inahusu yule mdogo.

**Kujitoa kiajira**
"alichukua kazi kwa" au "alianza kufanya kazi kwa ajili ya"

**moja wa mwananchi wa nchi ile**
"mtu wa nchi hiyo"

**kulisha nguruwe**
"kuwapa chakula nguruwe wa mtu yule"

**angefuraia kula**
"alitaka sana kwamba angeweza kula." Ina eleweka kwamba hii ni kwa sababu alikuwa na njaa sana. Hii inaweza kuwa alisema. "alikuwa na njaa ambayo angefurahia kula"

**maganda ya maharage**
Haya ni maganda ya maharagwe kwamba kukua juu ya mti ....... "maganda ......" au "maganda" au "maganda ya maharage "

## Luke 15:17

**alipopata ufahamu**
msemo huu una maana "akili yake kurejea." "kueleweka vizuri hali yake"

**Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula cha kutosha**
Hii ni sehemu ya mshangao, na si swali. "watumwa wa baba yangu wote wanachakula cha kutosha kula"

**kufa kutokana na njaa**
Hii pengine si kukisia. Kijana anaweza kweli kuwa amekuwa na njaa.

**Nimefanya dhambi dhidi ya mbingun**
Wayahudi wakati mwingine walikua wanaepuka kusema neno "Mungu" na walitumia neno "mbinguni" badala yake. "Mimi nimemkosea Mungu,"

**Sistahili hata kuitwa mwanao**
"Mimi sistahili hata kuitwa mwanao." Hii inaweza kusemwa "Mimi sistahili wewe uniite mwanao"

**sistahili tena**
"tena sistahili" Ina maana kwamba katika siku za nyuma alikuwa anastahili, lakini sasa hastahili.

**nifanye kama mmoja wa watumishi wako**
"niajiri kama mfanyakazi wako" au "niajiri nami nitakua mmoja wa wafanya kazi wako" Hili ni ombi, si amri. Na inaweza kuwa na manufaa kwa kuongeza "tafadhali" kama UDB ilivyo fanya.

## Luke 15:20

**Hivyo mwana mdogo akaondoka na akaja kwa baba yake**
"Hivyo aliondoka nchini na kuanza kurudi kwa baba yake." neno "hivyo" linaweka alama tukio hilo kuwa lilichotokea kwa sababu ya kitu kingine kwamba kilichotokea kwanza. Katika kesi hiyo, kijana alikuwa katika haja na aliamua kwenda nyumbani.

**aliwaonea huruma**
"alikuwa na huruma juu yake" au "alimpenda saana kutoka moyoni mwake"

**kumkumbatia na kumbusu**
baba alifanya hivyo ili kumuonyesha mwanawe kuwa yeye alimpenda na alikuwa na furaha kwamba mwana alikuwa anakuja nyumbani. Kama watu wanadhani kwamba ni vigumu au ni vibaya kwa mtu kumkumbatia na kumbusu mtoto wake, unaweza kubadilisha na kuweka njia ambayo wanaume katika utamaduni wako huonyesha upendo kwa watoto wao.

**mbele yako**
Hii ina maana "katika uwepo wako" au "dhidi yeko"

**Alipokuwa bado mbali**
"Alipokuwa bado mbali sana na nyumbani kwake" au "Alipokuwa bado mbali sana na nyumbani kwa baba yake"

**Sistahili kuitwa mwanao**
Tazama 15:17

## Luke 15:22

**joho bora**
"vazi bora katika nyumba." "koti bora" au "vazi bora"

**weka pete kidoleni**
pete ilikuwa ni ishara ya mamlaka ambayo wanaume walivaa kwenye moja ya vidole vyao.

**viatu**
Watu matajiri wa wakati huo walivaa viatu. Hata hivyo, katika tamaduni nyingi za kisasa itakuwa "viatu."

**ndama aliyenona**
ndama ni ng'ombe mdogo. Watu huwapa ndama moja ya chakula maalum ili aweze kukua vizuri, na kisha wakati wao humla huyo ndama siku wakitaka kuwa na sikukuu maalum "ndama bora" au "wanyama wadogo tumekuwa tukiwafanya wanenepe"

**na kumchinja**
maelezo yanaonyesha kuwa walikuwa wanapaswa kupika nyama zinaweza kufanywa safi. "na kumchinja na kuipika."

**mwanangu alikuwa amekufa, na sasa yeye yu hai**
Mfano huu unamuongelea mwana kuenda kana kwamba alikua amekufa.: "ni kama mwanangu alikuwa amekufa na akawa hai tena" au "nilihisi kama mwanangu alikuwa amekufa, lakini yeye sasa yu hai"

**Alikuwa amepotea, na sasa kapatikana**
Mfano huu unasema mwana kuwa wamekwenda kana kwamba alikuwa amepotea. "Ni kana kwamba mwanangu alikuwa amepotea na sasa nimemuona au "Mwanangu alikuwa amepotea na amerejea nyumbani"

**kumchinja**
maelezo yanaonyesha kuwa walikuwa wapike nyama na kuwekwa wazi.: "kumchinja na kumpika"

## Luke 15:25

**Sasa**
Neno hili limetumika hapa kuadhimisha mapumziko katika habari kuu. Hapa Yesu anaanza kwa kuwaambia sehemu mpya ya hadithi kuhusu mwana mkubwa.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**mtumishi**
neno lililotafsiriwa hapa kama "mtumishi" ni kawaida kutafsiriwa kama "kijana." inaweza kuonyesha kwamba mtumishi alikua mdogo sana.

**mambo haya yanaweka yakawa nini**
"nini kinatokea"

**nje katika shamba**
Inasemekana akilua shabani kwasababu alikua anafanya kazi uko.

**mwana kondoo alie nona**
Tazama 15:22

### Luke 15:28

**kamwe usivunje sheria yako**
"kamwe usiasi sheria yako yoyote" au "daima tii kila kitu ulichoniambia nifanya"

**na sikukuu**
"kusherehekea"

**mwanao**
"yule mwana wako" mwana mkubwa alikua anamaanisha ndugu yake kwa njia hii ili kuonyesha jinsi gani anahasira.

**aliyekula mali yako pamoja na makahaba**
"kupoteza utajiri wako wote juu ya makahaba" au "kutupa mbali fedha yako yote kwa kuwalipa makahaba." Maana inawezekana ni 1) alifikiria hivi ndivyo ndugu yake alitumia fedha au 2) anatumia mafumbo kwa makusudi kukuza dhambi za ndugu yake.

**hii miaka mingi**
"kwa miaka mingi"

**Mimi nimetumika kwa ajili yenu**
"Nimefanya kazi kwanguvu kwaajili yako" au "nimefanya kazi kwa bidii kama mtumwa kwa ajili yako"

**mwana mbuzi**
mwana mbuzi ilikuwa mdogo na sio ghali kuliko ndama aliye nona. "hata mwana mbuzi"

**mwana kondoo alie nona**
Tazama 15:22

### Luke 15:31

**baba akamwambia**
neno "yake" inahusu mwana mkubwa.

**huyu ndugu yako**
baba alikuwa anamkumbusha mwana mkubwa kwamba mtu ambaye alikuja nyumbani alikuwa ndugu yake.

**Alikua amekufa, na sasa yu hai**
Tazama 15:22

**Alikua amepotea na sasa amepatikana**
Tazama 15:24


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 16

1 Yesu aliwaambia tena wanafunzi wake, "Palikuwa na mtu mmoja tajiri aliyekuwa na meneja, na
alitaarifiwa ya kwamba meneja huyu anatapanya mali zake. 2 Hivyo tajiri akamwita, akamwambia, "Ni
nini hii ninayo isikia juu yako? Toa hesabu ya umeneja wako, kwa kuwa huwezi kuwa meneja tena.' 3 Yule
meneja akasema moyoni mwake, Nifanye nini, maana bwana wangu ananiondolea kazi yangu ya umeneja?
Sina nguvu za kulima, na kuomba naona haya. 4 Najua nitakalotenda ili nitakapotolewa katika kazi yangu
ya uwakili watu wanikaribishe nyumbani mwao. 5 Hivyo wakili akawaita wadeni wa bwana wake kila
mmoja akamwambia wa kwanza, 'unadaiwa kiasi gani na bwana wangu?' 6 Akasema vipimo mia moja vya
mafuta akamwambia 'chukua hati yako keti upesi andika hamsini.' 7 kisha akamwambia mwingine na
wewe unadaiwa kiasi gani?' akasema 'vipimo mia moja vya unga vya ngano.' Akamwambia 'twaa hati yako
andika themanini.' 8 Yule bwana akamsifu meneja dhalimu kwa vile alivyotenda kwa wereu. Kwakua
watoto wa ulimwengu huu ni werevu nyingi na hushughulika kwa ujanja na watu wa upande wao kuliko
walivyo watoto wa nuru. 9 Nami nawaambia jifanyieni marafiki kwa mali ya udhalimu ili itakapokosekana
wawakaribishe katika makao ya milele. 10 Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana huwa mwaminifu katika
lililo kubwa pia. na aliye dhalimu katika lililo dogo huwa dhalimu katika lililo kubwa pia. 11 Kama ninyi
hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu ni nani atakayewaamini katika mali ya kweli? 12 Na kama
hamkuwa waaminifu katika kutumia mali ya mtu mwingine ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe? 13
Hakuna mtumishi awezaye kutumikia mabwana wawili, kwamaana atamchukia mmoja na kumpenda
mwingine, ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu. Hamuwezi kumtumikia Mungu na mali." 14
Basi Mafarisayo, ambao walikuwa wanapenda fedha waliyasikia haya yote na wakamdhihaki. 15 Na
akawaambia, "Ninyi ndiyo mnaojidai haki mbele ya wanadamu, lakini Mungu anaijua mioyo yenu. Kwa
kuwa lililotukuka kwa wanadamu huwa chukizo mbele za Mungu. 16 Sheria na manabii vilikuwapo mpaka
Yohana alivyokuja. Tangu wakati huo, habari njema ya ufalme wa Mungu hutangazwa, na kila mtu
hujaribu kujiingiza kwa nguvu. 17 Lakini ni rahisi kwa mbingu na nchi vitoweke kuliko hata herufi moja ya
sheria ikosekane. 18 Kila amwachaye mkewe na kumwoa mke mwingine azini, naye amwooaye yeye
aliyeachwa na mumewe azini. 19 Palikua na mtu mmoja tajiri aliyevaa nguo za rangi ya zambarau na
kitani safi na alikua akifurahia kila siku utajiri wake mkubwa. 20 Na maskini mmoja jina lake Lazaro
aliwekwa getini pake, na ana vidonda. 21 Naye alikua akitamani kushibishwa kwa makombo yaliyoanguka
katika meza ya yule tajiri hata mbwa wakaja wakamlamba vidonda vyake. 22 Ikawa yule maskini alikufa
na akachukuliwa na Malaika mpaka kifuani kwa Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa akazikwa. 23 Na kule
kuzimu alipokua katika mateso aliyainua macho yake akamuona Ibrahimu kwa mbali na Lazaro kifuani
mwake. 24 Akalia akasema, 'Baba Ibrahimu, nihurumue umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake
majini, auburudishe ulimi wangu; kwa sababu ninateswa katika moto huu. 25 Lakini Ibrahimu akasema,
'Mwanangu kumbuka ya kwamba katika maisha yako uliyapokea mambo yako mema, na Lazaro vivyo
alipata mabaya. Ila sasa yupo hapa anafarijiwa na wewe unaumizwa. 26 Na zaidi ya hayo, kumewekwa
shimo kubwa na refu kati yetu, ili wale wanaotaka kutoka huku kwenda kwenu wasiweze wala watu wa
kwenu wasivuke kuja kwetu.' 27 Yule tajiri akasema, 'Nakuomba Baba Ibrahimu, kwamba umtume
nyumbani kwa baba yangu 28 kwa kuwa ninao ndugu watano ili awaonye, kwa hofu kwamba wao pia
watkuja mahali hapa pa mateso. ' 29 Lakini Ibrahimu akasema, 'Wanao Musa na manabii. Waache
wawasikilize wao. 30 Yule tajiri akasema, 'hapana, Baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye
kwa wafu watatubu.' 31 Lakini Ibrahimu akamwambia, 'wasipowasikia Musa na manabii
hawatashawishiwa hata mtu akifufuka katika wafu.

---

## Luka 16 Maelezo ya Jumla

#### Dhana maalum katika sura hii

#### Takwimu muhimu za matamshi katika sura hii

#### Kusema

Imeandikwa kama Abrahimu alisema "hawatajali hata kama mtu atafufuka kutoka wafu." Hii ni mwelekeo wa ukweli kwamba Yesu atafufuka kutoka kwa wafu na hawatajali ukweli huu.



generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

### "Sheria na manabii walikuwa wa kutegemewa hadi Yohana alipokuja"

Maneno haya hayamaanishi kanuni za sheria ya Musa zilimalizika wakati wa Yohana Mbatizaji. Ni wazi kutoka kwenye Injili kuwa Yesu aliishi na kuhudumia kulingana na sheria. Kilichobadilika ni ujumbe uliotangazwa. Ndio maana UDB inasema, "Sheria ambazo Mungu alimpa Musa na kile ambacho manabii waliandika zilihuburiwa mpaka Yohana Mbatizaji alifika."

---

## Luke 16:1

**Kuunganisha kauli:**
Yesu anaanza kuwaambia mfano mwingine. Ni kuhusu bwana na wakili wa wadaiwa wake. Hii bado ni sehemu moja ya hadithi na siku hiyo hiyo ambayo ilianza katika

**Yesu aliwaambia wanafunzi**
sehemu ya mwisho ilikuwa ilivyoagizwa kwa Mafarisayo na waandishi, ingawa wanafunzi wa Yesu walikua sehemu ya umati wakisikiliza.

**Kulikuwa na mtu mmoja tajiri**
huu ni utangulizi wa mhusika mpya katika mfano.

**iliripotiwa kwake**
Hii inaweza alisema kama "Watu waliripoti kwa tajiri"

**kufuja mali yake**
"kutumia mali ya tajiri kipumbavu"

**Ni nini hii ninayosikia juu yako?**
Tajiri anatumia swali kumkemea wakili. "Nimesikia nini unafanya"

**Kutoa hesabu ya usimamizi wako**
"panga rekodo zako ili kumkabidhi mtu mwingine" au "Andaa rekodi uliyo andika kuhusu fedha yangu"

## Luke 16:3

**Nifanye nini ... kazi?**
wakili anauliza kwa hiari yake mwenyewe, kama njia ya kupitia upya chaguzi zake.

**bwana wangu**
Hii ina maana ya mtu tajiri. Wakili hakuwa mtumwa. "mwajiri wangu"

**Sina nguvu kuchimba**
"Mimi sina nguvu za kulima ardhi" au "Sina uwezo wa kuchimba"

**wakati nikiondolewa kutoka kwenye kazi yangu ya usimamizi**
hii inaweza kusemwa "wakati nikipoteza kazi yangu ya usimamizi" au "wakati bwana wangu inachukua mbali usimamizi wangu kazi"

**Nifanye nini ... kazi?**
meneja anauliza kwa hiari yake mwenyewe, kama njia ya kupitia upya chaguzi zake. "Inabidi nifikirie kuhusu nini nitafanya...kazi"

**Watu wata nikaribisha katika nyumba zao**
Hii ina maana kwamba watu hao watatoa kazi, au mambo mengine ambayo anayahitaji ili aishi.

## Luke 16:5

**wadeni wa bwana wake**
"watu ambao walikuwa katika madeni kwa bwana wake" au "watu ambao wanadaiwa kitu na bwana wake." Katika hadithi hii wadaiwa wanadaiwa mafuta na ngano.

**Alisema ... Naye akamwambia**
"mdaiwa alisema ... Na wakili akamwambia mdaiwa"

**Mapipa mia ya mafuta**
Haya yalikuwa yapata lita 3,000 ya mafuta.

**mia ... hamsini ... themanini**
"100 ... 50 ... 80"

**vipimo mia vya ngano**
Hii ilikuwa yapata vikapu elfu vya ngano.

**Wakili akamwambia mtu mwingine ... Alisema ... Naye akamwambia**
"wakili akamwambia mdaiwa mwingine ... mdaiwa alisema ... wakili akamwambia mdaiwa"

**Alisema ... Naye akamwambia**
"mdaiwa alisema ... Na meneja akamwambia mdaiwa"

**mia ... hamsini ... themanini**
"100 ... 50 ... 80"

**Wakili akamwambia mtu mwingine ... Alisema ... Naye akamwambia**
"wakili akamwambia mdaiwa mwingine ... mdaiwa alisema ... wakili akamwambia mdaiwa"

## Luke 16:8

**Kuunganisha kauli:**
Yesu alimaliza mfano huo kuhusu bwana na wakili wa wadaiwa wake. Katika mstari wa 9, Yesu anaendelea kuwafundisha wanafunzi wake.

**bwana kisha alimpongeza**
maandiko hayaonyeshi jinsi bwana alitambua juu ya matendo ya wakili wake.

**alipongeza**
"kusifiwa" au "akamsifu" au "kumpitisha "

**yeye alikuwa ametenda ......**
"alikuwa alitenda vyema" au "Yesu alikuwa amefanya jambo la busara"

**Wana wa ulimwengu huu**
Hii ina maana ya wale kama meneja wa udhalimu ambao hawajui au kutokujali juu Mungu. "Watu wa dunia hii" au "watu wa kidunia"

**Wana wa nuru**
Hii inamaanisha watu wenye haki wasio na chakuficha. "wana wa nuru" au "watu waishio kwenye mwanga"

**Nina kwambia wewe**
"Nina" inasemea Yesu. maneno "nawaambia" yanaweka alama ya mwisho ya hadithi na sasa Yesu anasimulia watu jinsi ya kutumia hadithi kwa maisha yao.

**makao ya milele**
Hii ina maana ya mbinguni ambako Mungu anaishi.

**kujifanyieni marafiki kutokana kwa njia ya fedha isiyo halali**
lengo hapa ni juu ya kutumia fedha kusaidia watu wengine, sio kwa njiacambayo utajiri unapatikana kwa uongo.

**fedha isiyo ya halali**
Inawezekana Maana ni 1) "fedha iliyopatikana kidhuluma" au 2) fedha iliyo patikana kwa mambo ya kidunia.

**wanaweza kuwakaribisha**
Hii inaweza kutaja 1) Mungu wa mbinguni, ambaye ameridhika kwamba umetumia hela kuwasaidia watu, au 2) marafiki ulio wasaidia na fedha yako.

### Luke 16:10

**nani atakayewakabidhi na mali za kweli?**
Yesu anatumia swali kufundisha watu. "hakuna mtu atakayewakabidhi nyinyi mali ya kweli" au "hakuna mtu nitakupa utajiri wa kweli wa kusimamia"

**ambao nitakupa fedha yako mwenyewe?**
Yesu anatumia swali hili kufundisha watu. "hakuna mtu atakupa utajiri kwa nafsi yako"

**Yeyote aliye mwaminifu**
"Watu ambao ni waaminifu." Hii itakuwa ni pamoja na wanawake.

**mwaminifu katika jambo dogo**
'waaminifu hata kwa mambo madogo. " hakikisha hii haina sauti kama hao sio waaminifu sana.

**mwaminifu katika mambo madogo sana**
"wasio waadilifu hata katika mambo madogo." Kuhakikisha hii haina sauti kama sio waovu mara nyingi.

**fedha isiyo ya halali**
Tazama 16:08

**mali wa kweli**
hii inahusu mali ambayo ni zaidi ya kweli, halisi, au kudumu kuliko fedha ya udhalimu.

### Luke 16:13

**Taarifa kuu:**
Hii ni mapumziko katika mafundisho ya Yesu, kama mstari wa 14 inatuambia taarifa za msingi kuhusu jinsi Mafarisayo wakamdharau Yesu. Katika mstari wa 15, Yesu anaendelea kufundisha na anaitikia kwa Mafarisayo.

**Hakuna mtumishi anaweza**
"mtumishi hawezi"

**atamchukia**
"mtumishi chuki"

**kujitoa**
"kujitolea." Hii ina maana kimsingi ni sawa na "upendo" katika kifungu uliopita.

**kumdharau huyu**
"kushikilia mmoja katika dharau" au "chukia mwingine"

**Huwezi kumtumikia**
Yesu alikuwa akizungumza na kundi la watu, hivyo lugha ambazo zina wingi wa "wewe" bila kutumia hiyo.

**kutumika**
"kuwa mtumwa"

**kutumikia mabwana wawili**
"kutumikia mabwana wawili tofauti kwa wakati mmoja"

**kwa maana ata ... au pengine ata**
Vifungu hivi viwili ni vinafanana tofauti kubwa ni kwamba bwana kwanza amechukiwa katika kifungu cha kwanza, lakini bwana wa pili amechukiwa katika kifungu cha pili.

**kumdharau**
Hii ina maana kimsingi ni sawa na "chuki" katika kifungu kilichopita.

## Luke 16:14

**Sasa**
neno hili lina weka alama ya kuhama kutoka katika taarifa ya awali.

**ambao walikuwa wanapenda sana fedha**
"aliyependa kuwa na fedha" au "ambaye alikua na tamaa ya fedha"

**wao wakamdharau**
"Mafarisayo wakamdharau Yesu"

**Naye akawaambia**
"Na Yesu aliwaambia Mafarisayo"

**Nyie mnajihalalisha wenyewe mbele ya watu**
"wewe unajaribu kujifanya kuonekana vizuri kwa watu"

**Mungu anaijua mioyo yenu**
Hapa "mioyo" inahusu tamaa za watu."Mungu anaelewa tamaa yako kweli" au "Mungu anajua nia yako"

**Iyo iliyotukuka miongoni mwa watu**
hii inaweza semwa kama "Yale mambo ambayo watu wanadhani ni muhimu sana"

**ni machukizo mbele za Mungu**
"Mungu anachukia" au "ni mambo ambayo Mungu anayachukia"

**Taarifa kuu:**
Hii ni mapumziko katika mafundisho ya Yesu, kama mstari wa 14 unatuambia taarifa za msingi kuhusu jinsi Mafarisayo wakamdharau Yesu. Katika mstari wa 15, Yesu anaendelea kufundisha na anawajibu Mafarisayo.

## Luke 16:16

**sheria na manabii**
Hii inahusu maneno yote ya Mungu kwamba yalikuwa yameandikwa hadi wakati huo.

**Yohana alikuja**
Hii ina maana ya Yohana Mbatizaji. "Yohana mbatizaji alikuja"

**injili ya ufalme wa Mungu hutangazwa**
Hii inaweza semwa kama: "Mimi nafundisha watu kuhusu habari njema ya ufalme wa Mungu"

**kila mmoja anajaribu kulazimisha njia yao ndani yake**
Hii ina maana ya watu ambao walikuwa wakisikiliza na kukubali mafundisho ya Yesu. "Watu wengi wanafanya kila liwezekanalo kuingia"

**ni rahisi zaidi mbingu na dunia kupita, kuliko**
"kama unavyo jua kuwa mbingu na ardhi hawezi kupita, unaweza kuwa na uhakika kwamba"

**kuliko hata herufi moja ya sheria ikosekane**
maneno "herufi moja ya sheria" maana yake ni sehemu ndogo ya barua. Ni inahusu kitu katika sheria ambayo inaweza kuonekana kuwa haina umuhimu saana. "kuliko kwa mtu kuondoa hata undani ndogo ya sheria."

**ni rahisi zaidi mbingu na dunia kupita kuliko hata herufi moja ya barua ya sheria kukosekana**
Hii inaweza kusemwa kama, "hata herufi ndogo ya barua ya sheria itadumu saana kuliko mbingu na nchi kuwepo"

**kuliko hata herufi moja ya barua**
"Herufi" ni sehemu ndogo ya barua. Ni inahusu kitu katika sheria ambacho kinaweza kuonekana kuwa hakina umuhimu saana. "kuliko kwa hata undani mdogo wa sheria"

**kuwa batili**
"mwisho" au "kusitisha kuwepo"

## Luke 16:18

**Kila mtu amwachaye mkewe**
"Anayemwacha mkewe" au "Mtu yeyote anayemtalaka mke wake"

**anazini**
"ni hatia ya kufanya uzinzi"

**naye amwoaye moja**
"mtu yeyote anayemwoa mwanamke"

## Luke 16:19

**Kuunganisha kauli:**
Wakati Yesu akiendelea kufundisha watu akaanza kuwaambia mfano. Ni kuhusu tajiri na Lazaro.

**Taarifa kuu:**
Hii nistari inatoa taarifa kuhusu hadithi. Yesu anaanza kueleza kuhusu tajiri na Lazaro.

**ambaye alikuwa amevaa nguo ya zambarau na kitani safi**
"ambao walivaa mavazi yaliyo tengenezwa na kitani safi" au "ambao walivaa nguo ghali sana." rangi ya zambarau na kitani safi zilikua nguo ghali sana.

**alikua akifurahia kila siku utajiri wake**
"kufurahia kula chakula cha gharama kila siku" au "alitumia fedha nyingi na kununua chochote akitakacho"

**maskini mmoja jina lake Lazaro, aliwekwa mlangoni pake**
Hii inaweza semwakama "Watu walikuwa wamemlaza maskini mmoja jina lake Lazaro kwenye lango lake"

**kwenye lango lake**
"katika lango la nyumba ya tajiri" au "katika mlango wa kuingia kwenye mali ya tajiri"

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**kufunikwa na vidonda**
"na vidonda yote juu ya mwili wake"

**yeye alitamani sana kulishwa na kile kilichoanguka kutoka meza ya tajiri**
Hii inaweza semwa kama: "alitamana tajiri ampe makombo ya chakula ambayo atayatuma"

**kando na hayo**
hii inaonyesha kwamba kile kifuatavyo ni kibaya zaidi kuliko yale ambayo tayari yameelezwa kuhusu Lazaro. "katika nyiongez ya hayo" au "hata"

**Mbwa**
Wayahudi huchukuliwa mbwa kuwa wanyama wasio safi. Lazaro ni mgonjwa sana na dhaifu hata kufukuza mbwa wasimlambe vidonda vyake.

## Luke 16:22

**Ikawa kwamba**
maneno haya yametumika hapa kuadhimisha tukio katika hadithi. Kama lugha yako ina njia kwa ajili ya kufanya hii, unaweza kufikiria kutumia hapa.

**akachukuliwa na malaika**
Hii inaweza alisema katika fomu ya kazi. AT: "Malaika wakamchukua mbali"

**Upande wa Ibrahamu**
Inavyoonekana Ibrahim na Lazaro walikuwa wameketi karibu wakati wa sikukuu mbinguni. Hii ilikuwa ni desturi ya Kigiriki kualika wageni katika karamu. "kukaa karibu na Ibrahimu" au "uketi karibu na Ibrahimu."

**na alizikwa**
"na watu walimzika"

**na katika kuzimu, alipokuwa katika mateso**
"naye akaenda kuzimu ambapo alikuwa akiteseka katika maumivu ya kutisha"

**Akainua macho yake**
"akaangalia juu"

**na Lazaro dhidi ya kifua chake**
"Lazaro na ameketi karibu na Ibrahimu" au "na Lazaro pamoja naye"

**Upande wa Ibrahimu.... dhidi ya kifua chake**
Hii inaonyesha kwamba Ibrahimu na Lazaro walikua wameketi karibu, katika utamadunu wa kigiriki.

**alizikwa**
"Watu walimzika"

**katika kuzimu, alipokuwa katika mateso**
"alikwenda kuzimu, ambapo aliteseka katika maumivu ya kutisha"

**Lazaro dhidi ya kifua chake**
"Lazaro ameketi karibu na Ibrahimu" au "Lazaro karibu naye"

## Luke 16:24

**Naye akasema kwa sauti**
"na tajiri aliita na kusema" au "alipiga kelele kwa Ibrahimu"

**Baba Ibrahimu**
Ibrahimu alikuwa babu wa Wayahudi wote, ikiwa ni pamoja na mtu mmoja tajiri.

**nihurumie**
"tafadhali nihurumie" au "tafadhali uniwie radhi mimi"

**umtume Lazaro**
"kwa kumtuma Lazaro" au "na kuwaambia Lazaro kuja kwangu"

**achovye ncha ya kidole chake**
Hii inaonyesha udogo wa kiasi alichoomba. "aweze kuloanisha ncha ya kidole chake"

**Niko kwenye mateso katika moto huu**
"Niko kwenye mateso katika moto huu " au "Mimi naumia sana katika moto huu"

**alipiga kelele na kusema**
"tajiri alilia kwa kusema" au "alipiga kelele kwa Ibrahimu"

## Luke 16:25

**Mtoto**
tajiri alikuwa mmoja wa kizazi cha Ibrahimu.

**mambo mema**
"mambo mazuri"

**katika njia hiyohiyo mambo mabaya**
"katika njia hiyohiyo alipokea mambo mabaya" au "vivyo alipata mambo ambayo yalimfanya ateseke"

**yeye anatulizwa**
"yeye anatulizwa hapa" au "yeye anafuraha hapa"

**kwa uchungu**
"mateso"

**Zaidi ya hayo yote**
"kwa kuongeza sababu hii"

**shimo kubwa imara limewekwa**
Hii inaweza kusemwa kama. "Mungu ameweka bonde kubwa kati ya wewe na sisi"

**shimo kubwa**
"mwinuko, kina na bonde kubwa" au "kujitenga kubwa" au "bonde kubwa"

 

**wale ambao wanataka kuvuka**
"watu wale ambao wanataka kuvuka shimo" au "kama kuna mtu anataka kuvuka"

**wenyeji wake walifanya kama**
hii inahusu ukweli kwamba wao wote hupokea kitu wakati wao waliishi duniani. Si kusema kwamba kile walikipata mara moja. "wakati alipokuwa hai kupokea"

**Zaidi ya hayo yote**
"kwa kuongeza sababu hii"

## Luke 16:27

**kuwa wewe umtume aende nyumbani kwa baba yangu**
"kwamba utamwambia Lazaro aende nyumbani kwa baba yangu" au "tafadhali, umtume aende nyumbani kwa baba yangu"

**nyumba ya baba yangu**
hii inahusu watu katika nyumba. "familia yangu"

**ili apate kuwaonya**
"ili Lazaro inaweza kuwaonya"

**mahali hapa pa mateso**
"mahali hapa ambapo sisi kuteseka kwa adhabu" au "mahali hapa ambapo sisi tunateswa maumivu ya kutisha"

**kwa hofu kwamba**
Hii ina maana yeye hataki hili litokee "ili kwamba wao wasi"

## Luke 16:29

**Kuunganisha kauli:**
Yesu alimaliza kusimulia hadithi kuhusu tajiri na Lazaro.

**Wanao Musa na manabii**
Ina onyesha kuwa Abraham alikataa kumtuma Lazaro kwa ndugu wa tajiri. Hii inaweza kuwa alisema. "Hapana, sitaweza kufanya ivyo, kwa sababu ya ndugu zenu na yale ambayo Musa na manabii waliandika mda mrefu uliopita"

**waache wawasikilize**
"ndugu zako lazima wawe makini na Musa na Manabii"

**kama mtu aliamua kwenda kwao kutoka katika wafu**
"kama mtu ambaye amefariki aliamua kwenda kwao" au "kama mtu ambaye amefariki aliamua kwenda na kuwaonya"

**Kama hawata wasikiliza Musa na Manabii**
"Kama hawatakuwa makini kwa kilicho andikwa na Musa na manabii"

**wala hawataweza kushawishiwa kama mtu angefufuka kutoka wafu**
"Wala mtu ambaye atakuja kutoka kwa wafua atakua na uwezo wa kuwashawishi" au "hawatamini hata kama mtu angefufuka kutoka wafu"

**Musa na manabii**
Hii ina maana ya maandiko yao. "nini Musa na manabii aliandika"

---

## Chapter 17

**1** Yesu akawaambia wanafunzi wake, "mambo yasababishayo watu watende dhambi hayana budi kutokea,
Lakini ole wake mtu anayeyasababisha! **2** Ingekua ni heri kama mtu huyo angefungiwa jiwe zito la
kusagia shingoni na kutubwa baharini, kuliko kumfanya mmoja wa hawa wadogo atende dhambi. **3**
Jilindeni. Kama ndugu yako akikukosea mwonye, naye akitubu msamehe. **4** Kama akikukosea mara saba
kwa siku moja na mara saba kwa siku moja akaja kwako akisema, 'ninatubu,' msamehe!" **5** Mitume wake
wakamwambia Bwana, "tuongezee imani yetu." **6** Bwana akasema, "kama mgekuwa na imani kama punje
ya haradarii, mngeweza kuuambia mti huu wa mkuyu, 'n'goka na ukaote baharini,' nao ungewatii. **7** Lakini
nani miongoni mwenu, ambaye ana mtumishi anayelima shamba au anayechunga kondoo, atamwambia
arudipo shambani, 'Njoo haraka na keti ule chakula? **8** Je hatamwambia, 'Niandalie chakula nile, na
jifunge mkanda na unitumikie mpaka nitakapo maliza kula na kunywa. Baada ya hapo uta kula na
kunywa? **9** Hata mshukuru mtumishi huyo kwasababu katimiza yale aliyoamriwa? **10** Vivyo hivyo nanyi
mkiisha kufanya mliyoagizwa semeni 'Sisi tu watumishi tusiostahili. Tumefanya tu yale tuliyopaswa
kufanya.' **11** Ilitokea kwamba alivyokua akisafiri kwenda Yerusalemu, alipita mpakani mwa Samaria na
Galilaya. **12** Alipokua akiingia kwenye kijiji kimoja, huko alikutana na watu kumi waliokuwa na ukoma.
Wakasimama mbali **13** wakapaza sauti wakasema "Yesu, Bwana tuhurumie." **14** Alipowaona akawaambia,
"Nendeni mkajionyeshe kwa makuhani." nao walipokua wakienda wakatakasika. **15** Mmoja wao alipoona
kwamba amepona, akarudi kwa sauti kuu akimsifu Mungu. **16** Akapiga magoti miguuni mwa Yesu
akamshukuru. Yeye alikua msamaria. **17** Yesu akajibu, akasema, "Je hawakutakasika wote kumi? Wako
wapi wale wengine tisa? **18** Hakuna hata mmoja aliyeonekana kurudi ili kumtukuza Mungu, isipokuwa
huyu mgeni?" **19** Akamwambia, "Inuka na uende zako imani yako imekuponya." **20** Alipoulizwa na
mafarisayo ufalme wa Mungu utakuja lini, Yesu akawajibu akisema, "Ufalme wa Mungu sio kitu ambacho
kinaweza kuonekana. **21** Wala watu hawatasema, 'Angalia hapa!' au, 'Angalia kule!' kwa maana ufalme wa
Mungu umo ndani yenu." **22** Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Wakati utafika ambapo mtatamani
kuiona moja ya siku ya Mwana wa Adamu, lakini hamtaiona. **23** Watawaambia, 'Angalia, kule! Angalia,
hapa!' Lakini msiende kuangalia, wala kuwafuafata, **24** kama umeme wa radi umulikao katika anga
kuanzia upande mmoja hadi mwingine. Hivyo hata Mwana wa Adamu atakuwa ivyo katika siku yake. **25**
Lakini kwanza itampasa kuteseka katika mambo mengi na kukataliwa na kizazi hiki. **26** Kama ilivyokuwa
siku za Nuhu, ndivyo itakavyokua katika siku ya Mwana wa Adam. **27** Walikula, walikunywa, wakioa na
kuolewa mpaka siku ile ambayo Nuhu alipoingia katika safina na gharika ikaja na kuwaangamiza wote. **28**
Ndivyo ilivyokua katika siku za Lutu, walikula, kunywa, wakinunua na kuuza, kulima na walijenga. **29**
Lakini siku ile Lutu alipoondoka Sodoma, ikanyesha mvua ya moto na kiberiti kutoka mbinguni
ikawaangamiza wote. **30** Hivyo ndivyo itakavyo kuwa siku ile ya Mwana wa Adamu atakapofunuliwa. **31**
Siku hiyo, usimruhusu aliye kwenye dari ya nyumba ashuke kuchukue bidhaa zake ndani ya nyumba. Na
usimruhusu aliyeko shambani kurudi nyumbani. **32** Mkumbuke mke wa Lutu. **33** Ye yote anaejaribu
kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini ye yote atakayeyapoteza maisha yake atayaokoa. **34**
Nakwambia, usiku huo kutakua na watu wawili katika kitanda kimoja. Mmoja atachukuliwa, na mwingine
ataachwa. **35** Kutakua na wanawake wawili wanasaga nafaka pamoja, mmoja atachukuliwa na mwingine
ataachwa." **37** Wakamwuliza, "Wapi, Mungu?" Akawaambia, "Pale ulipo mzoga, ndipo tai hukusanyika kwa
pamoja."

---

## Luka 17 Maelezo ya Jumla

**Muundo na upangiliaji**

Katika utakaso wa watu 10

**Dhana maalum katika sura hii**

**Mifano ya Agano la Kale**

Sura hii inatumia mfululizo wa mifano kutoka Agano la Kale. Mifano zote hizi ni wakati ambapo watu hawakujihusisha na Mungu. Kuelewa vizuri maana ya kila mfano itakuwa vigumu bila kuanza kusoma na kuelewa kitabo cha Mwanzo.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

Those who read your translation may need help so they can understand what Jesus was teaching here.

### Takwimu muhimu za matamshi katika sura hii

### Ingekua afadhali

Hii ni aina maalum ya hali ya fikira. Katika hali hii, badala ya kuzungumza juu ya hali au vitu vingetokea, inatoa ufafanuzi juu ya hali ya baadaye ikiwa hali ya sasa haibadiliki.

### Hali ya Kufikiri na Hali ya Uhuishaji

Yesu anatumia takwimu mbili za misemo kwa wakati mmoja katika sura hii. Anashirikisha hali ya kufikiri pamoja na maswali ya uhuishaji kwa sababu jibu sahihi kwa hali ya kufikiri lazima iwe wazi.

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

### "Mwana wa Binadamu"

Yesu anajiita mwenyewe kama "Mwana wa Binadamu." Lugha zingine haziwezi kuruhusu mtu kujitaja mwenyewe kama 'mtu wa tatu.'

### Matumizi ya kitendawili

Kitendawili ni taarifa inayoonekana kuwa ya ajabu, ambayo ni kana kwamba inajikana yenyewe, lakini kwa hakika sio ya ajabu. Mfano wa kitendawili katika sura hii: "Yeyote anayetaka kupata uhai wake ataupoteza, lakini yeyote anayepoteza uhai wake atauokoa" (Luka 17:33).

---

## Luke 17:1

**Kuunganisha kauli:**
Yesu anaendelea kufundisha, lakini yeye ataelekeza nia yake kwa wanafunzi wake. Hii bado ni sehemu moja ya hadithi na siku hiyo hiyo ambayo ilianza

**Ni hakika kutakuwa na mambo ambayo yanaweza kutufanya kutenda dhambi**
"Mambo ambayo huwajaribu watu kutenda dhambi bila ya shaka vitatokea"

**kwa mtu huyo atakayevisababisha**
"kwa mtu yeyote ambaye husababisha majaribu kuja" au "kwa mtu yeyote ambaye anasababisha watu kujaribiwa"

**kama jiwe la kusagia likiwekwa shingoni kwake na angetupwa**
Hii inaweza kusemwa: "kama walikuwa waweka jiwe la kusagia shingoni mwake na kumtupa" au "kama mtu alikua awekewe jiwe zito shingoni mwake na kumsukuma"

**jiwe la kusagia**
Hili ni kubwa sana, jiwe zito la mviringo linalotumika kusaga nafaka za ngano kuwa unga" "jiwe nzito"

**hawa wadogo**
Hii hapa inahusu watu ambao imani bado ni dhaifu. "Watu hawa ambao imani yao ni ndogo"

**na mashaka**
Hii ilikua njia ya kumaanisha dhambi za kutokudhamiria. "dhambi"

**Itakuwa bora kwa ajili yake kama**
Ina maana kwamba adhabu ya mtu huyu kwa kusababisha watu kutenda dhambi itakua mbaya zaidi ya wazima baharini.

**kwa ajili yake ... shingo yake ... yeye walikuwa ... anapaswa**
Maneno haya rejea wanawake ikiwa ni pamoja na wanaume.

## Luke 17:3

**Kama ndugu yako akikosa**
Hii kauli inaonyesha kwamba tukio hilo pengine litatokea katika siku zijazo.

**ndugu yako**
"ndugu" hapa limetumika kwa maana ya mtu aliye na imani sawa. "mwamini mwenzetu"

**Mkemee**
"kumwambia kwanguvu kwamba aliyoyafanya ilikuwa ni makosa" au "msahishe"

**Na kama akikukosea mara saba**
Hii inaonyesha inaweza isitokee ila kama ikitokea Yesu anawaambia watu wasamehe.

**mara saba kwa siku**
namba saba katika Biblia ni ishara ya ukamilifu. "mara nyingi katika siku"

### Luke 17:5

**Habari kwa ujumla:**
Kuna mapumziko mafupi katika mafundisho ya Yesu wakati wanafunzi wakizungumza nae. Kisha Yesu anaendelea kufundisha.

**Kuongeza imani yetu**
"Tafadhali tuongezee imani"

**Kama imani yenu ingekuwa kama mbegu ya haradali**
"haradali" ni mbegu ndogo sana. Yesu ana maana kwamba hawakuwa na hata kiasi kidogo cha imani.

**mti huu wa mkuyu**
"mtini" au "mti"

**Kungooka na kupandwa baharini**
hii inaweza semwa kama: "kujing'oa mwenyewe na kujipanda mwenyewe baharini" au "Chukua mizizi yako nje ya ardhi, na kuweka mizizi yako ndani ya bahari"

**ungewatii**
"mti ungewatii." Matokeo haya ni masharti. ingeweza kutokea tu kama walikuwa na imani.

**mti huu wa mkuyu**
Kama aina hii ya mti haufahamiki, inaweza kuwa na manufaa mbadala aina nyingine ya mti. "mtini" au "mti"

### Luke 17:7

**Lakini ni nani katika yenu, ambaye ana mtumishi**
Yesu anauliza kundi kuhukumu hali fulani na mtumishi.

**mtumishi anaelima au kutunza kondoo**
"mtumishi anaelima shamba lako au analinda kondoo wako"

**Je hatambiambia**
Yesu anatumia swali kuwafundisha wanafunzi.

**jifunge mkanda na unitumikie**
"funga nguo yako katika kiuno chako na unitumikie mimi" au "vaa vizuri kisha unitumikie." Watu hufunga nguo zao karibu na viuno vyao ili nguo zao wakati wa kazi zisiwasumbue.

**Kisha baada ya hayo**
"Kisha baada ya kunitumikia"

**Lakini ni nani kati yenu ... atamwambiya ... kaa chini kula '?**
Yesu anauliza wanafunzi wake swali kuwasaidia kufikiri juu ya jukumu la mtumishi. Hii inaweza kuwa kauli. "Lakini mtu yeyote kati yenu ... siwezi kusema kwake ... kaa chini kula '"

**Je, yeye hatamwambia ... kula na kunywa?**
Yesu anatumia swali la pili kueleza jinsi wafuasi wangewa fanyia watumishi. Hii inaweza kuwa kauli. "Naye hakika humwambia ... kula na kunywa '"

### Luke 17:9

**Kuunganisha kauli:**
Yesu alimaliza kufundisha. Huu ni mwisho wa sehemu ya hadithi hii.

**Yeye hashukuru**
"Yeye hakutaka kuwashukuru" au "Wewe hutashukuru"

**mambo yaliyo amuriwa**
Hii inaweza kusemwa "Mambo uliyo muagiza afanye"

**gani?**
"haki?" au "ni hii si kweli?"

**wewe pia**
Yesu alikuwa akizungumza na wanafunzi wake, hivyo lugha ambazo zina wingi wa "wewe" itakuwa matumizi yake.

**yale uliyo amuriwa**
Hii inaweza kusemwa kama "kwamba Mungu alikuamuru"

**usema**
"ukusema kwa Mungu"

**Sisi ni watumishi tusiostahili**
Hii ni kueleza kuwa wao hawakufanya kitu cha kustaili kusifiwa. "Sisi watumishi wa kawaida" au "Sisi watumishi hatustahili sifa yako"

**Hamshukuru mtumishi ... alivyoamuru, je anafanya?**
Yesu anatumia swali hili ili kuonyesha jinsi watu wanavyo wafanyia watumishi. Hii inaweza kuwa kauli. "Yeye hakutaka kumshukuru mtumishi ... aliamuru"

### Luke 17:11

**Habari kwa ujumla:**
Hii ni sehemu ya pili ya hadithi. Yesu anaponya watu 10 wa ukoma. Mstari wa 11 na 12 unatoa taarifa za msingi na mazingira ya hadithi.

**Ikawa kwamba**
maneno haya yametumika hapa kuonyesha mwanzo wa sehemu mpya ya hadithi. Kama lugha yako ina njia kwa ajili ya kufanya hii, unaweza kufikiria kutumia hapa.

**na walipokua njiani kuelekea Yerusalemu**
"kama Yesu na wanafunzi walipokuwa wakisafiri kwenda Yerusalemu"

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**huko alikutana na watu kumi wenye ukoma**
Hii inaweza semwa kama. "watu kumi wenye ukoma walikutana naye" au "watu kumi waliokuwa na ukoma walikutana naye"

**wakapaza sauti zao**
kauli hii ina maana kusema kwa sauti kubwa. "wakamwita kwa sauti kubwa" au "wao kuita kwa sauti"

**Bwana**
neno lililotafsiriwa hapa kama "Bwana" siyo neno la kawaida kwa "Bwana." Hii moja inahusu mtu ambaye ana mamlaka, na si kwa mtu ambaye anamiliki mtu mwingine.

**utuhurumie**
Walikuwa hasa wanaomba kuponywa. "tafadhali tuonyeshe huruma na utuponye"

**alipokuwa akisafiri kwenda Yerusalemu**
"kama Yesu na wanafunzi walikuwa wakisafiri kwenda Yerusalemu"

**kijiji kimoja**
maneno haya haya elezei hicho kijiji.

**Nao wakasimama mbali mbali na yeye**
Hii ilikuwa ishara ya heshima , kwa sababu wenye ukoma hawakuruhusiwa kukaribia watu wengine.

## Luke 17:14

**mkajionyeshe kwa makuhani**
wenye ukoma walikuwa wanatakiwa kuthibitishwa na makuhani kwamba ukoma wao umepona. "jionyesheni wenyewe kwa makuhani ili waweze kuwachunguza"

**Na ikawa kwamba**
maneno haya yametumika hapa kuonyesha mwanzo wa sehemu mpya ya hadithi. Kama lugha yako ina njia kwa ajili ya kufanya hii, unaweza kufikiria kutumia hapa.

**wakatakasika**
Wakati watu waliponywa, wao hawakuwa tena najisi. Hii inaweza kufanywa wazi. "wakawa safi wakati walipo ponywa ukoma wao" au "walikuwa wametibiwa ukoma wao"

**alipoona kwamba ameponywa**
"kuona kwamba ameponywa" au "alitambua kwamba Yesu aliyemponya"

**akarudi**
"alirudi Yesu"

**kwa sauti kubwa akimtukuza Mungu**
"nakumtukuza Mungu kwa sauti kubwa"

**Akainama miguuni pa Yesu**
"akapiga magoti na kuweka uso wake karibu na miguu ya Yesu." Alifanya hivi kwa kumheshimu Yesu.

## Luke 17:17

**Kuunganisha kauli:**
Huu ni mwisho wa sehemu ya hadithi kuhusu Yesu alivyo ponya wenye ukoma.

**Yesu akajibu, akisema**
Yesu alijibu kulingana na kile mtu alichokifanya, lakini alikuwa akizungumza na kundi la watu karibu naye. "Basi Yesu akawaambia ule umati"

**Je hawakutakasika wote kumi?**
Hii ni moja ya maswali matatu. Yesu aliyatumia kwa kuonyesha watu walio karibu naye jinsi alivyo shangazwa na kukatishwa tamaa kwamba moja tu ya watu kumi alirudi kumtukuza Mungu. "Watu kumi waliponywa" au "Mungu akamponya watu kumi"

**Wale tisa wako wapi?**
"Kwa nini wengine tisa hawakurudi?" Hii inaweza kuwa kauli kwenye. "Watu wengine tisa wanapaswa kurudi, pia"

**Hakuna hata mmoja aliyeonekana kurudi ili kumtukuza Mungu, isipokuwa huyu mgeni?**
Hii inaweza kuwa kauli kwenye. "Hakuna mtu isipokuwa huyu mgeni akarudi kumtukuza Mungu" au "Mungu akaponya watu kumi, lakini tu huyu mgeni akarudi kumtukuza Mungu"

**huyu mgeni**
Wasamaria walikuwa hawana mababu Wayahudi na hawakuwa wakimwabudu Mungu kwa njia ile ile ambayo Wayahudi walivyofanya.

**imani yako imekuponya**
"Kwa sababu ya imani yeko umekuwa vizuri." "Imani" yaweza tajwa kama tendo "Kwa sababu unaamini, umeponywa"

## Luke 17:20

**Habari kwa ujumla:**
Hii ni sehemu ya pili ya hadithi. Hatujui ambapo hili limetokea; ni siku moja wakati Yesu akizungumza na Mafarisayo.

**Alipoulizwa na mafarisayo ufalme wa Mungu utakuja lini, Yesu akawajibu akisema,**
Hii inaweza semwa kama: "wakamuuliza 'Lini Utawala wa Mungu utakuja?"

**Alipoulizwa na Mafarisayo**
Huu ni mwanzo wa sehemu mpya ya hadithi. Baadhi ya tafsiri huanza kwa "Siku moja" au "Mara."

**Ufalme wa Mungu sio kitu ambacho kinaweza kuonekana**
Hii inaweza kusemwa: "Ufalme wa Mungu si kitu ambacho unaweza kuona kwa macho yako" au "Ingawa unanngalia Ufalme wa Mungu, huwezi kuuona"

**Utawala wa Mungu uko kati yenu**
"Utawala wa Mungu uko hapa" au "Mungu tayari ameanza kutawala kati yenu"

### Luke 17:22

**Kuunganisha kauli:**
Yesu anaanza kuwafundisha wanafunzi wake.

**wakati utafika ambapo**
"wakati utafika ambapo" au "Labda siku moja"

**mtatamani kuona**
"wewe utataka sana kuona" au "utakuwa wataka uzoefu"

**mojawapo ya siku za Mwana wa Adamu**
Hii ina maana ya Utawala wa Mungu. "moja ya siku wakati Mwana wa Adamu atatawala akiwa mfalme"

**wala msiwafuate**
"na wala kwenda pamoja nao ili kuona"

**maana kama vile radi uonekanavyo**
"kwa maana kama vile radi ni wazi kwa kila mtu wakati unaonekana na" au "maana kama vile umeme unaonekana ghafla"

**ndivyo naye Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku yake**
hii inahusu ufalme ujao wa Mungu. "itakuwa kana kwamba siku ile Mwana wa Adamu atafika kutawala"

**Mwana wa Adamu**
Yesu anazungumza juu yake mwenyewe.

**lakini huwezi kuiona**
"hutaweza kuihisi"

**Angalia, pale! Angalia, hapa!**
Hii ina maana ya kumtafuta Masihi. "Angalia, Masihi yuko pale! yuko huku!"

**maana kama vile radi huangaza**
Mwana wa Adamu ajae itakuwa wazi na ghafla, kama muonekano wa radi. "kwa maana kama vile radi ni wazi kwa kila mtu wakati unaonekana na" au "maana kama vile umeme unaonekana ghafla"

### Luke 17:25

**Lakini kwanza lazimu ateswe**
"Lakini kwanza Mwana wa Adamu lazima ateswe." Yesu anazungumza juu yake mwenyewe katika nafsi ya tatu.

**na kukataliwa na kizazi hiki**
"na kizazi hiki lazima kitamkataa"

**Kama ilivyotokea katika siku za Nuhu**
"siku za Nuhu" inahusu wakati wa maisha ya Nuhu kabla ya Mungu kuwaadhibu watu wa dunia. "Kama watu walivyokua wakifanya katika siku za Nuhu" au "Kama watu walivyokua wakifanya wakati Nuhu alivyokua akiishi"

**hata hivyo itakuwa pia kutokea katika siku za Mwana wa Adamu**
"siku za Mwana wa Adamu" inahusu kipindi kabla Mwana wa Adamu atakuja. "Watu watakuwa wakifanya mambo sawa katika siku za Mwana wa Adamu" au "watu watakuwa wakifanya mambo sawa wakati Mwana wa Adamu akikaribia kuja"

**Walikula, walikunywa, kuoa, na walipewa katika ndoa**
Watu walikuwa wanafanya mambo ya kawaida. Hawakujua au kujali ya kwamba Mungu alikuwa karibu kuwahukumu.

**walipewa katika ndoa**
hii inaweza semwa kama "Wazazi walikuwa wakiruhusu binti zao kuolewa na wanaume"

**Safina**
"meli" au "majahazi"

**kukataliwa na kizazi hiki**
Hii inaweza semwa kama "watu wa kizazi hiki lazima watamkataa"

**kuwaangamiza wote**
Hii sio pamoja na Nuhu na familia yake waliokuwepo katika safina. "kuharibiwa wale wote ambao hawakuwa katika meli"

### Luke 17:28

**Ndivyo ilivyokua katika siku za Lutu**
"siku za Lutu" inahusu wakati tu kabla ya Mungu haja adhibu miji wa Sodoma na Gomora. "Mfano mwingine ni jinsi ilivyotokea wakati wa Lutu" au "Kama watu walikuwa wakifanya wakati Lutu akiishi"

**nao wakala**
"watu wa Sodoma walikula"

**kulinyesha moto na kiberiti kutoka mbinguni**
"moto na kiberiti ukaanguka kutoka mbinguni kama mvua"

**kuwaangamiza wote**
hii haina ni pamoja Lutu na familia yake. "kuharibiwa wale wote ambao walikaa katika mji"

### Luke 17:30

**Baada ya namna hiyo itakuwa**
"Itakuwa kama hiyo." "Kwa njia hiyo hiyo watu hawtakuwa tayari"

**siku ile Mwana wa Adamu atakapofunuliwa**
Hii inaweza semwa kama "wakati Mwana wa Adamu ataonekana" au "wakati Mwana wa Adamu anakuja"

**usimlete aliye kwenye dari ya nyumba ashuke chini**
"yeyote alie juu ya nyumba asishuke" au "mtu akiwa darini kwake, ni lazima asiende chini"

**juu ya dari**
dari zao zilikuwa bapa na watu kuweza kutembea au kukaa juu zao.

**vitu vyake**
"mali zake" au "mambo yake"

**kurudi**
Walikua wasirudi nyumbani kuchukua kitu chochote

**Mwana wa Adamu**
Yesu anazungumza juu yake mwenyewe. "Mimi, Mwana wa Adamu"

### Luke 17:32

**Mkumbuke mke wa Lutu**
"Kumbuka kile kilichotokea kwa mke wa Lutu!" Hili ni onyo. Yeye aligeuka na kuangalia Sodoma na Mungu akamuadhibu pamoja na watu wa Sodoma. "Msifanye kile mke wa Lutu alichokifanya"

**Ye yote anaejaribu kuyaokoa maisha yake atayapoteza**
"Watu ambao hujaribu kuokoa maisha yao watayapoteza" au "Yeyote anajaribu kuokoa njia yake za zamani za maisha atapoteza maisha yake"

**lakini ye yote atakayeyapoteza maisha yake atayaokoa.**
"lakini watu ambao kupoteza maisha yao atawalinda" au "lakini mwenye kukataa njia yake ya zamani ya maisha kuokoa maisha yake"

### Luke 17:34

**Nawaambia**
Kama Yesu anaendelea kuhutubia wanafunzi wake, anasisitiza umuhimu wa nini alichokua akiwaambia.

**katika usiku huo**
Hii inahusu nini kitatokea kama yeye, Mwana wa Adamu, atakuja wakati wa usiku.

**kutakuwa na watu wawili katika kitanda kimoja**
mkazo si juu ya watu hawa wawili, lakini juu ya ukweli kwamba baadhi ya watu watachukuliwa na wengine wataachwa.

**kitanda**
"kochi"

**Mmoja atachukuliwa, na mwingine ataachwa**
"Mtu mmoja atachukuliwa na mtu mwingine ataachwa." Hii inaweza semwa kama "Mungu atachukua mtu mmoja na kumuacha mwingine" au "Malaika atachukua mmoja na kumuacha mwingine"

**Kutakuwa na wanawake wawili wakisaga nafaka pamoja**
mkazo si juu ya hawa wanawake wawili au shughuli zao, lakini juu ya ukweli kwamba baadhi ya watu watachukuliwa na wengine wataachwa.

**kusaga pamoja**
"wakisaga nafaka pamoja"

### Luke 17:37

**Habari kwa ujumla:**
wanafunzi walilomwuliza swali kuhusu mafundisho yake na akawajibu

**Ni wapi Bwana?**
"Bwana, wapi hii itatokea?"

**Ambapo kuna mzoga, ndipo tai hukusanyika pamoja**
Inavyoonekana huu ni msemo ukimaanisha "Itakuwa dhahiri" au "Mtaijua ni pale yanapotokea." "Kama tai mkutano inaonyesha kwamba kuna maiti, hivyo mambo hayo kuonyesha kwamba Mwana wa Adamu atakuja"

**Tai**
Tai ni ndege wakubwa ambao wanaruka pamoja na kula nyama za wanyama waliokufa wakiwapata. Unaweza kuelezea ndege kwa njia hii au kutumia neno kwa ndege wa kawaida wanaofanya hivi.

## Chapter 18

**1** Kisha akawaambia mfano wa namna wanavyopaswa kuomba daima, na wasikate tamaa. **2** akaisema,
'Kulikuwa na hakimu katika mji fulani, ambaye hakuwa anamwogopa Mungu na hakuwaheshimu watu. **3**
Kulikuwa na mjane katika jiji hilo, naye alimwendea mara nyingi, akisema, 'Nisaidie kupata haki dhidi ya
mpinzani wangu.' **4** Kwa muda mrefu hakuwa tayari kumsaidia, lakini baada ya muda akasema moyoni
mwake, `Ingawa mimi simwogopi Mungu au kuheshimu mtu, **5** lakini kwa vile huyu mjane ananisumbua
nitamsaidia kupata haki yake, ili asije akanichosha kwa kunijia mara kwa mara. '' **6** Kisha Bwana akasema,
'Sikiliza alivyosema huyo hakimu dhalimu. **7** Je Mungu pia hataleta haki kwa wateule wake ambao
wanamlilia mchana na usiku? Je, yeye hatakuwa mvumilivu kwao? **8** Nawaambia kwamba ataleta haki
kwao upesi. Lakini wakati Mwana wa Adamu atakapokuja, je, atakuta imani duniani? ' **9** Ndipo
akawaambia mfano huu kwa baadhi ya watu ambao wanajiona wenyewe kuwa wenye haki na kuwadharau
watu wengine, **10** 'Watu wawili walipanda kwenda hekaluni kusali: mmoja Mfarisayo mwingine mtoza
ushuru. **11** Farisayo akasimama akaomba mambo haya juu yake mwenyewe, 'Mungu, nakushukuru kwa
vile mimi si kama watu wengine ambao ni wanyang'anyi, watu wasio waadilifu, wazinzi, au kama huyu
mtoza ushuru. **12** Nafunga mara mbili kila wiki. Natoa zaka katika mapato yote ninayopata. ' **13** Lakini
yule mtoza ushuru, alisimama mbali, bila hakuweza hata kuinua macho yake mbinguni, akagonga kifua
chake akisema, 'Mungu, nirehemu mimi mwenye dhambi.' **14** Nawaambia, mtu huyu alirudi nyumbani
akiwa amehesabiwa haki kuliko yule mwingine, kwa sababu kila ajikwezaye atashushwa, lakini kila mtu
anayejinyenyekeza atainuliwa. ' **15** Watu walimletea watoto wao wachanga, ili aweze kuwagusa, lakini
wanafunzi wake walipoona hayo, wakawazuia. **16** Lakini Yesu akawaita kwake akisema, 'Waacheni watoto
wadogo waje kwangu, wala msiwazuie. Maana ufalme wa Mungu ni wa watu kama hao. **17** Amin,
nawaambia, mtu yeyote asiyeupokea ufalme wa Mungu kama mtoto ni dhahiri hatauingia. ' **18** Mtawala
mmoja akamwuliza, akisema, 'Mwalimu mwema, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?' **19** Yesu
akamwambia, 'Kwa nini unaniita mwema? Hakuna mtu aliye mwema, ila Mungu peke yake. **20** Unazijua
amri- usizini, usiue, Usiibe, usishuhudie uongo, waheshimu baba yako na mama yako. **21** Yule mtawala
akasema, 'Mambo haya yote nimeyashika tangu nilipokuwa kijana.' **22** Yesu alipoyasikia hayo
akamwambia, '"Umepungukiwa jambo moja. Lazima uuze vyote ulivyonavyo na uwagawie maskini, nawe
utakuwa na hazina mbinguni -kisha njoo, unifuate. ' **23** Lakini tajiri aliposikia hayo, alihuzunika sana, kwa
sababu alikuwa tajiri sana. **24** Kisha Yesu, akamwona alivyohuzunika sana akasema, 'Jinsi gani
itakavyokuwa vigumu kwa matajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu! **25** Maana ni rahisi sana kwa ngamia
kupita katika tundu la sindano, kuliko kwa tajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu. ' **26** Wale waliosikia
hayo, wakasema, 'Nani basi, atakayeweza kuokolewa?' **27** Yesu akajibu, 'Mambo yasiyowezekana kwa
mwanadamu kwa Mungu yanawezekana." **28** Petro akasema, 'Naam, sisi tumeacha kila kitu na
tumekufuata wewe. ' **29** Kisha Yesu akawaambia, Amin, nawaambia kwamba hakuna mtu aliyeacha
nyumba, au mke, au ndugu, au wazazi au watoto, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, **30** ambaye hatapokea
mengi zaidi katika ulimwengu huu, na katika ulimwengu ujao, uzima wa milele. ' **31** Baada ya
kuwakusanya wale kumi na wawibili, akawaambia, 'Tazama, tunapanda kwenda Yerusalemu, na mambo
yote ambayo yameandikwa na manabii kuhusu Mwana wa Adamu yatakamilishwa. **32** Kwa maana atatiwa
mikononi mwa watu wa Mataifa na atatendewa dhihaka na jeuri, na kutemewa mate. **33** Baada ya
kumchapa viboko watamwua na siku ya tatu atafufuka. ' **34** Hawakuelewa mambo haya, na neno hili
lilikuwa limefichwa kwao, na hawakuelewa mambo yaliyosemwa. **35** Ikawa Yesu ulipokaribia Yeriko, mtu
mmoja kipofu alikuwa ameketi kando ya barabara akiomba msaada, **36** aliposikia umati wa watu ukipita
aliuliza nini kinatokea. **37** Wakamwambia kwamba Yesu wa Nazareti anapita. **38** Hivyo yule kipofu akalia
kwa sauti, akisema, 'Yesu, Mwana wa Daudi, unirehemu.' **39** wale waliokuwa wakitembea walimkemea
huyo kipofu, wakamwambia anyamaze. Lakini yeye akazidi kulia kwa sauti, 'Mwana wa Daudi, unirehemu.
**40** Yesu akasimama akaamuru mtu yule aletwe kwake. Kisha yule kipofu alipomkaribia, Yesu akamwuliza,
**41** 'Unataka nikufanyie nini?' Akasema, 'Bwana, nataka kuona.' **42** Yesu akamwambia, 'Upate kuona. Imani
yako imekuponya. ' **43** Mara hiyo akapata kuona, akamfuata Yesu akimtukuza Mungu. Walipoona hili, watu
wote wakamsifu Mungu.

---


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Luka 18 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

Luka 18:6-8 inapaswa kuonekana kama maelezo ya mfano katika 18:1-5.

### Dhana maalum katika sura hii

### Hakimu asiye na haki

Waamuzi walitakiwa kuendesha haki bila masharti, lakini hakimu huyu hamtendei mwanamke haki. Badala yake, anapaswa kuomba mara nyingi kwa hakimu kufanya jambo linalofaa. Kwa hiyo, hakimu alionyeshwa kama 'asiye na haki." and )

### Mafarisayo na watoza ushuru

Luka mara kwa mara anaonyesha kuwa tofauti makundi haya mawili ya watu katika injili yake. Mafarisayo walijiona kuwa ni mifano ya wazi ya wenye haki na kuona watoza ushuru kuwa wenkye dhambi sana, mifano ya wazi ya uovu. , and )

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

### "Mwana wa Binadamu"

Yesu anajiita mwenyewe kama "Mwana wa Binadamu." Lugha zingine haziwezi kuruhusu mtu kujitaja mwenyewe kama 'mtu wa tatu.'

### "Aliomba mambo haya juu yake mwenyewe"

Sala ya Mfarisayo kwa hakika haielekezwi kwa Mungu, kwa hiyo kile anachofanya sio maombi. Yeye anadhani anaomba, lakini anazungumza tu ili watu wengine wamsikie na kufikiri kuwa ni mtakatifu.

### Maelekezo ya jumla na Maalum

Kuna nyakati ambapo Agano Jipya inatoa maelekezo maalum au amri ambazo zinahusu Wakristo wote. Kwa nyakati nyingine, maelekezo yake ni ya jumla au hata kupita kiasi. Kwa mfano, wakati Yesu anasema, "Uza vitu vyako," hazungumzii na Wakristo wote mahali pote wakati wote, lakini Wakristo wote wanapaswa kukumbuka kwamba wao ni mawakili tu wa kila kitu wanachopokea kutoka kwa Mungu, na anaweza kuwaomba kukitoa wakati wowote.

---

### Luke 18:1

**Maelezo yanayounganisha"**
Yesu anaanza kuwaambia mfano akiendelea kuwafundisha wanafunzi wake. Hii ni sehemu ile ile ya simulizi. Mstari wa 1 unatupa maelezo ya mfano ambao Yesu anataka kuusema.

**Kisha**
"Kisha Yesu"

**Wanapaswa kusali daima wala wasikate tamaa**
Sentensi hizi mbili zina maana sawa ambayo Yesu aliitumia ili kusisitiza. Lugha zingine zina namna tofauti za kusisitiza. "Daima muendelee kuomba."

**akasema**
Hii pia inaweza kuanza kwenye sentensi mpya "Akasema"

**Kulikuwa na hakimu katika mji fulani**
Neno "fulani" imetumika kuonyesha kuwa hii ilitokea, lakini bila kumuonyesha hakimu au mji.

**Kuogopa**
Ogopa

**Haeshimu watu**
"Hajali watu"

### Luke 18:3

**Sasa kulikuwa na mjane**
Yesu alitumia neno hili kumtambulisha mtu mwingine kwenye simulizi.

**Mjane**
Ni mwanamke ambaye mume wake amekufa. Watu waliomsikiliza Yesu watafikiri kuwa ni mtu ambaye


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

hamna mtu wa kumlinda kutoka kwa wale wanaotaka kumuumiza.

**Alimwendea mara nyingi**
Neno "yeye" linamaanisha hakimu.

**Nisaidie kupata haki dhidi**
"waadhibu" au "nisaidie"

**Mpinzani wangu**
"adui yangu" au "mtu anayejaribu kuniumiza." Huyu ni mpinzani katika mabo ya sheria. Hipo wazi kuwa mwanamke anamshitaki yule mtu au yule mtu anamshitaki mwanamke.

**Kumwogopa Mungu**
"ogopa Mungu"

**Mtu**
Hii inamaanisha "watu" kwa ujumla.

**Ananisababishia matatizo**
"Ananisumbua"

**Asinichoshe**
"asije akanisumbua"

**Kwa kunijia mara kwa mara**
"kwa kuja kwangu mara kwa mara"

### Luke 18:6

**Taarifa ya jumla:**
Yesu anamaliza kuwaambia mfano wake na anatoa maelezo kwa wanafunzi wake.

**Sikiliza alivyosema huyu hakimu mmbaya**
"Fikiri jinsi alivyosema huyu hakimu mmbaya.: Tafsiri kwa namna ambayo watu wataelewa kwamba Yesu tayari aliwaambia alichokisema jaji.

**Sasa**
Hili neno linaonyesha kuwa Yesu alimaliza kutoa mfano na akaanza kutoa maana yake.

**Mungu pia hataleta... usiku?**
Yesu alitumia swali kuwafundisha wanafunzi wale.

**Wateule wake**
"Watu aliowachagua"

**Hatakuwa mvumilivu kwao?**
Yesu alitumia swali kuwafundisha wanafunzi wake.

**Mwana wa Adamu**
Yesu alikuwa anajizungumzia mwenyewe.

**Atakuta imani duniani?**
Dhumuni la mfano huu ni kuwatia moyo wanafunzi wake waendelee kuamini na kuomba. Yesu hapa anatumia swali lingine anayotegemea jibu hasi. "Lakini najua mimi, Mwana wa Adamu, nikirejea, nitawakuta watu wasioniamini."

### Luke 18:9

**Taarifa ya jumla:**
Yesu anaanza kuwaambia mfano mwingine kwa watu wengine waliojiona kuwa wenye haki.

**Ndipo yeye**
"Ndipo Yesu"

**Baadhi**
"Baadhi ya watu"

**Ambao walijiona wenyewe kuwa wenye haki**
"waliokuwa na haki wenyewe" au "waliodhani kuwa wana haki"

**kuwadharau**
"Kutothamini" au "kudhani kuwa ni bora zaidi ya"

**Hekaluni**
"kwenye eneo la hekalu"

### Luke 18:11

**Mfarisayo akasimama, akasali mambo haya juu yake mwenyewe**
Maana kwenye maneno ya Kigiriki haipo wazi. inaweza kuwa na maana 1) "Mfarisayo alisimama akaomba juu yake mwenyewe kwa njia hii" au 2) Mfarisayo alisimama pekeyake na akasali."

**Majambazi**
Jambazi ni mtu anayeiba vitu kwa kumlazimisha mtu ampe au kwa kumtishia kwa nguvu.

**Ninayopata**
"Ninayopokea"

### Luke 18:13

**Maelezo yanayounganisha:**
Yesu alimaliza kuwaambia mfano. kwenye mstari wa 14, alitoa maelezo kuhusu maana ya mfano huo.

**Akainua macho yake juu**
"Akaangalia mbinguni" au "akaanalia mbele"

**Akapiga kifua chake**
Hii ni ishara ya nje ya masikitiko makuu, na kuonyesha namna huyu mtu anavyotubu na unyenyekevu.

**Mungu nirehemu mimi, mwenye dhambi**
Mungu nakuomba nirehemu mimi, japokuwa ni mtenda dhambi" Mungu, nakuomba unirehemu mimi. Ni mtenda dhambi"

**Huyu mtu alirudi nyumbani akiwa amehesabiwa haki.**
"Mungu alimsamehe yule mtoza ushuru"

**Kuliko yule mwingine**
"Kuliko yule mtu mwingine" au "na sio yule mtu mwingine." ' Lakini Mungu hakumsamehe Mfarisayo"

**Kwa sabau kila mtu atakayejikweza**
Kwenye sentensi hii, Yesu anahama kwenye simulizi na kutoa maelezo ya simulizi.

**Atashushwa**
"Mungu atamshusha"

**Atakwezwa**
"Mungu atampa heshima"

### Luke 18:15

**Maelezo ya kuunganisha:**
Hili ni tukio linalofuata kwenye sehemu ya simulizi inayoanza Yesu anawakaribisha watoto na anazungumza nao.

**Akawagusa, lakini**
Hii inaweza kutafsiriwa kama sentensi tofauti. "akawagusa. Lakini"

**Wakawazuia**
"Wanafunzi walijaribu kuwakataza wazazi wasiwalete watoto kwa Yesu"

**waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie**
Hizi sentensi mbili zina maana inayofanana na zimewekwa pamoja ili kutia msisistizo. Lugha nyingine zinasisitiza kwa namna tofauti. "Mnatakiwa muwaache watoto wadogo waje kwangu."

**Ni wa kwao**
"Ni wa watu waliokama hawa watoto"

**Amini nawaambia**
"Hakika nawaambia." Yesu alitumia maelezo haya kusisitiza umuhimu wa alichokuwa anataka kukisema.

**mtu yeyote asiyeupokea Ufalme wa Mungu kama mtoto ni dhahiri hataingia**
Mungu anataka watu wapokee ufalme wake kwa kuamini na unyenyekevu. "Yeyote anayetaka kuingia kwenye ufalme wa Munguataupokea kwa kuamini na unyenyekevu kama mtoto mdogo."

### Luke 18:18

**Maelezo yanayounganisha:**
Hii ni tukio linalofuata kwenye sehemu ya simulizi inayoanza. Yesu akaanza kuongea na kiongozi kuhusu kuingia katika ufalme wa Mungu.

**Nifanye nini**
"Ni kitu gani natakiwa kufanya" au "Ni kipi kinahitajika kwangu"

**Kurithi**
"kuwa mmiliki halali wa." Hii ina maanisha mali ya mtu aliyekufa. Luka anatumia neno hili kuonyesha kuwa mtawala anafahamu kuwa uzima wa milele hauwezi kuuchuma, na sio kila mtu ataishi milele.

**Hakuna mtu aliye mwema, ila Mungu peke yake**
"Hakuna mtu aliye mwema kabisa. Mungu pekee ndo mwema"

**Usiue**
"Usifanye mauaji"

**Mambo haya yote**
"Amri zote hizi"

### Luke 18:22

**Yesu aliposikia hayo**
"Yesu aliposikia yule mtu akisema hayo"

**Akamwambia**
"akamjibu"

**Umepungukiwa jambo moja**
"Bado unatakiwa kufanya jambo moja" au "Kuna jambo moja bado hujalifanya"

**Uza vyote ulivyonavyo**
"Uza mali zako zote" au "uza vyote unavyomiliki"

**Wagawie masikini**
"Wape hizo pesa masikini"

**Utakuwa na hazina mbinguni**
"Utakuwa na baraka za Mungu mbinguni"

### Luke 18:24

**Kisha Yesu akamwona alivyohuzunika sana**
Kifungu hiki hakipo kwenye maneno mengi ya Kigiriki na mara kadhaa huondolewa kwenye tafsiri za kiingereza.

**Ngamia kupita katika tundu la sindano**
Haiwezekani ngamia kuenea katika tundu la sindano. Kwa hiyo Yesu alitumia mafumbo kuonyesha ni jinsi gani ilivyo ngumu kabisa kwa tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu.

**Tundu la sindano**
Tundu la sindano ni shimo katika sindano ya kushonea ambapo uzi hupita.

### Luke 18:26

**Waliosikia wakasema**
"Watu waliomsikiliza Yesu wakasema"

**Je nani atakayeokoka?**
Inawezekana kuwa walikuwa wanataka jibu. Lakini ni dhahiri kwamba walitumia swali kuonyesha


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

mshangao wao kwa alichokisema Yesu. "Hivyo hakuna atakayeokoka na dhambi" au "Hivyo Mungu hatamuokoa hata mmoja"

**Yanawezekana kwa Mungu**
"inawezekana kwa Mungu kufanya"

### Luke 18:28

**Maelezo yanayounganisha**
Huu ni mwisho wa mazungumzo kuhusu kuingia kwenye ufalme wa Mungu.

**Kila kitu kilicho chetu**
"utajiri wetu wote" au "Mali zetu zote"

**Amini, nawaambia**
Yesu anatumia maelezo haya kuonyesha umuhimu wa kile anachotaka kukisema.

**Hakuna mtu aliyeacha....... ambaye hatapokea**
"kila aliyeacha... atapokea"

**Na katika ulimwengu ujao, uzima wa milele**
"na pia uzima wa milele katika ulimwengu ujao"

### Luke 18:31

**Maelezo yanayounganisha:**
Hii ni sehemu inayofuata ya sehemu ya simulizi inayoanza Yesu haongei tuu na wanafunzi wake tuu.

**Tazama**
Inaonyesha umuhimu wa mabadiliko katika huduma ya Yesu alivyokuwa akienda Yerusalemu kwa mara ya mwisho.

**Yaliyoandikwa na manabii**
"ambayo manabii waliandika"

**Manabii**
Hii inamaanisha Manabii wa Agano la kale.

**Mwana wa Adamu**
Yesu alikuwa anajielezea mwenyewe kama "mwana wa Adamu" na akatumia "yeye" kujielezea mwenyewe.

**Yatatimizwa**
"yatatokea" au "yatatimia"

**Atatiwa mikononi mwa Mataifa**
"Viongozi wa Kiyahudi watamkabidhi kwa Mataifa"

**watamtendea dhihaka na jeuri, na kutemewa mate**
"watamdhihaki, watamtendea vibaya na kumtemea mate"

**Siku ya tatu**
Hii inaelezea siku ya tatu baada ya kufufuka. Japokuwa wanafunzi wake hawakumuelewa, hivyo ni vizuri kutokuongeza maelezo haya unapotafsiri mstari huu.

### Luke 18:34

**Maelezo ya jumla:**
Mstari huu sio sehemu ya simulizi lakini ni mawazo kuhusu sehemu ya simulizi hii.

**Hawakuelewa mambo haya**
"Hawakuelewa kabisa mambo haya"

**Mambo haya**
Hii inaelezea namna ambavyo Yesu atateseka na kufa Yerusalemu, na atafufuka toka kwa wafu.

**Neno hili lilikuwa limefichwa kwao**
"Mungu aliwafanya wasielewe maana ya kile alichokuwa akiwaambia"

**Mambo ambayo aliyasema**
"Mambo ambayo Yesu aliyasema"

### Luke 18:35

**Taarifa ya jumla**
Hii ni sehemu nyingine ya simulizi. Yesu anamponya kipofu alipokuwa anakaribia Yeriko. Mistari hii inatupa historia kuhusu simulizi hii.

**Ikawa**
Neno hili linatumika kuonyesha mwanzo wa simulizi mpya.

**Alipokaribia**
"Alipokuwa karibu"

**Mtu mmoja kipofu alikuwa ameketi**
"kulikuwa na mtu kipofu ameketi" Hapa "mmoja" inaonyesha kuwa mtu huyu alikuwa wa muhimu katika simulizi hii lakini Luka hakutaja jina lale.

**Akiomba, na akasikia**
"Aliomba. aliposikia"

**Wakamwambia**
"Makutano wakamwambia kipofu"

**Yesu wa Nazareti**
Yeso toka mji wa Nazareti uliopo Galilaya.

**Anapiata**
"Alikuwa akimpita"

### Luke 18:38

**Hivyo**
Neno hili linaweka alama ya tukio limetokea kwa sababu kitu fulani kilitokea kwanza. Kwa hivyo makutano walimwambia kipofu kuwa Yesu anapita.

**Akalia kwa sauti**
"akaita kwa sauti" au "akapiga kelele"

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**Mwana wa Daudi**
Yesu alikuwa uzao wa Daudi, Mfalme muhimu kwa Israeli.

**Nihurumie**
"nionee huruma" au "nihurumie"

**Wale**
"watu"

**Anyamaze**
"awe kimya" au "asipige kelele"

**Akazidi kulia kwa sauti**
Hii inaweza kumaanisha alilia kwa sauti zaidi au alilia zaidi kwa kusisitiza.

### Luke 18:40

**Kwamba mtu yule aletwe kwake**
"watu wamlete kipofu kwake"

**nataka kuona**
aweze kuona tena

### Luke 18:42

**Imani yako imekuponya**
"Nimekuponya kwa sababu umeniamini"

**Akamfuata**
"Akaanza kumfuata"

**Akamtukuza Mungu**
"Akampa Mungu utukufu" au "Akamsifu Mungu"

---

## Chapter 19

1 Yesu aliingia na kupita katikati ya Yeriko. 2 Na hapo palikuwa na mtu mmoja aitwaye Zakayo. Ambaye
alikuwa mkuu wa watoza ushuru tena mtu tajiri. 3 Alikuwa anajaribu kumwona Yesu ni mtu wa namna
gani, lakini hakuweza kuona kwa sababu ya umati wa watu, kwa kuwa alikuwa mfupi wa kimo. 4 Hivyo,
alitangulia mbio mbele za watu, akapanda juu ya mkuyu ili aweze kumwona, kwa sababu Yesu alikaribia
kupita njia hiyo. 5 Wakati Yesu alipofika mahali pale, aliangalia juu akamwambia, 'Zakayo, shuka upesi,
maana leo ni lazima nishinde nyumbani mwako.' 6 Akafanya haraka, akashuka na kumkaribisha kwa
furaha. 7 Watu wote walipoona hayo, wakalalamika, wakisema, 'Amekwenda kumtembelea mtu mwenye
dhambi.' 8 Zakayo akasimama akamwambia Bwana, Tazama Bwana nusu ya mali yangu nawapa maskini,
na ikiwa nimemnyang'anya mtu yeyote kitu, nitamrudishia mara nne. ' 9 Yesu akamwambia, 'Leo wokovu
umefika katika nyumba hii, kwa sababu yeye pia ni mwana wa Ibrahimu. 10 Kwa maana Mwana wa Mtu
amekuja kutafuta na kuokoa watu waliopotea. ' 11 Waliposikia hayo, aliendelea kuongea na alitoa mfano,
kwa sababu alikuwa karibu na Yerusalemu, na wao walidhani ya kuwa ufalme wa Mungu ulikuwa karibu
kuonekana mara moja. 12 Hivyo akawaambia, 'Ofisa mmoja alikwenda nchi ya mbali ili apokee ufalme na
kisha aurudi. 13 Aliwaita watumishi wake kumi, akawapa mafungu kumi, akawaambia, 'fanyeni biashara
mpaka nitakaporudi.' 14 Lakini wananchi wake walimchukia na hivyo wakatuma wajumbe waende
kumfuata na kusema, 'Hatutaki mtu huyu atutawale.' 15 Ikawa aliporudi nyumbani baada ya kufanywa
mfalme, akaamuru wale watumishi aliokuwa amewaachia fedha waitwe kwake, apate kujua faida gani
waliyoipata kwa kufanya biashara. 16 Wa kwanza akaja, akasema, `Bwana, fungu lako limefanya mafungu
kumi zaidi. ' 17 Huyo Ofisa akamwambia, Vema, mtumishi mwema. Kwa sababu ulikuwa mwaminifu katika
jambo dogo, utakuwa na madaraka juu ya miji kumi. ' 18 Wa pili akaja, akasema, 'Bwana, fungu lako
limefanya mafungu matano.' 19 Huyo Afisa akamwambia, 'Chukua mamlaka juu ya miji mitano.' 20 Na
mwingine akaja, akasema, `Bwana hii hapa fedha yako, ambayo niliihifadhi salama katika kitambaa, 21
kwa maana niliogopa kwa sababu wewe ni mtu mkali. Unaondoa kile usichokiweka na kuvuna
usichopanda. ' 22 Huyo Ofisa akamwambia, 'Kwa maneno yako mwenyewe, nitakuhukumu, ewe mtumishi
mbaya. Ulijua kwamba mimi ni mtu mkali, nachukua nisichokiweka na kuvuna ambacho sikupanda. 23
Basi, mbona hukuweka fedha yangu katika benki, ili nikirudi niichukue pamoja na faida? 24 Ofisa
akawaambia watu waliokuwa wamesimama hapo, 'Mnyang'anyeni hilo fungu na kumpa yule mwenye
mafungu kumi.' 25 Wakamwambia, `Bwana, yeye ana mafungu kumi. ' 26 'Nawaambia, kila mtu ambaye
anacho atapewa zaidi, lakini ambaye hana, hata kile alicho nacho kitachukuliwa. 27 Lakini hawa maadui
zangu, ambao hawakutaka niwe Mfalme wao, waleteni hapa na kuwaua mbele yangu. '' 28 Baada ya
kusema hayo, aliendelea mbele akipanda kwenda Yerusalemu. 29 Ikawa alipokaribia Bethfage na
Bethania, karibu na mlima wa Mizeituni, aliwatuma wanafunzi wake wawili, 30 akisema: `Nendeni katika
kijiji cha jirani. Mkiingia, mtakuta mwana-punda hajapandwa bado. Mfungueni, mkamlete kwangu. 31
Kama mtu akiwauliza, `Mbona mnamfungua? ' Semeni, "Bwana anamhitaji. '' 32 Wale waliotumwa
wakaenda wakamwona mwana-punda kama Yesu alivyokuwa amewaambia. 33 Walipokuwa wanamfungua
mwana punda wamiliki wakawaambia, 'Kwa nini mnamfungua mwana punda huyu?' 34 Wakasema,
`Bwana anamhitaji. ' 35 Basi, wakampelekea Yesu, wakatandika nguo zao juu ya mwana punda na
wakampandisha Yesu juu yake. 36 Alipokuwa akienda watu wakatandaza mavazi yao barabarani. 37
Alipokuwa anateremka mlima wa Mizeituni, jumuiya yote ya wanafunzi wakaanza kushangilia na
kumtukuza Mungu kwa sauti kubwa, kwa sababu ya mambo makuu waliyoyaona, 38 wakisema, 'Ndiye
mbarikiwa Mfalme ajaye kwa jina la Bwana! Amani mbinguni, na utukufu juu!' 39 Baadhi ya Mafarisayo
katika mkutano wakamwambia, Mwalimu, wanyamazishe wanafunzi wako. ' 40 Yesu akajibu, akasema,
`Nawaambieni, kama hawa wakinyamaza, mawe yatapaza sauti. ' 41 Yesu alipoukaribia mji aliulilia, 42
akisema, laiti ungelijua hata wewe, katika siku hii mambo ambayo yanayokuletea amani! Lakini sasa
yamefichika machoni pako. 43 Kwa kuwa siku zinakuja ambapo adui zako watajenga boma karibu na
wewe, na kukuzunguka na kukukandamiza kutoka kila upande. 44 Watakuangusha chini wewe na watoto
wako. Hawatakuachia hata jiwe moja juu ya jingine, kwa sababu haukutambua wakati Mungu alipokuwa
anajaribu kukuokoa'. 45 Yesu aliingia Hekaluni, akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza, 46
akiwaambia, "Imeandikwa, 'Nyumba yangu itakuwa nyumba ya sala,' lakini ninyi mmeifanya kuwa pango
la wanyang'anyi". 47 Kwa hiyo, Yesu alikuwa akifundisha kila siku hekaluni. Makuhani wakuu na walimu
wa Sheria na viongozi wa watu walitaka kumuua, 48 lakini hawakuweza kupata njia ya kufanya hivyo, kwa
sababu watu wote walikuwa wakimsikiliza kwa makini.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Luka 19 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

Luka 19:11-27 ni mfano mmoja. Mfano huu unawafundisha Waumini jinsi ya kuishi katika Ufalme wa Mungu utakapokuja. Wasikilizaji wa Yesu waliamini kimakosa kwamba ufalme huo ungeonekana haraka sana. Ingawa ufalme unaweza kuonekana wakati wowote, maneno haya hayana maana ya kusema ufalme utatokea leo au kesho, lakini itawezekana.

### Dhana maalum katika sura hii

### "Mwenye dhambi"

Mafarisayo hutaja kundi la watu kuwa "wenye dhambi." Viongozi wa Kiyahudi walidhani watu hawa walikuwa wenye dhambi, lakini kwa kweli viongozi wenyewe walikuwa pia wenye dhambi. Hali hii inaweza kuchukuliwa kama kinaya. and

### Usimamizi

Ingawa neno hili haitumiwi katika sura hii, ni neno kubwa katika mafundisho haya. Usimamazi ni kuwa mwaminifu katika vitu umepewa kwa kuchungu. Mungu anatarajia kila mtu kutumia vipaji alivyompa. Hii sio tu vipaji au uwezo ambao Mungu amempa mwanadamu, lakini maisha ya mtu anayoyaishi katika matarajio ya uzima wa milele. Mungu pia anatarajia watu kuishi katika matarajio ya kurudi kwa Yesu.

### Mwana-punda

Jinsi ambavyo Yesu aliingia Yerusalemu, akiwa amepanda mnyama, ilikuwa sawa na vile ambavyo mfalme angeingia katika mji baada ya ushindi mkubwa. Na kwa wafalme wa Israeli, ilikuwa desturi kupanda punda badala ya farasi. Mathayo, Marko, Luka, na Yohana wote waliandika juu ya tukio hili, lakini hawakuandika maelezo sawa. Mathayo aliandika kuhusu kuwepo kwa punda na mwana-punda, lakini haijulikani ni yupi ambaye Yesu alipanda. Ni bora kutafsiri kila moja ya vifungu hivi kama inavyoonekana katika ULB bila kujaribu kuwafanya wote kusema jambo sawa. (Tazama:Mathayo 21:1-7 na Yohana 12:14-15)

### Kutandaza mavazi na matawi

Hii ilikuwa njia ya kumheshimu mfalme.

### "[Yesu] akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza"

Imeandikwa kama Yesu alisafisha hekalu kwa kufukuza wafanyabiashara wasio watu wa Mungu kutoka hekaluni. Tukio hili linaonyesha mamlaka ambayo Yesu alikuwa nayo juu ya hekalu na taifa la Israeli. and )

---

### Luke 19:1

**Taarifa ya jumla**
Hii ni sehemu iliyofuata ya simulizi. Zakayo anatambulishwa kwenye simulizi. mstari wa kwanza unaonyesha historia ya safari ya Yesu.

**Tazama kulikuwa na mtu pale**
Neno "tazama" linatuonyesha mtu mpya kwenye simulizi. Lugha yako inaweza kuwa na na njia ya kufanya hivi. "Kulikuwa na mtu ambaye alikuwa"

**Alikuwa mkuu wa watoza ushuru na alikuwa tajiri.**
Hii ni historia ya Zakayo.

### Luke 19:3

**Alijaribu**
"Zakayo alijaribu"

**Kwa sababu alikuwa mfupi wa kimo**
"kwa kuwa alikuwa mfupi"

**Mti wa mkuyu**
"Mti wa mkuyu." unazalisha matunda madogo ya duara yenye sentimita zipatazo 2.5.

### Luke 19:5

**Mahali**
"kwenye mtui" au "alipokuwa Zakaria"

**Alikwenda kumtembelea mtu mwenye dhambi**
"Yesu alikwenda kwenye nyumba ya mwenye dhambi kumtembelea"

**Mwenye dhambi**
"mwenye dhambi hasa"

### Luke 19:8

**Bwana**
Hii inamzungumzia Yesu

**Wokovu umekuja katika nyumba hii**
"Mungu ameokoa nyumba hii"

**Nyumba hii**
neno "nyumba" inamaanisha watu waishio kwenye nyumba hiyo au familia.

**Yeye pia**
"huyu mtu pia" au "Zakayo pia"

**Mwana wa Ibrahimu**
Inamaanisha 1)"kizazi cha Ibrahimu" na 2)"mtu aliyekuwa na imani kama ya Ibrahimu."

**Watu waliopotea**
"watu waliokua mbali na Mungu" au "wale ambao kutokana na dhambi wako mbali na Mungu"

### Luke 19:11

**Taarifa ya jumla**
Yesu alianza kuwaambia makutano mfano. mstari wa kumi na moja unaonyesha historia kwa nini Yesu aliwaambia mfano huo.

**kwamba ufalme wa Mungu ulikuwa karibu kuonekana mara moja.**
"kwamba Yesu ataanza kumiliki maramoja kwenye ufalme wa Mungu"

**Ofisa mmoja**
"Mtu mmoja ambaye alikuwa mmoja wa viongozi" au "mtu mmoja toka kwenye familia ya muhimu." "Mtu wa muhimu"

**Kupokea ufalme**
Hii ni picha ya mfalme mdogo kumwendea mfalme mkubwa. Mfalme mkubwa atampa mfalme mdogo mamlaka ya kuongoza nchi yake mwenyewe.

### Luke 19:13

**Aliwaita**
Ofisa aliwaita

**Akawapa mafungu kumi**
"akawapa kila mtu fungu moja"

**Mafungu kumi**
Fungu ni gramu 600. kila fungu linathamani ya malipo ya miezi minne ya mtu, "Sarafu kumi" au "kiasi kikubwa cha pesa"

**Fanya biashara**
"fanya biashara na pesa hizi" au "tumia hizi pesa ili upate zaidi"

**Wananchi wake**
Watu wa nchi yake"

**Mabalozi**
"wawakilishi" au "wajumbe"

**Ikawa**
Neno hili limetumika kuonyesha umuhimu wa tukio kwenye simulizi. Kama lugha yako ina namna nyingine ya kufanya hivi unaweza ukaitumia hapa.

**Baada ya kuupokea ufalme**
"Baada ya kuwa Mfalme"

**Waitwe kwake**
"kwenda kwake"

**Mmetengeneza faida kiasi gani**
"ni pesa kiasi gani waliipata"

### Luke 19:16

**Wa kwanza**
"Mtumishi wa kwanza"

**Akaja mbele yake**
"Akaja mbele ya Afisa"

**Umefanya vyema**
"wewe umefanya vyema" Lugha yako inaweza kutafsiri kifungu hiki kwamba mwajiri anatumia kuonyesha kiridhika, kama vile "kazi nzuri."

### Luke 19:18

**Fungu lako, Bwana, limefanya mafungu matano.**
"Bwana kwa pesa ulizonipa, nimezalisha mara tano"

**Chukua mamlaka juu ya miji mitano**
"Utakuwa na mamlaka juu ya miji mitano"

### Luke 19:20

**Mtu mkali**
'Mtu wakali' au 'mtu ambaye anatarajia mengi toka kwa watumishi wake'

**Unachukua kile usichokiweka**
Ni fumbo linaloelezea mtu mkorofi. "unaondoa kitu asichokiweka" au "unachukua kitu ambacho sio chako."

**Kuvuna kile usichopanda**
"Kuvuna usichokipanda." Mtumishi alikuwa anamfananisha bwana wake na mkulima anayechukua chakula ambacho mtu mwingine alikipanda.

**Kuvuna**
"kukusanya" au "kuweka"

### Luke 19:22

**Kwa maneno yako mwenyewe**
"Kutokana na ulichokisema"

**Kwamba mimi ni mtu mbaya, nachukua**
Afisa alirudia maneno aliyoyasema mtumishi juu yake. Hakusema kuwa ilikuwa kweli.

**Mtu mkali**
"mtu mkorofi"

**Kwa nini hukuweka pesa yangu...... faida?**
Afisa alitumia swali ili kumkemea Mtumishi dhalimu. "Ungeweka pesa yangu..... faida."

**Weka pesa yangu benki**
"Kopesha pesa zangu benki" Tamaduni ambazo hazina benki zaweka kutafsiri kuwa "Acha mtu aazime pesa zangu."

**Benki**
Benki ni biashara salama ya kuweka pesa za watu. Benki huwakopesha watu pesa kwa faida. Hivyo inalipa pesa ya ziada au faida kwa watu wanaoweka pesa zao benki.

**Nitakusanya na faida**
"Ningekusanya kiasi hicho cha fedha pamoja na faida iliyopatikana" au "ningepata faida"

**Faida**
Faida ni pesa ambayo benki humlipa mtu anayeweka pesa zake katika benki.

### Luke 19:24

**Afisa**
Afisa aliyekujakuwa mfalme. Tafsiri hivi kwa maneno ambayo yataeleweka kwa wasomaji.

**Waliokuwa wamesimama hapo**
"Watu waliokua wamesimama karibu nao"

### Luke 19:26

**Taarifa ya jumla**
Yesu amemaliza kuwaambia mfano wake na sasa anatoa mawazo juu ya makutano nyumbani kwa Zakayo.

**Nawaambia**
Hii ilikuwa kauli ya mfalme. Watafsiri wengine wanaweza kutaka kuanza mstari huu kwa kusema "Na mfalme akajibu, 'Nawaambia ninyi" au Lakini mfalme akasema, Namwaambia hivi"

**Kila aliyenacho**
"kila mtu atakayetumia vizuri alichopewa" au "kila mtu atakayetumia vizuri vitu nilivyompa"

**Atapewa zaidi**
"Ntampa zaidi"

**Toka kwake ambaye hana**
"Toka kwa mtu ambaye hatumii vizuri kile nilichompa"

**Kitaondolewa**
"Nitakichukua kutoka kwake"

**Hawa adui zangu**
Kwa kuwa adui zake hawakuwepo pale, lugha nyingine zawezasema "wale adui zangu."

### Luke 19:28

**Maelezo yanayounganisha**
Huu ni mwisho wa simulizi kuhusu Zakaria. Mstari huu unaelezea aliyoyafanya Yesu baada ya simulizi hii.

**Alipomaliza kusema maneno haya**
"Yesu alipomaliza kusema maneno haya"

**Kwenda Yerusalemu**
Yerusalemu ilikuwa kama mita 975 juu ya Yeriko.

### Luke 19:29

**Maelezo ya Jumla**
Hii ni sehemu nyingine ya simulizi. Yesu anakaribia Yerusalemu.

**Ikawa**
Aya hii imetumika kuonyesha mwanzo wa simulizi mpya. Kama lungha yako ina njia nyingine ya kusema hivi unaweza ukatumia hivyo.

**Alipofika karibu**
Neno "yeye" linamaanisha Yesu. Wanafunzi wake walisafiri pamoja naye.

**Bethfage**
Bethfage kilikuwa kijiji kwenye mlima wa Mizeituni, ambayo imepita katikati ya bonde la Kidron toka Yerusalemu.

**Mlima ulioitwa Mizeituni**
"Mlima ulioitwa Mlima wa Mizeituni" au Mlima ulioitwa "mlima wa mti wa Mizeituni"

**Mwanapunda**
"Punda mdogo" au "myama mdogo wa kumuendesha"

**Ambaye hajapandwa bado**
"ambae hamna mtu aliyemtumia"

### Luke 19:32

**Wale waliotumwa**
"Wale waliotumwa na Yesu" au "Wanafunzi wawili waliotumwa na Yesu"

**Walitandika mavazi yao juu ya mwanapunda**
"waliweka nguo zao juu ya mwanapunda." Mavazi ni nguo. Hapa inamaanisha mavazi ya nje au nguo.

**Walitandaza mavazi yapo**
"watu walitandaza mavazi yao" au "wengine walitandaza mavazi yao." Hii ni ishara ya kuonyesha heshima kwa mtu fulani.

### Luke 19:37

**Alipokuwa nateremka katibu**
"Yesu alipokaribia" au "Yesu alipokuwa anakaribia." Wanafunzi wa Yesu walikuwa wakisafiri pamoja naye.

**Mambo makubwa waliyoyaona**
"Mambo makubwa waliyoyaona yakifanywa na Yesu"

**Amebarikiwa Mfalme**
Walisema haya kuhusu Yesu

**Kwa jina la Bwana**
Hapa "jina" linaelezea nguvu na mamlaka. Pia "Bwana" linamaanisha Mungu

**Utukufu juu**
"Acha kila mtu amtukuze yeye aliye juu sana" au "acha kila mtu amsifu aliye juu"

### Luke 19:39

**Wanyamazishe wanafunzi wako**
"waambie wanafunzi wako waache kufanya mambo haya"

**Nawaambieni**
Yesu alisema hivi kuonyesha msisitizo wa alichotaka kukisema baadae.

**Hawa wakinyamaza**
Tafsiri zingine zinahitaji kuweka wazi kile ambacho Yesu alikuwa ikimaanisha pale aliposema 'Hapana, mimi sitawakemea, kwa maana hwa watu wakikaa kimya.'

**Mawe yatapaza sauti**
"Mawe yatasifu"

### Luke 19:41

**Kukaribia**
"Kusogelea" au "kuwa karibu"

**Mji**
Hii inamaanisha Yerusalemu.

**Aliulilia**
Neno "ule" linamaanisha mji wa Yerusalemu, lakini linawakilisha watu wanaoishi ndani ya mji huo.

**Laiti ungelijua**
Huu ni mshangao. Yesu alionyesha huzuni yake kwamba watu wa Yerusalemu hawakujua mambo haya. Maelezo haya yanaweza kuongezwa mwishoni mwa sentensi "hivyo mngeweza kuwa na amani." "Natamani mtambue au "nina huzuni kwa kuwa hamjui."

**Wewe**
Neno 'wewe' ni umoja kwa sababu Yesu alikuwa akizungumza na mji. Lakini kama hii haitakuwa na uhalisia katika lugha yako, unaweza kutumia wingi wa "wewe" kwa kutaja watu wa mji.

**Yanmefichwa machoni pako**
"Hamuawezi kuona tena" au "hamkuweza kufahamu"

### Luke 19:43

**Maelezo yanayounganisha**
Yesu akaendelea kuongea.

**Kwa**
Kilichofuata ni sababu ya Yesu kuhuzunika.

**Siku zinakuja juu yako**
Hii inaonyesha kwamba wangepitia nyakati ngumu. Baadhi ya lugha hawaongelei juu ya wakati ujao. 'Katika siku zijazo mambo haya yatatokea kwako' au 'hivi karibuni utavumilia wakati mgumu.'

**Wewe**
neno 'wewe' ni umoja kwa sababu Yesu alikuwa akizungumza na mji. Lakini kama hii haitakuwa na uhalisia katika lugha yako, unaweza kutumia wingi wa "wewe" kwa kutaja watu wa mji.

**Boma**
Boma ni ukuta unaolinda watu wasitoke nje ya mji.

**Watakuangusha chini kwenye ardhi**
Kwa kuwa Yesu alikuwa akiongea na mji, hii inaelezea ukuta na wajenzi wa ukuta wa mji. "Wataharibu kuta zako" au "Wataharibu kuta zako."

**Na watoto wako pamoja nawe**
Hii inaelezea watu wanaoishi kwenye mji. "na watawaua watu wa kwenye mji."

**Hawataacha jiwe moja juu ya lingine**
Huu ni mfano unaoelezea namna ambavyo maadui wataharibu kabisa mji uliojengwa kwa mawe. "Hawataacha jiwe lolote kwenye eneo hilo."

**Haukulitambua hilo**
"haukulijua"

### Luke 19:45

**Maelezo yanayounganisha:**
Hili ni tukio lingine kwenye sehemu hii ya simulizi. Yesu aliingia hekaluni.

**Kufukuza**
"Kutoa nje" au "kutoa kwa nguvu nje"

**Imeandikwa**
Hii imenukuliwa toka Isaya. "Maandiko yanasema" au "Nabii aliandika maneno haya kwenye maandiko"

**Nyumba yangu**
Neno "yangu" inamuelezea Mungu na "nyumba" linaelezea hekalu.

**Nyumba ya sala**
"sehemu ambayo watu wananiomba"

**Pango la wanyang'anyi**
"sehemu ambayo wanyang'anyi wanajificha." "Kama pango la wanyang'anyi."

### Luke 19:47

**Maelezo yanayounganisha.**
Huu ni mwisho wa sehemu ya simulizi hii. Aya hizi zinaelezea kuhusu hatua inayoendelea baada ya sehemu kuu ya simulizi kuisha.

**Hekaluni**
'Hekaluni' au 'kwenye hekalu'

**Makuhani wakuu**
'Mwenye cheo cha juu cha makuhani' 'makuhani muhimu zaidi '

**Walikuwa wakisikiliza kwa makini**
"Walisikiliza kwa makini kile alichokuwa akikisema Yesu"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 20

1 Ikawa siku moja, Yesu alipokuwa akiwafundisha watu Hekaluni na kuhubiri injili, makuhani wakuu na
walimu wa Sheria walimwendea pamoja na wazee. 2 Walizungumza, wakimwambia, 'Tuambie ni kwa
mamlaka gani unafanya mambo haya? Au ni nani huyo ambaye amekupa mamlaka haya? " 3 Naye akajibu,
akawaambia, 'Nami pia nitawauliza swali. Niambieni 4 ubatizo wa Yohana. Je, ulitoka mbinguni ama kwa
watu? ' 5 Lakini wakajadiliana wao kwa wao, wakisema, 'Tukisema, `litoka mbinguni, atatuuliza, ` Basi,
mbona hamkumwamini?' 6 Na tukisema; ilitoka kwa wanadamu; watu wote hapa watatupiga mawe,
maana wote wanaamini kwamba Yohana alikuwa nabii. ' 7 Basi, wakamjibu ya kwamba hawakujua
ilikotoka. 8 Yesu akawaambia, '"Wala mimi siwaambii ninyi ni kwa mamlaka gani ninafanya mambo haya."
9 Aliwaambia watu mfano huu, "Mtu mmoja alipanda shamba la mizabibu, akalikodisha kwa wakulima wa
mizabibu, na akaenda nchi nyingine kwa muda mrefu. 10 Kwa muda uliopangwa, alimtuma mtumishi kwa
wakulima mizabibu, kwamba wampe sehemu ya matunda ya shamba la mizabibu. Lakini wakulima wa
mzabibu wakampiga, wakamrudisha mikono- mitupu. 11 Kisha akamtuma tena mtumishi mwingine na nao
wakampiga, kumtendea vibaya, na wakamrudisha mikono- mitupu. 12 Alimtuma tena wa tatu na nao
wakamjeruhi na kumtupa nje. 13 Hivyo bwana wa shamba akasema, 'Nitafanya nini? Nitamtuma
mwanangu mpendwa. Labda watamheshimu. ' 14 Lakini wakulima wa mzabibu walipomwona, walijadili
wao kwa wao wakisema, `Huyu ndiye mrithi. Tumuue, ili urithi wake uwe wetu. ' 15 Wakamtoa nje ya
shamba la mizabibu na kumuua. Je bwana shamba atawafanya nini? 16 Atakuja kuwaangamiza wakulima
wa mzabibu, na atawapa shamba hilo wengine". 'Nao waliposikia hayo, wakasema, 'Mungu amekataa' 17
Lakini Yesu akawatazama, akasema, "Je andiko hili lina maana gani? 'Jiwe walilolikataa wajenzi, limekuwa
jiwe la pembeni'? 18 Kila mtu aangukaye juu ya jiwe hilo, atavunjika vipande vipande. Lakini yule ambaye
litamwangukia, litamponda. ' 19 Hivyo waandishi na wakuu wa makuhani walitafuta njia ya kumkamata
wakati huohuo, walijua kwamba alikuwa amesema mfano huu dhidi yao. Lakini waliwaogopa watu. 20
Walimuangalia kwa makini, wakatuma wapelelezi waliojifanya kuwa watu wa haki, ili wapate kupata kosa
kwa hotuba yake, ili kumpelekakwa watawala na wenye mamlaka. 21 Nao wakamwuliza, wakisema,
"Mwalimu, tunajua kwamba unasema na kufundisha mambo ya kweli na si kushawishiwa na mtu yeyote,
lakini wewe hufundisha ukweli kuhusu njia ya Mungu. 22 Je, ni halali kwetu kulipa kodi kwa Kaisari, au
la?" 23 Lakini Yesu alitambua mtego wao, akawaambia, 24 "Nionyesheni dinari. Sura na chapa ya nani ipo
juu yake?" Walisema, ' "Ya Kaisari." 25 Naye akawaambia, 'Basi, mpeni Kaisari yaliyo yake Kaisari, na
Mungu yaliyo yake Mungu.' 26 Waandishi na wakuu wa makuhani hawakuwa na uwezo wa kukosoa kile
alichosema mbele ya watu. Wakastaajabia majibu yake na hawakusema chochote. 27 Baadhi ya
Masadukayo wakamwendea, wale ambao wanasema kwamba hakuna ufufuo, 28 wakamwuliza, wakisema,
"Mwalimu, Musa alituandikia kwamba kama mtu akifiwa na ndugu mwenye mke ambaye hana mtoto basi
anapaswa kumchukuna mke wa ndugu yake na kuzaa nae kwa ajili ya kaka yake. 29 Kulikuwa na ndugu
saba Wa kwanza alioa, akafa bila kuacha mtoto, 30 na wa pili pia. 31 Wa tatu akamchukua vilevile, vivyo
hivyo wa saba hakuacha watoto na akafa. 32 Baadaye yule mwanamke pia akafa. 33 Katika ufufuo
atakuwa mke wa nani? Maana wote saba walikuwa wamemwoa. ' 34 Yesu akawaambia, "Wana wa
ulimwengu huu huoa na kuolewa. 35 Lakini wale wanastaohili kupokea ufufuo wa wafu na kuingia uzima
wa milele hawaoi wala hawaolewi. 36 Wala hawawezi kufa tena, kwa sababu huwa sawasawa na malaika
na ni watoto wa Mungu, wana wa ufufuo. 37 Lakini hiyo wafu wanafufuliwa, hata Musa alionyesha mahali
katika habari za kichaka, pale alimwita Bwana kama Mungu wa Ibrahimu na Mungu wa Isaka na Mungu
wa Yakobo. 38 Sasa, yeye si Mungu wa wafu, bali wa walio hai, kwa sababu wote huishi kwake. " 39
Baadhi ya walimu wa Sheria wakamjibu, 'Mwalimu, umejibu vema. ' 40 Hawakuthubutu kumwuliza
maswali mengine zaidi. 41 Yesu akawaambia, "Ki vipi watu wanasema kwamba Kristo ni mwana wa
Daudi? 42 Maana Daudi mwenyewe anasema katika Zaburi: Bwana alimwambia Bwana wangu: Keti
mkono wa kulia, 43 mpaka niwaweke adui zako chini ya miguu yako. ' 44 Daudi anamwita Kristo 'Bwana',
basi atakuwaje mwana wa Daudi?" 45 Watu wote walipokuwa wakimsikiliza akawaambia wanafunzi wake,
46 'Jihadharini na waandishi, wapendao kutembea wamevaa mavazi marefu, na wapenda salamu maalum
sokoni na viti vya heshima katika masinagogi, na maeneo ya heshima karamuni. 47 Wao pia hula nyumba
za wajane, na wanajifanya wanasali sala ndefu. Hawa watapokea hukumu kubwa zaidi. '


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

# Luka 20 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

Baadhi ya tafsiri hupendelea kuweka mbele kidogo nukuu za Agano la Kale. ULB na tafsiri nyingine nyingi za Kiingereza huingiza mistari ya 20:17, 42-43, ambayo ni nukuu kutoka Agano la Kale.

### Dhana maalum katika sura hii

### Mtego

Sura hii ina maswali mawili yaliyopangwa ili kumkamata mtu anayekubali kitu ambacho hataki kusema. Yesu anauliza swali kwa Mafarisayo ambalo linawatega kwa kuwalazimisha kukiri kwamba wanaamini Yohana Mbatizaji alikuwa nabii au kuwakasirisha Wayahudi kwa kukataa hili. Viongozi walijaribu kumtega Yesu kwa kumuuliza kuhusu kulipa kodi kwa serikali ya Kirumi. Kujibu ndiyo kungewakasirisha Wayahudi na kujibu hapana kungewakasirisha Warumi.

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

### Kitendawili

Kitendawili ni taarifa inayoonekana kuwa ya ajabu, ambayo ni kana kwamba inajikana yenyewe, lakini sivyo. Katika sura hii, Yesu ananukuu Zaburi ambayo inasema Daudi anamwita mwanawe "bwana," yaani, "mkuu." Hata hivyo, kwa Wayahudi, mababu walikuwa wakubwa kuliko uzao wao. Katika kifungu hiki, Yesu anajaribu kuwaongoza wasikilizaji wake kuelewa kweli kwamba Masihi mwenyewe atakuwa Mungu, na kwamba yeye mwenyewe ndiye Masihi. (Luka 20:41-44).

---

## Luke 20:1

**Maelezo yanayounganisha**
Makuhani wakuu, mafarisayo na wazee walimuuliza Yesu hekaluni.

**Ikawa**
neno hili linaonyesha mwanzo wa sehemu mpya ya simulizi.

## Luke 20:3

**Taarifa ya jumla**
Yesu anawajibu wakuu wa makuhani, mafarisayo na wazee.

**aliwajibu na kuwaambia**
"Yesu akawajibu"

**Ilitoka mbinguni au kwa watu?**
Yesu alijua mamlaka ya Yohana ilitoka mbinguni, Aliuliza swali ili vingozi wa kiyahudi waseme wanavyofikiri kwa wote waliowasikiliza. "mnafikiri mamlaka ya Yohana yalitoka mbinguni au kwa wanadamu?" au "mnadhani Mungu alimwambia Yohana abatize watu au watu walimwambia afanye hivyo?"

**Toka mbingini**
"toka kwa Mungu" Wayahudi waliepuka kumtaja Mungu kama "Yawe". Mara nyingi wanatumia neno "Mbingu" kumuelezea

## Luke 20:5

**Walijadiliana**
"Walijadili" au "walitafakari jibu lao"

**"tukisema imetoka mbinguni'**
Lugha nyingine zinatumia nukuu ya moja kwa moja. "Kama tukisema mamlaka ya Yohana yalitoka Mbinguni"

**Toka mbinguni**
"Toka kwa Mungu" inategemea na namna ambavyo swali lilitafsiriwa kwenye mistari iliyopita, hii inaweza kutafsiriwa kama "Mungu alifanya" au "Mungu alimpa mamlaka"

**Atasema**
Yesu atasema

**kutupia mawe**
"Kutuua kwa kutupiga mawe" Sheria ya Mungu imeamuru watu wake kuwapiga mawe watu wanaomdhihaki yeye au manabii zake.

## Luke 20:7

**Ndipo wakamjibu**
"ndipo wakuu wa makuhani na mafarisayo na wazee wakamjibu" Neno "ndipo" linaonyesha tukio limetokea kutokana na tukio limgine lililotokea kabla.

**Walijibu kuwa hawakujua ilikotoka**
Wakasema, "hatujui ilipotoka"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**Imetoka wapi**
"Yohana mbatizaji alitoka wapi." Mamlaka aliyokuwa nayo Yohana ya kubatiza yalitoka wapi" au "nani alimpa mamlaka Yohana ya kubatiza watu."

**Nami sitawaambia**
"Na sitawaambia" au "kama ambavyo hamniambii basi na mimi siwaambii"

### Luke 20:9

**Taarifa ya jumla**
Yesu alaanza kuwaambia mfano watu waliokuwa hekaluni

**Aliwakodisha wakulima wa mzabibu**
"aliwaruhusu baadhi ya wakulima wa mizabibu watumie kwa mabadilishano ya pesa" au "aliwaruhusu wakulima wa mizabibu walitumie ba baadae wamlipe pesa"

**Wakulima wa mizabibu**
Watu ambao hupanda na kukuza mizabibu. "wakulima wa mizabibu"

**matunda ya shambani**
"Baadhi ya mizabibu" au "baadhi ya walichozalisha kwenye shamba." Pia inaweza kuelezea vitu amabavyo vinatokana na zabibu au pesa zinazotokana na mauzo ya zabibu

**Wakamrudisha mikono mitupu**
"wakamrudisha bila kumlipa" au "wakamrudisha bila mizabibu"

### Luke 20:11

**Wakamtendea vibaya**
"Wakamdhalilisha"

**Wakamjeruhi**
"wakamsababishia majeraha"

**Na wa tatu**
Hata mtumishi wa tatu au na mtumishi mwingine. Neno

### Luke 20:13

**Wakati Wakulima wa mizabibu walipomuona**
"wakati wakulima walipomuona mtoto wa mwenye shamba"

**Tumuue**
Walisema hivyo ili kutiana moyo kuua

### Luke 20:15

**Maelezo yanayounganisha**
Yesu alimaliza kuwaambia mfano wake kwa makutano.

**Walimtupa nje ya shamba**
"Wakulima wa mzabibu walimtoa kwa nguvu mwana wa mwenye shamba nje ya shamba

**Je bwana shamba atawafanya nini?**
Yesu alitumia maswali ili wasikilizaji wake wawe makinijuu ya atakayoyafanya mwenye shamba. "sasa sikilizeni je Bwana shamba atawafanya nini."

**Yasitokee haya**
"Mungu ayaepushe yasitokee haya" au "Isitokee kamwe" Watu wanaelewa mfano huu kuwa unamaanisha kuwa Mungu atawaondoa Yerusalemu kwa kuwa wamemkataa Mesia. Wanaelezea kwa nguvu shauku yao kuwa jambo hili baya lisitokee.

### Luke 20:17

**Maelezo yanayounganisha**
Yesu anaendelea kuwafundisha makutano

**Yesu akawaangalia**
"Lakini yesu akawatazama" au "Lakini Yesu akawaangalia moja kwa moja." Alifanya hivi ili wamuelewe alichokuwa anakisema.

**Andiko hili lina maana gani?**
"Andiko hili linaelezea nini?" Yesu alitumia maswali kuwauliza makutano. "Mnatakiwa kuwa na uwezo kuelewa aandiko hili"

**Jiwe walilolikataa waashi limekuwa jiwe la msingi**
Fumbo hili ni unabii toka kitabu cha Zaburi kuhusu namna watu watakavyomkataa Masiha.

**Jiwe walilolikataa**
"Jiwe walilolikataa waashi wakisema halikuwa zuri kwa ajili ya ujenzi." Kipindi hicho watu walijenga kuta za nyumba na majengo mengine kwa kutumia mawe.

**Limekuwa jiwe la msingi**
Hili lilikuwa jiawe la muhimu kwa kufanya jengo liwe imara. "Limekuwa jiwe la Msingi" au "limekuwa jiwe la Muhimu"

**Kila atakayeanguka kwenye jiwe hilo.**
"Yeyote atakayeanguka kwenye jiwe hilo". Fumbo hili ni unabii kuhusu kitakachotokea kwa wote watakaomkataa Mesia.

**Atavunjika vipande vipande**
"Atavunjika vipande vipande." Haya ni matokeo ya kuanguka kwenye jiwe.

**Lakini kwa yeyote ambaye litamwangukia**
"Lakini kwa yeyote ambaye jiwe litamwangukia." Fumbo hili linaonyesha unabii kuhusu Mesia atakapowahukumu waliomkataa.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

### Luke 20:19

**Walitaka kumkamata**
"walitafta njia ya kumkamata Yesu"

**Wakati huo huo**
Mda huo huo

**Walikuwa wanawaogopa watu**
Hii ndiyo sanbabu hawakumkamata Yesu moja kwa moja. Watu walimuheshimu Yesu na viongozi wa dini waliogopa kile ambacho watu wangekifanya ikiwa wangemkamata Yesu. "Lakini hawakumkamata kwa kuwa waliwaogopa watu."

**Walituma wapelelezi**
"Mafarisayo na Makuhani wakuu walituma wapelelezi kumuangalia Yesu"

**Kama watapata kosa kwenye hotuba zake**
"kwa kuwa walitaka kumtuhumu Yesu kwa kusema jambo baya"

**ili kumpeleka**
"ili kumpeleka kwa" au "ili kumkabidhi kwa"

**Kwa uongozi na mamlaka ya Gavana**
Kuongoza na mamlaka ni njia mbili za kuelezea kitu kimoja.

### Luke 20:21

**Maelezo yanayounganisha.**
Hapa ni mwanzo wa tukio linalofuata kwenye sehemu ya simulizi hii. Muda sasa umepita tangu Yesu alipoulizwa maswali hekaluni na Makuhani wakuu. Wapelelezi sasa wanamuuliza Yesu.

**Hawakushawishiwa na mtu yeyote.**
Inamaanisha 1)wewe sema ukweli hata kama watu wa muhimu hwatapenda" au 2)"usimpendelee mtu mmoja juu ya mwingine."

**Lakini fundisha ukweli kuhusu njia ya Mungu**
Hii ni sehemu waliyosema wapelelezi kwamba wanafahamu kuhusu Yesu.

**Je ni halali kwetu kulipa kodi kwa Kaisari.**
Walitegemea kuwa Yesu atasema "ndio" au "hapana." Angesema "ndio" Wayahudi wangemkasirikia kwa kusema walipe kodi kwa serikali ya kigeni. Angesema "hapana" viongozi wa dini wangewaambia warumi kuwa Yesu aliawafundisha watu kuvunja sheria za warumi.

**Ni halali**
Walimuuliza Yesu kuhusu sheria za Mungu na sio sheria za Kaisari. "shheria zetu zinaruhusu."

**Kaisari**
kwa sababu kaisari alikuwa kiongozi wa serikali ya Roma hivyo wanaielezea serikali ya Roma kwa jina la Kaisari.

### Luke 20:23

**Yesu alielewa mtego wao**
"lakini Yesu alitambua mtego wao ulivyokuwa" au " lakini Yesu alione kuwa walikuwa wanajaribu wanamtega" neno "wao" linamaanisha wapelelezi"

**Dinari**
Hii ni sarafu ya Kirumi yenye thamani ya mshahara wa siku.

**Ni sura na chapa ya nani ipo juu yake**
Yesu alitumia swali kuwajibu waliokuwa wanamtega.

**Sura na chapa**
"picha na jina"

### Luke 20:25

**Maelezo yanayounganisha**
Hapa ni mwisho wa tukio hili kuhusu wapelelezi na sehemu ya simulizi inayoanza

**Aliwaambia**
"Kisha Yesu akawaambia"

**Kaisari**
Hapa "Kaisari" anamaanisha serikali ya Rumi

**Hatukuweza kukosoa alichokisema**
"hatukuweza kupata chochote kibaya kwa aliyoyasema"

**Wakastaajabu**
"Walishangaa" au wali

### Luke 20:27

**Taarifa ya jumla**
Hii ni sehemu inayofuata ya simulizi. hatufahamu ilitokea wapi, japo inaweza kuwa wapo hekaluni. Yesu anaongea na Masadukayo.

**Waliokuwa wanasema kuwa hamna ufufo**
Maneno haya yanatambulisha Mawadukayo ambao ni kundi la Wayahudi wanaosema hakuna atakayefufuliwa toka kwa wafu. Haimaanishi kuwa baadhi ya masadukayo wanaamini kuwa kuna ufufuo na wengine hawaamini.

**Ikiwa mtu akifiwa na kaka yake aliyekuwa na mke na hana mtoto.**
"Ikiwa mtu akifiwa na kaka yake wakati ana mke lakini hawana watoto"

**mtu atamchukua mke wa kaka yake**
"mtu atamuoa mjane aliyefiwa na mume wake"

### Luke 20:29

**Maelezo yanayounganisha**
Masadukayo wakamaliza kumuuliza Yesu maswali.

**Taarifa ya jumla**
Masadukayo walimwambia Yesu simulizi fupi kwenye mstari wa 29-32. Hii ni simulizi waliyoiweka kama mfano. kwenye mstari wa 33, walimuuliza Yesua swali kuhusu simulizi hiyo.

**Walikuwepo ndugu saba**
Hii inaweza kuwa imetokea au ni simulizi iliyotengenezwa ili kumjaribu Yesu.

**Walikufa bila kuwa na watoto**
"kufa bila kuwa na mtoto" au "na kufa lakini hawakuwa na mtoto yeyote"

**Na wa pili pia**
"wa pili alimuoa na kitu kilekile kikatokea" au "ndugu wa pili akamuoa na akafa bila kupata watoto"

**Wa tatu akamchukua**
"wa tatu akamuoa"

**vivyo hivyo wa saba hakuacha watoto na akafa**
"kwa njia ileile kama ndugu wote saba walimuoa na hawakupata watoto wa wakafa.

**Kwenye ufufuo**
"wakati watu watafufuliwa toka kwa wafu" au "wakati waliokufa wanakuwa hai tena." Baadhi ya lugha wananjia ya kuonyesha kuwa masadukayo hawaamini kuwa kuna ufufuo.

## Luke 20:34

**Maelezo yanayounganisha**
Yesu anaanza kuwajibu Masadukayo

**Wana wa ulimwengu huu**
"Watu wa ulimwengu huu" au "watu wa nyakati hizi." Hii inapingana na wale walioko mbingini na watu watakaoishi baada ya ufufuo.

**Kuoa na kuolewa**
Kwa tamaduni hiyo wanaongelea juu ya mwanaume kumuoa mwanamke na mwanamke kupelekwa kwenye ndoa kwa mume wake "kuolewa."

**Wao wanaostahili**
"watu ambao Mungu anawaona kuwa wanastahili"

**Kupokea ufufuo toka kwa waliokufa**
"kufufuliwa toka kwa wafu" au "kufufuka toka kwa wafu"

**Hawataoa wala hawataolewa**
"Hawataoa." Hii ni baada ya ufufuo.

**Hawatakufa tena**
Hii ni baada ya ufufuo. "Hawatakuwa na uwezo wa kufa tena."

**na wana wa Mungu watakuw wana wa ufufuo**
"ni watoto wa Mungu maana amewatoa toka kwenye kifo"

## Luke 20:37

**Maelezo yanayounganisha.**
Yesu alimaliza kuwajibu Masadukayo.

**Lakini wafu wanafufuliwa, hata Musa alionyeshwa.**
Neno "hata" lipo hapo kwa sababu Masadukayo hawakushangazwa na baadhi ya maandiko kuwa wafu wanafufuliwa, ila hawakutegemea kama Musa angeandika kitu kama hicho. "Lakini hata Musa alionyeshwa kuwa wafu wanafufuliwa"

**Mahali panapohusu kichaka**
"kwenye sehemu ya maandiko ameandika kuhusu kichaka kinachowaka moto" au "kwenye maandiko kuhusu kichaka kinachowaka moto"

**Alipomuita Bwana**
Ambapo Musa alimuita Bwana

**Mungu wa Ibrahimu na Mungu wa Isaka na Mungu wa Yakobo**
"Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo" walimuabudu Mungu huyuhuyu.

**Sasa**
Neno hili limetumika kuonesha ukomo wa mafundisho makuu. hapa Yesu anaelezzea namna ambavyo simulizi hii inathibitisha kuwa watu wanafufuliwa.

**Sio Mungu wa waliokufa bali wa waliohai**
Sentensi hizi zina maana moja lakini ni mbili kwa ajili ya kusisitiza. Lugha nyingine zina namna tofauti ya kuonyesha msisitizo. " Bwana ni Mungu wa walio hai katika uzima wa milele"

**Kwa sababu wote wanaishi kwake**
"kwa sababu kwenye macho ya Mungu wote wapo hai." "kwa sababu Mungu anajua ruho zao zipo hai"

## Luke 20:39

**Baadhi ya mafarisayo wakajibu**
"Baadhi ya mafarisayo wakamwambia Yesu." walikuwepo mafarisayo wakati Masadikayo walipokuwa wakimuuliza Yesu maswali.

**Hawakuthubutu kumuuliza**
"waliogopa kumuuliza" au hawakujitoa kumuuliza." hawakuendelea kumuuliza maswali ya mitego maana waliogopa majibu yake yenye hekima yatawafanya waonekane wajinga tena."

## Luke 20:41

**Taarifa ya jumla**
Yesu aliwauliza Mafarisayo swali.

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**"Kwa nini wanasema.... mwanangu"?**
Yesu alitumia swali kuwafanya mafarisayo wafikiri alichokuwa anakisema. "Tuwafikirie walivyosema... mwanangu" au "Nitaongea kuhusu wao wakisema... mwanangu"

**Mwana wa Daudi.**
"Kizazi cha Mfalme Daudi" Neno "mwana" limetumika kuelezea kizazi. Kwa sababu hii inamuelezea atakayetawala juu ya ufalme wa Mungu.

**Bwana akasema kwa Bwana wangu**
Hii imenukuliwa kutoka katika kitabu cha zaburi inasema "Yaweh" na mara nyingine inasema "Bwana" "Bwana Mungu akasema kwa Bwana wangu" au "Mungu akasema kwa Bwana wangu"

**Bwana wangu**
Daudi alikuwa akimuelezea Kristo kama "Bwana wake"

**Mkono wangu wa kulia**
upande wa kulia ni sehemu ya heshima. Mungu alimuheshimu Mesiya kwa kusema "keti upende wangu wa kulia"

**Mpaka nitakapowaweka adui zako chini yako**
Mpaka nitakapowashinda adui zako

**Amekuwaje mwana wa Daudi?**
"Imekuwaje Kristo akaawa mwana wa Daudi" "hii inaonyesha kuwa Kristo sio

## Luke 20:45

**Maelezo yanayounganisha**
Sasa Yesu alikuwa anaelekeza umakini wake kwa wanafunzi wake na kuzungumza nao.

**Jihadharini na**
Kujihadhari navyo

**Ambao hupenda kupita wamevaa mavazi marefu**
Mavazi marefu yanaonyesha kuwa walikuwa wa muhimu. walipenda kupitapita wakiwa wamevaa nguo zao za muhimu"

**Ambao Pia hula nyumba za wajane**
"Pia wanakula kwenye nyumba za wajane" "Pia wanachukua kile kinachomilikiwa na wajane"

**Wanajifanya wanasali sala ndefu**
"wanajifanya kuwa ni wenye haki na huomba maombi marefu" au "huomba maombi maraefu ili watu wawaone"

**Kujifanya**
hii inamaanisha Mafarisayo walifanya mambo yaliyowafanya waonekane wana umuhimu na wenye haki kuliko walivyo kiuhalisia.

**Hawa watapokea adhabu kubwa.**
"Watapokea adhabu kubwa kuliko wengine" au "Mungu atawaadhibu zaidi ya wengine"

---


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 21

1 Yesu alitazama akawaona wanaume matajiri waliokuwa wanaweka zawadi zao kwenye hazina. 2
Akamuona mjane mmoja masikini akiweka senti zake mbili. 3 Hivyo akasema, "Kweli nawaambieni, huyu
Mjane maskini ameweka nyingi kuliko wengine wote. 4 Hawa wote wametoa hizi zawadi kutoka katika
vingi walivyonavyo. Lakini huyu mjane, katika umaskini wake, ametoa fedha zote alizokuwa nazo kwa ajili
ya kuishi kwake." 5 Wakati wengine walipokuwa wakisema juu ya hekalu, namna lilivyokuwa limepambwa
na mawe mazuri na matoleo, alisema, 6 "Kwa habari ya mambo haya mnayoyaona, siku zitakuja ambazo
hakuna jiwe moja ambalo litaachwa juu ya jiwe jingine ambalo halitabomolewa." 7 Hivyo wakamuuliza,
wakasema, "Mwalimu, mambo haya yatatokea lini? Na nini ni itakuwa ishara kwamba haya mambo yako
karibu kutokea?" 8 Yesu akajibu, "Muwe waangalifu kwamba msidanganywe. Kwa sababu wengi watakuja
kwa jina langu, wakisema, 'Mimi ndiye, 'na 'Muda umekaribia'. Msiwafuate. 9 Mkisikia vita na
vuruguvurugu msiogope, kwa sababu haya mambo lazima yatokee kwanza, lakini mwisho hautatokea
upesi." 10 Kisha akawaambia, "Taifa litainuka kupigana na taifa jingine, na ufalme juu ya ufalme
mwingine. 11 Kutakuwa na matetemeko makubwa, na njaa na tauni katika maeneo mbalimbali. Kutakuwa
na matukio ya kutisha na ishara za kutisha kutoka mbinguni. 12 Lakini kabla ya mambo haya yote,
wataweka mikono yao juu yenu na kuwatesa, kuwapeleka kwenye masinagogi na magereza, kuwaleta
mbele za wafalme na wenye mamlaka kwa sababu ya jina langu. 13 Hii itawafungulia fursa kwa ushuhuda
wenu. 14 Kwahiyo amueni mioyoni mwenu kutoandaa utetezi wenu mapema, 15 kwa sababu nitawapa
maneno na hekima, ambayo adui zenu wote hawataweza kuipinga au kuikana. 16 Lakini mtakataliwa pia
na wazazi wenu, ndugu zenu, jamaa zenu na rafiki zenu, na watawaua baadhi yenu. 17 Mtachukiwa na
kila mmoja kwa sababu ya jina langu. 18 Lakini hakuna hata unywele mmoja wa vichwa vyenu
utakaopotea. 19 Katika kuvumilia mtaziponya nafsi zenu. 20 Mtakapoona Yerusalemu imezungukwa na
majeshi, basi jueni kwamba uharibifu wake umekaribia. 21 Hapo wale walioko Yudea wakimbilie milimani,
na wale walioko katikati ya jiji waondoke, na msiwaache walioko vijijini kuingia. 22 Maana hizi ni siku za
kisasi, ili kwamba mambo yote yaliyoandikwa yapate kutimilika. 23 Ole ni kwa wale walio na mimba na
kwa wale wanyonyeshao katika siku hizo! Kwa maana kutakuwa na adha kuu juu ya nchi, na ghadhabu
kwa watu hawa. 24 Na wataanguka kwa ncha ya upanga na watachukuliwa mateka kwa mataifa yote, na
Yerusalem itakanyagwa na watu wa mataifa, mpaka wakati wa watu wa mataifa utakapotimilika. 25
Kutakuwa na ishara katika jua, mwezi na nyota. Na katika nchi kutakuwa na dhiki ya mataifa, katika
kukata tamaa kutokana na mlio wa bahari na mawimbi. 26 Kutakuwa na watu wakizimia kwa hofu na
katika kutarajia mambo yatakoyo tokea juu ya dunia. Kwa maana nguvu za mbingu zitatikiswa. 27 Kisha
watamwona Mwana wa Adamu akija mawinguni katika nguvu na utukufu mkuu. 28 Lakini mambo haya
yatakapoanza kutokea, simameni, inueni vichwa vyenu, kwa sababu ukombozi wenu umesogea karibu." 29
Yesu akawaambia kwa mfano, "Uangalieni mtini, na miti yote. 30 Inapotoa machipukizi, mnajionea
wenyewe na kutambua kwamba kiangazi tayari kiko karibu. 31 Vivyo hivyo, mnapoona mambo haya
yanatokea, ninyi tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu umekaribia. 32 Kweli, nawaambieni, kizazi hiki
hakitapita, mpaka mambo haya yote yatakapotokea. 33 Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu
hayatapita kamwe. 34 Lakini jiangalieni wenyewe, ili kwamba mioyo yenu isije ikalemewa na ufisadi, ulevi,
na mahangaiko ya maisha haya. Kwa sababu ile siku itawajia ghafla 35 kama mtego. Kwasababu itakuwa
juu ya kila mmoja aishiye katika uso wa dunia nzima. 36 Lakini mwe tayari wakati wote, mwombe kwamba
mtakuwa imara vya kutosha kuyaepuka haya yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa
Adamu." 37 Hivyo wakati wa mchana alikuwa akifundisha hekaluni na usiku alitoka nje, na kwenda
kukesha katika mlima unaoitwa wa Mzeituni. 38 Watu wote walimjia asubuhi na mapemaili kumsikiliza
ndani ya hekalu.

---

## Luka 21 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

Luka 21:5-36 ni mafundisho yaliyopanuliwa kuhusu kurudi kwa Kristo.

### Dhana maalum katika sura hii

#### "Kwa maana wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, 'Mimi ndiye,'"

Yesu anafundisha kwamba kabla ya kurudi kwake watu wengi watajidai kuwa ni yeye anayerudi. Pia itakuwa wakati wa mateso makubwa.

#### "Mpaka nyakati za Mataifa zitimizwe"

Wayahudi walizungumzia wakati kati ya uhamisho wa Babeli na kuja kwa Masihi kama kipindi cha utawala wa Wayunani. Hii ni kwa sababu Wayahudi hawakuwa na mamlaka juu ya mambo yao wenyewe.

### Takwimu muhimu za matamshi katika sura hii

#### Kusema kwa mifano

Unabii katika sura hii ina lugha ya kusema kwa mifano. Ni bora kutafsiri habari yalioandikwa kama matukio halisi isipokuwa tafsiri hii haiwezekani au inatoa maana isiyosawa. Kwa mfano, maneno "yamevunjwa," "yatasimama dhidi," na "hakuna nywele kichwani mwako itakayoangamia" ni mifano. "Ishara mbinguni," "tetemeko la ardhi," na "vita" lazima pia zitafsiriwe kwa uhalisi.

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

#### "Mwana wa Binadamu"

Yesu anajiita mwenyewe kama "Mwana wa Binadamu." Lugha zingine haziwezi kuruhusu mtu kujitaja mwenyewe kama 'mtu wa tatu.'

---

### Luke 21:1

**mjane mmoja maskini**
Hii ni namna ya kutambulisha mtu mpya katika hadithi

**zawadi**
"zawadi za fedha"

**hazina**
"sanduku la makusanyo" au "sanduku la fedha". Hili lilikuwa moja ya masanduku pale hekaluni ambapo watu huweka fedha kama zawadi kwa Mungu.

**senti mbili**
"sarafu mbili ndogo" au "sarafu za shaba ndogo sana". Hizi zilikuwa ni sarafu zenye thamani ndogo sana ambazo watu walizitumia siku hizo.

**Nawaambieni**
Yesu alikuwa akiongea na wanafunzi wake.

**wametoa hizi zawadi kutoka katika vingi walivyonavyo**
Tafsiri mbadala:"kuwa na fedha nyingi na kutoa baadhi ya hizo"

**katika umaskini wake, ametoa zote**
Tafsiri mbadala:"alikuwa na vichache sana, na bado aliweka vyote"

### Luke 21:5

**matoleo**
"vitu ambavyo watu walimpa Mungu"

**siku zitakuja ambazo**
"kutakuwa na nyakati ambapo" au "siku fulani"

**hakuna jiwe moja ambalo litaachwa juu ya jiwe jingine**
"kila jiwe litatolewa mahali pake." Tafsiri mbadala: "adui hawataliacha jiwe juu ya jiwe juu ya jiwe jingine."

**ambalo halitabomolewa**
Hii inaweza kutafsiriwa kama sentensi mpya. Tafsiri mbadala: "Yote yatabomolewa chini" au " Adui watabomoa chini kila jiwe."

### Luke 21:7

**wakamuuliza**
"wanafunzi wakamuuliza Yesu" au "Wanafunzi wa Yesu wakamuuliza"

**mambo haya**
Hii inarejea kile ambacho Yesu amesema kuhusu adui kuliharibu hekalu.

**kwamba msidanganywe**
Yesu alikuwa akiwaambia wanafunzi wake.Tafsiri mbadala: "kwamba msiamini uongo" au "kwamba hakuna mmoja wa kuwadanganya."

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**kwa jina langu**
Tafsiri mbadala: "wanadai kuwa mimi" au "wanadai kuwa na mamlaka yangu"

**msiogope**
"Msiruhusu haya mambo yawaogofye" au "msiogope"

**mwisho hautatokea upesi**
Tafsiri Mbadala: "mwisho wa dunia hautatokea upesi baada ya vita na vurugu" au "dunia haitafikia mwisho upesi baada ya mambo hayo kutokea"

**mwisho**
" mwisho wa kila kitu" au "mwisho wa miaka"

### Luke 21:10

**Kisha akawaambia**
"Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake." Kwa sababu huu ni mwendelezo wa kuongea kwa Yesu kutokea kwenye mstari wa nyumba, baadhi ya lugha zisingependelea kusema "Kisha akawaambia."

**Taifa litainuka kupigana na taifa jingine**
Tafsiri mbadala: "taifa moja litashambulia taifa jingine"

**Taifa**
Hii inamaanisha makundi ya watu ya kikabila kuliko nchi.

**Ufalme juu ya ufalme mwingine**
Tafsiri mbadala: "Ufalme utainuka juu ya ufalme mwingine" au "majeshi kutoka ufalme mmoja utashambulia majeshi kutoka ufalme mwingine"

**njaa na tauni**
"kutakuwa na njaa na tauni" au "nyakati za njaa na magonjwa yanayouwa watu wengi"

**matukio ya kutisha**
"matukio yanayotisha watu" au "matukio yanayosababisha watu kuogopa sana"

### Luke 21:12

**mambo haya**
Hii inamaanisha mambo mabaya ya kutisha ambayo Yesu alisema yatatukia.

**wataweka mikono yao juu yenu**
Tafsiri mbadala: "watawakamata" au "watawashika"

**wata...**
"watu wata.." au "adui wata..."

**yenu**
Yesu alikuwa akiongea na wanafunzi wake.

**kuwapeleka kwenye masinagogi**
"kuwatoa ninyi kwa viongozi wa masinagogi." Viongozi wa masinagogi wangewakataza Wayahudi wengine wote kuingiliana na wanafunzi kwa sababu wanamfuata Yesu.

**na magereza**
"na kuwapeleka ninyi magerezani" au "na kuwaweka ninyi magerezani"

**kwa sababu ya jina langu**
Tafsiri mbadala: "kwa sababu yangu" au "kwa sababu mnanifuata mimi"

**kwa ushuhuda wenu**
"kwa ninyi kuwaambia wao ushuhuda wenu kunihusu mimi"

### Luke 21:14

**Kwahiyo**
"Kwa sababu ya hili." Yesu anatumia neno hili hapa kurejea kwenye kila kitu alichokisema.

**amueni mioyoni mwenu**
Tafsiri mbadala: "zingatieni akilini mwenu" au "amua kiuthabiti"

**kutoandaa utetezi wenu**
"kutokufikiri nini ambacho mtasema ili kujitetea kinyume cha mashitaka yao"

**nitawapa maneno na hekima**
"Nitawaambia maneno gani ya hekima ya kusema"

**maneno na hekima**
Tafsiri mbadala: "maneno ya hekima"

**ambayo adui zenu wote hawataweza kuipinga au kuikataa kwamba ni uongo.**
Hii inaweza kutafsiriwa kama sentensi mpya. Tafsiri mbadala: "Adui zenu hawataweza kubishana na ninyi au kusema kwamba hamko sahihi" au "Adui zenu lazima wakubali kwamba mko sahihi."

### Luke 21:16

**mtatolewa pia na wazazi wenu, ndugu zenu, jamaa zenu na rafiki zenu.**
Tafsiri mbadala: "wazazi wenu, ndugu zenu, jamaa zenu na rafiki zenu watawapeleka kwa wenye mamlaka"

**watawaua baadhi yenu**
"watawaua baadhi yenu." Pia inaweza kutafsiriwa kama 1) "wenye mamlaka watawaua baadhi yenu" au 2) "wale ambao watawaleta watawaua baadhi yenu." tafsiri ya kwanza ni kama iko sahihi zaidi.

**kwa sababu ya jina langu**
Tafsiri mbadala: "kwa sababu yangu" au "kwa sababu mnanifuata mimi"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**lakini hakuna hata unywele mmoja wa vichwa vyenu utakaopotea.**
Hii inaonyesha sehemu ndogo sana ya kiungo cha mwanadamu kusisitiza kwamba mtu katika ukamilifu wake hatapotea. Yesu aliishasema kwamba baadhi yao wanaweza kuuwawa. Kwahiyo baadhi walielewa kwamba hawatadhurika kiroho. Tafsiri mbadala: "Lakini mambo haya hayawezi kweli kuwadhuru ninyi" au "Hata kila unywele juu ya vichwa vyenu utakuwa salama.

**katika kuvumilia kwenu**
"kwa kusimama thabiti." Tafsiri mbadala: "Kama hamtaacha."

**mtaziponya nafsi zenu**
"mtapokea uzima" au "mtaishi milele"

### Luke 21:20

**Yerusalemu imezungukwa na majeshi**
Tafsiri mbadala: "Majeshi yanauzunguka Yerusalemu"

**kwamba uharibifu wake umekaribia**
"kwamba itaharibiwa hivi karibuni" au "kwamba watauharibu muda si mrefu"

**kimbia**
"kimbia mbali kutoka kwenye hatari"

**hizi ni siku za kisasi**
"hizi ni siku za adhabu" au "huu ni wakati ambapo Mungu atauadhibu mji"

**mambo yote yaliyoandikwa**
Tafsiri mbadala: "mambo yote ambayo manabii wameandika katika maandiko matakatifu zamani za kale"

**yatatimilika**
Tafsiri mbadala: "yatatokea"

### Luke 21:23

**kutakuwa na adha kuu juu ya nchi**
Yaweza kutafsiriwa kama 1) watu wakaao katika nchi watadhikika au 2) kutatokea maafa kabisa katika nchi.

**ghadhabu kwa watu hawa**
"kutakuwa na ghadhabu kwa watu hawa." Tafsiri mbadala: "hawa watu watapata uzoefu wa hasira ya Mungu" au "God atakasirika sana na atawaadhibu watu hawa."

**wataanguka kwa ncha ya upanga**
"watauwawa kwa ncha ya upanga." Tafsiri mbadala: "maaskari maadui watawauwa.

**watachukuliwa mateka kwa mataifa yote**
Tafsiri mbadala: "Maadui zao watawakama na kuwapeleka nchi nyingine"

**Yerusalemu itakanyagwa na watu wa mataifa**
Inaweza kutafsiriwa kama 1) watu wa Mataifa wataushinda Yerusalemu na kuukalia au 2) watu wa Mataifa watauharibu mji wa Yerusalemu au 3) watu wa Mataifa watawaharibu watu wa Yerusalemu.

**wakati wa watu wa Mataifa umekamilika**
Tafsiri mbadala: "wakati wa watu wa Mataifa umefika mwisho"

### Luke 21:25

**kutakuwa na dhiki ya mataifa**
Tafsiri mbadala: "watu wa mataifa mbalimbali watadhikika" au "watu wa mataifa mbalimbali watakuwa na fadhaa nyingi"

**katika hofu kutokana na mlio wa bahari na mawimbi**
"kwa sababu watachanganywa na mlio wa bahari na mawimbi" au "sauti kubwa ya bahari na machafuko yake yatawatisha watu." Hii inaoneka kumaanisha dhoruba isiyokuwa ya kawaida au machafuko yanayotokea baharini.

**mambo yatakayotokea juu ya dunia**
"mambo ambayo yatatokea duniani" au "mambo yatakayotokea kwa dunia"

**nguvu za mbingu zitatikiswa**
Inaweza kutafsiriwa kama 1) vitu vya huko angani kama jua, mwezi, na nyota hazitaenda kwa utaratibu wake wa kawaida au 2) roho zenye nguvu sana huko mbinguni zitafadhaishwa. Tafsiri ya kwanza inapendekezwa. Tafsiri mbadala: "Mungu atatikisa vitu vyenye nguvu huko mbinguni.

### Luke 21:27

**Mwana wa Adamu**
Yesu anarejea kwake mwenyewe

**akija mawinguni**
Tafsiri mbadala: "akija chini katika mawingu"

**katika nguvu na utukufu mkuu**
Hapa "nguvu" inawezekana inarejea katika mamlaka yake kuuhukumu ulimwengu. Hapa "utukufu" unaweza kurejea mwanga angavu. Mungu wakati mwingine anaonyesha ukuu wake na mwanga angavu sana. Tafsiri mbadala: "a nguvu na utukufu" au "atakuwa na wa nguvu na wa utukufu sana."

**simameni**
Wakati mwingine watu wanapoogopa, hujiinamisha chini ili kuepuka kuonekana au kuumizwa. Wakati wanapokuwa hawaogopi tena, wananyanyuka. Tafsiri mbadala: "simameni na ujasiri."

**inueni vichwa vyenu**
Tafsiri mbadala: "tazameni juu." Kwa kutazama juu, wataweza kumuona mwokozi akija kwao.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**kwa sababu ukombozi wenu unasogea karibu**
Tafsiri mbadala: "kwa sababu mkombozi wenu anakuja kwenu" au "kwa sababu Mungu mara atawaokoa"

### Luke 21:29

**Inapopukutisha majani yake**
"Wakati majani yake yaanzapo kukuwa"

**mnajionea wenyewe na kutambua**
Tafsiri mbadala: "watu wanajionea wenyewe na kutambua"

**kiangazi tayari kiko karibu**
"kiangazi kiko karibu kuanza." Kiangazi katika Israel ni wakati wa ukavu sana, hivyo mazao huvunwa mwanzo wa kiangazi. Tafsiri mbadala: "wakati wa mavuno u tayari kuanza."

**ufalme wa Mungu u karibu**
Mungu atausimamisha ufalme wake hivi karibuni" Tafsiri mbadala: Mungu atatawala kama Mfalme hivi karibuni."

### Luke 21:32

**kizazi hiki**
Inaweza kutafsiriwa kama 1) kizazi ambazho kitaona moja ya ishara ambazo Yesu aliziongelea au 2) kizazi amacho Yesu alikuwa anakizungumzia. Tafsiri ya kwanza ni kama iko sahihi zaidi.

**hakitapita, mpaka**
Tafsiri mbadala: "kitakuwa bado hai wakati..."

**Mbingu na nchi zitapita**
"Mbingu na nchi zitakoma kuwepo." Neno "mbingu" hapa linamaanisha anga na ulimwengu mwingine juu yake.

**maneno yangu hayatapita**
"maneno yangu hayatakoma kuishi" au "maneno yangu hayatashindwa kamwe." Tafsiri mbadala: "Nikisemacho hakika kitatokea."

### Luke 21:34

**ili kwamba mioyo yenu isije ikalemewa**
Tafsiri mbadala: "ili msije mkawa mmetingwa na"

**ufisadi**
"tamaa isiyoweza kuzuiwa" au " kujiweka kwenye kutamani na kutumia vitu ambavyo vinakufanya ujisikie vizuri." Tafsiri mbadala: "Anasa nyingi."

**mahangaiko ya maisha haya**
"kujitaabisha au kujihangaisha sana kuhusu maisha haya"

**kwa sababu siku ile itawajia ghafula**
Wengine wangependa kuongeza habari elekezi: "Kwamba kama hamtakuwa waangalifu ile siku itawajia ghafula." Ujio wa siku hiyo utaonekana kuwa wa ghafula na wakutotarajiwa kwa wale ambao hawako na hawaisubiri.

**ile siku**
Tafsiri mbadala: "siku ambayo Mwana wa Adamu atakuja"

**ghafula kama mtego**
Tafsiri mbadala: "wakati ambapo hamuitarajii, kama mtego unapofunga ghafula kwa mnyama"

**itakuwa juu ya kila mmoja**
"itamuathiri kila mmoja" au "tukio la siku hiyo litamuathiri kila mmoja"

**katika uso wa dunia nzima**
Tafsiri mbadala: "katika eneo la dunia nzima" au "juu ya dunia nzima"

### Luke 21:36

**imara vya kutosha kuyaepuka haya yote**
Inaweza kutafsiriwa kama 1) "imara vya kutosha kuyavumilia haya mambo" au 2) "kuweza kuyaepuka haya mambo."

**haya yote yatakayotokea**
"mambo haya yatakayotokea." Yesu alikuwa amewaambia si muda mrefu juu ya mambo mabaya ambayo yangetokea kama vile kuteswa, vita, na kuchukuliwa mateka.

**kusimama mbele za Mwana wa Adamu**
"Kusimama kwa ujasiri mbele ya Mwana wa Adamu." Hii inaweza kumaanisha wakati ambapo Mwana wa Adamu anamhukumu kila mmoja. Mtu ambaye hayuko tayari atamuogopa Mwana wa Adamu na hataweza kusimama kwa ujasiri.

### Luke 21:37

**wakati wa mchana alikuwa akifundisha**
"wakati wa mchana angeweza kufundisha." Mistari inayofuata kuhusu vitu ambavyo Yesu na watu walifanya kila siku katika wiki kabla hajafa.

**hekaluni**
Tafsiri mbadala: "katika hekalu" au "kwenye uwanja wa ndani wa hekalu"

**usiku alitoka nje**
"usiku angeliweza kwenda nje ya mji" au "alikwenda nje kila usiku"

**Watu wote**
Tafsiri mbadala: "idadi ya watu wengi sana" au "karibu kila mmoja"

**walimuijia asubuhi na mapema**
"wangekuja asubuhi na mapema" au "walikuja mapema sana kila asubuhi"

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**kumsikiliza**
"kumsikiliza akifundisha"

---

## Chapter 22

1 Basi Sikukuu ya Mkate Usiyotiwa Chachu ilikuwa imekaribia, ambayo inaitwa Pasaka. 2 Makuhani
wakuu na waandishi wakajadiliana namna ya kumuua Yesu, kwa sababu waliwaogopa watu. 3 Shetani
akaingia ndani ya Yuda Iskariote, mmoja wa wale wanafunzi Kumi na mbili. 4 Yuda akaenda kujadiliana na
wakuu wa makuhani na wakuu namna ambavyo atamkabidhi Yesu kwao. 5 Walifurahi, na kukubaliana
kumpa fedha. 6 Yeye aliridhia, na alitafuta fursa ya kumkabidhi Yesu kwao mbali na kundi la watu. 7 Siku
ya mikate isiyotiwa chachu ikafika, ambapo kondoo wa Pasaka lazima atolewe. 8 Yesu akawatuma Petro
na Yohana, akasema, "Nendeni mkatuandalie chakula cha Pasaka ili tuje tukile." 9 Wakamuuliza, "Wapi
unataka tuyafanyie hayo maandalizi?" 10 Akawajibu, "Sikilizeni, mtakapokuwa mmeingia mjini,
mwanamume ambaye amebeba mtungi wa maji atakutana na ninyi. Mfuateni kwenye nyumba ambayo
ataingia. 11 Kisha mwambieni bwana wa nyumba, "Mwalimu anakwambia, "Kiko wapi chumba cha
wageni, mahali ambapo nitakula Pasaka na wanafunzi wangu?" 12 Atawaonyesha chumba cha ghorofani
ambacho kiko tayari. Fanyeni maandalizi humo." 13 Hivyo wakaenda, na wakakuta kila kitu kama
alivyowaambia. Kisha wakaandaa chakula cha Pasaka. 14 Muda ulipofika alikaa na wale mitume. 15 Kisha
akawaambia, "Nina shauku kubwa ya kula sikukuu hii ya Pasaka na ninyi kabla ya kuteswa kwangu. 16
Kwa maana nawaambieni, sitakula tena mpaka itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu." 17 Kisha Yesu
akachukua kikombe, na alipokwisha kushukuru, akasema, "Chukueni hiki, na mgawane ninyi kwa ninyi. 18
Kwa maana nawaambia, sitakunywa tena mzao wa mzabibu, mpaka ufalme wa Mungu utakapokuja." 19
Kisha akachukua mkate, na alipokwisha kushukuru, akaumega, na kuwapa, akisema, "Huu ni mwili wangu
ambao umetolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi." 20 Akachukua kikombe vivyo
hivyo baada ya chakula cha usiku akisema, "Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, ambayo
imemwagika kwa ajili yenu. 21 Lakini angalieni. Yule anisalitie yuko pamoja nami mezani. 22 Kwa maana
Mwana wa Adamu kwa kweli aenda zake kama ilivyokwisha amuliwa. Lakini ole kwa mtu yule ambaye
kupitia yeye Mwana wa Adamu asalitiwa!" 23 Wakaanza kuulizana wao kwa wao, nani miongoni mwao
ambaye angefanya jambo hili. 24 Kisha yakatokea mabishano katikati yao kwamba ni nani anaye dhaniwa
kuwa mkuu kuliko wote. 25 Akawaambia, "Wafalme wa watu wa mataifa wana ubwana juu yao, na wale
mwenye mamlaka juu yao wanaitwa waheshimiwa watawala. 26 Lakini haitakiwi kabisa kuwa hivi kwenu
ninyi. Badala yake, acha yule ambaye ni mkubwa kati yenu awe kama mdogo. Na yule ambaye ni wa
muhimu sana awe kama atumikaye. 27 Kwa sababu yupi mkubwa, yule akaaye mezani au yule
anayetumika? Je si yule aketie mezani? Na mimi bado ni kati yenu kama atumikaye. 28 Lakini ninyi ndio
ambao mmeendelea kuwa nami katika majaribu yangu. 29 Nawapa ninyi ufalme, kama vile Baba
alivyonipa mimi ufalme, 30 kwamba mpate kula na kunywa mezani kwangu kwenye ufalme wangu. Na
mtakaa kwenye viti vya enzi mkizihukumu kabila kumi na mbili za Israel. 31 Simoni, Simoni, fahamu
kwamba, Shetani ameomba awapate ili awapepete kama ngano. 32 Lakini nimekuombea, kwamba imani
yako isishindwe. Baada ya kuwa umerudi tena, waimarishe ndugu zako." 33 Petro akamwambia, "Bwana,
niko tayari kwenda na wewe gerezani na hata katika mauti." 34 Yesu akajibu, "Nakwambia, Petro, Jogoo
hatawika leo, kabla hujanikana mara tatu kwamba unanijua." 35 Kisha Yesu akawaambia, "Nilipowapeleka
ninyi bila mfuko, kikapu cha vyakula, ua viatu, je mlipungukiwa na kitu?" Wakajibu "Hakuna." 36 Kisha
akawaambia, "Lakini sasa, kila mwenye mfuko, na auchukue pamoja na kikapu cha vyakula. Yule ambaye
hana upanga imempasa auze joho lake anunue mmoja. 37 Kwa sababu nawaambia, yote ambayo
yameandikwa kwa ajili yangu lazima yatimilike, 'Na alichukuliwa kama mtu ambaye anavunja torati.' Kwa
sababu kile kilichotabiriwa kwa ajili yangu kinatimizwa." 38 Kisha wakasema, "Bwana, tazama! Hizi hapa
panga mbili." Na akawaambia"yatosha." 39 Baada ya chakula cha usiku, Yesu aliondoka, kama ambavyo
amekuwa akifanya mara kwa mara, akaenda mlima wa Mzeituni, na wanafunzi wakamfuata. 40
Walipofika, aliwaambia, "Ombeni kwamba msiingie majaribuni." 41 Akaenda mbali na wao kama mrusho
wa jiwe, akapiga magoti akaomba, 42 akisema, "Baba, kama unataka, niondolee kikombe hiki. Lakini si
kama nitakavyo mimi, lakini mapenzi yako yafanyike." 43 Kisha malaika kutoka mbinguni akamtokea,
akamtia nguvu. 44 Akiwa katika kuugua, akaomba kwa dhati zaidi, na jasho lake likawa kama matone
makubwa ya damu yakidondoka chini. 45 Wakati alipoamka kutoka katika maombi yake, alikuja kwa
wanafunzi, na akawakuta wamelala kwa sababu ya huzuni yao, 46 na akawauliza, "Kwanini mnalala?
Amkeni muombe, kwamba msiingie majaribuni." 47 Wakati alipokuwa bado akiongea, tazama, kundi
kubwa la watu likatokea, na Yuda, mmoja wa mitume kumi na wawili akiwaongoza. Akaja karibu na Yesu
ili ambusu, 48 lakini Yesu akamwambia, "Yuda, je unamsaliti Mwana wa Adamu kwa busu?" 49 Wakati
wale waliokuwa karibu na Yesu walipoona hayo yanayotokea, wakasema, "Bwana, je tuwapige kwa

upanga?" 50 Kisha mmoja wao akampiga mtumishi wa kuhani mkuu, akamkata sikio lake la kulia. 51 Yesu
akasema, "hii inatosha. Na akagusa sikio lake, akamponya. 52 Yesu akasema kwa kuhani mkuu, na kwa
wakuu wa hekalu, na kwa wazee waliokuja kinyume chake, "Je mnakuja kana kwamba mnakuja
kupambana na mnyang'anyi, na marungu na mapanga? 53 Nilipokuwa pamoja nanyi siku zote kwenye
hekalu, hamkuweka mikono yenu juu yangu. Lakini hii ni saa yako, na mamlaka ya giza." 54
Wakamkamata, wakamuongoza, wakamleta nyumbani mwa kuhani mkuu. Lakini Petro akamfuatilia kwa
mbali. 55 Baada ya kuwa wamewasha moto katika ule uwanda wa ndani na walipokwisha kukaa chini
pamoja, Petro akakaa katikati yao. 56 Mtumishi mmoja wa kike akamuona Petro alipokuwa amekaa katika
mwanga utokanao na moto, akamtazama akamwambia, "Huyu mtu pia alikuwa pamoja naye." 57 Lakini
Petro akakana, akasema, "mwanamke, mimi simjui." 58 Baada ya muda kidogo, mtu mwingine akamuona
akasema "Wewe pia ni mmoja wao". Lakini Petro akajibu, "Mwanaume, mimi siyo." 59 Baada ya kama saa
moja hivi, mwanaume mmoja akasisitiza akasema, "Kweli kabisa huyu mtu pia alikuwa pamoja naye,
maana ni Mgalilaya." 60 Lakini Petro akasema, "Mwanaume, sijui usemalo." Na mara, wakati akiongea,
jogoo akawika. 61 Akageuka, Bwana akamtazama Petro. Na Petro akalikumbuka neno la Bwana, pale
alipomwambia, "Kabla ya jogoo kuwika leo, utanikana mimi mara tatu." 62 Akienda nje, Petro akalia kwa
uchungu mwingi. 63 Kisha wale wanaume waliokuwa wakimlinda Yesu, wakamdhihaki na kumpiga. 64
Baada ya kumfunika macho, wakamuuliza, wakisema, "Tabiri! Ni nani aliyekupiga?" 65 Wakaongea
mambo mengine mengi kinyume cha Yesu na kumkufuru yeye. 66 Mara ilipokuwa asubuhi, wazee wa watu
walikusanyika pamoja, wakuu wa makuhani na waandishi. Wakampeleka kwenye Baraza, 67 wakisema,
"Kama wewe ni Kristo, tuambie." Lakini yeye akawaambia, "Kama nikiwaambia, hamtaniamini, 68 na
kama nikiwauliza hamtanijibu." 69 Lakini kuanzia sasa na kuendelea, Mwana wa Adamu atakuwa amekaa
mkono wa kuume wa nguvu ya Mungu." 70 Wote wakasema, "Kwa hiyo wewe ni Mwana wa Mungu?" Na
Yesu akawaambia, "Ninyi mmesema mimi ndiye." 71 Wakasema, "Kwa nini bado tunahitaji tena ushahidi?
Kwa sababu sisi wenyewe tumesikia kutoka katika kinywa chake mwenyewe."

---

## Luka 22 Maelezo ya Jumla

**uundo na upangiliaji**

Matukio ya sura hii hujulikana kama "jioni ya mwisho." Sikukuu ya Pasaka kwa njia nyingi inafanana na dhabihu ya Yesu kama kondoo wa Mungu.

**Dhana maalum katika sura hii**

**Kula mwili na damu**

Hadi leo, hatua hii inafanyika karibu na makanisa yote kukumbuka dhabihu ya Kristo kwa ajili ya dhambi za mwanadamu.

**Agano Jipya**

Yesu anataja Agano Jipya wakati wa jioni la mwisho. Agano Jipya ni chanzo cha utata kati ya wasomi. Kuna maoni mengi tofauti kuhusu wakati agano hili linapoanza na uhusiano wa kanisa na agano jipya.

**Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii**

**"Mwana wa Binadamu"**

Yesu anajiita mwenyewe kama "Mwana wa Binadamu." Lugha zingine haziwezi kuruhusu mtu kujitaja mwenyewe kama 'mtu wa tatu.'

**"hii ndiyo saa yako"**

Katika tamaduni nyingi, kuna imani kwamba mambo mabaya hutokea tu katikati ya usiku, wakati watu wema wamelala. Maneno haya ni kejeli yanayoonyesha kwamba watu wanaomkamata Yesu wanatenda mabaya.

---


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Luke 22:1

**Maelezo ya ujumla:**
Hii ni sehemu inayofuata ya simulizi. Yuda anakubali kumsaliti Yesu. Mistari hii inatupa taarifa za msingi kuhusu sehemu hii ya simulizi.

**Basi**
Neno hili linatumika hapa sehemu mpya ya simulizi

**sikukuu ya mkate usiyotiwa chachu**
sikukuu hii ilikuwa inaitwa kwa jina hili kwa sababu wakati wa sikukuu, Wayahudi hawakula mkate ambao ulikuwa umetengenezwa na chachu. Tafsiri mbadala: "Sikukuu ambapo wangekula mkate usiyotiwa chachu"

**Mkate usiyotiwa chachu**
Huu ni mkate ambao hauna chachu au hamila ili kuufanya uumuke. Tafsiri mbadala: "Mkate bila Hamila."

**ilikuwa imekaribia**
"ilikuwa tayari sana kuanza"

**namna ya kumuua Yesu**
Makuhani na waandishi hawakuwa na mamlaka ya kumuua Yesu wao wenyewe, lakini walitegemea kupata watu wengine wa kumuua. Tafsiri mbadala: "Namna gani ambavyo wangesababisha Yesu kuuwawa" au "namna ambavyo wangesababisha mtu amuuwe Yesu."

**waliwaogopa watu**
Inaweza kutafsiriwa kama 1) "walikuwa na wasiwasi wa kile ambacho watu wangefanya" au 2) "walikuwa na wasiwasi kwamba watu wangemfanya Yesu mfalme."

## Luke 22:3

**Maelezo ya ujumla:**
Huu ndio mwanzo wa matukio katika sehemu hii ya simuli.

**Yesu akaingia ndani ya Yuda Iskariote**
Hii inawezekana ilikuwa sawa na kupagawa na pepo.

**wakuu wa makuhani**
"viongozi wa makuhani"

**wakuu**
'viongozi wa walinzi wa hekalu'"

**namna ambavyo atamkabidhi Yesu kwao**
Tafsiri mbadala: "namna ambavyo angewasaidia kumkamata Yesu"

## Luke 22:5

**Wali..**
"Wakuu wa makuhani na wakuu"

**kumpa fedha**
"kumpa Yuda fedha"

**alilidhia**
"alikubali"

**alitafuta fursa ya kumkabidhi Yesu kwao mbali na kundi la watu**
hiki ni kitendo kinachoendelea baada ya sehemu hii ya simulizi kuisha.

**kumkabidhi**
"kuwasaidia kumkamata Yesu"

**mbali na kundi la watu**
"kwa usiri" au "wakati ambapo hakuna kundi la watu wakimzunguka"

## Luke 22:7

**Maelezo ya ujumla:**
Hii ni sehemu nyingine ya simulizi. Yesu anawatuma Petro na Yohana kuandaa kwa ajili ya chakula cha Pasaka. Mstari wa saba utatupa habari au taarifa za msingi kuhusu simulizi inavyoanza.

**Siku ya mkate usiyotiwa chachu**
"Siku ya mkate bila hamila" au "Siku ya chapati." Hii ilikuwa ni siku ambayo Wayahudi wangetoa nje ya nyumba zao mikate yote ambayo ilikuwa imetengenezwa na hamila. Kisha wangesherehekea sikukuu ya mkate usiyotiwa chachu au hamila kwa siku saba.

**kondoo wa Pasaka lazima atolewe**
Kila familia au kikundi cha watu wangemchinja kondoo na kumla pamoja, hivyo kondoo wengi sana walichinjwa. Tafsiri mbadala: "watu ilikuwa lazima wachinje kondoo kwa ajili ya chakula cha Pasaka."

**ili tuje tukile**
Yesu alikuwa anawajumuisha Petro na Yohana aliposema "tu.." Petro na Yohana wangekuwa sehemu ya kundi ambalo lingekula chakula kile.

**mkatuandalie**
Hili ni neno la kiujumla linalomaanisha "fanya tayari." Yesu si kwamba alikuwa akiwaambia Petro na Yohana kufanya mapishi yote.

**unataka tufanyie hayo maandalizi**
Neno "tu.." halimuhusishi Yesu. Yesu asingekuwa sehemu ya kundi ambalo lingeandaa chakula kile.

**tufanye maandalizi**
"kufanya maandalizi ya chakula" au "kuandaa chakula"

## Luke 22:10

**Akawajibu**
"Yesu akawajibu Petro na Yohana"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**mwanaume ambaye amebeba mtungi wa maji atakutana na ninyi.**
"mtamuona mtu amebeba mtungi wa maji"

**amebeba mtungi wa maji**
"amebeba mtungi wenye maji ndani yake." Inawezekana angekuwa amebeba mtungi begani mwake.

**Mfuateni kwenye nyumba ambayo ataingia**
Tafsiri mbadala: "Mfuateni, na ingieni kwenye hiyo nyumba"

**Mwalimu anakwambia**
Hii inaanzisha nukuu elekezi ambapo Yesu aliwaambia wanafunzi wake nini cha kusema.

**Mwalimu**
Hii inaongela juu ya Yesu.

**Kula Pasaka**
"kula mlo wa Pasaka"

## Luke 22:12

**Atawaonyesha**
"Mwenye nyumba atawaonyesha"

**ghorofani**
"vyumba vya juu ya nyumba"

**Hivyo wakaenda**
"Hivyo Petro na Yohana wakaenda"

## Luke 22:14

**Nina shauku kubwa**
"Nimetaka sana"

**Kwa maana nawaambieni**
Hii sentensi inatumika kusisitiza umuhimu wa kile Yesu atakisema baada ya hicho.

**mpaka itakapotimizwa**
Inaweza kutafsiriwa kama 1) "mpaka kusudi la Sikukuu ya Pasaka litakapokuwa limetimizwa" au 2) "mpaka tutakapokula na kushangilia Sikukuu ya mwisho ya Pasaka." Tafsiri mbadala: "Mpaka Mungu atakapoitimiliza" au "mpaka Mungu atakapolitimiliza kusudi la Sikukuu ya Pasaka."

## Luke 22:17

**alipokwisha kushukuru**
"alipokwisha toa shukurani kwa Mungu"

**akasema**
"akasema kwa mitume wake"

**mgawane ninyi kwa ninyi**
Tafsiri mbadala: "mgawane divai miongoni mwenu" au "ninyi wote mnywe divai kidogo kutoka katika hiki"

**kwa maana nawaambia**
Hii sentensi inatumika kusisitiza wa kile ambacho Yesu atakisema baada ya hiki.

**mzao wa mzabibu**
Hii inarejea "jwisi" ambayo inakamuliwa kutoka katika zabibu inayoota kwenye shamba la mizabibu. Divai inatokana na "jwisi" ya zabibu iliyochacha.

**mpaka ufalme wa Mungu utakapokuja**
Tafsiri mbadala: "Mpaka Mungu atakapoimarisha ufalme wake" au "mpaka Mungu atakapotawala katika ufalme wake.

## Luke 22:19

**mkate**
Huu mkate ni ule ambao haukuwa na hamila ndani yake, hivyo ilikuwa na chapati.

**akaumega**
"akaukata" au "akauchana." Aliugawanya kwenye vipande vingi vingi au aliugawanya kwenye vipande viwili na akawapa mitume kugawana miongoni mwao.

**Huu ni mwili wangu**
Inaweza kutafsiriwa kama 1) "Huu mkate ni mwili wangu" au 2) "Huu mkate unawakilisha mwili wangu."

**mwili wangu ambao umetolewa kwa ajili yenu**
"mwili wangu ambao nitautoa kwa ajili yenu" au "mwili wangu ambao nitautoa sadaka kwa ajili yenu" Tafsiri mbadala: "mwili wangu, ambao nautoa kwa wenye mamlaka kuuuwa kwa ajili yenu."

**Fanyeni hivi**
"kula huu mkate"

**kwa kunikumbuka mimi**
"ili kunikumbuka mimi"

**kikombe hiki**
Neno "kikombe" linamaanisha au linarejea divai ndani ya kikombe. Tafsiri mbadala: "Divai kwenye kikombe hiki" au "Divai hii."

**ni agano jipya katika damu yangu**
"ni agano jipya, ambalo litatoa matunda kwa damu yangu" au "ni agano jipya ambalo litahalarishwa kwa damu yangu" au "linawakirisha agano jipya, ambalo Mungu ataliimarisha wakati damu yangu itakapomwagwa"

**ambayo imemwagika kwa ajili yenu**
"damu yangu, ambayo imemwagwa katika kifo kwa ajili yenu" au "damu yangu, ambayo itatoka katika vidonda vyangu kwa ajili yenu nitakapokufa." Yesu aliongea kuhusu kifo chake kwa kurejea mwili wake kuvunjwa na damu yake kumwagwa.

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Luke 22:21

**Yeye anisalitie**
"Yeye atakaye nisaliti"

**Kwa maana Mwana wa Adamu kwa kweli aenda zake**
"Kwa kweli Mwana wa Adamu atakwenda" au "Kwa maana Mwana wa Adamu atakufa"

**kama ilivyokwisha amuliwa**
Tafsiri mbadala: "kama Mungu alivyokwisha amua" au "kama Mungu alivyokwisha kupanga"

**Lakini ole kwa mtu yule ambaye kupitia yeye Mwana wa Adamu asalitiwa**
Tafsiri mbadala: "Lakini ole kwa mtu yule amsalitie Mwana wa Adamu!" au "Lakini ni hatari kiasi gani kwa mtu yule amsalitie Mwana wa Adamu!"

## Luke 22:24

**Kisha yakatokea mabishano katikati yao**
"Kisha mitume wakaanza kubishana wao kwa wao"

**ni nani aliye mkubwa**
Tafsiri mbadala: "watu wangefikiri ni wa muhimu sana"

**Akawaambia**
"Yesu akawaambia mitume"

**wana ubwana juu yao**
"wanatawala kwa ukatili juu yao" au "wanapenda kutumia nguvu juu yao"

**wanaitwa**
Watu inawezekana hawakuwafikiria wale watawala kama watawala wakuheshimiwa. Tafsiri mbadala: "walipenda kuitwa" au "walijiita wenyewe."

**waheshimiwa watawala**
Tafsiri mbadala: "wafadhili" au "viongozi wanaowasaidia watu"

## Luke 22:26

**haitakiwi kuwa hivi kwenu ninyi**
"msifanye kama hivyo"

**mdogo kabisa**
Viongozi walikuwa mara nyingi watu wazima na waliitwa "wazee," "vijana wadogo" walikuwa na uwezekano mdogo wa kuongoza. Tafsiri mbadala: "enye umuhimu wa mwisho"

**Kwa**
Hii inaunganisha amri ya Yesu mstari wa 26 na mstari mzima wa 27. Inamaanisha kwamba mtu wa muhimu zaidi anatakiwa kutumika kwa sababu Yesu ni mtumishi.

**yule anayetumika**
"yule anayehudumia chakula" au "yule anayewahudumia waliokaa." Hii inamaanisha mtumishi.

**yupi mkubwa....tumika?**
"nani aliye wa muhimu....atumike?" Yesu anatumia swali kutambulisha jibu lake kwa swali la mitume kuhusu ukubwa. Tafsiri mbadala: "Nataka ninyi mfikiri kuhusu nani aliye mkubwa...atumike."

**yule aketie mezani**
"yule anayekula chakula"

**si yule aketiye mezani?**
Yesu anatumia swali jingine kuwafundisha wanafunzi. Tafsiri mbadala: "Bila shaka yule aketie mezani ni wa muhimu zaidi kuliko mtumishi!"

**Na mimi bado ni kati yenu kama atumikaye**
"Bado nawatumikia." Neno "bado" liko hapa kwasababu kunautofautishaji kati ya kile ambacho watu wangetegemea Yesu kuwa na kile ambacho kweli yuko.

## Luke 22:28

**mmeendelea kuwa nami katika majaribu yangu**
"mmekaa nami katika mapito yangu"

**Nawapa ninyi ufalme, kama vile Baba alivyonipa mimi ufalme**
Lugha nyingine zinaweza hitaji kubadilisha mpangilio. "Kama baba alivyonipa mimi ufalme, nami nawapeni."

**Nawapa ninyi ufalme**
"Nawafanya ninyi watawala katika Ufalme wa Mungu" au "Nawapa ninyi mamlaka kutawala katika ufalme" au "Nitawafanya ninyi wafalme"

**kama Baba alivyonipa mimi ufalme**
"kama Baba alivyonipa mimi mamlaka kutawala kama mfalme katika ufalme wake"

**Mtakaa kwenye viti vya enzi**
Tafsiri mbadala: "mtafanya kazi kama wafalme" au "mtafanya kazi za wafalme"

**Viti vya enzi**
Tafsiri mbadala: "Viti vya wafalme" au "viti vilivyotengenezwa kwa wafalme"

## Luke 22:31

**Taarifa ya kijumla:**
Yesu anaongea moja kwa moja na Simoni.

**Simon, Simon**
Yesu alilisema jina lake mara mbili kuonyesha kwamba kile ambacho alikuwa akiseme kwake kilikuwa cha muhimu sana.

**awapate, ili awapepete**
Neno "awa" linaonyesha mitume wote.

**awapepete kama ngano**
Hii inamaanisha kwamba Shetani alitaka kuwajaribu mitume ili kupata makosa.

**Lakini nimekuombea**
Hapa inamaanisha amemuombea kipekee kabisa SImoni.

**kwamba imani yako isishindwe**
"kwamba utaendelea kuwa na imani" au "utaendelea kunitegemea mimi"

**Baada ya kuwa umerudi tena**
"Baada ya kuanza kunifuata tena" au "Baada ya kuanza kunitumikia mimi tena"

**ndugu zako**
Hii inamaanisha wanafunzi wengine wa Yesu. Tafsiri mbadala: "Waamini wenzako" au "mitume wengine."

## Luke 22:33

**Jogoo hatawika leo, kabla hujanikana mara tatu kwamba unanijua**
Mpangilio wa maneno unaweza kubadilishwa na kusomeka: "Utanikana mara tatu kwamba unanijua kabla jogoo hajawika siku hii ya leo"

**Jogoo hatawika leo, kabla hujanikana**
Hii inaweza kuongelewa kwa namna chanya: "Jogoo atawika siku hii ya leo mara tu baada ya kunikana."

**Jogoo hatawika**
Hapa, kuwika kwa Jogoo kunaonyesha muda fulani katika siku. Jogoo mara nyingi huwika kabla ya jua kuchomoza asubuhi.

**siku hii**
Siku ya Kiyahudi huanza wakati wa kuzama kwa jua. Yesu alikuwa anaongea baada ya jua kuwa limezama. Jogoo angeliwika muda mchache kabla ya asubuhi. Asubuhi ilikuwa sehemu ya "siku hii." Tafsiri mbadala: "Usiku wa leo" au "asubuhi."

## Luke 22:35

**Nilipowapeleka ninyi**
Yesu alikuwa akiongelea kuhusu mitume wake.

**mfuko**
Mfuko ni begi la kuwekea fedha. Hapa inatumika kumaanisha "fedha."

**kikapu cha vyakula**
Tafsiri mbadala: "Begi la msafiri" au "chakula"

**Je mlipungukiwa na kitu? Wakajibu, "Hapana."**
Yesu anatumia swali kuwasaidia mitume kukumbuka namna ambavyo watu waliwahudumia vizuri walipokuwa wakisafiri. Tafsiri mbadala: Wakati ule...bado mlikuwa na kila kitu mlichokihitaji.' Na wanafunzi walikubali wakasema 'Ndiyo, tulikuwa na kila kitu tulichokihitaji."

**Hakuna**
"Hatukupungukiwa na kitu" au "Tulikuwa na kila kitu tulichokihitaji"

**Yule ambaye hana upanga, imempasa auze joho lake.**
Yesu alikuwa hamaanishi mtu falani kipekee ambaye hakuwa na upanga. Tafsiri mbadala:"Kama mtu hana upanga, anapaswa kuuza joho lake."

**joho**
"koti" au "nguo ya nje"

## Luke 22:37

**ambayo yameandikwa kwa ajili yangu**
Tafsiri mbadala:"ambayo nabii ameandika kuhusu mimi katika maandiko"

**lazima yatimilike**
Mitume wangelimuelewa Mungu kwamba angesababisha yote yaliyoandikwa kwenye maandiko kutokea. Tafsiri mbadala: "Mungu atatimiliza" au "Mungu atayafanya yatokee."

**alichukuliwa kama mtu ambaye anavunja torati**
Hapa Yesu ananukuu maandiko. Tafsiri mbadala: " watu walimchukulia kama mtu ambaye hafuati au hana sheria."

**Mvunja sheria**
"Wale wanaovunja sheria" au "waharifu"

**Kwa sababu kile kilichotabiriwa kwa ajili yangu**
Inaweza kumaanisha 1) "Yale ambayo mtume ametabiri kuhusu mimi yako tayari kutokea" au 2) "Kwa kuwa maisha yangu yanafikia ukingoni."

**wakasema**
Hii inamaanisha angalau wawili wa mitume wa Yesu.

**yatosha**
Inaweza kumaanisha 1) "Hizo panga zinatosha" au 2) "Hiyo inatosha kuiongelea." Yesu aliposema wanatakiwa kununua panga, alikuwa hasa akiwaambia kuhusu hatari ambazo wote watazikabili. Inawezekana si kwamba aliwataka wanunue panga na wapigane.

## Luke 22:39

**Baada ya chakula cha usiku**
Hii inamaanisha kukamilika kwa chakula cha Pasaka.

**kwamba msiingie majaribuni**
"kwamba hamjaribiwi" au "hakuna kitu cha kuwajaribu na kuwafanya kutenda dhambi"

### Luke 22:41

**mrusho wa jiwe**
"kama umbali wa mtu kurusha jiwe." Tafsiri mbadala: "umbali mfupi" au kwa kipimo cha kukadilia kama "umbali wa mita 30"

**Baba, kama unataka**
Yesu atabeba adhabu ya dhambi zote katika historia ya mwanadamu kwa adhabu ya msalabani. Anaomba kwa Baba yake akimuuliza kama kuna njia nyingine.

**Baba**
Hiki ni cheo muhimu kwa Mungu

**niondolee kikombe hiki**
Yesu anamaanisha juu ya mateso ambayo yuko karibu kuyapitia kana kwamba yalikuwa ndani ya kikombe na kwamba alikuwa anakwenda kukinywa. Tafsiri mbadala: "niondolee hiki kikombe cha mateso" au "niondolee haya mateso" au "niokoe kutoka katika kuteseka kwa namna hii."

**Lakini si kama nitakavyo mimi, lakini mapenzi yako yafanyike."**
Tafsiri mbadala: "Hata hivyo, nataka kufanya yale ambayo ni sawasawa na mapenzi yako kuliko yale ambayo ni sawasawa na mapenzi yangu.

### Luke 22:43

**akamtokea**
"akamtokea Yesu"

**akamtia nguvu**
"akamtia moyo"

**Akiwa katika kuugua, akaomba**
"Alikuwa katika kuugua, na akaomba"

### Luke 22:45

**Alipoamka kutoka katika maombi yake**
Tafrisi mbadala: "Wakati Yesu alipoamka baada ya kuomba" au "Baada ya kuomba, Yesu aliamka na"

**akawakuta wamelala kwa sababu ya huzuni nyingi**
"aliwaona kwamba walikuwa wamelala kwa sababu walikuwa na huzuni sana"

**Kwanini mnalala?**
Inaweza kumaanisha 1) "Nashangazwa kwamba mnalala sasa" au 2) "Hampaswi kuwa mmelala sasa hivi!"

**kwamba msiingie majaribuni**
"msijaribiwe" au "hakuna kitu cha kuwajaribu na kuwafanya mtende dhambi"

### Luke 22:47

**tazama, kundi kubwa la watu likatokea**
Neno "tazama" linatutazamisha kuhusu kundi jipya katika simulizi.

**akiwaongoza**
Yuda alikuwa akiwaonyesha watu Yesu alipo. Alikuwa hawaambii kundi la watu nini cha kufanya. Tafsiri mbadala: "akiwaongoza kwa Yesu."

**ili ambusu**
"kumsalimia kwa busu" au "kumsalimia kwa kumbusu." Wakati wanaume walipowasalimia wanaume wengine ambao walikuwa wa familia au marafiki, waliwakumbatia.

**je unamsaliti Mwana wa Adamu kwa busu**
Yesu anatumia swali kumkemea Yuda kwa kumsaliti kwa busu. Kwa kawaida busu ni ishara ya upendo. Tafsiri mbadala: "Ni busu unayotumia kumsaliti Mwana wa Adamu!"

**Mwana wa Adamu**
Yesu anatumia neno hili kujiongelea yeye.

### Luke 22:49

**wale waliokuwa karibu na Yesu**
Hii inaonyesha wanafunzi wa Yesu.

**hayo yanayotokea**
Tafsiri mbadala: "kwamba makuhani na maaskari walikuwa na watu wa kumkamata Yesu"

**akampiga mtumishi wa kuhani mkuu**
"akampiga mtumishi wa kuhani mkuu kwa panga"

**akagusa sikio lake**
Tafsiri mbadala: "akamgusa mahali ambapo sikio lake lilikuwa limekatwa"

### Luke 22:52

**Je mnakuja kana kwamba mnakuja kupambana na mnyang'anyi, na marungu na mapanga?**
"Je mnakuja na marungu na mapanga kwa sababu mnafikiri mimi ni mnyang'anyi?" Yesu anatumia hili swali kuwa tahayarisha viongozi wa Kiyahudi. Tafsiri mbadala: "Mnajua kwamba mimi si mnyang'anyi, na bado mnanijia mkileta mapanga na marungu."

**Nilipokuwa pamoja nanyi siku zote**
"Nilikuwa kati yenu kila siku"

**hekalu**
Tafsiri mbadala: "Uwanda wa ndani ya hekalu" au "katika hekalu"

**kuweka mikono yenu juu yangu**
Tafsiri mbadala: "kunikamata"

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**saa yako**
"muda wako"

**mamlaka ya giza**
Hii inamaanisha mtawala muovu, Shetani. Tafsiri mbadala: "muda kwa mtawala wa giza" au "muda ambao Shetani anafanya mambo maovu kama anavyopenda kufanya"

### Luke 22:54

**wakamuongoza**
"wakamuongoza Yesu kutoka kwenye bustani mahali ambapo walikuwa wamemkamata"

**walikuwa wamewasha moto**
Moto ulikuwa ni wakuwapa watu joto. Tafsiri mbadala: "baadhi ya watu walikuwa wamewasha moto."

**katikati ya uwanda wa ndani**
Huu ulikuwa uwanda katika nyumba ya kuhani mkuu. Ulikuwa na kuta pande zote, lakini bila paa.

### Luke 22:56

**akamtazama akamwambia**
"akamtazama moja kwa moja Petro na kusema na watu wengine pale uwandani"

**Huyu mtu pia alikuwa pamoja naye**
Mwanamke alikuwa anawaambia watu kuhusu Petro kuwa na Yesu. Inawezekana kwamba hakulijua jina la Petro.

**Lakini Petro akakana**
"Lakini Petro akasema haikuwa kweli"

**Mwanamke, mimi simjui**
Petro hakulijua jina la yule mwanamke. Hivyo alikuwa hamtukani kwa kumuita "mwanamke".

**Mwanaume, mimi siyo**
Petro hakulijua jina la yule mwanaume. Hivyo alikuwa hamtukani kwa kumuita "mwanaume".

### Luke 22:59

**akasisitiza akasema**
"alisema kwa msisitizo" au "alisema kwa sauti"

**Kweli kabisa huyu mtu**
Hapa "huyu mtu" inamaanisha Petro. Muongeaji inawezeka hakulijua jina Petro.

**ni Mgalilaya**
Mwanaume aliweza kuonyesha Petro alitokea Galilaya kutokana na jinsi alivyoongea.

**sijui usemalo**
Tafsiri mbadala: "kile ulichosema si kweli kabisa" au "kile ulichosema na uongo kabisa"

**wakati akiongea**
"wakati Petro alipokuwa akiongea"

### Luke 22:61

**neno la Bwana**
Tafsiri mbadala: "Neno la Yesu" au "Kile ambacho Yesu alikuwa amekisema"

**leo**
Yesu alikuwa ameishaongea jioni iliyopita kile kitakacho tokea muda si mrefu kabla ya jua kuchomoza au katika kuchomoza kwa jua. Tafsiri mbadala: "Usiku wa leo."

### Luke 22:63

**Baada ya kumfunika macho**
"Baada ya kuwa wamemfunika macho yake ili kwamba asiweze kuona"

**Tabiri! Ni nani aliyekupiga?**
Wale walinzi hawakuamini kwamba Yesu ni nabii. Badala yake waliamini kwamba nabii wa ukweli angemjua aliyempiga hata kama alikuwa hawezi kuona. Walimuita Yesu nabii, lakini walitaka kuonyesha kwamba hakuwa nabii. Tafsiri mbadala: "Jionyeshe kwamba wewe ni nabii. Tuambie nani amekupiga? au "Haloo nabii, nani amekupiga?"

**Tabiri**
"Kuongea neno kutoka kwa Mungu!" Taarifa kutokana na ukweli huu ni kwamba Mungu angelimwambia Yesu nani alimpiga kwa sababu Yesu alikuwa amefunikwa macho na hakuweza kuona.

### Luke 22:66

**Wakampeleka kwenye Baraza**
Inaweza kumaanisha 1) "Wazee walimleta Yesu kwenye baraza" au 2) "Walinzi walimpeleka Yesu mbele ya baraza la wazee."

**wakisema**
Hii inaweza kutafsiriwa kama sentensi mpya. Tafsiri mbadala: "Wazee wakamwambia Yesu"

**tuambie**
"tuambie kwamba wewe ni Kristo"

**Kama nikiwaambia...Kama nikiwauliza**
Yesu alisema kwamba haikuwa na maana kama angesema au angewauliza kusema, wasingejibu kwa ufasaha. Hizo sentensi mbili kwa pamoja zinaelezea mtazamo wa Yesu kwamba baraza lilikuwa kwa kweli halitafuti ukweli.

**Kama nikiwaambia hamtaniamini**
Hii ni moja ya maelezo ya kinadharia aliyoyatoa Yesu. Ilikuwa ni njia ya Yesu kujibu bila kuwapa sababu ya kusema kwamba alikuwa anahatia ya kukufuru.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**kama nikiwauliza hamtanijibu**
Haya yalikuwa maelezo ya pili ya kinadharia

### Luke 22:69

**kuanzia sasa**
"kuanzia siku hii" au "kuanzia kutoka leo"

**Mwana wa Adamu**
Yesu alitumia sentensi hii kumaanisha Kristo. Alimaanisha kwamba alikuwa akijiongelea mwenyewe, lakini wazee iliwalazimu kuuliza kuona kama hivyo ndivyo kweli alikuwa akisema.

**amekaa mkono wa kuume wa nguvu ya Mungu**
Wayahudi walielewa kwamba hakuna hata mmoja ambaye angeweza kukaa pale.Waliiona hii ni sawa na kusema "atakuwa na Mungu kama Mungu."

**nguvu ya Mungu**
"Mungu mwenye nguvu zote." Hapa "nguvu" inamaanisha mamlaka yake kuu.

**Kwa hiyo wewe ni Mwana wa Mungu?**
Baraza lilimhukumu Yesu kusulubiwa kwa sababu alijithibitishia kwamba yeye alikuwa "Mwana wa Mungu," akijua Baraza litamhukumu kifo.

**Mwana wa Mungu**
Hiki ni cheo muhimu kwa Yesu.

**Ninyi mmesema mimi ndiye**
"Ndiyo, ni kama mlivyosema"

**Kwanini bado tunahitaji tena ushahidi?**
Walitumia swali kwa kuweka msisitizo. Tafsiri mbadala: "Hatuna haja tena ya kuwa na ushahidi!"

**tumesikia kutoka katika kinywa chake mwenyewe**
Tafsiri mbadala: "tumesikia moja kwa moja kutoka kwake kwamba anaamini yeye ni Mwana wa Mungu"

---



generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 23

1 Mkutano wote wakasimama, wakampeleka Yesu mbele ya Pilato. 2 Wakaanza kumshutumu, wakisema,
"Tumemkuta mtu huyu akipotosha taifa letu, kwa kukataza tusitoe kodi kwa Kaisari, na akisema kwamba
yeye mwenyewe ni Kristo, Mfalme." 3 Pilato akamuuliza, akisema, "Je wewe ni Mfalme wa Wayahudi?" Na
Yesu akamjibu akisema, "Wewe wasema hivyo". 4 Pilato akamuambia kuhani mkuu na makutano, "Sioni
kosa kwa mtu huyu". 5 Lakini wao wakasisitiza, wakisema, " Amekuwa akiwachochea watu, akifundisha
katika Uyahudi yote, kuanzia Galilaya na sasa yuko hapa." 6 Pilato aliposikia haya, akaulizia kama mtu
huyo ni wa Galilaya? 7 Alipotambua kuwa alikuwa chini ya utawala wa Herode, akampeleka Yesu kwa
Herode, ambaye naye alikuwa Yerusalemu kwa siku hizo. 8 Herode alipomuona Yesu, alifurahi sana
kwasababu alitaka kumuona kwa siku nyingi. Alisikia habari zake na alitamani kuona moja ya miujiza
ikifanywa na yeye. 9 Herode alimhoji Yesu kwa maneno mengi, lakini Yesu hakumjibu chochote. 10
Makuhani wakuu pamoja na waandishi walisimama kwa ukali wakimshitaki. 11 Herode pamoja na
maaskari wake, walimtukana na kumdhihaki, na kumvika mavazi mazuri, kisha akamrudisha Yesu kwa
Pilato. 12 Herode na Pilato wakawa marafiki kuanzia siku hiyo, (kabla ya hapo walikuwa maadui). 13
Pilato akawaita pomoja makuhani wakuu na watawala na umati wa watu, 14 Akawaambia, "Mmeniletea
mtu huyu kama mtu anaye waongoza watu wafanye mabaya, na tazama, baada ya kuwa nimemhoji mbele
yenu, sikuona kosa kwa mtu huyu kuhusu mambo yote ambayo ninyi mnamshitaki yeye. 15 Hapana, wala
Herode, kwa maana amemrudisha kwetu, na tazama hakuna chochote alichokifanya kinachostahili
adhabu ya kifo. 16 Kwahiyo basi nitamuadhibu na kumuachilia. 17 (Sasa, Pilato anawajibika kumuachilia
mfungwa mmoja kwa wayahudi wakati wa sikukuu). 18 Lakini wote wakapiga kelele pamoja, wakisema,
"Mwondoe huyo, na tufungulie Baraba!" 19 Baraba alikuwa ni mtu ambaye amewekwa gerezani kwa
sababu ya uasi fulani katika jiji na kwa kuua. 20 Pilato akawaambia tena, akitamani kumwachilia Yesu. 21
Lakini wao wakapiga kelele, wakisema, "Msulibishe, msulibishe." 22 Akawauliza kwa mara ya tatu, "kwa
nini, huyu mtu amefanya maovu gani? Sikupata kosa linalostahili adhabu ya kifo kwake. Kwahiyo nitakapo
maliza kumuadhibu nitamuachilia." 23 Lakini wakasisitiza kwa sauti ya juu, wakitaka asulubiwe. Na sauti
zao zikamshawishi Pilato. 24 Hivyo Pilato akaamua kuwapatia matakwa yao. 25 Akamuachilia yule
waliyemtaka ambaye alifungwa kwa kusababisha ghasia na kuua. Lakini akamtoa Yesu kwa matakwa yao.
26 Walipokuwa wakimpeleka, walimkamata mtu mmoja aitwaye Simoni wa Ukirene, akitokea katika nchi,
wakamtwika msalaba ili abebe, akimfuata Yesu. 27 umati mkubwa wa watu, na wanawake ambao
walihuzunika na kuomboleza kwa ajili yake, walikuwa wakimfuata. 28 Lakini akawageukia, Yesu
akawaambia, 'Mabinti wa Yerusalemu, msinililie mimi, bali jililieni ninyi wenyewe na kwa ya ajili watoto
wenu. 29 Tazama, siku zinakuja ambazo watasema, "Wamebarikiwa walio tasa na matumbo yasiyozaa, na
matiti ambayo hayakunyonyesha. 30 Ndipo watakapo anza kuiambia milima, 'Tuangukieni,' na vilima,
'Mtufunike.' 31 Maana kama wakifanya mambo haya ikiwa mti mbichi, itakuwaje ukiwa mkavu?" 32
wanaume wengine, wahalifu wawili, walipelekwa pamoja naye ili wauwawe. 33 Walipofika mahali
paitwapo Fuvu la kichwa, ndipo wakamsulubisha pamoja na wale wahalifu, mmoja upande wa kulia na
mwingine upande wa kushoto. 34 Yesu alisema, "Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo. "Nao
wakapiga kura, kugawa mavazi yake. 35 Watu walikuwa wamesimama wakiangalia huku watawala
wakimdhihaki, wakisema, "Aliwaokoa wengine. Sasa ajiokoe mwenyewe, kama yeye ni Kristo wa Mungu,
mteule". 36 Askari pia walimdharau, walimkaribia yeye na wakumpa siki, 37 wakisema, "Kama wewe ni
Mfalme wa Wayahudi jiokoe mwenyewe" 38 Kulikuwa pia na alama juu yake iliyoandikwa "HUYU NDIYE
MFALME WA WAYAHUDI." 39 Mmoja wa wahalifu aliyesulubishwa alimtukana akisema, "Wewe si Kristo?
jiokoe mwenyewe na sisi" 40 Lakini yule mwingine akajibu, akimkemea na akisema, "Je wewe humuogopi
Mungu, nawe uko katika hukumu hiyo hiyo? 41 Sisi tupo hapa kwa haki, kwa maana sisi tunapokea kile
tunachostahili kwa matendo yetu. Lakini mtu huyu hakufanya chochote kibaya." 42 Na aliongeza, "Yesu,
nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako." 43 Yesu akamwambia, "Amini nakuambia, leo hii utakuwa
pamoja nami Paradiso." 44 Hapo ilikuwa karibu saa ya sita, giza likaja juu ya nchi yote hadi saa ya tisa, 45
Mwanga wa jua ulizimika. Kisha pazia la hekalu likagawanyika katikati kuanzia juu. 46 Akilia kwa sauti
kuu, Yesu alisema, "Baba mikononi mwako naiweka roho yangu," baada ya kusema haya, akafa. 47 Wakati
Akida alipoona yaliyotendeka alimtukuza Mungu akisema, "Hakika huyu alikuwa mtu mwenye haki." 48
Wakati umati wa watu waliokuja pamoja kushuhudia walipoona mambo yaliyofanyika, walirudi huku
wakipiga vifua vyao. 49 Lakini marafiki zake, na wanawake waliomfuata toka Galilaya, walisimama kwa
mbali wakiangalia hayo mambo. 50 Tazama, palikuwepo na mtu aitwaye Yusufu, ambaye ni mmoja wa
baraza, mtu mzuri na mwenye haki, 51 (alikuwa hajakubaliana na maamuzi au matendo yao), kutoka

Armathaya, mji wa Kiyahudi, ambao ulikua ukisubiria ufalme wa Mungu. **52** Mtu huyu, alimkaribia Pilato,
akaomba apewe mwili wa Yesu. **53** Alimshusha, na akauzungushia sanda, na akaumweka katika kaburi
lililokuwa limechongwa katika jiwe, ambalo hakuna aliyewahi kuzikwa. **54** Ilikuwa ni siku ya maandalizi,
na Sabato inakaribia. **55** Wanawake, waliokuja nao kutoka Galilaya, walimfuata, na wakaona kaburi na
jinsi mwili wake ulivyolazwa. **56** Walirudi na kuanza kuandaa manukato na marashi. Kisha siku ya sabato
walipumzika kwa mujibu wa sheria.

---

## Luka 23 Maelezo ya Jumla

### Muundo na upangiliaji

ULB huweka mbele kidogo mstari wa mwisho wa sura hii kwa sababu unaunganishwa zaidi na sura ya 24 kuliko sura ya 23.

### Dhana maalum katika sura hii

### "Walianza kumshtaki"

Watu hawa hawakuwa wakimshtaki Yesu kwa kufanya uovu, bali mashtaka yao yalikuwa ya uwongo. Waligeuza ukweli ili kumfanya Pilato kumhukumu Yesu kufa.

### "Pazia la hekalu likagawanyika na kuwa vipande viwili"

Hii ni ishara muhimu. Pazia ilikuwa mfano ya utenganisho kati ya Mungu na mwanadamu. Mungu hakuweza kupatikana moja kwa moja kwa sababu ya utakatifu wake. Kifo cha Kristo kilibadilisha hii.

### Desturi ya Mazishi

Ilikuwa ni desturi katika Israeli ya kale kumzika mtu aliyeheshimika katika kaburi na kutumia mwamba mkubwa kuifunga.

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

### "Sioni kosa lolote katika mtu huyu.""

Baada ya swali moja rahisi, inaonekana kwamba Pilato anamtangaza Yesu kutokuwa na hatia haraka sana. Hii ni kwa sababu Luka hajaweka maelezo mengi ya mazungumzo ya Yesu na Pilato. Habari hii imeandikwa katika Injili nyingine.

---

### Luke 23:1

**Mkutano wote**
"Viongozi wote wa Kiyahudi"

**wakasimama**
"kusimama" au "kusimama kwa miguu yao"

**mbele ya Pilato**
"kuwa mbele ya Pilato". Kusimama kwa kumuangalia Pilato"

**akipotosha taifa letu**
"kusababisha ghasia kwa kuelezea uongo kwa watu"

**kwa kukataza tusitoe kodi**
"kwa kuwaambia wasitoe kodi"

### Luke 23:3

**Pilato akamuuliza**
"Pilato akamuuliza Yesu"

**Wewe wasema**
"Ulichokisema ni sawa" au " Ni kama ulivyo niuliza mimi"

**makutano**
"Mkusanyiko wa watu"

**Sioni kosa kwa mtu huyu**
"Sijaona kuwa mtu huyo ana hatia ya kitu chochote)

**akiwachochea**
"kusababisha ghasia miongoni"

**kuanzia Galilaya na sasa yuko hapa**
Hii inaweza kutafsiriwa kama sentensi mpya. "Alianza kusababisha ghasia huko Galilaya na sasa anasababisha ghasia hapa"

### Luke 23:6

**aliposikia haya**
"kusikia kuwa Yesu alianza kufundisha huko Galilaya"

**kama**
kama

**mtu huyu**
Hii inamaanisha Yesu

**alipotambua**
"Pilato akatambua"

**alikuwa chini ya utawala wa Herode**
Kifungu hiki hakitaji ukweli unaoelekea kuwa Herode alikuwa Mtawala wa Galilaya. "Yesu alikuwa chini ya utawala wa Herode kwasababu Herode alitawala Galilaya"

**akatuma**
"Pilato alituma"

**ambaye mwenyewe**
Hii inamaanisha Herode

**kwa siku hizo**
"Wakati wa sherehe za Pasaka"

### Luke 23:8

**alifurahi sana**
"Herode alifurahi sana"

**alitaka kumuona**
"Herode alihitaji kumuona Yesu"

**Alisikia habari zake**
"Herode alisikia habari ya Yesu"

**na alitamani**
"Herode alitamani"

**kuona baadhi ya miujiza anayoifanya**
"kumuona yeye akifanya baadhi ya miujiza"

**Herode alimhoji Yesu kwa maneno mengi**
"Herode alimuuliza Yesu maswali mengi"

**hakumjibu chochote**
"Hakumjibu" au "hajampa Herode majibu"

**walisimama**
"walisimama pale"

**kwa ukali kumshutumu**
"walimshutumu Yesu kwa ukali" au "walimshutumu yeye kwa hasira"

### Luke 23:11

**na kumvika mavazi mazuri**
Tafsiri hii haimaanishi walifanya hivyo ii kumuheshimu au kumjali Yesu. Walifanya hivyo kumdhalilisha na kumdhihak Yesui"

**Herode na Pilato wakawa marafiki kuanzia siku hiyo**
Maelezo yaha yana maanisha walianza urafiki kwasababu Herode alifurahia kitendo cha Pilato kumruhusu kumuhukumu Yesu. "Herode na Pilato wakawa marafiki kuanzia siku hiyo kwasababu Pilato alituma Yesu apelekwe kwa Herode ili akahukumiwe"

**kabla**
"kabla ya siku ile"

### Luke 23:13

**akawaita pomoja makuhani wakuu, watawala na umati wa watu**
"Aliwaita Makuhani na watawala na umati wa watu kuja kukutana pamoja"

**tazama nimemuhoji mbele yenu**
"Nimemuuliza Yesu Mbele yenu". Nimemuhoji Yesu wakati ninyi mnashuhudia hapa"

**na sikuona kosa**
"Na sifikiri kwamba ana hatia"

### Luke 23:15

**Hapana, hata Herode hajaona**
"Hata Herode hafikiri kwamba ana hatia" au "Hata Herode anafikiri kuwa hana hatia"

**kwa**
"kwasababu" au "tunjua hili ni kwasababu"

**amemrudisha kwetu**
"Herode alituma Yesu arudishwe kwetu" Neno "kwetu" linamaanisha Pilato na askari wake,na siyo makuhani na waandishi waliokwenda kwa Herode pamoja na Yesu, wala sio makutano.

**hakuna chochote alichokifanya kinachostahili adhabu ya kifo**
"hakufanya kitu chochote kinachostahili adhabu ya kifo"

**Kwahiyo basi nitamuadhibu**
Kwa sababu Pilato alikuwa hakuona kosa kwa Yesu anapaswa kumtoa bila adhabu. Siyo lazima kujaribu kufanya kauli hii iendane na tafsiri kifikra. Pilato alimuadhibu Yesu, ambaye alijua kuwa hana hatia, kwa sababu tu alikuwa na hofu ya umati wa watu.


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

### Luke 23:18

**wote wakapiga kelele pamoja**
"Watu wote kwenye mkusanyiko walipiga kelele"

**Mwondoe mtu huyu**
"Mchukue mtu huyu mbali ". Mchukuwe mtu huyu mbali na kumnyonga"

**ambaye amewekwa gerezani**
"ambaye Warumi walimuweka gerezani"

**kwa**
"kwasababu ya kujihusisha" au " kwasababu ya uhalifu wake"

**ya uasi fulani**
"alijarubu kuwahamasisha watu wa mji kuasi dhidi ya serikali ya Kirumi"

### Luke 23:20

**akawaambia tena**
"akaongea nao tena" au "aliongea tena na watu kwenye mkusanyiko"

**akitamani kumuachilia Yesu**
"kwasababu alitaka kumuachilia Yesu"

**Akawaambia kwa maraya tatu**
"Pilato akasema na mkutano tena, kwa mara ya tatu"

### Luke 23:23

**wakasisitiza**
"Mkusanyo walisisitiza"

**kwa sauti ya juu**
"kwa kupiga kelele"

**wakitaka asulubiwe**
"Kwa Pilato kuwaamuru askari wake wamsulubishe Yesu"

**Na sauti zao zikamshawishi Pilato**
"Na umati wakandelea kupiga kelele hadi wakamshawishi Pilato"

**kuwapa matakwa yao**
"kufanya kile ambacho umati walitaka"

**Akamuachilia yule waliyemtaka**
"Pilato akamuachilia Barnaba ambaye umati walimuomba aachiliwe"

**Aliyefungwa Jela**
"ambaye Warumi walimuweka Jela"

**Akamtoa Yesu kwa matakwa yao**
"Pilato aliwaruhusu umati wafanye kwa Yesu chochote walivyotaka" au "Pilato alimtoa Yesu kwa umati wa watu na kuwaruhu umati kufanya kwa Yesu kile walicho kitaka."

### Luke 23:26

**Walipokuwa wakimpeleka**
"wakati maaskari wakimpeleka Yesu mbali na alipokuwapo Pilato"

**walimkamata Simon wa Ukirene**
Maaskari wa Kirumi wana mamlaka ya kuwashurutisha watu kuwabebea mizigo yao". Usitafsiri kana kwamba Simoni amekamatwa au alifanya kosa fulani.

**mmoja**
"mtu aitwaye "

**akitokea katika nchi**
"aliyekuwa anakuja Yerusalemu akitokea nje ya mji"

**wakamtwika msalaba**
"kuweka msalaba juu ya mabega yake"

### Luke 23:27

**waliomboleza kwa ajili yake**
"kuomboleza kwa ajili ya Yesu"

**wakimfuata**
"waliokuwa wakimfuata Yesu"

**Mabinti wa Yerusalemu**
"Mabinti" wa mji maana yake watu wa mji . "ninyi wanawake mliotoka Yerusalemu"

**msinililie mimi**
"kulia kwaajili ya hali yangu"

**bali jililieni ninyi wenyewe na kwa ajili ya watoto weno**
"badala yake mlie kwa ajili ya mambo yanayokwenda kutokea kwa ajili yenu na watoto wenu"

### Luke 23:29

**ambao watasema**
"watu watakaposema"

**waliotasa**
"wanawake ambao hawakuzaa watoto"

**ndipo**
"Kwa wakati huo"

**kuambia milima**
"wataiambia milima"

**Maana kama wakifanya mambo haya ikiwa mti mbichi, itakuwaje kwa mti uliokauka?**
Yesu anatumia swali kusaidia umati kuelewa kwamba watu wanafanya mambo mabaya sasa katika nyakati nzuri, hivyo kwa hakika watafanya mambo mabaya zaidi katika nyakati mbaya siku


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

zijazo. "Unaweza kuona kwamba wanafanya mambo hayo mabaya wakati mti ni mbichi, hivyo unaweza kuwa na uhakika kwamba watafanya mambo kuwa mabaya wakati mti ni kavu."

**mti mbichi (kijani)**
mti mbichi(kijani) ni mfano wa kitu kilichokizuri kwa sasa . Kama lugha yako ina mfano mzuri unaweza kutumia hapa.

**uliokauka**
"Mti uliokauka ni mfano wa kitu kibaya baadaye"

**wakifanya**
hapa alikuwa akimaanisha aidha Warumi au viongozi wa kiyahudi au hakuna aliyelengwa moja kwa moja "

### Luke 23:32

**wanaume wengine, wahalifu wawili, walipelekwa pamoja naye ili wauwawe**
"Maaskari waliwapeleka wahalifu wengine wawili pamoja na Yesu ili wakauwawe pia.

### Luke 23:33

**walipofika**
Neno "walipofika" inajumuisha maaskari, wahalifu na Yesu.

**wakamsulunisha**
"maaskari wakamsulubisha Yesu"

**mmoja upande wa kulia**
"mmoja wa wahalifu aliwekwa upande wa kulia wa Yesu"

**na mwingine upande wa kushoto**
" na muhalifu mwingine aliwekwa upande wa kushoto mwa Yesu"

**Baba, uwasamehe wao**
Neno "wao" inamaanisha wale wanao msulubisha Yesu. Yesu aliongea kwa huruma na Baba yake juu ya wanaume waliokuwa wanamsulubisha"

**Baba**
Hii ni cheo muhimu kwa Mungu

**kwa kuwa hawajui watendalo**
"kwasababu hawajui kile wanachokifanya". Maaskari hawakujua kuwa wanamsulubisha Mwana wa Mungu. Kwasababu hakika hawamjui ni nani wanayemsulubisha"

**wakapiga kura**
Maaskari walifanya aina ya kamari "walifanya kamari"

**kugawa mavazi yake**
"kuamua nani kati ya maaskari atapeleka nyumbani sehemu ya mavazi ya Yesu"

### Luke 23:35

**walisimama**
"walisimama pale"

**Yeyey**
Hii inamaanisa Yesu.

**ajiokoe mwenyewe**
"Yesu atakuwa na uwezo wa kujiokoa" au "Tunataka kuona akijionyesha yeye ni nani kwa kujiokoa mwenyewe kutoka msalabani"

**aliyechaguliwa**
"mmoja ambaye Mungu alimchagua"

### Luke 23:36

**yeye**
"Yesu"

**walimkaribia yeye**
"kuja karibu na Yesu"

**wakampa siki**
" walimpa Yesu siki ili anywe" Siki ni aina ya kinyaji kirahisi ambayo watu wa kawaida hunywa. Maaskari walimdhihaki Yesu kwa kumpa siki mtu aliyesema yeye ni mfalme.

**alama juu yake**
" kitu kama ubao juu ya msalaba wa Yesu iliyoandikwa"

**HUYU NDIYE MFALME WA WAYAHUDI**
Watu walioweka alama juu ya Yesu walikuwa wakimdhihaki yeye. Hawakuamini kweli kuwa yeye ni mfalme.

### Luke 23:39

**Aliyesulubiwa**
"aliyeangikwa pia msalabani"

**alimtukana**
"alimtukana Yesu"

**Wewe si Kristo?**
Muhalifu alitumia swali kumdhihaki Yesu."umedsi kuwa wewe ni Kristo"

**Jiokoe mwenyewe na sisi pia**
Muhalifu hakufikiri kweli kuwa Yesu angeweza kuwaokoa kutoka kwenye msalaba"

**yule mwingine akajibu**
"muhalifu mwingine alijibu"

**akimkemea na kusema**
"na kumkemea yule muhalifu akisema"

**Je wewe humuogopi Mungu, kwani uko katika hukumu hiyo hiyo**
Muhalifu alitumia swali kumkemea yule muhalifu mwingine. " Hauna hofu ya Mungu , kwani unamdhihaki Yesu wakati umetundikwa msalabani kama yeye.

**sisi tupo hapa kwa haki**
"Kiukweli sisi tunastahili adhabu hii"

**mtu huyu**
Hii inamaanisha Yesu.

### Luke 23:42

**Na akaongeza**
"Muhalifu pia akasema "

**utakapokuja katika ufalme wako**
"Utakapo anza kutawa kama Mfalme"

**Ukweli nakuambia**
"Ukweli" inaongeza msisitizo wa kile ambacho Yesu anaongea. "Nataka wewe uelewe kuwa"

**Paradiso**
Hii ni sehemu ambayo watu wema huenda wanapokufa. Yesu alikuwa akimthibitishia mtu yule kuwa atakuwa na Mungu na Mungu atamkubali yeye. "Ni mahali pa furaha" au 'Ni mahali pa watu wenye haki" au "Ni mahali ambapo watu wanaishi vizuri."

### Luke 23:44

**ilikuwa karibu saa sita**
"Ilipokaribi mchana" . Hii huonyesha desturi ambayo watu huanza kuhesabu saa kuanzia saa 12 asubuhi.

**giza likaja juu ya ardhi yote**
"ardhi yote ikawa giza"

**hadi saa tisa**
"Hadi 9 Mchana" Hii huonyesha desturi ambayo watu huanza kuhesabu saa kuanzia saa 12 asubuhi.

**pazia la hekalu**
"Pazia ndani ya Hekalu"

**likagawanyika katikati**
"ilichanika vipande viwili" . "Mungu alichana pazia la hekalu katika vipande viwili"

### Luke 23:46

**Akilia kwa sauti kuu, Yesu alisema, "Baba mikononi mwako naiweka roho yangu,"**
Mungu Baba alikuwa amemtuma Mungu Mwana kufa msalaba ili afanyike sadaka ya mwisho kwa ajili ya dhambi za binadamu. Lakini, Mwana bado alimpenda Baba na kumkabidhi maisha yake kwa Baba yake

**Akilia**
"kupasa sauti"

**Baba**
Hii ni cheo muhimu kwa Mungu

**mikononi mwako naiweka roho yangu**
"Naiweka roho yangu kwako" au " Nakupa roho yangu, nikijua utaitunza"

**baada ya kusema hivyo**
"Baada ya Yesu kusema hivyo"

**akafa**
"Yesu akafa"

**yaliyotendeka**
"mambo yaliyotokea"

### Luke 23:48

**umati**
"Mkusanyiko wa watu"

**tukio**
"tukio"au "kile kinachotokea"

**waliokuja pamoja**
"waliokusanyika pamoja"

**mambo yaliyofanyika**
"kitu kilichofanyika"

**walirudi**
"kurudi majumbani mwao"

**wakipiga matiti yao**
"wakipiga vifuani mwao wakionyesha jinsi walivyosikitika"

**marafiki zake**
"wale waliomjua Yesu" au "wale waliokutana na Yesu huko nyuma"

**waliomfuata yeye**
"walimfuata Yesu"

**kwa mbali**
"umbali fulani kutoka alipo Yesu"

**hayo mambo**
"yaliyotokea"

### Luke 23:50

**Tazama, palikuwa na mtu**
Neno 'tazama' inatufanya tuweze kumuona mtu mpya katika hadithi. Lugha yako inaweza kuwa njia ya kufanya hili. "Kulikuwa na mtu ambaye alikuwa".

**ambaye ni mmoja wa baraza**
"na Yeye alikuwa mmoja wapo wa wajumbe wa baraza la Wayahudi"

**mzuri na mwenye haki**
Hii inaweza kutafsiriwa kama sentensi mpya. "Yeye alikuwa mtu mzuri na mweye haki"

**alikuwa hajakubaliana na maamuzi au matendo yao**
Hii inaweza kutafsiriwa kama sentensi mpya." Joseph hakukubaliana na uamuzi wa baraza hilo kumuua Yesu na hatua ya baraza hilo"

**kutoka Armathaya, Mji wa Kiyahudi**
Hii inaweza kutafsiriwa kama sentensi mpya." Josefu alitokea kwenye mji wa kiyahudi ulioitwa Arimathaya"

**ambaye alikua akisubiri**
Hii inaweza kutafsiriwa kama sentensi mpya."Josefu alikuwa akisubiri"

### Luke 23:52

**Mtu huyu**
"Josefu "

**alimkaribia Pilato, akaomba**
"alikwenda kwa Pilato na kuomba"

**Alimshusha chini**
"Josefu alichukua mwili wa Yesu kutoka msalabani"

**akauzungushia sanda**
"Akafunga mwili katika nguo nzuri ya kitani'

**akamweka katika kaburi**
"kuweka mwili wa Yesu kwenye kaburi" au "Kuweka mwili wa Yesu kwenye chumba cha kuzikia"

**lililokuwa limechongwa katika jiwe**
"Kaburi ambalo mtu alilichonga kwenye mwamba"

**ambalo hakuna aliyewahi kulazwa**
Hii inaweza ikatafsiriwa kama sentensi mpya. "Hakuna aliyewahi kuweka mwili katika kaburi hilo"

### Luke 23:54

**Ni siku ya maandalizi**
"Ni siku ambayo watu wanajiandaa kwa siku ya Wayahudi kupumzika iitwayo Sabato"

**Sabato inakaribia**
"Inakaribia kuwa jioni, kuanza kwa Sabato" Alfajiri hapa ni mfano kwa ajili ya mwanzo wa siku. Kwa Wayahudi, siku ilianza jioni.

**waliokuja nao kutoka Galilaya**
"waliosafiri na Yesu kutoka jimbo la Galilaya"

**walimfuata baada**
"walimfuata Josefu na wanaume waliokuwa pamoja naye"

**wakaona kaburi**
"wanawake wakaona kaburi"

**na jinsi mwili wake ulivyolazwa**
"Wanawake waliona jinsi hao wanaume walivyomlaza mwili wa Yesu ndani ya kaburi"

**walirudi**
"wanawake walienda kwenye nyumba ambayo wanawake hao wanakaa"

**kuandaa manukato na marashi**
"kuandaa manukato na marashi ili kuandaa Mwili wa Yesu kwa ajili ya mazishi".

**walipumzika**
"wanawake wale hawakufanya kazi"

**kulingana na amri**
"Kulingana na sheria za Wayahudi" au "kama sheria ya Wayahudi inavyotaka"

 generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

## Chapter 24

1 Mapema sana siku ya kwanza ya juma, walikuja kaburini, wakileta manukato ambayo walikuwa
wameyaandaa. 2 Wakakuta jiwe limevingirishwa mbali na kaburi. 3 Wakaingia ndani, lakini hawakuukuta
mwili wa Bwana Yesu. 4 Ilitokea kwamba, wakati wamechanganyikiwa kuhusu hili, ghafla, watu wawili
walisimama katikati yao wamevaa mavazi ya kung'aa. 5 Wanawake wakiwa wamejaa hofu na
wakiinamisha nyuso zao chini, wakawaambia wanawake, "Kwanini mnamtafuta aliye hai miongoni mwa
wafu? 6 Hayupo hapa, ila amefufuka! Kumbukeni alivyosema nanyi alipokuwa angali Galilaya, 7 akisema
kwamba Mwana wa Adamu lazima atolewe kwenye mikono ya watu wenye dhambi na asulubishwe, na
siku ya tatu, afufuke tena." 8 Wale wanawake wakakumbuka maneno yake, 9 na wakarudi kutoka kaburini
na wakawaambia mambo haya yote wale kumi na moja na wengine wote. 10 Basi Maria Magdalena, Joana,
Maria mama wa Yakobo, na wanawake wengine pamoja nao wakatoa taarifa hizi kwa mitume. 11 Lakini
ujumbe huu ukaonekana kama mzaha tu kwa mitume, na hawakuwaamini wale wanawake. 12 Hata hivyo
Petro aliamka, na akakimbia kuelekea kaburini, na akichungulia na kuangalia ndani, aliona sanda peke
yake. Petro kisha akaondoka akaenda nyumbani kwake, akistaajabu nini ambacho kimetokea. 13 Na
tazama, wawili miongoni mwao walikuwa wakienda siku hiyo hiyo katika kijiji kimoja kiitwacho Emmau,
ambacho kilikuwa maili sitini kutoka Yerusalemu. 14 Wakajadiliana wao kwa wao kuhusu mambo yote
yaliyotokea. 15 Ikatokea kwamba, wakati walipokuwa wakijadiliana na kuulizana maswali, Yesu akasogea
karibu akaambatana nao. 16 Lakini macho yao yalizuiliwa katika kumtambua yeye. 17 Yesu akawaambia,
"Nini ambacho ninyi wawili mnakiongelea wakati mnatembea?" Wakasimama pale wakionekana na
huzuni. 18 Mmoja wao, jina lake Cleopa, akamjibu, "Je wewe ni mtu pekee hapa Yerusalemu ambaye hajui
mambo yaliyotokea huko siku hizi?" 19 Yesu akawaambia, "Mambo gani?" Wakamjibu, "Mambo kuhusu
Yesu Mnazareti, ambaye alikuwa nabii, muweza katika matendo na maneno mbele za Mungu na watu
wote. 20 Na kwa jinsi ambayo wakuu wa makuhani na viongozi wetu walivyomtoa kuhukumiwa kifo na
kumsulubisha. 21 Lakini tulitumaini kwamba yeye ndiye atakaye waweka huru Israeli. Ndiyo, mbali na
haya yote, sasa ni siku ya tatu tangu mambo haya yatokee. 22 Lakini pia, baadhi ya wanawake kutoka
katika kundi letu walitushangaza, baada ya kuwapo kaburini asubuhi na mapema. 23 Walipoukosa mwili
wake, wakaja, wakisema kwamba waliona pia maono ya malaika waliosema kwamba yu hai. 24 Baadhi ya
wanaume ambao walikuwa pamoja nasi walienda kaburini, na kukuta ni kama vile wanawake
walivyosema. Lakini hawakumuona yeye." 25 Yesu akawaambia, "Ninyi watu wajinga na wenye mioyo
mizito ya kuamini yote ambayo manabii wamesema! 26 Je haikuwa lazima Yesu kuteseka kwa mambo
haya, na kuingia katika utukufu wake?" 27 Kisha kuanzia kutoka kwa Musa na manabii wote, Yesu
akawatafsiria mambo yanayomuhusu yeye katika maandiko yote. 28 Walipokaribia kile kijiji, huko
walikokuwa wakienda, Yesu akafanya kana kwamba anaendelea mbele. 29 Lakini walimlazimisha,
wakisema, "Kaa pamoja nasi, maana inaelekea jioni na siku ni kama imeisha." Hivyo Yesu akaingia
kwenda kukaa nao. 30 Ilitokea kwamba, wakati amekaa nao kula, alichukua mkate, akaubariki, na
kuuvunja, akawapa. 31 Kisha macho yao yakafunguliwa, wakamjua, na akatoweka ghafla mbele ya macho
yao. 32 Wakasemezana wao kwa wao, "Hivi mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, wakati alipoongea nasi
njiani, wakati alipotufungulia maandiko?" 33 Wakanyanyuka saa hiyo hiyo, na kurudi Yerusalemu.
Wakawakuta wale kumi na mmoja wamekusanyika pamoja, na wale waliokuwa pamoja nao, 34 wakisema,
"Bwana amefufuka kwelikweli, na amemtokea Simoni." 35 Hivyo wakawaambia mambo yaliyotokea njiani,
na namna Yesu alivyodhihirishwa kwao katika kuumega mkate. 36 Wakati wakiongea mambo hayo, Yesu
mwenyewe alisimama katikati yao, na akawaambia, "Amani iwe kwenu." 37 Lakini waliogopa na kujawa
na hofu, na wakafikiri kwamba waliona roho. 38 Yesu akawaambia, Kwanini mnafadhaika? Kwanini
maswali yanainuka mioyoni mwenu? 39 Angalieni mikono yangu na miguu yangu, kwamba ni mimi
mwenyewe. Niguseni na muone. Kwa maana roho haina nyama na mifupa, kama mnionavyo mimi kuwa
navyo." 40 Alipokwisha kusema hivi, akawaonyesha mikono yake na miguu yake. 41 Walipokuwa bado na
furaha iliyochanganyikana na kutokuamini, na kustaajabu, Yesu akawaambia, "Je mna kitu chochote cha
kula?" 42 Wakampa kipande cha samaki aliyechomwa. 43 Yesu akakichukua, na kukila mbele yao. 44
Akawaambia, "Nilipokuwa nanyi, niliwaambia kwamba yote yalioandikwa kwenye sheria ya Musa na
manabii na Zaburi lazima yatimilike." 45 Kisha akafungua akili zao, kwamba waweze kuyaelewa
maandiko. 46 Akawaambia, "Kwamba imeandikwa, Kristo lazima ateseke, na kufufuka tena kutoka katika
wafu siku ya tatu. 47 Na toba na msamaha wa dhambi lazima ihubiriwe kwa jina lake kwa mataifa yote,
kuanzia kutokea Yerusalemu. 48 Ninyi ni mashahidi wa mambo haya. 49 Angalia, nawapelekea ahadi ya
Baba yangu juu yenu. Lakini subirini hapa jijini, mpaka mtakapovishwa nguvu kutoka juu. 50 Kisha Yesu


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

akawaongoza nje mpaka walipokaribia Bethania. Akainua mikono yake juu, na akawabariki. 51 Ikatokea
kwamba, wakati alipokuwa akiwabariki, aliwaacha na akabebwa juu kuelekea mbinguni. 52 Basi
wakamwabudu, na kurudi Yerusalemu na furaha kuu. 53 Waliendelea kuwepo hekaluni, wakimbariki
Mungu.

---

## Luka 24 Maelezo ya Jumla

### Dhana maalum katika sura hii

### Imani ya wanawake

Katika sura hii inaonekana kuwa Luka kwa makusudi anatofautisha imani ya wanawake na imani ya wanafunzi kumi na wawili.

### Ufufuo

Luka katika sura hii anatumia maelezo mengi ili kuonyesha ufufuo wa Yesu kutoka kwa wafu. Luka anaonyesha kwamba haikuwezekana kwa mtu mwingine kufa kwa niaba ya Yesu. Anaonyesha pia kwamba ufufuo haukuwa mfano. and

### Changamoto nyingine za kutafsiri katika sura hii

### "Mwana wa Binadamu"

Yesu anajiita mwenyewe kama "Mwana wa Binadamu." Lugha zingine haziwezi kuruhusu mtu kujitaja mwenyewe kama 'mtu wa tatu.'

### "Siku ya tatu"

Inasemekana kuwa Yesu alifufuka kutoka wafu siku ya tatu. Alikufa siku ya Ijumaa alasiri (kabla ya kutua kwa jua) na kufufuliwa Jumapili. Katika Israeli ya kale, siku ilianza na kumalizika wakati wa kutua kwa jua. Pia walihesabu sehemu yoyote ya siku kama "siku."

### Watu wawili wenye mavazi ya kuangaza

Mathayo, Marko, Luka, na Yohana wote waliandika juu ya malaika waliovalia nguo nyeupe wakiwa pamoja na wanawake katika kaburi la Yesu. Waandishi wawili kati yao waliwaita wanaume, lakini ni kwa sababu tu malaika walikuwa katika hali ya kibinadamu. Waandishi wawili waliandika kuhusu malaika wawili, lakini waandishi wengine wawili waliandika juu ya moja tu. Ni bora kutafsiri kila moja ya vifungu hivi kama inavyoonekana katika ULB bila kujaribu kufanya vifungu vyote kufanana. (Angalia: Mathayo 28:1-2, Marko 16: 5 na Luka 24: 4 na Yohana 20:12)

---

### Luke 24:1

**Mapema sana siku ya kwanza ya wiki**
"Kabla jua halijachomoza siku ya Jumapili"

**walikuja**
"wanawake walifika kwenye."

**kaburini**
Kaburi lilikuwa limechongwa katika mwamba wa karibu na bahari.

**jiwe limeviringishwa**
Tafsiri mbadala: "kwamba mtu fulani alikuwa ameriviringisha lile jiwe"

**jiwe**
Hili lilikuwa kubwa, limechongwa, jiwe la duara kubwa la kutosha kuweza kuziba kabisa mlango wa kuingilia kaburini. Lilihitaji watu wengi kulivingirisha.

### Luke 24:4

**Ilitokea**
Hii sentensi ilitumika hapa kuweka alama ya tukio muhimu katika simulizi.

**mavazi ya kung'aa**
"wamevaa angavu, mavazi yanayong'aa"

**wamejaa hofu**
"wakaogopa"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**Kwanini mnamtafuta aliye hai miongoni mwa wafu?**
Wale wanaume wanatumia swali kuwapinga wale wanawake kumtafuta kwenye kaburi mtu aliyehai. Tafsiri mbadala: " Mnamtafuta mtu aliye hai kati ya au miongoni mwao wafu" au "Hamtakiwi kumtafuta mtu ambaye yu hai katika sehemu wanapozika watu waliokufa!"

**Kwanini mnamtafuta**
Hapa inamaanisha wengi, inaongelea juu ya wanawake waliokuja.

### Luke 24:6

**Kumbukeni alivyo..**
"Kumbukeni yale"

**alivyosema nanyi**
Yesu alikuwa amekwisha kusema haya wiki moja mapema.

**nanyi**
Neno "nanyi" linaonesha wingi. Inaongelea juu ya wale wanawake na wanafunzi wengine.

**kwamba Mwana wa Adamu**
Huu ni mwanzo wa kunukuu jambo si kwa njia ambayo imenyooka.

**Mwana wa Adamu lazima atolewe kwenye mikono ya watu wenye dhambi na asulubishwe.**
Hii ni jamboa bila shaka lingetokea kwa sababu alikuwa ameamua kwamba litatokea. Tafsiri mbadala: "ilikuwa ni lazima wamtoe Mwana wa Adamu kwa watu wenye dhambi ili waweze kumsulubisha .

**kwenye mikono**
Hapa "mkono" unaonyesha nguvu au uthibiti.

### Luke 24:8

**wakakumbuka maneno yake**
Tafsiri mbadala: "walikumbuka yale aliyoyasema Yesu"

**wengine wote**
"wanafunzi wengine wote waliokuwa na mitume kumi na mmoja"

**Basi**
Neno hili limetumika hapa kuonyesha pumziko katika simulizi kuu. Hapa Luka anatoa majina ya baadhi ya wanawake na kuelezea namna ambavyo mitume waliitikia kwa kile ambacho walisema.

### Luke 24:11

**Lakini ujumbe huu ukaonekana kama mzaa tu kwa mitume**
"Lakini mitume walifikiri kwamba kile ambacho wanawake walisema yalikuwa ni maongezi yasiyo na maana"

**akichungulia na kuangalia ndani**
"akainama." Petro ilimlazimu ainame ili aweze kuangalia au kutazama kaburini.

**sanda ziko peke yake**
"sanda tu"

### Luke 24:13

**Tazama**
Hii inaashiria mwanzo wa tukio jingine tofauti na lile linalowahusisha wale wanawake na Petro.

**siku hiyo hiyo**
"siku ile ile "

**Emmau**
Hili ni jina la mji

**maili sitini**
"kilometa kumi na moja."

### Luke 24:15

**Ikatokea kwamba**
Hii sentensi inatumika hapa kuashiria pale ambapo kitendo kinaanza. Kinaanza na Yesu kuwasogelea karibu.

**macho yao yalizuiliwa katika kumtambua yeye**
Tafsiri mbadala: "Kuna kitu kiliwazuia hivyo hawakuweza kumtambua."

### Luke 24:17

**Cleopa**
Hii ni jina la mwanamume

**Je wewe ni mtu pekee ...siku hizi?**
Cleopa anatumia swali kuonyesha mshangao wake kwamba huyu mtu anaonekana kutokujua juu ya mambo ambayo yametokea Yerusalemu.

### Luke 24:19

**Mambo gani?**
"Mambo gani yametokea?" au "Mambo gani yaliyofanyika?"

**muweza katika matendo na maneno mbele za Mungu na watu wote**
Hii inamaanisha kwamba Mungu alimfanya Yesu kuwa mwenye nguvu na kwamba watu walimuona kwamba alikuwa muwez. Tafsiri mbadala: "na Mungu alimpa nguvu kufanya na kufundisha mambo makubwa ambayo yaliwashangaza watu wote."

**walivyomtoa kuhukumiwa kifo na kumsulubisha**
Tafsiri mbadala: "walimtoa Yesu kwa kiongozi wa Kirumi ili kiongozi huyo aweze kumuua kwa kumsulubisha"

### Luke 24:21

**atakaye waweka huru Israel**
Warumi walitawala juu ya Wayahudi. Tafsiri mbadala: "atakaye tuweka huru Waisraeli kutoka kwa adui zetu wa Kirumi."

**tangu mambo haya yatokee**
"tangu walipomuua"

### Luke 24:22

**Lakini pia**
Wale wanaume waliichukulia taarifa ya wale wanawake kuwa ni kitu kizuri, siyo kitu kingine kibaya cha kuongezea juu ya kifo cha Yesu.

**baada ya kuwapo kaburini**
Wale wanawake ndiyo waliokuwa pale kaburini.

**maono ya malaika**
"malaika katika maono"

### Luke 24:25

**mioyo mizito ya kuamini**
Tafsiri mbadala: "akili zenu ni nzito sana kuamini" au "ninyi ni wazito kuamini"

**Je haikuwa lazima ...utukufu?**
Yesu anatumia swali kuwakumbusha wanafunzi juu ya kile ambacho manabii walisema. Tafsiri mbadala: "Ilikuwa ni lazima...utukufu."

**kuingia katika utukufu wake**
Hii inamaanisha juu ya nyakati ambazo Yesu atamuonyesha kila mmoja uzuri wake na ukuu wake na kupokea heshima na ibada.

### Luke 24:28

**Walipokaribia**
"Walipokuja karibu"

**Yesu alifanya kana kwamba anaendelea mbele**
Wale watu wawili walieelewa kutokana na kitendo chake kwamba alikuwa anaendelea kuelekea sehemu nyingine. Inawezekana labda aliendelea kutembea barabarani walipochipuka kuingia kwenye geti la kijiji. Hakuna kiashiria kwamba Yesu aliwadanganya kwa maneno.

**Wakamsihi**
"Walimuomba kwa nguvu sana." Neno la kiyunani linamaanisha kutumia nguvu za mwili juu ya muda wa ziada. Iliwachukua muda fulani na jitihada fulani kumshawishi.

**Yesu akaingia**
"Yesu akaingia ndani ya nyumba"

### Luke 24:30

**Ilitokea**
Neno hili limetumika hapa kuashiria tukio muhimu katika simulizi.

**mkate**
Hii inazungumzia juu ya mkate unaotengenezwa bila hamila. Haimaanishi chakula kwa ujumla.

**akaubariki**
"akashukuru kwa ajili ya huo mkate" au "Akamshukuru Mungu kwa ajili ya mkate"

**Kisha macho yao yakafunguliwa**
Tafsiri mbadala: "kisha wakaelewa" au "kisha wakatambua"

**akatoweka ghafla mbele ya macho yao**
Hii inamaanisha kwamba ghafula hakuwa tena pale. Haimaanishi kwamba akawa haonekani kwa macho.

**Hivi mioyo yetu haikuwaka... maandiko?**
Wanatumia swali kuweka msisitizo namna walivyo shangazwa juu ya kukutana kwao na Yesu. Tafsiri mbadala: "Mioyo yetu ilikuwa ikiwaka ndani yetu...maandiko."

**ikiwaka ndani yetu**
Hii ni lugha ya picha inayoelezea hisia kali walizokuwa nazo walipokuwa wakiongea na Yesu. Tafsiri mbadala: "Tulikuwa na hisia kali alipokuwa akiongea na sisi."

**wakati alipotufungulia maandiko**
Yesu hakufungua kitabu au gombo la chuo. Tafsiri mbadala: "wakati alipokuwa akituelezea maandiko.

### Luke 24:33

**Wakanyanyuka**
Inahusiana na wale watu wawili

**nyanyuka**
"kuamka" au "kusimama"

**wale kumi na moja**
Hii inaongelea wale mitume wa Yesu. Yuda hakuwa pamoja nao.

**wakisema, "Bwana amefufuka kwelikweli**
Wale mitume kumi na moja na wale waliokuwa pamoja nao walisema hivyo.

**Hivyo wakawaambia**
"Hivyo wale watu wawili wakawaambia"

**mambo yaliyotokea njiani**
Hii inamaanisha Yesu alivyowatokea wakiwa njiani kuelekea kijiji cha Emmau.

**namna Yesu alivyodhihirishwa kwao**
Tafsiri mbadala: "namna walivyomtambua Yesu"


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023

**katika kuumega mkate**
"wakati Yesu alipouvunja mkate" au "wakati Yesu alipouchana mkate"

### Luke 24:36

**Yesu mwenyewe**
Neno "mwenyewe" linakazia juu ya Yesu na mshangao wa Yesu kiuhakika kuwatokea. Wengi wao walikuwa hawajamuona baada ya ufufuko wake.

**katikati yao**
Tafsiri mbadala: "mahali ambapo wote wanaweza kumuona"

**Amani iwe kwenu**
"Basi iweni na amani" au "Basi Mungu awape amani!"

**waliogopa na kujawa na hofu**
"walishikwa na mshangao na kuogopa"

**wakafikiri kwamba waliona roho**
Walikuwa hawajaelewa kiuhalisia kwamba Yesu kwelikweli yu hai.

**roho**
Hapa inamaanisha roho ya mtu aliyekufa.

### Luke 24:38

**Kwa nini mnafadhaika?**
Yesu anatumia swali kuwatia moyo. Tafsiri mbadala: "Msiogopeshwe."

**Kwanini maswali yanainuka mioyoni mwenu?**
Yesu anatumia swali kuwakemea kidogo. Yesu alikuwa anawaambia wasitie mashaka kwamba yu hai. Tafsiri mbadala: "Msitie mashaka katika akili zenu!" au "Acheni kutia mashaka!"

**nyama na mifupa**
Hii ni namna ya kumaanisha mwili

### Luke 24:41

**bado na furaha iliyochanganyikana na kutokuamini**
"bado hawakuweza kuamini kwamba ni ukweli kabisa." Walikuwa na furaha sana, lakini wakati huohuo, ilikuwa ngumu kwao kuamini kwamba ni kweli kabisa imetukia.

**na kustaajabu**
"na walishangazwa" au "na kustaajabu hili laweza kutokeaje"

**mbele yao**
"mbele yao" au "wakiwa wanatazama"

### Luke 24:44

**Nilipokuwa nanyi**
"Wakati bado nilipokuwa nanyi"

**yote yaliyoandikwa kwenye sheria ya Musa na manabii na zaburi**
Tafsiri mbadala: "yote ambayo Musa, manabii, na waandishi wa Zaburi waliandika kuhusu mimi"

**lazima yatimilike**
Tafsiri mbadala: "Mungu atayatimiliza" au "Mungu atayafanya yatokee"

### Luke 24:45

**Kisha akafungua akili zao, kwamba waweze kuyaelewa maandiko.**
Tafsiri mbadala: "Kisha akawawezesha kuyaelewa maandiko"

**Kwamba imeandikwa**
Tafsiri mbadala: "Hivi ndivyo watu hapo zamani waliandika"

**siku ya tatu**
"baada ya usiku mbili"

**toba na msamaha wa dhambi lazima ihubiriwe**
Tafsiri mbadala: "wafuasi wa Kristo inawapasa kuhubiri kwamba watu wanahitaji kutubu ili Mungu awasamehe dhambi zao"

**kwa jina lake**
Tafsiri mbadala: "kama wawakilishi wake" au "na mamlaka yake"

**mataifa yote**
"makabila yote kwenye jamii" au "makundi yote ya watu"

### Luke 24:48

**Ninyi ni mashahidi**
"Mnatakiwa kuwaambia wengine kwamba mliyoyaona kuhusu mimi ni kweli." Wanafunzi walikuwa wameyaona maisha ya Yesu, kufa kwake, kufufuka kwake, na waliweza kueleza kwa wengine kitu gani alifanya.

**Nawapelekea ahadi ya Baba yangu juu yenu**
"Nitawapa kile ambacho Baba yangu aliahidi kuwapa." Yesu, Mungu Mwana, atatoa kile Mungu Baba alikiahidi kwa wafuasi wake wote, ambacho ni Mungu Roho Mtakatifu.

**Baba**
Hiki ni cheo muhimu kwa Mungu

**mtakapovishwa nguvu**
Nguvu ya Mungu itawafunika kwa namna ileile nguo inavyomfunika mtu. Tafsiri mbadala: "mnapokea nguvu."

**kutoka juu**
"kutoka juu" au "kutoka kwa Mungu"

### Luke 24:50

**Ikatokea**
"Ilitokea"

**alipokuwa akiwabariki**
"wakati Yesu alipokuwa anamuomba Mungu kuwatendea mema"

**akabebwa**
Kwa sababu Luka haelezei kiuwazi nani alimbeba Yesu kwenda juu, hatujui kama alikuwa Mungu mwenyewe au malaika mmoja au malaika wengi.

### Luke 24:52

**Taarifa za jumla:**
Mistari hii inaelezea matendo ya Mitume

**walimwabudu yeye**
"Mitume walimwabudu Yesu"

**na kurudi**
kisha walirudi

**waliendelea kubaki hekaluni**
hii inamaanisha kuwa walienda hekaluni kila siku

**hekaluni**
makuhani peke yao ndio waliruhusiwa kuingia hekaluni

**wakimbariki Mungu**
wakimsifu Mungu

---


generated on Wed Oct 25 06:31:01 2023